

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA TISA

Kikao cha Ishirini na Nane – Tarehe 13 Mei, 2020

(Bunge Lilianza Saa Tatu Kamili Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa, tukae.

Katibu!

NDG. NEEMA MSANGI - KATIBU MEZANI:

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:

Taarifa ya mwaka ya Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha kwa mwaka 2018/2019 (*The Annual Report of Arusha International Conference Centre for the Year 2018/2019*).

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

MHE. BONNAH L. KAMOLI - K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha 2019/2020 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, hayupo.

MASWALI NA MAJIBU

(Maswali yafuatayo yameulizwa na kujibiwa kwa njia ya mtandao)

Na. 259

Ujezi wa Hospitali ya Mpimbwe –Jimbo la Kavuu

MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Hospitali ya Halmashauri ya Mpimbwe katika Jimbo la Kavuu ili kupunguza wagonjwa katika Hospitali ya Wilaya ya Mpanda?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Wilfred Kikwembe, Mbunge wa Kavuu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2018/2019, Serikali iliipatia Halmashauri ya Wilaya ya

Mpimbwe shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri ambapo hadi Machi, 2020 ujenzi wa majengosaba ya awali umefikia asilimia 97.

Aidha, katika mwaka wa fedha 2019/20, Hospitali hiyo imeidhinishiwa shilingi milioni 500 kwa ajili ya kumalizia ujenzi wa majengo saba. Vilevile, kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Hospitali hiyo imeidhinishiwa shilingi milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa wodi tatu na shilingi milioni 500 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba.

Na. 260

Usafiri wa Mabasi ya Mwendokasi

MHE. AISHAROSE N. MATTEMBE aliuliza:-

Uamuzi wa Serikali kutengeneza miundombinu ya usafiri wa mabasi ya mwendokasi ulilenga kuondoa kero kwa wananchi Jijiini Dar es Salaam lakini usafiri huu umekuwa kero kubwa kwa watumiaji ikiwemo kujaza abiria bila kujari athari za watumiaji.

Je, Serikali ina mpango gani wa kudhibiti ujazaji abiria pamoja na kuweka utaratibu mzuri kwa watumiaji wake?

WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Aysharose Ndogholi Mattembe, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kupunguza msongamano wa abiria, Wakala wa Mabasi yaendayo Haraka Jijiini Dar es Salaam (*DART*) unaendelea na taratibu za ununuzi ili kumpata mzabuni atakayeongeza idadi ya mabasi kutoka 140 yaliyopo sasa hadi 305. Aidha, wakala unakamilisha utengenezaji wa mfumo wa kielektroniki wa ukusanyaji wa nauli na kuongozea

utakaosaidia kupunguza msongamano kwenye vituo kwani abiria wataweza kupata taarifa za mabasi kwa wakati na hivyo kupanga safari zao kwa ufasaha.

Na. 261

Hitaji la Shule za Kidato cha Tano na Sita Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba

MHE. JASSON S. RWEIKIZA aliuliza:-

Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba haina Shule hata moja ya kiwango cha Kidato cha Tano na Sita. Wananchi wamejitolea na kuweka miundombinu yote inayohitajika katika Shule za Sekondari za Lyamahoro na Rubale ili Shule hizo ziweze kutoa elimu ya Kidato cha Tano na Sita.

Je, ni kwa nini Serikali haitoi kibali ili huduma hii ianze kutolewa katika shule hizi?

WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2020/21, Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba imeidhinishiwa shilingi milioni 120 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya shule ya Sekondari Lyamahoro na Rubale ili ziweze kukidhi sifa za kusajiliwa kuwa za shule za Kidato cha Tano na Sita.

Na. 262

Matukio ya Unyanyasaji na Ukatili wa Kijinsia Nchini

MHE. ANNA J. GIDARYA aliuliza:-

Matukio ya unyanyasaji na ukatili wa kijinsia nchini yameongezeka kwa kiasi kikubwa hasa ubakaji wa watoto pamoja na kulawitiwa jambo ambalo linaathiri watoto kisaikolojia:-

(a) Je, ni lini sasa Serikali itachukua hatua kali dhidi ya watuhumiwa hawa wanaodhalilisha utu wa mtoto wa kitanzania?

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Anna Joram Gidaya, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikichukua hatua kali dhidi ya watuhumiwa wanaodhalilisha utu wa mtoto ikiwa ni pamoja na ubakaji, ulawiti na mimba kwa watoto kwa kusimamia utekelezaji wa Sheria mbalimbali ikiwemo Sheria ya makosa ya Jinai Sura ya 16 Kifungu cha 130 (1) 2 (e) ambayo adhabu yake imeainishwa katika Kifungu 131 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2002 ambacho kinatoa adhabu ya kifungo cha miaka 30 jela au Kifungo cha maisha kwa yejote atakayebainika kuwa na mahusiano ya kingono na mwanafunzi. Aidha, Sheria ya Elimu ya Mwaka 1978 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2016 Kifungu 60 (a) kinatoa adhabu ya kifungo cha miaka 30 jela kwa mtu yejote atakayempa mwanafunzi mimba.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Julai hadi Desemba, 2019 jumla ya mashauri ya unyanyasaji ya watoto 11,270 yalipokelewa ambapo mashauri 1,431 yalipelekwa mahakamani na kati ya hayo, 974 yalitolewa hukumu.

(b) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuandaa maeneo maalum na Madaktari Maalum kwa ajili ya Watoto hawa badala ya kuwaachia jukumu Jeshi la Polisi pekee?

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeanzisha vituo vya mkono kwa mkono (*one stop centers*) ambapo huduma za matibabu, polisi, sheria na ushauri nasaha hutolewa kwa pamoja. Hadi kufikia Machi 2020, jumla ya Vituo vya Mkono

kwa Mkono 13 vimeanzishwa katika hospitali za Amana, Mwananyamala, Tumbi, Kitete, Sekou Toure, Mbeya FFU, Hai, Shinyanga Manispaa, Kahama Hospital, Mt Meru na Nindo-Iringa. Vituo hivyo vinasaidia katika utoaji huduma kwa waathirika wa Ukatili.

Na. 263

Skimu ya Umwagiliaji ya Chela – Msalala

MHE. EZEKIEL M. MAIGE aliuliza:-

Serikali imekusudia kuboresha Kilimo kwa kuanzisha skimu mbalimbali za umwagiliaji na mwaka 2007 Serikali ilianzisha skimu ya umwagiliaji katika Bonde la Cheka Wilayani Msalala:-

(a) Je, Skimu hiyo ya Chela hivi sasa ina mafanikio gani?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kupanua/kuboresha skimu hiyo ili kunufaisha wakulima wengi zaidi?

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza skimu zingine za umwagiliaji Msalala amabapo kuna mabonde mengi kama Bumva, Segese, Kabondo, Mwanyanguli, Igundi, Mwakuhenga na Izuga ambayo yanafaa kwa Kilimo hicho?

WAZIRI WA KILIMO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ezekiel Magolyo Maige, Mbunge wa Jimbo la Msalala lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Skimu ya Chela imekuwa na mafanikio mbalimbali kwa wakulima wa jimbo la Chela na mkoa wa Shinyanga kwa ujumla. Baadhi ya mafanikio hayo ni pamoja na kuongezeka kwa uzalishaji wa mpunga kutoka magunia 10 hadi magunia 22 kwa ekari, kuongezeka

kwa kipato cha wakulima na kuwepo kwa uhakika wa chakula, kuwepo chanzo cha maji chenye uhakika katika kipindi chote cha kilimo kwa mwaka na kusajiliwa kwa kikundi cha wakulima wa mpunga chenye wanachama 150.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatekeleza mipango mbalimbali ili kuhakikisha uwepo wa chanzo kingine cha maji ili kupata maji ya kutosha kwa ajili ya kupanua/ kuboresha skimu hiyo ili kunufaisha wakulima wengi zaidi. Mipango hiyo ni pamoja na kuiingiza Skimu ya Chela katika Mpango Kabambe wa Taifa wa Umwagiliaji (*Revised National Irrigation Master Plan 2018*) na kushirikisha sekta binafsi na Taasisi za kifedha kutafuta vyanzo vingine vya fedha kwa kushirikishana na Halmashauri ya Wilaya na Umoja wa Wakulima ikiwa ni pamoja na kuona jinsi ya kupata mkopo kutoka Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (*TADB*) kwa ajili ya kukamilisha au kuongeza eneo la umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikakati ya Serikali ya kuendeleza kilimo cha umwagiliaji nchini ikiwemo kuongeza skimu zingine za umwagiliaji katika jimbo la Msalala ni pamoja na; kutambua na kuainisha mabonde ya Bulige, Buvya, Butondolo, Kashishi, Mega, Mwaningi, Mwashiboyi na Ntobo ambayo yanafaa kwa Kilimo cha umwagiliaji; kusimamia utekelezaji wa Sheria ya kukusanya tozo ya gharama za uendeshaji na ukarabati wa skimu kwa mujibu wa Sheria; kuanzisha mfuko wa umwagiliaji wa taifa ili kuongeza vyanzo vya mapato ya Serikali kwa ajili ya kuendeleza kilimo cha umwagiliaji katika skimu hizo; kuendelea kutenga fedha za kibajeti kwa kuzingatia upatikanaji wa fedha na kushirikisha sekta binafsi katika kujenga, kuendesha na kusimamia skimu za umwagiliaji.

Na. 264

Soko la Uhakika la Tumbaku Serengeti

MHE. LUCY S. MAGERELI aliuliza: -

Wananchi wa Wilaya ya Serengeti ni wakulima na wafugaji ambao hujishughulisha na kilimo cha Mazao ya

biasara hasa pamba na Tumbaku. Lakini kwa bahati mbaya sana Kampuni pekee ya *Alliance One Tobacco (T) Ltd* iliyokuwa inategemewa kununua zao la Tumbaku ilishafunga shughuli zake Wilayani Serengeti na hivyo kuwaacha Wakulima wa Tumbaku njiapanda:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuchukua hatua za dharura za kuwatafutia soko la uhakika wakulima Wilayani Serengeti ili wafanikiwe kuuza Tumbaku yao?

MHE. WAZIRI WA KILIMO alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lucy Simoni Magereli, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuhakikisha kunakuwa na upatikanaji wa soko la uhakika wa mazao ya kilimo nchini ikiwa ni mamoja na tumbaku. Aidha, katika msimu wa mauzo ya zao la tumbaku mwaka 2019/2020 zao la tumbaku liliweza kununuliwa kwa njia ya mkataba na nje ya mkataba na ambapo jumla ya kilo 68,920,243 zilinunuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya hizo, kilo 57,305,127 za tumbaku yenye madaraja stahili na zenyе thamani ya dola za kimarekani 93,014,785 zilinunuliwa kwa mkataba na jumla ya kilo 11,615,116 za tumbaku (kilo 10,555,519 madaraja stahili zenyе thamani ya Dola za kimarekani 7,983,609 na kilo 1,059,597 za tumbaku iliyokataliwa - Machakala zenyе thamani ya shilingi 356,971,845 sawa na dola za kimarekani 156,704) zilinunuliwa nje ya mkataba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Wilaya ya Serengeti kwa msimu wa mauzo mwaka 2019/2020 Serikali imefanya jitihada za kumpata mnunuzi ambaye ni kampuni ya *MAGEFA GROWERS CO. Ltd* kununua jumla ya kilo 66,667 za tumbaku yenye thamani ya Dola za kimarekani 88,414. Katika msimu wa mwaka 2020/2021 Wilaya ya Serengeti inakadiriwa kuzalisha jumla ya kilo 665,000 na vilevile Serikali

inaendelea na mazungumzo ili Kampuni hiyo ya MAGEFA na kampuni nyingine ziweze kutoa mikataba ya kununua tumbaku hiyo kutoka kwa wakulima wa tumbaku wa Wilaya ya Serengeti. Aidha, kuna majaribio ya mbegu kutoka China ambapo kama zitafaa zitapelekwa pia kwa wakulima wa Serengeti ili kuongeza tija na uzalishaji.

Na. 265

Wawekezaji wa Kujenga Daraja la Mto Wami

MHE. ZAINAB M. AMIRI aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatafuta wawekezaji wa kujenga daraja la Wami Mkao wa Pwani ili liwe la Kisasa na liweze kutozwa tozo kwa watumiaji wa vyombo vyta moto kwenye daraja la Kigamboni Dar es salaam ili liwe mojawapo ya vyanzo vyta mapato nchini?

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zainab Mndolwa Amiri, Mbunge Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Daraja la Wami lenye urefu wa mita 88.75 lililoko Mkao wa Pwani ni kiungo muhimu kutoka Chalinze kwenda Mikoa ya Kaskazini mwa nchi yetu na nchi jirani ya Kenya. Daraja hilo liko umbali wa kilometra 47.4 kutoka njia panda ya Chalinze katika Barabara ya Chalinze – Segera. Kwa sasa Daraja hili halikidhi mahitaji ya magari yanayopita kwa kuwa lilijengwa miaka mingi iliyopita na ni jembamba lenye njia moja. Vilevile, barabara zinazounganisha daraja hili ziko kwenye miinuko mikali na kona mbaya hivyo ajali zimekuwa zikitokea mara kwa mara katika eneo la daraja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ongezeko la magari yanayopita kwenye daraja hili na kwa kuzingatia umuhimu wa daraja hili katika kukuza uchumi wa nchi yetu

Serikali inajenga daraja litakalokidhi mahitaji ya sasa na baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa Daraja Jipyia la Wami ulikamilika Machi 2016. Daraja la Wami ilimesanifiwa kuwa na urefu wa mita 513.5 na upana wa mita 11.85 na litajenga umbali wa mita 670 pemberi mwa daraja linalotumika sasa. Upana wa daraja hili limezingatia sehemu ya barabara, watembea kwa miguu pamoja na vizuizi kwa ajili ya usalama. Mkataba wa ujenzi wa Daraja Jipyia la Wami ulisainiwa tarehe 28/6/2018 kati ya Serikali na Mkandarasa *Power Construction Corporation* wa China kwa muda wa miezi 24. Ujenzi huu utajumuisha ujenzi wa barabara unganishi kwa pande zote mbili zenye jumla ya urefu wa kilometra 3.82 ili kuweza kuunganisha daraja jipyia na barabara kuu ya Chalinze – Segera. Hadi kufikia Machi 2020 ujenzi wa Daraja ulikuwa umefikia asilimia 37.5 na unagharamiwa na Serikali ya Tanzania kwa asilimia 100. Aidha, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kuwa daraja hili halitatozwa tozo.

Na. 266

Hitaji la Mawasiliano ya Simu Kata ya Kala – Nkasi

MHE. SILAFU J. MAUFI aliuliza:-

Mkoa wa Rukwa ulianzishwa mwaka 1974, lakini bado kuna maeneo kama Kata ya Kala hayana mawasiliano yoyote ya simu ingawa Kata hiyo ipo mpakani karibu na Nchi ya Kongo – DRC katika mwambao wa Ziwa Tanganyika Wilaya ya Nkasi:-

Je, ni lini wananchi wa Kata ya Kala watapata mawasiliano ya simu ?

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO
alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Silafu Jumbe Maufi, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (*UCSAF*) immeendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya kufikisha huduma za Mawasiliano nchini. Kata ya Kala ilijumuishwa kwenye zabuni ya awamu ya tatu iliopewa jina la Mradi wa Mipakani na Kanda Maalum (*Border and Special Zone Project, Phase 3*), ikiwa na vijiji tisa (9) na kupata mtoe huduma Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL). Mkataba baina ya TTCL na UCSAF ulisainiwa tarehe 4 Mei, 2018 na utekelezaji wa ujenzi wa mnara wa mawasiliano katika Kata hiyo ulipaswa kukamilika Februari, 2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kutohana na sababu zilizokuwa nje ya uwezo wao, TTCL haikuweza kukamilisha mradi huo kwa wakati kulingana na Mkataba na hivyo Shirika hilo liliomba nyongeza ya muda wa kukamilisha ujenzi ambapo nyongeza ya muda ilitolewa. Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote inaendelea kufanya ufuatiliaji ili Shirika la TTCL likamilishe ujenzi wa mnara katika Kata hiyo mapema, ifikapo mwezi Agosti, 2020.

Na. 267

Tathmini Juu ya Viwanda 100 kwa kila Wilaya

MHE. ZACHARIA P. ISSAAY aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza kufanya tathmini ya mafanikio ya Viwanda 100 kwa kila Wilaya ili kuchochea uchumi wa nchi yetu?

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Zacharia Paul Issaay, Mbunge wa Mbulu Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuweka kumbukumbu sahihi kwamba, Ofisi ya Rais TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara ilianzisha kampeni mahsusini yenye lengo la kufanikisha ujenzi wa viwanda vinya 100 kwa kila Mkao ili kuunga mkono azma ya Serikali ya Awamu ya Tano ya ujenzi wa uchumi wa viwanda, na si viwanda 100 kwa kila wilaya kama swali la msingi linavyouliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilifanya tathmini ya jumla ya upimaji wa mafanikio ya azma ya ujenzi wa viwanda mwezi Februari, 2020, matokeo yalionesha kwamba, jumla ya viwanda 8,477 vimeanzishwa katika mikoa 26 ya Tanzania Bara tangu Serikali ya Awamu ya Tano iingie madarakani. Kati ya viwanda hivyo, viwanda vikubwa ni 201, viwanda vya kati ni 460 viwanda vidogo ni 3,406 na viwanda vidogo sana ni 4,410.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Ofisi ya Taifa ya Takwimu, imeandaa mpango mahsusini wa kufanya tathmini pana ya viwanda vyote vilivyopo Tanzania Bara mwaka 2020/2021 kuititia zoezi maalum linalojulikana kama Industrial Mapping. Zoezi hilo litazingatia pia kufanya tathimini ya mpango wa viwanda 100 kila mkao na litabainisha idadi na aina ya viwanda vilivyopo nchini; ajira; bidhaa zinazozalishwa; mapato; teknolojia zinazohitajika pamoja na malighafi zinazotumika ili uanzishwaji wa viwanda uendane pia na malighafi zinazopatikana hapa nchini ili kuwa na viwanda endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Aidha, Wizara yangu kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali za Serikali pamoja na Sekta Binafsi, inaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuendeleza ujenzi wa viwanda ili azma ya kuifanya Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa kati unaojengwa kuititia viwanda, iweze kufanikiwa ifikapo mwaka 2025.

NAIBU SPIKA: Katibu!

NDG. NEEMA MSANGI-KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 - Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge sasa nimwite Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Profesa Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo katika Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa mpango na bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Aidha, naomba Bunge lako Tukufu lijadili na kuitisha mpango na bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, rahimu, mwingi wa rehema kwa kuniruzuku uhai na kunijalia afya njema ya kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali ya Awamu ya Tano inahitimisha ngwe yake ya kwanza ya miaka mitano mwaka huu, niruhusu kwa namna ya kipekee kabisa kumpongeza, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake mahiri ambao umelilettea Taifa hili maendeleo makubwa katika kipindi hiki cha uongozi wake. Aidha, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan,

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi; na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuiongoza vyema nchi yetu na kutekeleza kwa mafanikio makubwa llani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2015 - 2020. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa umahiri na uongozi wake madhubuti katika uendeshaji wa shughuli za Bunge. Aidha, nakupongeza Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson Mwansasu (Mbunge), Naibu Spika; Wenyeviti wa Bunge; na Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge kwa kazi nzuri wanazozifanya kumsaidia Mheshimiwa Spika katika kusimamia na kuendesha shughuli za Bunge. Naomba Mwenyezi Mungu azidi kuwajaalia afya njema, busara na hekima katika kuiongoza mhimili huu muhimu katika Taifa letu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya kipekee napenda kuipongeza na kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama chini ya uongozi wa Mheshimiwa Salim Mwinyi Rehani, kwa kazi nzuri ya kizalendo inayofanya ya kuishauri Serikali hususan Wizara yangu. Aidha, napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira ambaye alikuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa kipindi kirefu cha miaka 15. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa pole kwa familia, ndugu, jamaa, marafiki kwa vifo vya Waheshimiwa Rashid Ajali Akbar, aliyekuwa Mbunge wa Newala; Mchungaji Dkt. Getrude Rwakatare, aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum; Richard Mganga Ndassa, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Sumve; na Dkt. Augustine Philip Mahiga, aliyekuwa Waziri wa Katiba na Sheria na kabla ya hapo Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki

Mwenyezi Mungu azilaze roho za Marehemu mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba yangu ni kama inavyoonekana katika katibu cha hotuba ya bajeti ya Wizara kilichowasilishwa kwako, hivyo basi nitasoma muhtasi wake na naomba hotuba hiyo yote iingizwe kwenye Kumbukumbu za Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mafanikio ya Wizara katika Kipindi cha Serikali ya Awamu ya Tano, kwa kuwa hii ni hotuba yangu ya mwisho nikiwa Waziri mwenye dhamana ya kusimamia masuala ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa kipindi cha kwanza cha Serikali ya Awamu ya Tano, ninayo heshima kuelezea kwa ufupi baadhi ya mafanikio makubwa ambayo Wizara inajivunia kuyaratibu kwa ufanisi mkubwa na kufanikisha utekelezaji wake kwa kipindi cha kwanza cha Serikali ya Awamu ya Tano kama ifuatavyo:-

(a) Ufunguzi wa balozi mpya nane za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika nchi za Qatar; Uturuki; Sudan; Cuba; Israel; Algeria; Jamhuri ya Korea; na Namibia. Kufunguliwa kwa Balozi hizo, kunaifanya Tanzania kuwa na jumla ya Balozi 43 na Konseli Kuu tatu Kadhalika, Balozi za Ethiopia na Poland zilifunguliwa hapa nchini katika kipindi hicho na kuifanya Tanzania kuwa mwenyeji wa Balozi 62 na Mashirika ya Kimataifa 30;

(b) Tumefanya jitihada kubwa katika kuifanya lugha ya Kiswahili kutumika katika Jumuiya ya Kimataifa na nchi mbalimbali. Juhudi hizo za Tanzania zimefanya Kiswahili kitumike katika eneo la Maziwa Makuu, Umoja wa Afrika, Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika, Jumuiya ya Afrika Mashariki na vyombo mbalimbali vya habari vya Kimataifa.

(c) Kufanikisha kufanyika kwa viwango vya juu Mkutano wa 39 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (*SADC*) uliofanyika Dar es Salaam mwezi Agosti, 2019 ambapo Tanzania ilikabidhiwa

rasmi Uenyekiti wa Jumuiya hiyo utakaodumu kwa kipindi cha mwaka mmoja hadi Agosti 2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uenyekiti wetu wa SADC, tumepata mafanikio mbalimbali ikiwemo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu imekuwa mwenyeji wa maadhimisho ya Maonesho ya Awamu ya Nne ya Wiki ya Viwanda ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika ambayo yalifanyika mwezi Agosti 2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imefanikiwa kuhamasisha watalii kuja nchini kutembelea vivutio mbalimbali vya utalii. Kwa mfano, kuanzia mwaka 2015 hadi 2018, watalii milioni 5,234,448 wametembelea vivutio mbalimbali vya utalii nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeratibu ziara za Wakuu wa Nchi na Serikali mbalimbali wanaokuja nchini ambapo pia husaini makubaiano ya ushirkiano katika sekta mbalimbali. Ziara hizo zina umuhimu mkubwa katika kuimarisha mahusiano ya kidiplomasia na yana faida kubwa kwenye maendeleo ya sekta husika na nchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumefanikisha Uenyekiti wa Tanzania katika Jumuiya ya Afrika Mashariki ambapo mwezi Machi, 2016 nchi yetu iliteuliwa kwa mara ya pili mfululizo kuwa Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo. Katika kipindi cha Uenyekiti wa, Tanzania katika Jumuiya ya Afrika Mashariki Tanzania ilifanikisha utekelezaji wa masuala mbalimbali yakiwemo kuweka mifumo bora matumizi ya rasilimali za Jumuiya; Kuimarisha miundombinu yenyeye sura ya Kikanda; Kuweka mazingira wezeshi ya kibiashara kwa Nchi Wanachama; Kuratibu utumiaji wa Bendera ya Jumuiya ya Afrika Mashariki katika Ofisi zote za Umma nchini; na Matumizi ya Wimbo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki katika Taasisi za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kuratibu Mkutano wa 18 wa Mawaziri wa Mambo ya Nje wa Afrika na *Nordic*

yaani (*Africa-Nordic Foreign Ministers Summit*) uliofanyika kwa mafanikio makubwa mwezi Novemba, 2019 Jijini Dar es Salaam. Ilikuwa ni mara ya kwanza kwa Tanzania kuwa mwenyeji wa Mkutano huo tangu kuanzishwa kwake mwaka 2001. Tofauti na mikutano iliyopita ambayo ilijikita katika masuala ya misaada, mkutano huu ulijielekeza zaidi katika ushirikiano na kuimarisha biashara, uwekezaji, uchumi wa viwanda, mazingira na kukuza utalii pamoja na masuala ya amani na usalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kufanikisha ujumuishwaji wa miradi ya Tanzania katika miradi ya kipaumbele ya miundombinu iliyoidhinishwa na Wakuu wa Nchi za Jumuiya za Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika kipindi cha mwaka 2015 – 2019, Tanzania ilifanikiwa kwa kiasi kikubwa katika utekelezaji wa Itifaki ya Umoja wa Forodha na Itifaki ya Soko la Pamoja za Jumuiya ya Afrika Mashariki kama vile:-

Kuondoa vikwazo vyatia biashara visivyo vyatia kiforodha; kutoa vyeti 32,536 vyatia usajili wa bidhaa kwa wafanyabiashara wa Tanzania wanaofanya biashara katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki; Kutoa vibali vyatia kuingia nchini milioni 1,117,056 kwa raia wa Nchi Wanachama wa Jumuiya na wananchi wetu 851,470 walipata vibali vyatia kuingia katika nchi nyingine za Jumuiya; Kufanikisha Watanzania 1,555 kupata vibali vyatia kufanya kazi katika Nchi nyingine Wanachama wa Jumuiya na Tanzania ilitoa vibali 2,309 vyatia kufanya kazi nchini kwa raia wengine wa Nchi Wanachama wa Jumuiya; Kutoa vibali vipatavyo 879 kwa wanafunzi wa nchi nyingine wanachama wa Jumuiya kuingia na kusoma nchini na wanafunzi Watanzania 3,129 walipata vibali vyatia kusoma katika Nchi Wanachama wa Jumuiya; na Kutoa vibali vyatia ukaazi 3,128 kwa raia wengine wa Nchi Wanachama wa Jumuiya na Watanzania 1,002 walipata vibali vyatia ukaazi katika Nchi Wanachama wa Jumuiya.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kuratibu upatikanaji wa mkopo wa masharti nafuu kutoka Benki ya

Maendeleo Afrika (*AfDB*) wenye thamani ya Dola za Marekani Milioni 200 kwa ajili ya ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa Msalato Jijini Dodoma na upatikanaji wa mkopo wenye masharti nafuu wenye thamani ya Dola za Marekani Milioni 180 kutoka Benki hiyo kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya pete katika Jiji la Dodoma na kushawishi nchi marafiki kutufutia madeni, kuyapunguza au kuweka masharti nafuu ya kuyalipa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutohana na ziara ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki nchini Iran mwezi Oktoba 2017, Serikali ya nchi hiyo iliridhia na kutangaza kusamehe riba ya deni lilitokopwa mwaka 1984 ambayo ilifikia kiasi cha Dola za Marekani Milioni 150. Vile vile, mwezi Septemba 2017, Serikali ya Brazil ilitoa msamaha wenye thamani ya Dola za Marekani Milioni 203.6 ambayo ni asilimilia 86 ya deni lote tunalodaiwa na nchi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo ni baadhi tu ya mafanikio niliyyoyataja hapa taarifa nzima kuhusu mafanikio ya Wizara katika kipindi cha Awamu ya Kwanza ya Serikali ya Awamu ya Tano inapatikana kwenye aya ya 14 kipengele cha kwanza hadi cha 20 katika kitabu cha hotuba ya bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Misingi ya Tanzania Katika Mahusiano ya Kimataifa; historia ya Tanzania imesheheni misingi na misimamo imara inayofanya iendelee kuwa mionganoni mwa nchi zilizo na ushawishi mkubwa kikanda na kimataifa tangu uhuru. Msingi ya nchi yetu kuheshimika kimataifa iliwekwa na Baba wa Taifa Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ambaye alikuwa mstari wa mbele katika kulaani ubabe, uonevu na ukandamizaji popote pale ulipotokea duniani na alipigania uhuru wa Afrika na kusitiza mshikamano kati ya nchi zinazoendelea. Kupitia misingi hii ambayo viongozi wetu wameendelea kuienzi, Tanzania imeendelea kuheshimika sana kikanda na kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kusimamia misingi hiyo, Serikali ya Awamu ya Tano imeendelea kulinda uhuru wa nchi, haki yetu ya kujamulia mambo yetu wenyewe bila

kuingiliwa, mipaka ya nchi yetu; kuimarisha ujirani mwema; na kutekeleza Sera ya Kutofungamana na Upande Wowote kama dira na msimamo wetu kwenye mahusiano na nchi nyininge za Jumuiya ya Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini ya hali ya dunia kwa mwaka 2019/2020; katika kipindi cha mwaka 2019/2020 hali ya uchumi na siasa duniani ilionesa kuendelea kuimarika na kutoa matumaini ya kuimarika zaidi kwa kipindi cha miaka michache ijayo licha ya kuwepo changamoto za kiulinzi na kiusalama kwa baadhi ya maeneo. Hata hivyo, mlipuko wa maambukizi ya ugonjwa wa homa kali ya mapafu unaosababishwa na virusi vya Corona yaani (*COVID- 19*) unaashiria tishio kubwa la kuporomoka kwa uchumi wa dunia. Taarifa zaidi kuhusu tathmini ya hali ya uchumi, siasa Ulinzi na Usalama ya Dunia inapatikana kwenye aya ya 18 hadi ya 69 katika kitabu cha hotuba ya bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Nafasi ya Tanzania ya Kimataifa na Kikanda; Tanzania imeendelea kulipa umuhimu mkubwa suala la amani na usalama duniani ambalo ni mionganini mwa tunu za Taifa letu tangu kupata uhuru. Ili kuenzi tunu hizi na kutambua umuhimu wa kulinda na kudumisha amani na usalama duniani, nchi yetu imeendelea kushirikiana na Jumuiya ya Kimataifa katika ulinzi na amani duniani. Katika kutekeleza hilo, hadi kufikia mwezi Januari, 2020 nchi yetu imepeleka walinda amani kwenye misheni za kulinda amani za Umoja wa Mataifa zilizopo katika nchi za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Jamhuri ya Afrika ya Kati, Lebanon, Darfur - Sudan, Sudan Kusini na Jimbo la Abyei.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo ya kina kuhusu nafasi ya Tanzania Kimataifa na Kikanda yanapatikana kwenye aya ya 70 hadi ya 81 katika kitabu cha hotuba ya bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kujenga na Kulinda Taswira ya Nchi Kimataifa; Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatambua na

kuheshimu wajibu wake Kikatiba na mikataba ya Kitaifa ya kulinda na kudumisha haki zote za binadamu ikiwemo za kisiasa, kluchumi, kijamii na kiutamaduni zote zikiwa na umuhimu ulio sawa kwa ustawi na maendeleo ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ikiwa Nchi Mwanachama wa Umoja wa Mataifa imeendelea kushiriki kikamilifu katika shughuli za Umoja wa Mataifa, Taasisi na Mashirika yake na pia katika mikutano, mijadala na shughuli mbalimbali za umoja huo, miongoni mwa mijadala ilifanyika kwenye kikao cha 74 cha Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa mwezi Septemba, 2019 katika Jiji la New York, Marekani ambapo nilipata heshima ya kumwakilisha Mheshimiwa Dkt. John Joseph Magufuli Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika kikao hicho nilitoa hotuba iliyoeleza mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Tano kwenye sekta za afya, elimu, maji usafiri wa anga, nishati na ujenzi. Aidha, nilisisitiza juu ya umuhimu wa Umoja wa Mataifa na hasa katika kipindi hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jitihada za Serikali kuufahamisha ulimwengu namna inavyotetea na kusimamia haki za binadamu hapa nchini mwezi Februari, 2020, Jijini Geneva, Uswisi nilongoza ujumbe wa Tanzania kwenye kikao cha 43 cha Baraza la Umoja wa Mataifa la Haki za Binadamu. Kwenye kikao hicho nilieleza kuhusu mafanikio ya Serikali katika kulinda na kusimamia haki za elimu, afya, upatikanaji wa maji safi na salama, umeme na maendeleo ya kiuchumi. Aidha, nilielezea mafanikio yaliyopatikana katika kuongeza uwajibikaji kwa watumishi na viongozi wa umma, kupambana na vitendo vya rushwa, vita dhidi ya biashara za dawa za kulevyta, kuongezeka kwa kiwango cha ukusanyaji kodi na kupanua wigo wa vyanzo vya mapato ili kuwashudumia Watanzania wetu ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo ya kina kuhusu kujenga, kulinda taswira ya nchi Kimataifa yanapatikana kwenye aya ya 82 hadi aya ya 90 katika kitabu cha hotuba ya bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania kwenye nafasi za Kimataifa; baadhi ya Watanzania wamechaguliwa na kuteuliwa kushika nafasi mbalimbali za uongozi Kikanda na Kimataifa kama inayoonekana kwenye aya ya 91 hadi ya 98 katika kitabu cha hotuba ya bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba nitoe taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara katika kipindi cha mwaka 2019/2020 na mpango wa bajeti katika mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapitio ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka 2019/2020; katika kuiwezesha Wizara kutekeleza majukumu yake mwaka 2019/2020, Bunge lako hili Tukufu liliidhinisha kiasi cha Sh.166,929,820,000. Kati ya hizo, Sh.162,926,820,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Sh. 4,000,000,000 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Katika fedha zilizotengwa kwa Matumizi ya Kawaida, Sh.152,717,723,000 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na Sh.10,209,097,000 ni kwa ajili ya Mishahara.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2020 Wizara ilikuwa imepokea kiasi cha Sh.133,300,900,671. Kiasi hicho cha fedha ni sawa na asilimia 79.8. ya fedha zote za bajeti zilizoidhinishwa katika mwaka wa fedha 2019/2020. Kati ya fedha hizo, Sh.124,186,236,675 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na Sh.8,626,758,000.00 ni kwa ajili ya mishahara. Aidha, katika kipindi hicho Wizara imepokea fedha za bajeti ya miradi ya maendeleo kiasi cha Sh.487,905,996. kwa ajili ya miradi ya ukarabati wa nyumba ya makazi ya Balozi wa Tanzania Ottawa, Canada na ujenzi wa vyumba vya madarasa katika Chuo cha Diplomasia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika fedha zilizotolewa, Wizara imetumia kiasi cha Sh. 99,324,222,786. Kiasi hicho cha fedha ni sawa na asilimia 75 ya fedha zilizopokelewa. Kati ya fedha hizo, Sh.91,390,079,647 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na Sh.7,596,237,142 ni kwa ajili ya mishahara. Aidha, Wizara imetumia kiasi cha Sh.337,905,996 kwa ajili ya

mradi wa maendeleo wa ujenzi wa vyumba vyataga madarasa katika Chuo cha Diplomasia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 Wizara ilipanga kukusanya shilingi 2,558,079,072, kati ya kiasi hicho shilingi 67,980,000.00 ni maduhuli ya Makao Makuu ya Wizara na Shilingi 2,482,899,072 ni maduhuli kutoka Balozi za Tanzania nje ya nchi. Vyando vyataga mapato hayo ni pamoja na uhakiki wa nyaraka, pango la majengo ya Serikali nje ya nchi na mauzo ya nyaraka za zabuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Julai 2019 hadi tarehe 30 Aprili, 2020 Wizara imekusanya jumla ya shilingi 5,253,091,600 sawa na asilimia 206 ya lengo liliopangwa kwa mwaka 2019/2020. Ongezeko la maduhuli limetokana na baadhi ya Balozi kuendelea kukusanya maduhuli ya viza kupitia utaratibu wa kawalda kabla ya kuanza kwa utaratibu wa kielektroniki yaani *e-visa*. Aidha, kuanzia mwezi Novemba 2019, Wizara inaendelea kukusanya maduhuli ya visa kwa njia ya kielektroniki baada ya Balozi zetu kufungiwa mtandao huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa taarifa ya mapato na matumizi ya Wizara kwa Mwaka 2019/2020, naomba sasa nitumie fursa hii kueleza kwa kifupi mapitio ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kubuni na Kusimamia Utekelezaji wa Sera ya Nchi ya Mambo ya Nje kama nilivyoeleza kwenye sehemu ya mafanikio ya Wizara kwa kipindi cha kwanza cha Serikali ya Awamu ya Tano kuwa Tanzania ni Mwenyekiti na Mwenyeji wa Mikutano ya Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika yaani SADC kwa kipindi cha mwaka mmoja. Tangu tulipopokea Uenyekiti tumeratibu, kuandaa na kuongoza Mikutano sita ya Kisekta kama inavyoonekana kwenye Aya ya 200 hadi 207 katika Kitabu cha Hotuba ya Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi hiki Wizara imeratibu kwa mafanikio makubwa na kufanikisha kufanyika

kwa Mkutano wa Baraza la Mawaziri wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika uliofanyika tarehe 18 Machi, 2020. Mkutano huo ulifanyika kwa mara ya kwanza kwa njia ya mtandao yaani *video conference* ikiwa ni tahadhari dhidi ya maambukizi ya ugonjwa wa homa kali ya mapafu unaosababishwa na virusi vya Corona.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na mwenendo wa mlipuko wa ugonjwa wa *COVID -19* duniani, ni dhahiri kwamba ili kukabiliana nao kunahitajika ufanisi na ushirikiano wa hali ya juu katika ngazi za kitaifa, kikanda na kimataifa. Kufuatia hali hiyo, kwa mara nyingine tena naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa *SADC* pamoja na Dkt. Stergomena Lawrence Tax, Katibu Mtendaji wa *SADC* kwa maelekezo na ushauri wanaoendelea kuutoa kwa Nchi Wanachama illi kuhakikisha kwamba ukanda wetu hauathiriki sana na janga hili la *COVID-19*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mapambano dhidi ya ugonjwa huu zifuatazo ni hatua mbalimbali ambazo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imefanikisha katika *SADC*, hatua hizo ni kufanyika kwa Mkutano wa dharura wa Mawaziri Afya wa *SADC* kuhusu *COVID-19* tarehe 9 Machi, 2020 chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Ummy Ally Mwalimu, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Mkutano huu ulifanyika kwa njia ya mtandao. Mkutano huo pamoja na mambo mengine, ulipendekeza kuundwa kwa Kamati ya Wataalam kwa ajili ya kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Itifaki ya Afya ya *SADC* kufuatia mlipuko wa ugonjwa wa homa kali ya mapafu unaosababishwa na virusi vya Corona yaani *COVID-19*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mapendekezo hayo ya Mawaziri wa Afya, yaliridhiwa na Baraza la Mawaziri wa *SADC* katika mkutano uliofanyika tarehe 18 Machi, 2020. Aidha, tarehe 31 Machi 2020, Kamati ya Wataalam wa *SADC* iliyofanya kikao kwa njia ya mtandao na kwa kushirikiana na Sekretarieti ya *SADC* ilipendekeza kuandaliwa kwa mkutano

huu wa Dharura wa Baraza la Mawaziri. Aidha, Kamati hiyo pia iliridhia mapendekezo 11 baadhi yake yakiwa;

- (i) Ufuatiliaji na utekelezaji wa Itifaki ya Afya kuhusu magonjwa ya mlipuko;
- (ii) Uelimishaji wa madhara na ushirikishwaji wa jamii;
- (iii) Uratibu wa Kikanda wa kukabiliana na *COVID-19*;
- (iv) Uwezeshaji wa usafirishaji wa bidhaa muhimu miongoni mwa nchi za SADC wakati wa mlipuko wa ugonjwa wa *COVID-19*; na
- (v) Masuala ya Uwezeshaji wa biashara katika ukanda kwa kipindi hiki cha ugonjwa wa *COVID-19*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 6 Aprili, 2020 niliongoza Mkutano wa Dharura wa Baraza la Mawaziri uliofanyika kwa njia ya mtandao. Mkutano huo ulipokea taarifa ya Kamati ya Wataalam ya kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Itifaki ya Afya ya SADC, kufuatilia mlipuko wa *COVID-19*.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha Mkutano uliidhinisha mwongozo wa Urazinshaji (*harmonization*) na uwezeshaji wa usafirishaji wa bidhaa muhimu na huduma katika nchi za SADC katika kipindi hiki cha janga la *COVID-19*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hatua nyingine Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa SADC ameendelea kuzisisitiza Taasisi za Fedha za Kimataifa na Washirika wengine wa Maendeleo kuzifutia madeni Nchi za SADC ili ziweze kutumia fedha hizo katika kukabiliana na janga hili la COVID 19, huo ndio mchango wa Tanzania katika SADC katika kupambana na *COVID-19*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, mwezi Machi, 2020 Wizara iliratibu na

kushiriki katika Mkutano wa Dharura wa pamoja wa Baraza la Mawaziri la Kisekta la masuala ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Baraza la Mawaziri la Kisekta la Afya uliofanyika kwa njia ya mtandao. Mkutano huo ulitoa azimio la Mkakati wa pamoja wa kukabiliana na mlipuko wa Homa kali ya mapafu inayosababisha na virusi vyta Corona na mipango ya kutatua changamoto zinazojitokeza kutokana na hatua zilizochukuliwa na Nchi wanachama katika kukabiliana na ugonjwa huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya maazimio ya Mkutano huo yameorodheshwa katika hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi Desemba 2019 nilimwakilisha Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mkutano wa Tisa wa Wakuu wa Nchi, Nchi za Afrika, Caribbean na *Pacific* uliofanyika huko Nairobi, na Jumuiya hiyo sasa inafahamika kama *Organization of Africa, Caribbean and Pacific states* uliofanyika jijini Nairobi, Kenya. Katika Mkutano huo, Tanzania ilifanikiwa kuzishawishi Nchi Wanachama pamoja na mambo mengine kukubali kujumuisha zao la Korosho kwenye orodha ya mazao ya Kimkakati ndani ya ACP ambayo yananufaika na Programu ya Mnyororo wa Thamani wa ACP.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya kina kuhusu kusimamia utekelezaji wa sera ya Mambo ya Nchi za Nje ni kama inavyooneshwa katika Aya ya 107 hadi 235 katika Kitabu cha Hotuba ya Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Masuala ya Diplomasia na Itifaki, Kufuatilia na Kusimamia Utekelezaji wa Mikataba iliyosainiwa. Katika kipindi cha mwaka 2019/2020, Wizara iliratibu na kushiriki katika majadiliano na kusimamia uwekwaji wa saini wa Mikataba na Hati za Makubaliano na Nchi mbalimbali. Mikataba na hati za makubaliano zilizosainiwa ni kama inavyoonekana kwenye aya ya 236 – 237 katika kitabu cha Hotuba ya Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Masuala ya Diplomasia, Itifaki, Uwakilishi na Huduma za Kikonseli. Katika kuimarisha mahusiano ya Tanzania na Nchi nyingine, Wizara imeendelea Kuandaa, Kuratibu Ziara mbalimbali za Viongozi Wakuu wa Kitaifa Nje ya Nchi. Aidha, Wizara imeratibu na kufanikisha ziara za Viongozi wa Mataifa mbalimbali na Mashirika ya Kimataifa waliokuja Tanzania kwenye ziara rasmi, kushiriki katika mikutano, makongamano na kutekeleza majukumu mbalimbali ya kitaifa. Taarifa zaidi kuhusu masuala ya kidiplomasia, itifaki, uwakilishi na huduma za kikonseli inapatikana kwenye Aya ya 242 hadi 45 katika kitabu cha Hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ushirikishwaji wa Watanzania wanaoishi ughaibuni. Wizara imeendelea kuwashirikisha Watanzania wanaoishi ughaibuni (*Diaspora*) katika kuchangia maendeleo ya nchi yao kama inavyoonekana kwenye Aya ya 246 hadi 251 katika Kitabu cha Hotuba ya Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utawala na Maendeleo ya Watumishi, Wizara imeendelea kusimamia masuala ya Utawala na Maendeleo ya Watumishi kwa lengo la kuimarisha utendaji wa kazi. Wizara ina jumla ya watumishi 439 wa kada mbalimbali. Katika kuimarisha utendaji kazi wa Wizara, masuala mbalimbali yanayohusu Utawala na Maendeleo ya Watumishi yameendelea kusimamiwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Uteuzi wa Viongozi, katika kipindi cha Mwaka 2019/2020 Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alimteua Balozi Kanali Wilbert Augustin Ibuge kuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Vilevile Mheshimiwa Rais aliwateua Mabalozi 17 ambapo 14 kati yao wanaiwakilisha Tanzania katika nchi mbalimbali duniani na watatu wanaofanya shughuli zao hapa nchini. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Mwaka 2019/2020, watumishi 19 walipandishwa vyeo kwa mserereko. Kati ya watumishi hao, watano walipandishwa kuwa Maafisa Mambo ya Nje Wakuu Daraja I na watumishi 14 walipandishwa kuwa Maafisa Mambo ya Nje Wakuu Daraja la II. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Umiliki wa majengo, Wizara imeendelea kujenga na kukarabati majengo yake ikiwa ni utekelezaji wa Mpango wa Miaka 15 yaani 2017/2018 hadi 2031/2032 wa Ujenzi, Ununuzi na Ukarabati wa Majengo ya Ofisi na Makazi ya Watumishi Balozini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Tanzania inamiliki majengo 106 pamoja na viwanja 12. Taarifa kamili kuhusu Utawala na maendeleo ya Watumshi inapatikana kwenye Aya ya 255 hadi 260 katika Kitabu cha Hotuba ya Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kuratibu na Kusimamia Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Wizara na Taasisi zilizo chini ya Wizara. Katika Mwaka wa Fedha 2019/2020, Wizara ilipangiwa bajeti ya maendeleo ya shilingi 4,000,000,000 kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo iliyopo ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia tarehe 30 Aprili 2020, Wizara imepokea kiasi cha shilingi 487,905,996 sawa na asilimia 12.2 ya fedha zilizoidhinishwa. Tayari ukarabati wa makazi ya Balozi wa Tanzania Ottawa nchini Canada umeanza ambao utagharimu shilingi 150,000,000.00. Vilevile, shilingi 337,905,996 zinatumika katika ujenzi wa vyumba vya madarasa unaoendelea kwenye Chuo cha Diplomasia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utekelezaji wa Majukumu ya Taasisi zilizo chini ya Wizara. Katika kipindi hiki, Wizara imeendelea kuzisimamia taasisi zilizo chini yake ambazo ni Kituo cha Maendeleo cha Kimataifa cha Arusha (*AICC*); Chuo cha Diplomasia (*CFR*) na Mpango wa Kutathmini Kiutawala Bora Barani Afrika (*APRM*) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Kituo cha Kimataifa cha Arusha hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2020 Kituo kimekusanya mapato ya shilingi 11,815,516,916 kati ya fedha hizo shilingi 4,199,883,072 (bilioni nne milioni mia moja tisini na tisa, themanini na sita laki nane elfu, themanini na tatu na sabini na mbili) zimetokana na Huduma za Kumbi za Mikutano za AICC na JNICC. shilingi 3,514,566,238 zimetokana upangishaji wa ofisi na nyumba za kuishi. Shilingi 3,314,067,603 zimetokana na huduma za hospitali. Vilevile katika kipindi cha 2019/2020, Kituo kilitoa shilingi 200,000,000 kama gawio la awali kwa Serikali. Maelezo zaidi yanapatikana katika aya ya 264 hadi 268 katika kitabu cha Hotuba ya Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha Diplomasia kimeendelea kutoa mafunzo na kufanya tafiti katika masuala ya Diplomasia, Uhusiano wa Kimataifa, Strategia, Usuluhishi wa migogoro na Ujenzi wa Amani. Lengo ni kufanya chuo kuwa taasisi iliyobobea katika elimu ya juu na ushauri katika Nyanja hizo .

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia tarehe 30 Aprili 2020, Chuo kilipokea shilingi 2,641,642,486 kati ya fedha hizo, Shilingi 1,637,072,490 ni kwa ajili ya mishahara, na shilingi 666,664,000 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na shilingi 337,905,996 ni kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa vyumba vyaa madarasa. Aidha, Chuo kilikusanya jumla ya shilingi 1,510,514,650 sawa na asilimia 97 ya lengo la mwaka la shilingi 1,545,001,530. Taarifa zaidi zinapatika kwenye aya 269 hadi 275 katika kitabu cha Hotuba ya Bajeti.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri sasa omba fedha.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Naibu Spika, niombe fedha eeeeeh! Naomba msaada, naomba bajeti.

NAIBU SPIKA: Namba 14.0 hitimisho.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Hahaha, hitimisho.

NAIBU SPIKA: Ukurasa wa 183.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Naibu Spika, Okay, ili kuweza kutekeleza kikamilifu majukumu ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2020/2021, naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 199,750,684,000. Kati ya fedha hizo shilingi 179,750,684,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 20,000,000,000 ni kwa ajili ya Bajeti ya Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchukua nafasi hii adhimu kukushukuru tena wewe binafsi na Waheshimiwa Wabunge kwa kuniskiliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.
(*Makofi*)

HOTUBA YA MHESHIMIWA PROF. PALAMAGAMBA JOHN AIDAN MWALUKO KABUDI (MB), WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021- KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

1.0 UTANGULIZI

1. Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo katika Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama (NUU), naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa mpango na bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Aidha, naomba Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha mpango na bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

2. Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kuniruzuku uhai na kunijalia afya njema ya kuniwezesha kusimama mbele ya

Bunge Iako Tukufu kuwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

3. Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali ya Awamu ya Tano inahitimisha ngwe yake ya kwanza ya miaka mitano mwaka huu, niruhusu kwa namna ya kipekee kabisa kumpongeza, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake mahiri ambao umeliletea Taifa hili maendeleo makubwa katika kipindi hiki cha uongozi wake. Aidha, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi; na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuiongoza vyema nchi yetu na kutekeleza kwa mafanikio makubwa llani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2015 - 2020.

4. Mheshimiwa Spika, mtakuwa mashahidi kwamba chini ya uongozi wa viongozi wetu hawa mahiri nchi yetu imepiga hatua kubwa sana kimaendeleo ikiwemo kutekeleza miradi muhimu ya maendeleo. Aidha, dira na maono ya viongozi wetu hawa imeifanya nchi yetu kuendelea kuwa ya amani na utulivu na Watanzania tumeendelea kudumisha mshikamano na umoja wa kitaifa, na hapana shaka tumeendelea kuwa mfano wa kuigwa kwa nchi nyiningine za Afrika na duniani kote.

5. Mheshimiwa Spika, ninapenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hotuba yake aliyowasilisha hapa Bungeni ambayo imetoa dira na mwongozo wa utekelezaji wa kazi za Serikali katika mwaka wa fedha 2020/2021. Aidha, ninawapongeza pia Waheshimiwa Mawaziri wenzangu walionitangulia kuwasilisha hoja zao hapa Bungeni.

6. Mheshimiwa Spika, vilevile napenda kumpongeza Mheshimiwa Job Yustino Ndugai (Mb) Spika wa Bunge la

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa umahiri na uongozi wake madhubuti katika uendeshaji wa shughuli za Bunge. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Dkt. Tulla Ackson Mwansasu (Mb), Naibu Spika; Wenyeviti wa Bunge; na Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge kwa kazi nzuri wanazozifanya kumsaidia Spika katika kusimamia na kuendesha shughuli za Bunge. Naomba Mwenyezi Mungu azidi kuwajaalia afya njema, busara na hekima katika kuongoza mhimili huu muhimu katika Taifa letu.

7. *Mheshimiwa Spika*, kwa namna ya kipekee napenda kuipongeza na kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama chini ya uongozi wa Mheshimiwa Salim Mwinyi Rehani (Mb), kwa kazi nzuri na ya kizalendo inayoifanya ya kuishauri Serikali hususan Wizara yangu. Aidha, napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Mussa Azan Zungu (Mb), Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira ambaye alikuwa Mwenyezeki wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa kipindi kirefu. Naomba nikiri kuwa miongozo na ushauri wao katika masuala mbalimbali umekuwa na mchango mkubwa katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

8. *Mheshimiwa Spika*, naomba pia kumpongeza Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu, Mbunge wa Singida Mashariki kwa kuchaguliwa katika kipindi cha mwaka huu wa fedha 2019/2020. Kuchaguliwa kwake ni kielelezo cha kuaminiwa na wananchi wa Jimbo la Singida Mashariki katika kuwaletaa maendeleo.

9. *Mheshimiwa Spika*, kwa masikitiko makubwa naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa pole kwa familia, ndugu, jamaa, marafiki na wananchi wa jimbo la Newala Vijijini kwa kifo cha Mheshimiwa Rashid Ajali Akbar aliyekuwa Mbunge wa Jimbo hilo kilichotokea tarehe 15 Januari 2020. Vilevile, napenda kutoa pole kwako na Bunge lako Tukufu kwa kifo cha Mheshimiwa Askofu Dkt. Getrude Rwakatare, (Mb), kilichotokea tarehe 20 Aprili 2020.

10. Mheshimiwa Spika, pia naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa pole kwa familia, ndugu, jamaa, marafiki na wananchi wa Jimbo la Sumve kwa kifo cha Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa aliyekuwa Mbunge wa Jimbo hilo kilichotokea tarehe 29 Aprili 2020. Kwa masikitiko makubwa natoa pole kwa familia, ndugu, jamaa na marafiki kwa kifo cha Mheshimiwa Balozi Dkt. Augustine Philip Mahiga (Mb), aliyekuwa Waziri wa Katiba na Sheria na kabla ya hapo Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kilichotokea tarehe 1 Mei 2020.

11. Mheshimiwa Spika, naomba nikiri kuwa vifo hivi ni pengo kubwa kwa Taifa kutokana na michango yao adhimu katika kulitumikia Taifa hili. Sisi sote ni wa Mwenyezi Mungu na kwake tutarejea, Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahala pema peponi. Amina.

12. Mheshimiwa Spika, kimataifa pia kulitokea misiba ya viongozi mbalimbali ambayo Serikali ilituma salamu za rambirambi na kutuma wawakilishi. Kwa mara nyingine tena, kwa niaba ya Serikali naomba kutoa salamu za pole kwa ndugu zetu wa Jamhuri ya Kenya kwa kifo cha Hayati Daniel Toroitich Arap Moi, Rais Mstaafu wa nchi hiyo; ndugu zetu wa Jamhuri ya Zimbabwe kwa kifo cha Muasisi wa Taifa hilo Hayati Robert Gabriel Mugabe; ndugu zetu wa Jamhuri ya Misri kwa kifo cha Hayati Hosni Mubarak, Rais Mstaafu wa nchi hiyo; ndugu zetu wa Oman kwa kifo cha Muadham Sultan Qaboos Bin Said al Said; ndugu zetu wa Tunisia kwa kifo cha Hayati Beji Caid Essebsi, aliyekuwa Rais wa nchi hiyo; na ndugu zetu wa Ufaransa kwa kifo cha Hayati Jacques Chirac, Rais Mstaafu wa nchi hiyo. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahala pema peponi. Amina.

13. Mheshimiwa Spika, vilevile naomba kutoa salamu za pole kwa Serikali za nchi zilizokumbwa na mashambulizi ya kigaidi yakiwemo yaliyotokea katika Ukanda wa Pembe ya Afrika, Ukanda wa Sahel, Ukanda wa Bonde la Mto Chad na sehemu ya Kusini mwa Afrika. Mashambulizi hayo yamesababisha vifo, ulemavu na uharibifu wa mali. Tanzania inaungana na

mataifa mengine duniani kukemea na kulaani vikali vitendo hivyo vyakikatili dhidi ya binadamu.

2.0 MAFANIKIO YA WIZARA KWA KIPINDI CHA SERIKALI YA AWAMU YA TANO

14. *Mheshimiwa Spika*, kwa kuwa hii ni hotuba yangu ya mwisho nikiwa Waziri mwenye dhamana ya kusimamia masuala ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa kipindi cha kwanza cha Serikali ya Awamu ya Tano, ninayo heshima kuelezea kwa ufupi baadhi ya mafanikio makubwa ambayo Wizara inajivunia kuyaratibu kwa ufanisi mkubwa na kufanikisha utekelezaji wake kwa kipindi cha kwanza cha Serikali ya Awamu ya Tano kama ifuatavyo:

- i) Ufunguzi wa balozi mpya nane za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika nchi za Qatar; Uturuki; Sudan; Cuba; Israel; Algeria; Jamhuri ya Korea; na Namibia. Kufunguliwa kwa Balozi hizo, kunaifanya Tanzania kuwa na jumla ya Balozi 43 na Konseli Kuu tatu katika mijini ya Mombasa, Dubai na Jeddah. Kadhalika, Balozi za Ethiopia na Poland zilifunguliwa hapa nchini katika kipindi hicho na kuifanya Tanzania kuwa mwenyeji wa Balozi 62 na Mashirika ya Kimataifa 30;
- ii) Tumefanya jitihada kubwa katika kuifanya lugha ya Kiswahili kutumika katika Jumuiya ya Kimataifa na nchi mbalimbali. Juhudi hizo za Tanzania zimefanya Kiswahili kitumike katika eneo la Maziwa Makuu, Umoja wa Afrika, Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika, Jumuiya ya Afrika Mashariki na vyombo mbalimbali vyaa habari vyaa Kimataifa.
- iii) Kufanikisha kufanyika kwa viwango vyaa juu Mkutano wa 39 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) uliofanyika Dar es Salaam mwezi Agosti 2019 ambapo Tanzania ilikabidhiwa rasmi Uenyekiti wa Jumuiya hiyo utakaodumu kwa kipindi cha mwaka mmoja hadi Agosti 2020. Katika uenyekiti wetu wa SADC, tumefanikiwa mambo makuu yafuatayo:

- a) Kushawishi na kufanikiwa kupitishwa kwa lugha ya Kiswahili kuwa lugha rasmi ya nne ya SADC kwa kutambua lugha ya Kiswahili ni lugha ya ukombozi Kusini mwa Afrika iliyotumika wakati wa mapambano ya kuzikomboa nchi hizo kutoka katika ukoloni na utawala wa ubaguzi wa rangi wa Afrika Kusini. Aidha, katika kukuza lugha yetu ya Kiswahili kwenye Jumuiya ya AfrikaMashariki mitaala ya kufundishia lugha hiyo imeandaliwa na kuanza kutumika;
- b) Kufanikiwa kuzishawishi Nchi Wanachama wa SADC kukubaliana na azimio la kutenga tarehe 25 Oktoba ya kila mwaka kuwa siku maalum ya kupaza sauti ya pamoja kwa nchi za SADC, kuzitaka Marekani na baadhi ya Nchi Wanachama za Jumuiya ya Ulaya kuiondolea nchi ya Zimbabwe vikwazo vyta kiuchumi vya muda mrefu mpaka hapo vitakapoondolewa;
- c) Kufanikiwa kuzishawishi Nchi Wanachama wa Jumuiya ya nchi za Afrika, Karibeani na Pasifikasi (OACPS) kuunga mkono jitihada za SADC katika kuhimiza vikwazo vyta kiuchumi vilivyowekwa dhidi ya Zimbabwe kuondolewa. Nchi za OACPS ziliunga mkono kwa kauli moja wito wa kuondolewa vikwazo dhidi ya Zimbabwe kwa kujumuishwa kwenye maazimio ya Mkutano wa Tisa wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya nchi za Afrika, Karibeani na Pasifikasi (OACPS) uliofanyika mwezi Desemba, 2019 Jijini Nairobi, Kenya; na
- d) Kuwa mwenyeji wa maadhisho ya Maonesho ya Awamu ya Nne ya Wiki ya Viwanda ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) ambayo yalifanyika mwezi Agosti 2019. Lengo la Maonesho hayo lilikuwa ni kuwawezesha wafanyabiashara wa nchi za SADC kutangaza bidhaa zao kwa lengo la kupanua soko ndani ya Jumuiya hiyo. Vilevile, kupitia Maonesho hayo, wafanyabiashara walipata fursa ya kubadilishana uzoefu wa namna ya kuzalisha bidhaa zenye ubora ili kukidhi mahitaji ya soko la ndani na nje ya Jumuiya hiyo. Maonesho hayo yalishirikisha wajasiriamali wapatao 5,352 kutoka ndani na nje ya nchi, Taasisi za umma, viwanda

mbalimbali, Taasisi za huduma za fedha na Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Viwanda.

- iv) Wizara imefanikiwa kuhamasisha watalii kuja nchini kutembelea vivutio mbalimbali vya utalii. Kwa mfano, kuanzia mwaka 2015 hadi 2018, watalii 5,234,448 wametembelea vivutio mbalimbali vya utalii nchini. Watalii hao walitoka nchi mbalimbali zilizopo Bara la Afrika; Ulaya; Amerika ya Kaskazini; Asia; Mashariki ya Kati; Australasia na nchi za Karibeani;
- v) Kuratibu ujio wa Madaktari Bingwa wa fani tofauti kutoka nchi mbalimbali kama vile: Umoja wa Falme za Kiarabu; Saudi Arabia; Misri; Israel; Italia; China; India; Pakistan; Marekani; Ujeruman na Cuba. Madaktari hao walitoa huduma za kitabibu katika baadhi ya hospitali zilizopo Tanzania Bara na Zanzibar na kufanikisha msaada wa ujenzi wajengo la Kitengo cha Magonjwa ya Dharura katika Hospitali ya Benjamin William Mkapa iliyopo jijini Dodoma.
- vi) Kuratibu ushiriki wa Tanzania katika kurejesha na kuimarishe amani na utulivu kwa kushiriki katika utatuzi wa migogoro na operesheni za kulinda amani kikanda na kimataifa. Hadi sasa Tanzania ina jumla ya walinda amani 2,303 kwenye misheni sita za kulinda amani za Umoja wa Mataifa kama ifuatavyo: MINUSCA 455, MONUSCO 969, UNAMID 686, UNIFIL 159, UNISFA 12 na UNIMISS 22;
- vii) Kuratibu ziara za Wakuu wa Nchi na Serikali mbalimbali wanaokuja nchini ambapo pia husaini Makubaliano ya Ushirikiano katika Sekta mbalimbali zikiwemo za kilimo, utalii, afya, uwekezaji, usafiri wa anga na utamaduni. Ziara hizo zina umuhimu mkubwa kwenye kuimarishe mahusiano ya kidiplomasia, pia Makubaliano hayo yana faida kubwa katika maendeleo ya sekta husika na nchi kwa ujumla;
- viii) Kuratibu na kushiriki katika mikutano 12 ya Tume za Pamoja za Ushirikiano kati ya Tanzania na nchi za Kenya, Zambia, Rwanda, Afrika Kusini, Uganda (mikutano mitatu), Zimbabwe, Namibia, Misri, Umoja wa Falme za Kiarabu na Uturuki. Mikutano hiyo imeweza Serikali yetu kufikia makubaliano

na nchi hizo katika maeneo mbalimbali ya ushirikiano kwa manufaa ya Taifa letu;

ix) Kuratibu na kufanikisha ziara za kimataifa za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar. Baadhi ya ziara za viongozi hao zilifanyika katika nchi za Kenya, Rwanda, Uganda, Malawi, Afrika Kusini, Namibia, Zimbabwe, Misri, Ethiopia, China, Djibouti, Indonesia, India, Jordan, Mauritius, Niger, Angola, Eswatini, Umoja wa Falme za Kiarabu, Urusi, Canada, Uingereza, Cuba na Japan. Ziara hizi zimekuwa na mafanikio makubwa katika kuimarishe mahusiano yetu na nchi hizo. Aidha, nchi ilipata fursa mbalimbali za ushirikiano wa kimaendeleo kupitia ziara hizo;

x) Kufanikisha uenyekiti wa Tanzania katika Jumuiya ya Afrika Mashariki ambapo mwezi Machi 2016 nchi yetu iliteuliwa kwa mara ya pili mfululizo kuwa Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo. Katika kipindi cha uenyekiti wake, Tanzania ilifanikisha utekelezaji wa masuala mbalimbali ikiwemo:

- a) Kuweka mifumo bora ya matumizi ya rasilimali za Jumuiya;
- b) Kuimarishe miundombinu yenyeye sura ya Kikanda;
- c) Kuweka mazingira wezeshi ya kibashara kwa Nchi Wanachama;
- d) Kuratibu utumiaji wa Bendera ya Jumuiya ya Afrika Mashariki katika Ofisi zote za Umma nchini; na
- e) Matumizi ya Wimbo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki katika Taasisi zote za Serikali.

xi) Kuratibu Mkutano wa 18 wa Mawaziri wa Mambo ya Nje wa Afrika na Nordic (Africa - Nordic Summit) uliofanyika kwa mafanikio makubwa mwezi Novemba 2019 jijini Dar es Salaam. Ni mara ya kwanza kwa Tanzania kuwa mwenyeji

wa Mkutano huo tangu kuanzishwa kwake mwaka 2001. Tofauti na mikutano iliyopita mkutano huu ulijikita katika kuimarisha masuala ya biashara, uwekezaji, uchumi wa viwanda, mazingira, kukuza utalii pamoja na masuala ya amani na usalama;

xii) Kuratibu ujenzi wa vituo vinane vya Kutoa Huduma kwa Pamoja Mipakani (OSBPs) ambapo vituo saba vipo katika mipaka ya Tanzania na nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na kituo kimoja kipo mpakani mwa Tanzania na Zambia. Uwepo wa vituo hivyo, umerahisisha ufanyaji wa biashara katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na nchi za jirani;

xiii) Kufanikisha ujumuishwaji wa miradi ya Tanzania katika miradi ya kipaumbele ya miundombinu iliyoidhinishwa na Wakuu wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ambayo baadhi yake ni ujenzi wa Jengo la Tatula Abiria katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNIA Terminal III) uliokamilika; barabara ya Kikanda ya Simiyu/Mara Border – Musoma (km 85.5); mradi wa ujenzi, upanuzi na ukarabati wa barabara kwa kiwango cha Iami za kupunguza msongamano wa magari katika jiji la Dar es Salaam zenyet zaidi ya km 43 na ukarabati wa kiwanja cha ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro (KIA); uwanja wa ndege wa Karume; na bandari za Zanzibar ikiwemo Maruhubi;

xiv) Katika kipindi cha mwaka 2015 – 2019, Tanzania ilifanikiwa kwa kiasi kikubwa katika utekelezaji wa Itifaki ya Umoja wa Forodha na Itifaki ya Soko la Pamoja za Jumuiya ya Afrika Mashariki kama vile:

a) Kuondoa vikwazo vya biashara visivyo vya kiforodha 15 kati ya vikwazo 24 vilivyoripotiwa dhidi ya Tanzania;

b) Kutoa vyeti 32,536 vya uasili wa bidhaa kwa wafanyabiashara wa Tanzania wanaofanya biashara katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki;

- c) Kutoa vibali nya kuingia nchini 1,117,056 kwa raia wa Nchi Wanachama wa Jumuiya na wananchi wetu 851,470 walipata vibali nya kuingia katika nchi nyingine za Jumuiya;
 - d) Kufanikisha Watanzania 1,555 kupata vibali nya kufanya kazi katika nchi nyingine wanachama wa Jumuiya na Tanzania ilitoa vibali 2,309 nya kufanya kazi nchini kwa raia wengine wa Nchi Wanachama wa Jumuiya;
 - e) Kutoa vibali vipatavyo 879 kwa wanafunzi wa nchi nyingine wanachama wa Jumuiya kuingia na kusoma nchini na wanafunzi Watanzania 3,129 walipata vibali nya kusoma katika Nchi Wanachama wa Jumuiya; na
 - f) Kutoa vibali nya ukaazi 3,128 kwa raia wengine wa Nchi Wanachama wa Jumuiya na Watanzania 1,002 walipata vibali nya ukaazi katika Nchi Wanachama wa Jumuiya.
- xv) Kuendelea kuhakikisha kuwa Tanzania inanufaika ipasavyo na fursa za kibiashara zitokanazo na uanachama wetu kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki. Katika kipindi cha mwaka 2015-2018, thamani ya mauzo ya Tanzania katika Soko la Jumuiya ya Afrika Mashariki iliongezeka kutoka Dola za Marekani **350,169,250** mwaka 2015 na kufikia Dola za Marekani **448,644,006** mwaka 2018 sawa na ongezeko la asilimia 28. Thamani ya ununuza wa bidhaa kutoka Nchi Wanachama wa Jumuiya imeongezeka kutoka Dola za Marekani **227,216,173** mwaka 2015 hadi kufikia Dola za Marekani **302,728,624** mwaka 2018 sawa na ongezeko la asilimia 33.
- xvi) Kuratibu mchakato wa upatikanaji wa Kampuni za *Arab Contractors na El Sewedy Electric* za Misri kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa kuzalisha umeme wa Megawati 2,115 katika Bonde la mto Rufiji (Mwalimu Julius Nyerere Hydropower Project). Ujenzi wa mradi huo ulizinduliwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 26 Julai, 2019. Aidha, itakumbukwa kuwa mwaka 2017 wakati Tanzania ilipokuwa mwanachama wa Kamati ya Urithi wa Dunia (World Heritage Committee) ya

UNESCO, Serikali yetu ilijulisha rasmi Kamati hiyo wakati wa Mkutano wake wa 41 azma ya Serikali ya Awamu ya Tano, chini ya Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Maguli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ya kutekeleza mradi huo mkubwa;

xvii) Kuratibu upatikanaji wa mkopo wa masharti nafuu kutoka Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB) wenyе thamani ya Dola za Marekani Milioni 200 kwa ajili ya ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa Msalato jijini Dodoma na upatikanaji wa mkopo wenyе masharti nafuu wenyе thamani ya Dola za Marekani Milioni 180 kutoka Benki hiyo kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya pete katika jiji la Dodoma. Ujenzi wa barabara hiyo utasaidia kuboresha miundombinu na kupunguza msongamano wa magari katika jiji la Dodoma;

xviii) Kuratibu upatikanaji wa Kampuni ya SENER ya Korea Kusini kwa ajili ya kujenga meli mpya ya kisasa katika Ziwa Victoria yenye uwezo wa kubeba abiria 1,200 na tani 400 za mizigo; ujenzi wa Chelezo na ukarabati wa meli za MV Victoria na MV Butiama. Ujenzi wa meli mpya unatekelezwa kwa ubia kati ya kampuni ya Korea Kusini kwa kushirikiana na SUMA JKT na unatarajiwa kukamilika mwaka 2021;

xix) Kuratibu upatikanaji wa mkopo wa masharti nafuu kwa ajili ya ujenzi wa daraja jipya la Selander jijini Dar es Salaam lenye urefu wa kilomita 1.03. Mkopo huo kutoka Serikali ya Korea Kusini ni Shilingi Bilioni 556.5 wakati Serikali ya Tanzania inachangia kiasi cha Shilingi Bilioni 266 ambazo ni fedha za ndani za walipa kodi. Ujenzi wa daraja hilo, utajumuisha barabara za maungio zenyе urefu wa kilomita 5.2 na hivyo kufanya mradi mzima kuwa na kilomita 6.23, mradi utagharimu Dola za Marekani Milioni 126.26; na

xx) Kushawishi nchi marafiki kutufutia madeni, kuyapunguza au kuweka masharti nafuu ya kuyalipa. Kutokana na ziara ya Mhe. Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki nchini Iran mwezi Oktoba 2017, Serikali ya nchi hiyo iliridhia na kutangaza kusamehe riba ya deni lilitokwa mwaka 1984 ambayo ilifikia kiasi cha Dola za Marekani Milioni

150. Vile vile, mwezi Septemba 2017, Serikali ya Brazil pia ilitoa msamaha wa thamani ya Dola za Marekani Millioni 203.6 ambayo ni asilimia 86 ya deni lote tunalodaiwa na nchi hiyo. Misamaha hiyo ni wazi itaipa nafuu nchi yetu katika kulipa madeni na kuelekeza fedha hizo katika maeneo mengine ili kukuza uchumi na kupunguza umaskini.

3.0 MISINGI YA TANZANIA KATIKA MAHUSIANO YA KIMATAIFA

15. *Mheshimiwa Spika*, historia ya Tanzania imesheheni misingi na misimamo imara inayofanya iendelee kuwa mionganii mwa nchi zilizo na ushawishi mkubwa kikanda na kimataifa tangu Uhuru. Misingi ya nchi yetu kuheshimika kimataifa iliwekwa na Baba wa Taifa Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ambaye alikuwa mstari wa mbele katika kulaani ubabe, uonevu na ukandamizaji popote pale ulipotokea duniani na alipigania uhuru wa Afrika na kusisitiza mshikamano kati ya nchi zinazoendelea. Kupitia misingi hii ambayo viongozi wetu wameendelea kuienzi, Tanzania imeendelea kuheshimika sana kikanda na kimataifa.

16. *Mheshimiwa Spika*, katika kusimamia misingi hiyo, Serikali ya Awamu ya Tano imeendelea kulinda uhuru wa nchi, haki yetu ya kujiamulia mambo yetu wenyewe bila kuingiliwa, mipaka ya nchi yetu; kuimarisha ujirani mwema; na kutekeleza Sera ya Kutofungamana na Upande Wowote kama dira na msimamo wetu kwenye mahusiano na nchi nyingine za Jumuiya ya Kimataifa. Kwa muktadha huo, Tanzania imeendelea kushiriki katika kulinda amani, kudumisha umaja na mshikamano, kuhimiza maendeleo na kupinga dhuluma.

17. *Mheshimiwa Spika*, napenda kutoa wito kwa Jumuiya ya Kimataifa kuendeleza ushirikiano katika kutokomeza umaskini, kuboresha utoaji wa huduma za kijamii, kiwango cha elimu, kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi, kudumisha amani na usalama, kuleta haki na kuifanya dunia kuwa sehemu salama ya kuishi.

TATHMINI YA HALI YA DUNIA KWA MWAKA 2019/2020

18. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa fupi kuhusu hali ya dunia kama ifuatavyo:

Hali ya Uchumi Duniani

19. Mheshimiwa Spika, hadi mwanzoni mwa mwaka 2020, uchumi wa dunia ulionesha kuendelea kuimarika na kutoa matumaini ya kuimarika zaidi kwa kipindi cha miaka michache ijayo. Uimara wa uchumi katika mataifa makubwa na nchi zinazoibukia kiuchumi uliongeza upatikanaji wa mitaji, kuimarika kwa bei ya bidhaa na kukua kwa biashara ya kimataifa. Nchi za kusini mwa jangwa la Sahara, ikiwemo Tanzania, zilitarajiwu kunufaika zaidi na mwenendo huo wa uchumi wa dunia. Hata hivyo, mlipuko wa maambukizi ya ugonjwa wa homa kali ya mapafu unaosababishwa na virusi vya Corona (COVID-19) unaashiria tishio kubwa la kuporomoka kwa uchumi wa dunia.

20. Mheshimiwa Spika, ni matumaini yetu kuwa Jumuiya ya Kimataifa itaendelea kushirikiana kwa karibu ili kusaidia juhudzi za kukabiliana na janga hili. Kadhalika, ni muhimu kwa Jumuiya ya Kimataifa kusaidia nchi zinazoendelea ili kuimarisha sera za kiuchumi na fedha na kuweka mifumo madhubuti ya kukabiliana na madhara ya kiuchumi yatakayotokana na COVID-19.

21. Mheshimiwa Spika, hivi karibuni kumeibuka mlipuko wa ugonjwa wa homa kali ya mapafu unaosababishwa na virusi vya Corona (COVID-19) ulioripotiwa kwa mara ya kwanza mwezi Desemba 2019 katika mji wa Wuhan, Jimbo la Hubei nchini China na kusababisha vifo, tahiruki na athari kubwa za kiuchumi duniani. Aidha, ugonjwa huo umekuwa ukienye kwa kasi kubwa kutoka nchi moja hadi nyingine ambapo kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani hadi kufikia **tarehe 5 Mei 2020** takribani watu **3,525,116** kote duniani walibainika kuwa na maambukizo ya ugonjwa huo na watu takribani **243,540** walikuwa wamepoteza maisha.

22. Mheshimiwa Spika, athari za ugonjwa wa COVID-19 kwenye sekta zote za uchumi zinakadiriwa kuwa kubwa sana. Taarifa ya mwezi Aprili 2020 iliyotolewa na Shirika la Fedha Duniani (IMF) kuhusu hali ya uchumi duniani pamoja na taarifa ya Benki ya Dunia kuhusu athari za COVID-19 kwenye uchumi wa Afrika, zinaashiria kuwa kuna uwezekano mkubwa uchumi wa dunia kuporomoka kwa kiwango kibaya kinachowenza kulinganishwa na mdodoro wa uchumi wa dunia uliotokea miaka ya 1929 hadi 1933 (*Great Depression*). Tishio hili linatarajiwa kuathiri bei za bidhaa, kupunguza uzalishaji viwandani, kuathiri upatikanaji wa mitaji, ajira na kudorora kwa uwekezaji wa Kimataifa.

23. Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kuliomba Bunge lako Tukufu na wananchi kwa ujumla kuchukua tahadhari zote muhimu za kujikinga na maambukizi ya virusi vinavyosababisha ugonjwa huu kwa kuzingatia ipasavyo miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na Serikali kwa ujumla.

24. Mheshimiwa Spika, katika muktadha huu, Tanzania inaungana na Umoja wa Afrika, pamoja na viongozi mbalimbali wa nchi za Afrika kumwunga mkono Dkt. Tedros Adhanom Ghebreyesus, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Afya Duniani (WHO) kwa namna anavyoendelea kuliongoza vyema Shirika hili kwenye mapambano dhidi ya ugonjwa wa COVID-19. Tunapenda kulitia moyo Shirika hilo chini ya uongozi mahiri wa Dr. Tedros kuendelea kufanya kazi kwa weledi ili kuiokoa dunia yetu dhidi ya magonjwa mbalimbali ikiwemo COVID-19. Tanzania inalishukuru Shirika hilo kwa miongozo na misaada linayotoa kwenye mapambano dhidi ya maambukizi ya ugonjwa wa COVID-19. Kadhalika, tunawashukuru sana washirika wetu wote wa maendeleo kwa kuunga mkono jitihada za Serikali katika kupambana na ugonjwa huo hatari.

Hali ya siasa, ulinzi na usalama

25. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa fupi kuhusu hali ya Siasa, Ulinzi na Usalama wa dunia kama ifuatavyo:

Afrika

26. Mheshimiwa Spika, naomba kutumia nafasi hii kuzipongeza nchi za Algeria, Botswana, Komoro, Namibia, Msumbiji, Mauritius, Togo na Tunisia, kwa kufanya chaguzi katika hali ya amani na utulivu katika kipindi cha mwaka 2019/2020. Hali hii, inaashiria kuimarika kwa misingi ya demokrasia na utawala bora katika Bara la Afrika. Aidha, pamoja na hali ya kisiasa kuwa ya kuridhisha, tishio la ugaidi, uwepo wa vikundi vyta waasi, biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu, biashara ya dawa za kulevya na utakatishaji wa fedha haramu bado ni changamoto kwa nchi nydingi za Bara la Afrika na duniani kwa ujumla.

Algeria

27. Mheshimiwa Spika, hali ya usalama nchini Algeria imeimarika baada ya uchaguzi wa Rais uliofanyika mwezi Desemba 2019 na kumpata Rais mpya wa nchi hiyo Mheshimiwa Abdelmadjid Tebboune. Ni matumaini yetu kuwa, kuimarika kwa usalama wa nchi hiyo kutaendelea kuwa na mchango mkubwa katika kudumisha amani Barani Afrika.

Burundi

28. Mheshimiwa Spika, hali ya siasa, ulinzi na usalama nchini Burundi imeimarika hasa katika kipindi hiki cha kuelekea Uchaguzi Mkuu unaotarajiwa kufanyika mwezi Mei, 2020. Aidha, tunaupongeza uamuzi wa Mheshimiwa Pierre Nkurunziza, Rais wa Jamhuri ya Burundi kwa kutangaza kuondoka madarakani kwa amani baada ya kumaliza muda wake. Uamuzi huo wa kurithishana madaraka kwa njia ya amani ni ishara njema ya kuimarika kwa demokrasia nchini humo. Ni matumaini yetu kwamba Jumuiya ya Kimataifa itaiunga mkono Serikali mpya ya nchi hiyo ili iweze kutimiza matarajio ya Warundi katika harakati za maendeleo ya nchi hiyo na ya ukanda mzima wa Afrika Mashariki.

Cameroon

29. Mheshimiwa Spika, hali ya kisiasa nchini Cameroon ni tulivu ingawa imeendelea kukabiliwa na tofauti kati ya Majimbo yanayozungumza Kifaransa dhidi ya majimbo

yanayozungumza Kiingereza. Majimbo yanayozungumza Kiingereza kwa muda mrefu yamekuwa yakidai kujitenga kutoka Cameroon inayoongozwa na jamii inayozungumza Kifaransa na kuunda Taifa lao la Ambazonia. Sababu zinazochangia kuwepo madai hayo ni jamii hiyo inayozungumza Kiingereza kutoridhishwa na muundo wa utawala, kukosekana kwa usawa wa kisiasa, kiuchumi na kijamii na kutoridhishwa na uendeshaji wa chaguzi nchini humo kama ilivyodhihirika mwezi Februari, 2020 ambapo Cameroon ilifanya uchaguzi wa Serikali za Mitaa uliosusiwa na Majimbo ya jamii inayozungumza Kiingereza chini ya Chama Kikuu cha Upinzani cha “Movement for Rebirth of Cameroon” kwamba haukuwa huru na wa haki.

30. Mheshimiwa Spika, hatua iliyochukuliwa na Serikali ni pamoja na kutoa hadhi maalum ya kiutawala kwa Majimbo hayo ya Klingereza, kuitisha mijadala ya amani ya kitaifa pamoja na kuwaachia huru wafungwa wa kisiasa akiwemo Bw. Maurice Kamto, Kiongozi Mkuu wa upinzani. Tunazisihi pande zinazohasimiana kuendelea na majadiliano ili kumaliza tofauti zao kwa njia ya amani na hatimaye kupata suluhi ya kudumu.

Jamhuri ya Afrika ya Kati

31. Mheshimiwa Spika, hali ya kisiasa nchini Jamhuri ya Afrika ya Kati inaendelea kuimarika kufuatia kusainiwa kwa Makubaliano ya Kisiasa ya Amani na Maridhiano baina ya Serikali na vikundi vyenye silaha mwezi Februari 2019 kwa lengo la kusitisha mapigano. Hivi sasa nchi hiyo inaendelea na ujenzi wa taasisi za kisiasa na utendaji ili kukabiliana na changamoto za kusuasua kufikia malengo ya makubaliano. Aidha, nchi hiyo inatarajia kufanya uchaguzi mkuu katika mwaka 2020 na 2021. Ni matumaini yetu kuwa uchaguzi huo utafanyika katika mazingira huru na ya haki.

Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo

32. Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Felix Antoine Tshisekedi Tshilombo, Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) aliunda Baraza la Mawaziri mwezi Agosti 2019 lenye

kujumuisha mawaziri kutoka chama cha upinzani cha *Common Front for Congo* (FCC) kinachoongozwa na Mheshimiwa Joseph Kabila aliyekuwa Rais wa nchi hiyo. Tangu aingie madarakani na kuunda Baraza la Mawaziri, Mheshimiwa Felix Tshisekedi ameendelea kujenga umoja wa kitaifa, kuimarisha amani na utulivu, kuhuisha taasisi za umma na kujenga mahusiano mema kwa majirani zake. Hata hivyo, hali ya usalama Mashariki mwa DRC haijatengamaa kutokana na kukabiliwa na mashambulizi kutoka kwa vikundi vya waasi vyenye silaha. Serikali ya nchi hiyo kwa kushirikiana na vikosi vya Umoja wa Mataifa inaendelea na jitihada za kuimarisha ulinzi na usalama katika eneo hilo.

33. Mheshimiwa Spika, tunatoa rai kwa Jumuiya ya Kimataifa kuendelea kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo katika juhudini za kurejesha amani jumuishi na ya kudumu nchini humo.

Kenya

34. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuimarisha uhusiano na ushirikiano wa kidugu na wa kihistoria kati ya nchi yetu na nchi ya Kenya. Uhusiano huo mzuri umewezesha nchi zetu kuendelea kushirikiana katika masuala mbalimbali kama ilivyodhihirishwa na hatua ya Mhe. Uhuru Muigai Kenyatta, Rais wa Jamhuri ya Kenya ambapo tarehe 24 alimtuma Mjumbe wake Maalum, Mhe. Monica Kathina Juma, aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Nje, kwa Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuja kukabidhi fedha kiasi cha Shilingi za Tanzania milioni 170, Shilingi za Kenya 171,000 na Dola za Marekani 77,500 zilizoibowiwa mwaka 2004 katika Benki ya NBC, Tawi la Moshi; pamoja na vipande vya dhahabu vyenye uzito wa kilo 35.267 vilivyokuwa vimetoroshwa kutoka hapa nchini mwaka 2018 na kukamatwa nchini Kenya.

35. Mheshimiwa Spika, kukabidhiwa kwa dhahabu na fedha hizo ni ishara ya uhusiano mzuri uliopo baina ya nchi hizi mbili na pia ni matokeo ya utekelezaji wa Sera yetu ya Mambo ya Nje katika kulinda maslahi ya nchi yetu.

36. Mheshimiwa Spika, tarehe 26 Novemba, 2019, Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alinituma kuwasilisha ujumbe wake maalum kwa Mhe. Uhuru Muigai Kenyatta, Rais wa Jamhuri ya Kenya. Nikiwa nchini humo, nilialikwa na Mhe. Rais Kenyatta kumwakilisha Mhe. Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kupewa fursa ya kuzungumza katika uzinduzi wa mpango wa amani na maridhiano ujulikanao kama "Building Bridges Initiatives - BBI" wenye lengo la kujenga umoja wa kitaifa kufuatia mpasuko wa kisiasa baada ya kumalizika kwa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2017. Katika hotuba yangu, niliwaomba Wakenya kumaliza tofauti zilizopo na kujenga Kenya yenye umoja na maelewano. Nitumie fursa hii, kuwatachia kila la kheri wenzetu Wakenya katika kutekeleza mpango huo.

Komoro

37. Mheshimiwa Spika, hali ya usalama nchini Komoro kwa ujumla ni ya kuridhisha licha ya kuendelea kuwepo kwa changamoto za kisiasa. Msingi wa changamoto hizo ni madai ya vyama vyaa upinzani kwamba Uchaguzi Mkuu wa Rais uliofanyika tarehe 24 Machi, 2019 haukuwa huru na wa haki. Kutokana na madai hayo, vyama hivyo vilisusia Uchaguzi wa Wabunge na Magavana uliofanyika mwezi Februari, 2020.

38. Mheshimiwa Spika, madai mengine ya wapinzani ni kwamba Katiba ya nchi hiyo, iliyofanyiwa mabadiliko mwezi Julai 2018, haitoi mgawanyo sawa wa madaraka kwa visiwa vitatu vinavyounda Muungano wa Komoro, kinyume na Makubaliano ya Ugawaji wa Madaraka (Fomboni Agreement) ya mwaka 2002 ambayo yalileta amani, maelewano na muafaka wa kitaifa nchini humo. Tunatoa rai kwa pande zinazohasimiana kumaliza tofauti zao kwa njia ya mazungumzo ili kupata suluhi ya kudumu.

Somalia

39. Mheshimiwa Spika, nchi ya Somalia inaendelea kupiga hatua katika kuimarisha usalama ikiwa ni matokeo ya Serikali ya nchi hiyo kusimamia vyema vipaumbele vilivyoainishwa

katika makubaliano ya amani na ukuaji wa uchumi. Pamoja na kupiga hatua katika utekelezaji wa makubaliano hayo, Somalia bado inaendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na uwepo wa vikundi vyta kigaidi ambavyo vinaendeleza mashambulizi yanayolenga kudhoofisha taasisi za umma, Misheni ya Afrika ya Kulinda Amani Somalia (AMISOM) na kuleta madhara kwa raia wasio na hatia. Tunatoa rai kwa Jumuiya ya Kimataifa na wapenda amani wote kushirikiana na Serikali ya Somalia katika kutatta changamoto za kiusalama zinazoikabili nchi hiyo.

Sudan

40. Mheshimiwa Spika, kufuatia kusainiwa kwa Makubaliano ya Kikatiba tarehe 17 Agosti, 2019 kati ya Baraza la Mpito la Jeshi la Sudan na Vyama vya Kiraia vya Kutetea Uhuru na Mabadiliko, hali ya amani nchini humo imeendelea kuimarika. Katika kutekeleza makubaliano hayo, Serikali ya Mpito iliundwa kuliongoza Taifa hilo kwa kipindi cha miezi 39. Pamoja na kuundwa kwa Serikali ya Mpito changamoto za kiusalama zimeendelea kujitokeza. Mathalani, mwezi Machi 2020 Mheshimiwa Abdallah Hamdok, Waziri Mkuu wa nchi hiyo alinusurika katika jaribio la kuuawa. Tanzania inaungana na Jumuiya ya Kimataifa kulaani vikali jaribio hilo ovu.

Sudan Kusini

41. Mheshimiwa Spika, kufuatia makubaliano yaliyofanyika mwezi Februari 2020 ya kuunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa nchini Sudan Kusini, hali ya kisiasa na usalama imeanza kuimarika. Makubaliano hayo yanalenga kujenga umoja wa kitaifa baina ya jamii ndani ya nchi hiyo. Tunazisihi pande zote zinazohusika kuendelea kuheshimu na kutekeleza makubaliano yaliyofikiwa.

Libya

42. Mheshimiwa Spika, hali ya usalama nchini Libya bado si nzuri kutohana na kuendelea kwa mapigano kati ya vikosi vya Serikali ya Mpito inayotambulika na Jumuiya ya Kimataifa

na vikundi vinavyoipinga Serikali. Tanzania inasikitishwa na hali hiyo na inaungana na Jumuiya ya Kimataifa kuzitaka pande hizo mbili kuheshimu Makubaliano ya kusitisha mapigano pamoja na Azimio la Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa juu ya vikwazo vya silaha dhidi ya Libya. Hivyo, Tanzania inatoa wito kwa pande zinazohusika na mgogoro huo kurejea katika meza ya mazungumzo ili kutafuta suluhisho la kudumu kwa njia ya amani. Aidha, tunatoa rai kwa Jumuiya ya Kimataifa na wadau wa amani nchini Libya kushirikiana katika kumaliza changamoto za kiusalama zinazoikabili nchi hiyo.

Msumbiji

43. Mheshimiwa Spika, hali ya kisiasa nchini Msumbiji inaendelea kuimarika kufuatia kusainiwa kwa makubaliano ya amani baina ya Serikali na chama cha upinzani cha RENAMO mwezi Agosti, 2019. Makubaliano hayo yalifatiwa na uchaguzi uliofanyika mwezi Oktoba 2019 ambapo chama cha RENAMO kilishiriki. Hata hivyo, Msumbiji imeendelea kukabiliwa na matukio ya mashambulizi ya kigaidi hususan katika Jimbo la Cabo Delgado liliopo kaskazini mwa nchi hiyo linalopakana na nchi yetu. Tanzania na Msumbiji zinaendelea kushirikiana ili kuimarisha ulinzi na usalama katika eneo la mpaka.

Guinea Bissau

44. Mheshimiwa Spika, hali ya usalama inaendelea kuimarika nchini Guinea Bissau baada ya uchaguzi mkuu uliofanyika mwezi Desemba 2019 kuwa wa amani, huru na haki. Katika uchaguzi huo, chama cha MADEM – G15 kilichokuwa cha upinzani kilitangazwa kuwa mshindi ingawa matokeo ya uchaguzi huo yalipingwa na chama kilichokuwa madarakani cha PAIGC, hali iliyosababisha vurugu na kushindwa kubadilishana madaraka kwa njia ya amani. Ni matarajio yetu kuwa, pande zinazokinzana nchini humo zitarudi kwenye meza ya mazungumzo kwa lengo la kutafuta suluhu ya kudumu kwa manufaa ya Taifa hilo.

Ulaya na Amerika

45. Mheshimiwa Spika, kwa ujumla hali ya siasa, ulinzi na usalama katika nchi za Ulaya na Amerika imeendelea kuimarika. Pamoja na kuimarika kwa hali hiyo, eneo hilo limeendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali kama ifuatavyo:

Venezuela

46. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2019/2020, nchi ya Venezuela imeendelea kukabiliwa na mgogoro wa kisiasa unaotokana na maandamano ya kupinga Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Nicolas Maduro, Rais wa Venezuela. Mgogoro huo, uliibuka baada ya kambi ya upinzani kupinga matokeo ya uchaguzi wa mwaka 2018 yaliyomweka madarakani Rais Nicolas Maduro kwa madai kuwa hayakuwa halali.

47. Mheshimiwa Spika, kudumu kwa muda mrefu kwa mgogoro huo kumeleta athari kubwa za kiuchumi na kijamii katika nchi hiyo. Tunatoa rai kwa pande zinazohasimiana kukaa kwenye meza ya mazungumzo kwa ajili ya kupata suluhisho la kudumu kwa maendeleo na ustawi wa watu wa Venezuela.

Umoja wa Ulaya

48. Mheshimiwa Spika, Bara la Ulaya limeshuhudia matukio machache yenye viashiria vya ugaidi ikilinganishwa na miaka ya nyuma. Baadhi ya matukio ya kigaidi yaliyopotiwa katika kipindi hiki ni pamoja na yale yaliyotokea katika miji ya Milan, Italia na Hanau, Ujeruman. Aidha, kufuatia hatua ya Uturuki kufungua mipaka yake, eneo la Umoja wa Ulaya linakabiliwa na ongezeko kubwa la wakimbizi kutoka Syria na nchi nyingine za Mashariki ya Kati na zinazokabiliwa na migogoro ya kivita na wahamiaji kutoka bara la Afrika. Hali hii, imeleta tahiruki miongoni mwa viongozi na wananchi katika Umoja huo.

Uingereza

49. *Mheshimiwa Spika*, mwezi Januari 2020 nchi ya Uingereza ilijitoa katika Umoja wa Ulaya (Brexit). Mchakato wa kujitoa ulanza tangu mwezi Juni 2016, baada ya wananchi wa nchi hiyo kupiga kura ya kujiondoa kwenye Umoja huo. Kufuatia matokeo ya Uchaguzi Mkuu uliofanyika mwezi Desemba 2019 na kukipa ushindi Chama cha Wahafidhina (Conservatives), suala ambalo lilitoa mamlaka zaidi kwenye mchakato wa Brexit, kwa sasa, nchi hiyo inaendelea kujadiliana na Umoja wa Ulaya ili kufikia makubaliano ya ushirikiano baada ya kujiondoa rasmi katika Umoja huo ifikapo mwezi Desemba 2020.

50. *Mheshimiwa Spika*, kwa kuwa Uingereza na Umoja wa Ulaya wote ni mionganoni mwa washirika muhimu wa Tanzania katika maendeleo, biashara na uwekezaji, Wizara inaendelea kufuatilia kwa karibu majadiliano hayo.

Ubelgiji

51. *Mheshimiwa Spika*, mwezi Machi 2020, Ubelgiji ilifanikiwa kuunda Serikali ya Shirikisho kufuatia uchaguzi uliofanyika mwezi Mei 2019. Serikali hiyo inayoundwa na mseto wa vyama vyta wachache (Reformist Movement (MR), Christian Democratic and Flemish (CD&V), Open Flemish Liberals and Democrats (Open VLD) inaongozwa na Mhe. Sophie Wilméts ambaye anakuwa mwanamke wa kwanza kuwa Waziri Mkuu wa nchi hiyo. Tofauti na chaguzi zingine zilizopita, katika uchaguzi huo, vyama vyta mrengo wa kushoto vimepata uungwaji mkono zaidi, hali iliyosababisha kuwepo na ugumu zaidi katika kufikia makubaliano ya kuunda Serikali ya shirkisho kutokana na kuwepo na tofauti kubwa za kimtzamo na kitiakadi. Huu ni mwendelezo wa vuguvugu la vyama vyenye misimamo mikali kuendelea kuungwa mkono katika chaguzi zilizofanyika katika nchi mbalimbali za Ulaya katika kipindi cha miaka ya hivi karibuni.

Ufaransa

52. *Mheshimiwa Spika*, mwaka 2019, Ufaransa ilishuhudia maandamano makubwa yajulikanayo kama *yellow vests*

kupinga uamuzi wa kufanya mabadiliko/mageuzi katika Mfuko wa Hazina wa Pensheni ya Uzeeni kwa wafanyakazi, kuongezeka kwa bei ya dizeli, kupanda kwa gharama za maisha na mabadiliko ya kodi yasiyokuwa na uwiano. Mageuzi hayo ni mojawapo kati ya mambo ambayo Mhe. Emmanuel Macron, Rais wa Jamhuri ya Ufaransa aliahidi kutekeleza katika kipindi cha uongozi wake. Kwa wafanyakazi wengi, mabadiliko haya yameonekana kuwa ya kinyanyasaji na yasiyo na usawa kwa kuwa yatawachelewesha kustaa fu kinyume na umri uliowekwa kisheria wa miaka 62 au malipo yao ya izeeni kupunguzwa.

53. *Mheshimiwa Spika*, maandamano hayo yalipelekea shughuli nydingi nchini humo kusimama ikiwemo huduma za kijamii, usafiri wa umma ambapo asilimia 90 ya safari za treni za mwendokasi na zile za kawaida zilifutwa. Vilevile, kwa upande wa usafiri wa anga maandamano hayo yalipelekea kampuni nydingi za ndege za nchini humo kufuta asilimia 30 ya safari zake za Ndani na zile za kimataifa.

54. *Mheshimiwa Spika*, kwa sasa maandamano nchini Ufaransa yametulia na mpango wa kubadilisha Mfuko wa Hazina wa Pensheni ya Uzeeni kwa wafanyakazi umepelekwa Bungeni kama Muswada kwa ajili ya kufanyiwa mapitio na baadaye kuitishwa na Wabunge ili kuanza utekelezaji wake.

Asia na Australasia China

55. *Mheshimiwa Spika*, dunia ilishuhudia machafuko na ghasia katika eneo la Hong Kong yaliyoanza mwezi Juni 2019 na kudumu takriban kwa miezi sita ambapo chanzo chake kilikuwa kulalamikiwa kwa muswada wa sheria ya kutaka wahalifu wa kisiwa cha Hong Kong wapelekwe kushtakiwa upande wa China Bara. Hata hivyo, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali Kuu ya China illfanikiwa kusitisha machafuko hayo kwa njia ya mazungumzo baina ya Serikali Kuu ya China na Serikali ya Eneo Maalum la Kiutawala la Hong Kong ambapo viongozi wa pande zote mbili walikubaliana Kuendelea kuitambua Sera ya China Moja, Mifumo Miwili (One China, Two Systems).

56. Mheshimiwa Spika, hatua nyingine iliyochukuliwa ni kwa Serikali Kuu ya China kumteua kada wake wa ngazi za juu wa Chama cha Kikomunisti cha China (CPC) kuwa Mkuu wa Ofisi ya Uhusiano kati ya Serikali Kuu ya China na Serikali ya Eneo Maalum la Kiutawala la Hong Kong. Ni dhahiri kuwa uteuzi huo utasaidia kuimarisha uhusiano mzuri uliopo sambamba na kuchochea maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Jamhuri ya Korea

57. Mheshimiwa Spika, Jamhuri ya Korea ilifanya Uchaguzi Mkuu wa Wabunge tarehe 19 Aprili 2020. Kwa mujibu wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi ya Korea, Chama tawala cha Korea, *Democratic Party of Korea* kilishinda uchaguzi huo kwa kishindo kwa kupata viti 180 sawa na asilimia 60 ya viti vyote 300 vilivyo kuwa vinashindaniwa. Ushindi huo ni mkubwa kwa Chama tawala tangu kuanzishwa kwa mfumo wa demokrasia huru katika uchaguzi wa mwaka 1987 na imedhihirisha ukomavu wa demokrasia nchini humo.

58. Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kwamba, Jamhuri ya Korea ilifanya uchaguzi huo katika kipindi kigumu ambacho dunia ikiwa inaandamwa na janga la homa kali ya mapafu inayosababishwa na Virusi vya Corona (Covid- 19). Kwa muktadha huo, Serikali ya Tanzania inaipongeza Jamhuri ya Korea kwa kufanikisha Uchaguzi Mkuu pamoja na changamoto ya uwepo wa ugonjwa huo.

Japan na Jamhuri ya Korea

59. Mheshimiwa Spika, mgogoro wa kisiasa kati ya Japan na Jamhuri ya Korea bado umeendelea kuwa changamoto. Hali hii imetokana na Japan kuiondoa Korea katika nchi za kipaumbele kwenye masuala ya kibashara hususan ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA). Hatua hii imefikiwa na Japan baada ya mwaka 2019 Korea kuibua tena madai ya kulipwa fidia kutokana na vitendo vinavyodaiwa kuwa vya unyanyasaji ambavyo wananchi wake walipata wakati nchi hiyo ikitawaliwa na Japan.

60. *Mheshimiwa Spika*, athari ya mgogoro huo siyo tu kwa nchi hizo mbili bali pia kwa nchi mbalimbali duniani ikiwemo Tanzania kutokana na ukweli kwamba nchi hizo ni miongoni mwa wazalishaji na wauzaji wakubwa wa bidhaa za viwandani zikiwemo za TEHAMA ambazo Tanzania ni mnufaika. Aidha, Tanzania inaunga mkono juhudi zinazochukuliwa na viongozi wa mataifa hayo katika kutatua mgogoro huo kwa njia ya mazungumzo ya kidiplomasia.

Mashariki ya Kati

61. *Mheshimiwa Spika*, baadhi ya nchi za Mashariki ya Kati zimeendelea kukabiliwa na machafuko ya kisiasa na vita vyatweri kwa wenyewe yanayotishia hali ya usalama katika eneo lote la ukanda huo na duniani kwa ujumla. Nchi za Syria, Yemen na Iraq ndizo zilizoathiriwa zaidi na machafuko hayo. Hali hiyo, imesababisha silaha kuzagaa kiholela, kuwepo kwa vikundi vyatweri kigaidi, uharamia na uhalifu mwengine. Aidha, machafuko hayo yamesababisha kuongezeka kwa idadi ya wakimbizi katika mataifa mbalimbali duniani kutoka nchi hizo. Katika kipindi hiki, kumetokea maandamano katika nchi za Iraq na Lebanon, kutokana na wananchi kudai kuwepo kwa hali mbaya ya kiuchumi. Maandamano hayo, yamesababisha kuijuzulu kwa Mheshimiwa Saad Hariri, Waziri Mkuu wa Lebanon na Mheshimiwa Adel Abdul Mahdi, Waziri Mkuu wa Iraq.

62. *Mheshimiwa Spika*, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeendelea kuimarisha ushirikiano na nchi za Mashariki ya Kati, ambalo ni eneo la kimkakati katika utekelezaji wa diplomasia ya uchumi. Pamoja na changamoto za kisiasa na kiusalama zilizopo katika eneo hilo zipo fursa nyingi za kiuchumi ambazo tunanufaika nazo. Mathalan, kuititia balozi zetu katika miji ya Doha, Tel Aviv, Muscat, Riyadh, Kuwait na Abu Dhabi tumeendelea kuhakikisha Taifa linanufaika na fursa za uwekezaji na biashara zinazotokana na kuimarika kwa uchumi wa eneo hilo hususan nchi za ghuba.

63. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi hiki ambacho uchumi wa dunia unatabiriwa kudorora, ni ukweli usiopingika kuwa

nchi za Mashariki ya Kati zenyе uchumi uliojengwa kwa mipango thabiti katika sekta ya nishati ya mafuta na gesi asilia zitaendelea kuwa mshirika muhimu na kimkakati kwa Tanzania.

64. Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kuwa Tanzania inaendelea kutumia fursa zinazotokana na ushirikiano na nchi za ukanda huo, Wizara itaendelea kuimarisha mawasiliano yatakayowezesha upatikanaji wa masoko ya bidhaa zinazozalishwa nchini, kuhamasisha utalii na kuvutia uwekezaji nchini.

65. Mheshimiwa Spika, aidha, tutaendelea kuimarisha ushirikiano na mifuko ya fedha pamoja na taasisi za misaada ikiwemo Mfuko wa Maendeleo wa Kuwait (*Kuwait Fund*), Mfuko wa Maendeleo wa Saudi Arabia (*Saud Fund*), Mfuko wa Maendeleo wa Abu Dhabi (*Abu Dhabi Fund*), Mfuko wa Maendeleo wa Khalifa (*Khalifa Fund*), Benki ya Nchi za Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika (*BADEA*) pamoja na Mfuko wa Maendeleo wa Nchi zinazozalisha Mafuta (*OFID*) kwa ajili ya kupata mikopo ya masharti nafuu na misaada ya kuboresha huduma za jamii nchini.

66. Mheshimiwa Spika, vile vile, Wizara imekuwa ikifuatilia kwa karibu na kuchambua hali ya siasa na usalama katika nchi mbalimbali za Mashariki ya Kati na kutoa ushauri kuhusu namna ya kuboresha mahusiano na nchi hizo utakaosaldia kuleta amani ya kudumu kwa maslahi ya kiuchumi kwa Taifa katika eneo hilo. Sehemu ya juhudzi zinazofanyika ni pamoja na kushiriki katika mijadala na kuunga mkono maazimio mbalimbali ya jumuiya ya kimataifa yanayolenga kumaliza migogoro kwa njia za kidiplomasia katika nchi za eneo hilo. Mpango wa Amani wa Israel na Palestina

67. Mheshimiwa Spika, mwezi Januari 2020 Serikali ya Marekani ilitangaza mpango mpya wa Amani wa Mashariki ya Kati unaohusu Palestina na Israel kupata suluhisho la kuwa nchi mbili zinazokaa kwa amani. Mpango huo haujaungwa mkono na Palestina na Jumuiya ya nchi za Kiarabu.

68. Mheshimiwa Spika, naomba kutumia nafasi hii kueleza msimamo wa Tanzania katika mgogoro wa Israel na Palestina kuwa nchi yetu itaendelea kuzingatia misingi tulyoachiwa na waasisi wa Taifa letu ambayo ndiyo nguzo ya Sera yetu ya Mambo ya Nje ya kupigania haki ya kujitawala wenyewe, kuheshimu mipaka ya nchi na kuunga mkono maazimio ya Umoja wa Mataifa na Umoja wa Afrika kuhusiana na mgogoro huo. Hivyo, Tanzania itaendelea kuzishauri pande zote husika, kuheshimu makubaliano yaliyofikiwa kwa pamoja. Tanzania inaamini suluhisho la kudumu katika mgogoro huo ni la kuwa na nchi mbili ambazo zitakaa kwa pamoja ikiwa ni Israel salama na Palestina huru.

Mgogoro katika Nchi za Ghuba

69. Mheshimiwa Spika, mahusiano katika nchi za Ghuba yameendelea kuimarika. Hivi karibuni kati ya mwezi Novemba 2019 na mwezi Januari 2020 yaliyofikiwa vikwazo ikiwemo Saudi Arabia, Umoja wa Falme za Kiarabu, Bahrain, Misri na Sudan. Ni matumaini yetu kuwa mazungumzo hayo yataendelea kwa lengo la kumaliza tofauti zilizojitekeza baina ya nchi hizo.

5.0 NAFASI YA TANZANIA KIMATAIFA NA KIKANDA

70. Mheshimiwa Spika, Tanzania ikiwa Nchi Mwanachama wa Umoja wa Mataifa imeendelea kushiriki kikamilifu katika shughuli za Umoja wa Mataifa, Taasisi na Mashirika yake na pia katika mikutano, mijadala na shughuli mbalimbali za Umoja huo. Miiongoni mwa mijadala hiyo ilifanyika kwenye Kikao cha 74 cha Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa ambapo nilimwakilisha Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika kikao hicho nilitoa hotuba iliyoelezea mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Tano kwenye sekta za afya; elimu; maji; usafiri wa anga; nishati na ujenzi.

Aidha, hotuba hiyo ilieleza utekelezaji wa miradi ya kimkakati kama vile ujenzi wa reli ya kisasa; bwawa la ufuaji umeme la Mwalimu Nyerere; ufuaji wa Shirika la Ndege la Tanzania; ujenzi na ukarabati wa viwanja vya ndege; na usambazaji

wa umeme vijiji. Vilevile, nilieleza mafanikio ya Serikali katika mapambano dhidi ya rushwa, matumizi mabaya ya madaraka na kukuza demokrasia nchini.

71. Mheshimiwa Spika, katika hotuba hiyo nilieleza pia msimamo wa Tanzania katika kupinga vikwazo vya kiuchumi dhidi ya Zimbabwe pamoja na vipaumbele vyetu katika nafasi ya Uenyekiti wa SADC kwa mwaka 2019/2020. Aidha, Tanzania ilizisihi Nchi Wanachama wa Umoja wa Mataifa kushirikiana kiuchumi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo baada ya hali ya amani nchini humo kuanza kuimarika.

72. Mheshimiwa Spika, Tanzania imeendelea kutekeleza majukumu yake kimataifa kwa mujibu wa mikataba na makubaliano mbalimbali tuliyosaini na kuridhia, ikiwemo Ajenda ya Afrika ya mwaka 2063 iliyopitishwa na Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika mwaka 2015 na Ajenda ya Malengo ya Maendeleo Endelevu ya mwaka 2030 iliyopitishwa na Umoja wa Mataifa mwaka 2015. Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli imewianisha mikakati ya maendeleo iliyopo kwenye ajenda hizo na Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2016/2017 – 2020/2021.

73. Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Mpango huu, umeleta manufaa makubwa katika kujenga Tanzania ya uchumi wa viwanda na hivyo kuungeza kasi ya ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu. Naomba kulieleza Bunge lako Tukufu kuwa mwezi Julai 2019, Tanzania iliwasilisha taarifa yake ya hiari kwenye Umoja wa Mataifa kuhusu utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030 (Voluntary National Review 2019) yanayoenda sanjari na utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano.

74. Mheshimiwa Spika, Tanzania pia imeendelea kupokea na kuhifadhi wakimbizi na waomba hifadhi kutoka nchi mbalimbali duniani ikiwa ni pamoja na Burundi. Kufuatia kuimarika kwa hali ya amani nchini Burundi, Tanzania kwa kushirikiana kwa karibu na wadau wote wanaohusika ikiwemo

Serikali ya Burundi, Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi na Shirika la Kimataifa la Wahamaji, imeendelea na zoezi la kuwarejesha kwa hiari wakimbizi wa Burundi nchini mwao. Zoezi hili linatekelezwa kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu zote za kitaifa na kimataifa.

75. Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kuishukuru Jumuiya ya Kimataifa kwa kuunga mkono utekelezaji wa zoezi hili. Aidha, nitumie fursa hii kuzisihi nchi na taasisi zisizo za kiserikali kuacha mara moja hujuma na propaganda za kukwamisha zoezi hili. Tanzania inaamini wakimbizi wa Burundi walipo hapa nchini wakirejea nchini mwao watakuwa na mchango mkubwa katika ujenzi na ustawi wa Taifa lao.

76. Mheshimiwa Spika, Tanzania inaendelea kushirikiana na mataifa mengine katika kushughulikia changamoto ya mabadiliko ya tabianchi ambayo yanahatarisha maisha, ustawi na maendeleo ya nchi zetu. Aidha, nchi mbalimbali zimeendelea kukabiliana na majanga yatokanayo na mabadiliko ya tabianchi. Mathalan, katika kipindi hiki, baadhi ya nchi za SADC, zikiwemo Komoro, Malawi, Msumbiji, Madagascar na Zimbabwe zilikabiliwa na majanga ya asili ikiwemo mafuriko na ukame uliosababisha kuwepo kwa upungufu wa chakula katika nchi hizo.

77. Mheshimiwa Spika, napenda kutoa pole kwa nchi zote zilizopata majanga hayo ambayo yanatukumbusha umuhimu wa Jumuiya ya Kimataifa kushirikiana katika kuzuia athari zitokanazo na mabadiliko ya tabianchi. Natoa rai kwa mataifa yote duniani kushirikiana katika kuzuia na kukabiliana na athari zitokanazo na mabadiliko ya tabianchi ikiwa ni pamoja na kutekeleza Mikataba mbalimbali ya kimataifa, ukiwemo Mkataba wa Paris wa mwaka 2015.

78. Mheshimiwa Spika, Tanzania imeendelea kulipa umuhimu mkubwa suala la amani na usalama duniani ambalo ni mionganoni mwa tunu za Taifa letu tangu kupata uhuru. Ili kuenzi tunu hizi na kutambua umuhimu wa kulinda na kudumisha amani na usalama duniani, nchi yetu imeendelea kushirikiana na Jumuiya ya Kimataifa katika ulinzi wa amani duniani. Katika

kutekeleza hilo, hadi sasa nchi yetu imepeleka walinda amani 2,303 kwenye misheni za kulinda amani za Umoja wa Mataifa zilizopo katika nchi za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Jamhuri ya Afrika ya Kati, Lebanon, Darfur - Sudan, Sudan Kusini na Jimbo la Abyei.

79. Mheshimiwa Spika, kwa nafasi yetu ya uenyekiti wa SADC tutaendelea kushirikiana na mataifa mengine kushughulikia masuala ya amani na usalama katika Bara letu la Afrika, hususan hali ya usalama nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Lesotho. Nitumie fursa hii kuisihi Jumuiya ya Kimataifa kuendelea kuunga mkono jitahada za kudumisha amani katika nchi hizo na maeneo mengine duniani.

80. Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea kuratibu ushiriki wa Tanzania katika shughuli mbalimbali za Jumuiya ya Nchi za Afrika, Karibeani na Pasifikasi (OACPS), ikiwa ni pamoja na kushiriki katika maamuzi kupitia mikutano mbalimbali. Katika kutekeleza azma hii, nilongoza ujumbe wa Tanzania kwenye Mkutano wa Tisa wa Wakuu wa Nchi na Serikali uliofanyika mwezi Desemba 2019 jijini Nairobi, Kenya nikimwakilisha Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

81. Mheshimiwa Spika, kupitia Mkutano huo, Tanzania ilifanikiwa kujumuisha zao la korosho kwenye orodha ya mazao ya kimkakati ndani ya OACPS ambayo yatanufalka na Programu ya Mnyororo wa Thamani wa OACPS. Programu hii, iliyotengewa kiasi cha Euro milioni 140 itatoa fursa kwa wakulima kupata mikopo kwa ajili ya kuongeza uzalishaji, kuongeza thamani ya bidhaa za kilimo na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

6.0 KUJENGA NA KULINDA TASWIRA YA NCHI KIMATAIFA

82. Mheshimiwa Spika, hivi karibuni kumekuwa na tuhuma dhidi ya Tanzania kutoka kwa baadhi ya nchi, taasisi za kimataifa na taasisi zisizo za kiserikali kuhusu ukiukwaji wa haki za binadamu ikiwemo haki ya kujieleza na kutoa maoni pamoja na haki ya kujumuika na kukusanyika. Tuhuma hizo zinahusishwa na marekebisho ya baadhi ya sheria zetu

ambazo ni: Sheria ya Vyombo vya Habari ya Mwaka 2016; Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta ya Mwaka 2018; Sheria ya Vyama vya Siasa ya Mwaka 2018; Sheria ya Takwimu ya Mwaka 2018; na Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya Mwaka 2019.

83. *Mheshimiwa Spika*, naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, tuhuma hizo hazina ukweli wowote na zina nia ovu za kuibagaza nchi yetu kwa kuwa imepiga hatua kubwa katika kujiletea maendeleo kwenye nyanja mbalimbali. Tuhuma zinazotolewa hutokana na uwepo wa tofauti za kimtaalamo baina yetu na nchi au taasisi zinazotoa tuhuma hizo.

84. *Mheshimiwa Spika*, Wizara yangu imeendelea kutumia majukwaa mbalimbali ya Kimataifa ikiwemo Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa na Baraza la Umoja wa Mataifa la Haki za Binadamu kutoa ufanuzi kuhusu tuhuma hizo kwa sababu uwongo na upotoshaji hautakiwi kukaliwa kimya. Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatambua na kuheshimu, wajibu wake Kikatiba na Mikataba ya Kimataifa ya kulinda na kudumisha haki zote za binadamu ikiwemo za kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiutamaduni zote zikiwa na umuhimu ulio sawa kwa ustawi na maendeleo ya Watanzania.

85. *Mheshimiwa Spika*, katika jitihada za Serikali kuufahamisha ulmwengu namna inavyotetea na kusimamia haki za binadamu hapa nchini, mwezi Februari 2020, niliongoza ujumbe wa Tanzania kwenye Kikao cha 43 cha Baraza la Umoja wa Mataifa la Haki za Binadamu. Kwenye Kikao hicho nilieleza kuhusu mafanikio ya Serikali katika kulinda na kusimamia haki za elimu, afya, upatikanaji wa maji safi na salama, umeme na maendeleo ya kiuchumi. Aidha, nilielezea mafanikio yaliyopatikana katika kuongeza uwajibikaji kwa watumishi na viongozi wa umma; kupambana na vitendo vya rushwa; vita dhidi ya biashara ya dawa za kulevy; kuongezeka kwa kiwango cha ukusanyaji kodi; na kupanua wigo wa vyanzo vya mapato ili kuwashudumia wananchi wetu ipasavyo.

86. Mheshimiwa Spika, kufuatia ufanuzi wa mara kwa mara kuhusu tuhuma hizo kwenye Baraza la Umoja wa Mataifa la Haki za Binadamu, Jumuiya ya Kimataifa imeanza kutambua mafanikio makubwa ya Serikali ya Awamu ya Tano katika kulinda na kusimamia haki za binadamu. Kwa mfano, kwenye Kikao cha 43, cha Baraza la Umoja wa Mataifa la Haki za Binadamu, Bi. Michelle Bachelet, Kamishna wa Haki za Binadamu wa Umoja wa Mataifa, aliipongeza Serikali ya Tanzania katika mapambano dhidi ya rushwa, kupunguza umaskini, kuimarisha miundombinu na kuongeza uwajibikaji kwa watumishi wa umma. Vilevile, Tanzania ilitajwa kwenye taarifa ya Mpango wa *Africa Landscape Restoration Initiative* kuwa ni mionganoni mwa nchi chache duniani zinazotambua haki ya maji na mazingira safi kwa wananchi wake.

87. Mheshimiwa Spika, ninayo furaha kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, kutopteka na mikakati mbalimbali iliyowekwa na Serikali ya Awamu ya Tano katika kulinda haki za watu wenye ulemavu wa ngozi, sasa Tanzania inatambulika kimataifa katika kulinda na kuboresha maisha ya watu wenye ulemavu wa ngozi. Hatua hii, imedhihirika baada ya Tanzania kupongezwa katika taarifa ya Umoja wa Mataifa inayohusu haki za watu wenye ulemavu wa ngozi iliyowasilishwa mbele ya Baraza la Umoja wa Mataifa la Haki za Binadamu mwezi Februari 2020.

88. Mheshimiwa Spika, Tanzania inatambua umuhimu wa uhuru wa vyombo vyaya habari na kuheshimu mchango wa vyombo hivyo katika kuchagiza maendeleo. Kwa umuhimu huo, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa kwa takwimu zilizopo, nchi yetu ina jumla ya vituo vyaya radio 152 ambapo vituo vitatu tu ndivyo vinavyomilikiwa na Serikali. Aidha, vituo vyaya televisheni vipo 34 na ni vituo viwili tu ndivyo vinamilikiwa na Serikali. Vilevile, kwa upande wa magazeti Serikali imetoa jumla ya leseni 172 ambapo asilimia 90 ya leseni hizo zimetolewa kwa sekta binafsi. Kwa kuzingatia takwimu hizi, ni wazi kuwa Tanzania imepiga hatua kubwa katika suala la uhuru wa vyombo vyaya habari.

89. Mheshimiwa Spika, mwezi Oktoba 2020 Tanzania inatarajia kufanya Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge, Wawakilishi na Madiwani ambapo Watanzania wenyе sifa watapata haki yao ya msingi ya Kikatiba ya kuchagua na kuchaguliwa. Hii ni moja ya nguzo kuu ya demokrasia tuliojiwekea tangu tulipoingia kwenye mfumo wa vyama vingi.

90. Mheshimiwa Spika, kupitia Bunge lako Tukufu, naomba niithibitishie Jumuiya ya Kimataifa kuwa Serikali imejipanga kuhakikisha kuwa Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 unafanyika katika mazingira ya uwazi, amani, uhuru na haki. Kama ilivyo kawaida yetu, wakati ukifika, tutazialika nchi na taasisi mbalimbali za Kimataifa kuja kuangalia uchaguzi wetu ili kujiona jinsi nchi yetu ilivyokomaa kidemokrasia na kuwa ni mfano wa kuigwa Barani Afrika na duniani kwa ujumla. Kwa kuwa Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Uongozi Mahiri wa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli umefanya mambo makubwa, mazuri na ya kihistoria kwa nchi na kwa Watanzania, ni dhahiri kuwa uchaguzi huu utakuwa ni wa kihistoria.

7.0 WATANZANIA KWENYE NAFASI ZA KIMATAIFA

91. Mheshimiwa Spika, kama ilivyo ada, Watanzania wameendelea kuheshimika na kuaminika kwenye duru za kimataifa. Kwenye ngwe hii ya kwanza ya Serikali ya Awamu ya Tano tumeshuhudia Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Raіs wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akiteuliwa kuwa mmoja wa wajumbe wa Jopo la Ngazi za Juu la kumshauri Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa kuhusu masuala ya Uwezeshaji wa Wanawake Kiuchumi; na Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Serikali ya Awamu ya Nne wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliteuliwa kuwa mwakilishi wa Umoja wa Afrika kwenye utatuzi wa mgogoro wa Libya.

92. Mheshimiwa Spika, kadhalika, Dkt. Stergomena Lawrence Tax alichaguliwa kuwa Katibu Mtendaji wa SADC kwa awamu ya pili mfululizo; na Dkt. Agnes Kijazi, Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania alichaguliwa kuwa

Makamu wa Tatu wa Rais wa Shirika la Hali ya Hewa Duniani. Aidha, Bw. Gabriel Rugalema ameteuliwa kuwa Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Chakula na Kilimo Duniani (FAO) katika nchi ya Sierra Leone.

93. *Mheshimiwa Spika*, wengine ni Balozi Profesa Kennedy Gaston, ambaye alichaguliwa kuwa Katibu Mkuu wa Jumuia ya Mashauriano ya Masuala ya Kisheria katika nchi za Asia na Afrika; Bw. Donatius Kamamba, alichaguliwa kuwa Mjumbe kwenye Kamati ya Urithi wa Dunia ya Shirika la Umoja wa Mataifa Linaloshughulikia Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO); Mhandisi Steven Mlote aliteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Jumuia ya Afrika Mashariki; na Mheshimiwa Jaji Sauda Mjasiri aliyeetuuliwa kuwa Jaji katika Mahakama ya Afrika Mashariki.

94. *Mheshimiwa Spika*, aidha, Mheshimiwa Stephen Masele (Mb) alichaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Bunge la Afrika; Mheshimiwa Jaji Iman Aboud alichaguliwa kuwa Jaji wa Mahakama ya Umoja wa Afrika ya Haki za Binadamu na Watu; Dkt. Nyamajeje Wegoro aliteuliwa kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) Kanda ya Afrika Mashariki; Bi. Donatha Rugarabamu, Mkurugenzi wa Kitengo cha Sheria, Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP); Balozi Ali Mchumo aliyeetuuliwa kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Kimataifa linalosimamia mianzi; Mhe. Mboni Mhita (Mb), alichaguliwa kuwa Rais wa Bunge la Vijana la Afrika; Bi. Maryam Salim Ahmed Salim aliyeetuuliwa kuwa Meneja Mkazi wa Benki ya Dunia nchini Albania; Bi. Joyce Msuya aliyeetuuliwa kuwa Naibu Mkurugenzi Mkuu wa Mpango wa Mazingira Duniani (UNEP); na Bi. Sabina Seja aliyeetuuliwa kuwa Mjumbe wa Bodi ya Ushauri ya kupambana na Rushwa ya Afrika.

95. *Mheshimiwa Spika*, hawa ni baadhi tu nilioweza kuwataja, hapana shaka kuna Watanzania wengi ambao wanashikika nafasi za juu kwenye Mashirika na Taasisi mbalimbali za kimataifa. Tunawapongeza sana wote na tunajivunia.

96. Mheshimiwa Spika, Watanzania wameendelea kuheshimika siyo tu na Mashirika na Taasisi za Kimataifa bali pia na nchi moja moja. Mathalani, mwezi Septemba 2019, Wizara iliratibu zoezi la mapokezi ya nishani ya juu ya urafiki ya Jamhuri ya Watu wa China iliyotolewa na Mheshimiwa Xi Jinping, Rais wa Jamhuri ya Watu wa China kwa Mheshimiwa Dkt. Salim Ahmed Salim, Waziri Mkuu Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwa ni ishara ya kutambua na kuenzi mchango wake katika kukuza urafiki kati ya China na Tanzania na Bara la Afrika kwa ujumla.

97. Mheshimiwa Spika, nishani hiyo hutolewa kwa watu mashuhuri waliota mchango mkubwa kwa Taifa la Watu wa China. Mheshimiwa Dkt. Salim anakuwa Mwfrika wa kwanza kupata Nishani ya Juu ya Urafiki ya Taifa la China kutokana na mchango wake alipokuwa Balozi na Mwakilishi wa Kudumu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Umoja wa Mataifa uliochangia kuiwezesha Jamhuri ya Watu wa China kuwa Mwanachama wa Kudumu wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa mwaka 1971. Aidha, Serikali ya China ilieleza kuwa Mheshimiwa Dkt. Salim alitoa mchango mkubwa katika kuimarisha uhusiano kati ya China na Tanzania wakati akishikilia nyadhifa mbalimbali za Kimataifa ikiwa ni pamoja na nafasi ya Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Umoja wa Nchi Huru za Afrika.

98. Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii kumponeza Mheshimiwa Dkt. Salim Ahmed Salim siyo tu kwa kupokea nishani hiyo bali pia kwa kuendelea kulijengea Taifa letu heshima kubwa kimataifa.

MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA KWA MWAKA 2019/2020

99. Mheshimiwa Spika, katika kuiwezesha Wizara kutekeleza majukumu yake kwa mwaka 2019/2020, Bunge lako Tukufu liliidhinisha kiasi cha **Shilingi 166,926,820,000**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 162,926,820,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi **4,000,000,000** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Katika fedha zilizotengwa kwa Matumizi ya Kawaida, **Shilingi**

152,717,723,000 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na **Shilingi 10,209,097,000** ni kwa ajili ya Mishahara.

100. Mheshimiwa Spika, hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2020 Wizara ilikuwa imepokea kutoka HAZINA kiasi cha Shilingi **133,300,900,671.84**. Kiasi hicho cha fedha ni sawa na **asilimia 79.8**. ya fedha zote za bajeti zilizoidhinishwa katika mwaka wa fedha 2019/2020. Kati ya fedha hizo, Shilingi **124,186,236,675.44** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na Shilingi **8,626,758,000.00** kwa ajili ya mishahara. Aidha, katika kipindi hicho Wizara imepokea fedha za bajeti ya miradi ya maendeleo kiasi cha Shilingi **487,905,996.40** kwa ajili ya miradi ya ukarabati wa nyumba ya makazi ya Balozi wa Tanzania Ottawa na ujenzi wa vyumba vya madarasa katika Chuo cha Diplomasia.

101. Mheshimiwa Spika, katika fedha zilizotolewa, Wizara imetumia kiasi cha Shilingi **99,324,222,786.14**. Kiasi hicho cha fedha ni sawa na **asilimia 75** ya fedha zilizopokelewa. Kati ya fedha hizo, Shilingi **91,390,079,647.28** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na Shilingi **7,596,237,142.46** kwa ajili ya mishahara. Aidha, Wizara imetumia kiasi cha Shilingi **337,905,996.40** kwa ajili ya mradi wa maendeleo wa ujenzi wa vyumba vya madarasa katika Chuo cha Diplomasia.

102. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Wizara ilipanga kukusanya **Shilingi 2,550,879,072**. Kati ya kiasi hicho **Shilingi 67,980,000.00** ni maduhuli ya Makao Makuu ya Wizara na **Shilingi 2,482,899,072** ni maduhuli kutoka Balozi za Tanzania nje ya nchi. Vyanzo vya mapato hayo ni pamoja na uhakiki wa nyaraka, pango la majengo ya Serikali nje ya nchi na mauzo ya nyaraka za zabuni.

103. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2019 hadi tarehe 30 Aprili, 2020 Wizara imekusanya jumla ya Shilingi **5,253,091,650.07** sawa na asilimia **206** ya lengo liliopangwa kwa mwaka 2019/2020. Ongezeko la maduhuli limetokana na baadhi ya balozi kuendelea kukusanya maduhuli ya viza kupitia utaratibu wa kawaida kabla ya kuanza kwa utaratibu wa kielektroniki (*e-visa*). Aidha, kuanzia mwezi Novemba 2019,

Wizara inaendelea kukusanya maduhuli ya visa kwa njia ya kielektroniki baada ya Balozi kufungiwa mtandao huo.

104. *Mheshimiwa Spika*, baada ya kutoa taarifa ya mapato na matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2019/2020, naomba sasa nitumie fursa hii kueleza kwa kifupi mapitio ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara katika kipindi hicho.

105. *Mheshimiwa Spika*, utekelezaji wa majukumu ya Wizara unaongozwa na llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya 2015 - 2020; Sera ya Mambo ya Nje ya Mwaka 2001; Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025; Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya mwaka 2020; Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17 - 2020/21); Ajenda ya Afrika ya mwaka 2063; Ajenda ya mwaka 2030 ya Malengo ya Maendeleo Endelevu; Mkakati wa Maendeleo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wa Mwaka 2017/2018 - 2021/2022; Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Itifaki zake; Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na Itifaki zake pamoja na Mikataba mingine ya Kikanda na Kimataifa; Mpango wa Maendeleo wa SADC uliofanyiwa maboresho wa mwaka 2015 – 2020; Mpango Mkakati wa Pili wa Asasi ya Ushirikiano katika Siasa, Ulinzi na Usalama ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika kwa mwaka 2016 – 2020; maoni na mapendekezo ya Waheshimiwa Wabunge wakati wa kujadili Mpango na Bajeti ya Wizara kwa kipindi cha mwaka 2019/2020; Mwongozo wa kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa kipindi cha mwaka 2019/2020 – 2021/2022 na Maagizo mbalimbali yaliyotolewa kwa nyakati tofauti kwa Wizara na Viongozi wa Kitaifa, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali.

106. *Mheshimiwa Spika*, kwa kuzingatia miongozo hiyo, kwa mwaka wa fedha 2019/2020 Wizara imetekeliza majukumu yake kama ifuatavyo:

Kubuni na Kusimamia Utekelezaji wa Sera ya Nchi ya Mambo ya Nje Ushirikiano wa Tanzania na Nchi za Afrika

Afrika Kusini

107. Mheshimiwa Spika, Wizara iliratibu ziara ya Mheshimiwa Cyril Matamela Ramaphosa, Rais wa Jamhuri ya Afrika Kusini iliyofanyika mwezi Agosti 2019. Tanzania na Afrika Kusini zilikubaliana kuimarisha ushirikiano katika masuala ya biashara na uwekezaji pamoja na kukuza matumizi ya lugha ya Kiswahili. Kufuatia makubaliano hayo, mwezi Septemba 2019 Serikali ya Afrika Kusini ilitangaza kuanza rasmi kufundisha lugha ya Kiswahili kuanzia mwaka 2020. Wizara inaendelea kuratibu suala hili kwa kushirikiana na wadau wa kisekta.

Uganda

108. Mheshimiwa Spika, kutokana na mahusiano mazuri na ya kidugu kati ya nchi yetu na Uganda, mwezi Septemba 2019, Wizara iliratibu ziara ya Mheshimiwa Yoweri Kaguta Museveni, Rais wa Jamhuri ya Uganda hapa nchini. Wakati wa ziara hiyo, Mheshimiwa Rais Museveni na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania walizindua Jengo la Taasisi ya Mwalimu Nyerere lililopo jijini Dar es Salaam. Viongozi hao pia, walishiriki katika Kongamano la Biashara kati ya nchi hizi mbili lililofanyika kwa lengo la kutangaza fursa za biashara na uwekezaji. Fursa hizo, ni pamoja na huduma za uchukuzi zinazotolewa na Shirika la Ndege la Tanzania, Shirika la Reli Tanzania, Kampuni ya Huduma za Meli Tanzania na Mamlaka ya Bandari Tanzania.

109. Mheshimiwa Spika, vilevile, mwezi Agosti 2019, Wizara iliratibu ziara ya wataalam kutoka sekta ya uchukuzi kwa lengo la kutangaza na kuhamasisha matumizi ya Ushoroba wa Kati kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza kwa njia ya reli na kutoka Mwanza hadi Bandari ya Portbell, Uganda kwa njia ya maji kupitia Ziwa Victoria. Ziara hiyo ilitoa fursa kwa Mamlaka ya Bandari Tanzania, Shirika la Reli Tanzania na Kampuni ya Huduma za Meli kujitangaza kwa

wafanyabiashara wa ndani na nje ya nchi hususan Uganda kutumia ushoroba huo kusafirisha mizigo yao.

110. Mheshimiwa Spika, katika ziara hiyo, Shirika la Umoja wa Mataifa la Mpango wa Chakula Duniani (WFP) ililikubali kuendelea kutumia ushoroba huo kusafirisha chakula cha msaada kwenda kambi za wakimbizi zilizopo katika nchi za Uganda na Sudan Kusini.

Misri

111. Mheshimiwa Spika, katika kuenzi mahusiano ya kihistoria kati ya Tanzania na Misri, mwezi Julai 2019, Wizara iliratibu na kushiriki katika ziara ya Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Misri. Akiwa nchini Misri, Mheshimiwa Waziri Mkuu alifanya mazungumzo rasmi na Mheshimiwa Dkt. Mostafa Madbouly, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Kiarabu ya Misri. Mheshimiwa Waziri Mkuu alipata nafasi ya kufanya mukutano na wafanyabiashara wa Misri na Watanzania wanaoishi nchini humo. Kutokana na ziara hiyo, Tanzania na Misri zilikubaliana kuimarisha ushirikiano katika sekta za nishati; kilimo; mifugo na uvuvi; afya; biashara na uwekezaji; ulinzi na usalama; ujenzi, uchukuzi na mawasiliano.

Rwanda

112. Mheshimiwa Spika, mwezi Julai 2019, Wizara iliratibu ziara ya Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Rwanda kwa ajili ya kushiriki Maadhimisho ya Siku ya Ukombozi wa Rwanda. Ushiriki wa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwenye maadhimisho hayo ni ishara ya uhusiano mzuri uliopo kati ya Tanzania na Rwanda pamoja na desturi ya Tanzania katika kudumisha ujirani mwema.

Burundi

113. Mheshimiwa Spika, mwezi Julai 2019, Wizara iliratibu na kushiriki kwenye ziara ya Mawaziri watatu kutoka Serikali ya

Jamhuri ya Burundi iliyofanyika nchini kwa lengo la kuimarisha ushirikiano katika sekta ya uchukuzi. Ujumbe huo ukiwa nchini, ulitembelea Bandari ya Dar es Salaam; Bandari Kavu ya kisasa inayojengwa eneo la Kwala mkoani Pwani na Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa. Kufuatia ziara hiyo, mwezi Agosti 2019, Serikali za Tanzania na Burundi zilisaini Hati ya Makubaliano ya Ushirikiano katika Ujenzi wa Reli ya Kisasa ya Uvinza - Msongati - Gitega. Ziara hiyo iliihamasisha Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) kuijunga kwenye mradi huo ili ufile katika maeneo ya Uvira na Kindu nchini DRC. Maandalizi ya utekelezaji wa Mradi huo ikiwemo upembuzi yakinifu yameanza.

Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC)

114. Mheshimiwa Spika, katika kutumia fursa zilizopo katika maeneo ya kimkakati ikiwemo eneo la Mashariki mwa DRC, mwezi Septemba 2019, Wizara iliratibu na kuwezesha majadiliano kati ya maafisa waandamizi wa Benki ya CRDB PLC ya Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Majadiliano hayo, yalilenga kuiwezesha benki ya CRDB kuanzisha shughuli za kibenki hususan katika eneo la Lubumbashi, mashariki mwa nchi hiyo. Hatua ya benki hiyo kuanzisha huduma zake nchini DRC itachochea kukua kwa wigo wa biashara na uwekezaji kati ya Tanzania na DRC kwa kurahisisha miamala ya kibenki kwa wafanyabiashara.

Ushirikiano kati ya Tanzania na Nchi za Asia na Australasia

Viet Nam

115. Mheshimiwa Spika, mwezi Julai 2019, Wizara iliratibu ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Trinh Dinh Dung, Naibu Waziri Mkuu wa Viet Nam ambaye aliambatana na ujumbe wa wafanyabiashara. Katika ziara hiyo, Mheshimiwa Trinh na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania walifanya mazungumzo na kukubaliana kuimarisha uhusiano wa kidiplomasia ikiwemo Tanzania kufungua Ubalozi nchini Viet Nam na kuanzisha Tume ya Pamoja ya Kudumu ya Ushirikiano. Mafanikio

mengine yaliyopatikana wakati wa ziara hiyo ni pamoja na kampuni ya TNT ya Viet Nam kununua korosho za Tanzania kiasi cha tani 113,913.5.

116. *Mheshimiwa Spika*, kiongozi huyo pia alitembelea Zanzibar na kufanya mazungumzo na Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar ambapo walikubaliana kuimarisha ushirikiano katika sekta ya kilimo na uvuvi.

China

117. *Mheshimiwa Spika*, mwezi Julai 2019 nilifanya mazungumzo na Mheshimiwa GE Huijun, Kiongozi wa Baraza la Ushauri la Bunge la Jimbo la Zhejiang la nchini China alipofanya ziara hapa nchini. Kiongozi huyo, aliambatana na wafanyabiashara kutoka kampuni 25 na viongozi 13 wa Serikali ya Zhejiang. Katika mazungumzo hayo, Tanzania na Serikali ya jimbo hilo zilikubaliana kuendelea kukuza uhusiano mzuri uliopo kati ya Tanzania na China na kuwahimiza wafanyabiashara na wawekezaji wa nchi zetu kuongeza ushirikiano wa kiuchumi kwa manufaa ya pande zote mbili.

118. *Mheshimiwa Spika*, ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa maazimio hayo, wafanyabiashara wa Tanzania na wale wa Jimbo la Zhejiang walifanya makongamano ya biashara Jijini Dar es Salaam na Zanzibar. Kupitia makongamano hayo, kampuni za Tanzania na Zhejiang zilisaini Hati za Makubaliano ya kuanzisha ushirikiano wa kibiashara katika maeneo ya teknolojia, mawasiliano, miundombinu, afya na madini.

119. *Mheshimiwa Spika*, mwezi Julai 2019, Wizara iliratibu ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Lin Bin, Naibu Waziri wa Afya wa Jamhuri ya Watu wa China aliyeongoza ujumbe wa wataalam wa afya kutoka Kamisheni ya Afya ya nchi hiyo. Mheshimiwa Lin na ujumbe wake walifanya mazungumzo na uongozi wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na kukubaliana kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa miradi ya ushirikiano kwenye sekta ya afya kati ya Tanzania na China.

120. Mheshimiwa Spika, ujumbe huo ulipata fursa ya kutembelea baadhi ya miradi ya afya inayofadhiliwa na Serikali ya China kupitia mfuko wa fedha za misaada ikiwemo Mradi wa Kudhibiti Malaria kwa Kuua Viluwiluvi nya Mbu wanaosababisha Malaria (*China - Tanzania Cooperation on Malaria Control*). Kufuatia Mradi huo kutekelezwa kwa mafanikio katika kata tatu za Wilaya ya Rufiji, Serikali ya China imeridhia ombi la Serikali la kuendelea kutekeleza mradi huo katika kata zilizosalia.

121. Mheshimiwa Spika, ujumbe huo pia ulitembelea Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) ambapo Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi hiyo na Makamu wa Rais wa Hospitali ya Jimbo la Shandong, China walisaini Makubaliano ya Ushirikiano katika Mafunzo na Matibabu ya Moyo. Makubaliano hayo yatawezesha wataalam wa afya kutoka taasisi hiyo kupata mafunzo ya matibabu ya moyo kwa kutumia vifaa nya kisasa katika hospitali ya Shandong, China. Vilevile, chini ya Mpango wa *China - Tanzania Heart to Heart Mission*, ulifanyika uzinduzi wa awamu ya pili ya kupokea madaktari wa moyo kutoka jimbo la Shandong. Katika uzinduzi huo, Hospitali ya Shandong ilitoa msaada wa vifaa tiba na dawa wenye thamani ya Dola za Marekani 200,000 kwa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete.

122. Mheshimiwa Spika, mwezi Septemba 2019, Wizara iliratibu ziara ya wafanyabishara na wawekezaji kutoka jimbo la Shandong nchini China iliyofanyika Zanzibar. Wafanyabiashara na wawekezaji hao walifanya majadiliano na Wizara ya Biashara na Viwanda; na Wizara ya Fedha na Mipango. Katika ziara hiyo, Hati ya Makubaliano kati ya Kampuni ya Linghang Group ya China na Mamlaka ya Uwekezaji Zanzibar ilisainiwa kwa ajili ya uendelezaji wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Aman Karume na eneo la viwanda la Fumba.

123. Mheshimiwa Spika, katika kuenzi misingi iliyoasiwa na Baba wa Taifa Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere pamoja na muasisi wa Taifa la China Hayati Mao Ze Dong, Wizara iliratibu ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Guo Yezhou,

Naibu Waziri anayeshughulikia Masuala ya Mambo ya Nje kutoka Chama cha Kikomunisti cha China (CPC) mwezi Oktoba 2019. Ziara hiyo, inaendelea kuimarisha misingi imara katika ushirikiano wa kisiasa ambao unajumuisha ziara rasmi za Viongozi Wakuu wa China na Tanzania, mawasiliano ya viongozi wa Serikali, ushirikiano wa kiuchumi na kisiasa.

124. *Mheshimiwa Spika*, katika kudumisha na kuimarisha uhusiano kati ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Bunge la Jamhuri ya Watu wa China, mwezi Julai 2019 Wizara iliratibu ziara ya Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Spika wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, nchini China. Katika ziara hiyo, Bunge la China liliahidi kuendeleza ushirikiano katika masuala ya kibunge.

125. *Mheshimiwa Spika*, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania katika Maonesho ya Pili ya Kimataifa ya Bidhaa zinazotoka nje ya China (China International Importation Expo) yaliyofanyika mwezi Novemba 2019 jijini Shanghai, China. Katika Maonesho hayo, Tanzania ilikuwa miongoni mwa nchi 64 zenye banda la Taifa kati ya nchi 123 zilizoshiriki. Aidha, banda la Tanzania ilikuwa miongoni mwa mabanda sita yaliyotembelewa na Mheshimiwa Xi Jinping, Rais wa Jamhuri ya Watu wa China likiwa banda pekee la nchi za Afrika lilitotembelewa na kiongozi huyo ambaye alivutiwa zaidi na bidhaa ya korosho na madini ya Tanzanite. Vyombo vyta habari vya nchini China villionesha tukio hilo mubashara ambapo inakadiriwa lilitazamwa na watu wapatao milioni 100 ulimwenguni.

126. *Mheshimiwa Spika*, kupitia maonesho hayo, jumla ya kampuni 3,000 kutoka duniani kote zikiwemo kampuni 10 kutoka Tanzania zilishiriki kwa ajili ya kuonesha bidhaa zake kwenye soko la China. Banda la Tanzania lilitembelewa na takribani wageni 6,000 ambao walivutiwa na bidhaa za korosho, kahawa, karafuu, chai, ufuta, unga wa muhogo, mazao ya misitu, vito vilivytengenezwa kwa madini ya Tanzanite, dhahabu, *saphire*, *rubby*, *spinel*, *tsavorite* na *tourmaline* na bidhaa za ngozi. Vilevile, katika banda hilo,

vivutio vya utalii vya Tanzania vilioneshwa kupitia picha za mnato na *video*.

127. Mheshimiwa Spika, Wizara iliratibu mapokezi ya kundi la watalii 120 kutoka Hong Kong, China ambao walizuru Tanzania mwezi Julai 2019 na kutembelea Mbuga za Wanyama za Serengeti na Ngorongoro. Ujumbe wa watalii hao ulijumuisha wafanyabiashara 20 ambao walipata fursa ya kufanya mazungumzo na Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), Mamlaka ya Ukanda Maalum wa Uwekezaji (EPZA) na Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TANTRADE) kwa ajili ya kupata taarifa kuhusu fursa za uwekezaji na biashara zilizopo nchini.

Indonesia

128. Mheshimiwa Spika, mwezi Oktoba 2019, Wizara iliratibu mafunzo ya usindikaji nafaka, mazao ya mizizi, matunda na mbogamboga yaliyofanyika mkoani Mbeya kwa ufadhili wa Serikali ya Indonesia. Mafunzo hayo ni sehemu ya mpango wa nchi hiyo kuleta wakufunzi kwa ajili ya kutoa elimu katika usindikaji wa mazao ya kilimo ili kuyaongezea thamani na kupunguza upotevu baada ya mavuno. Kupitia mafunzo hayo, Watanzania 40 wameweza kujengewa uwezo wa usindikaji na uhifadhi wa vyakula mbalimbali.

129. Mheshimiwa Spika, mwezi Novemba 2019, Wizara iliratibu na kushiriki katika Kongamano la Kwanza la Viwanda katи ya Tanzania na Indonesia liliyofanyika jijini Dar es Salaam. Kongamano hilo lilienga kukuza wigo wa biashara ya moja kwa moja katи ya pande mbili pamoja na kufungua fursa za uwekezaji katи ya Tanzania na Indonesia. Katika kongamano hilo, wawekezaji 21 kutoka kampuni 10 za Indonesia walioshiriki walifanya mazungumzo na Taasisi za Umma na binafsi za Tanzania.

130. Mheshimiwa Spika, mionganoni mwa mafanikio yaliyotokana na kongamano hilo ni pamoja na Kampuni ya Indesso na Kampuni ya *CV Ocean Fresh* za Indonesia kusaini Makubaliano ya Ushirikiano wa Kibiashara na Shirika la

Biahsara la Taifa – Zanzibar katika kuanzisha viwanda viwili vya kuzalisha mafuta yanayotokana na majani ya mimea pamoja na kuchakata zao la mwani. Tayari kiwanda cha kuzalisha mafuta kimeshaanza uzalishaji tangu mwezi Februari 2020.

131. *Mheshimiwa Spika*, vilevile, mwezi Agosti 2019, Wizara iliratibu na kushiriki katika Tamasha la Miundombinu kati ya Indonesia na Afrika liliofanyika kisiwa cha Bali nchini Indonesia. Wakati wa Tamasha hilo, Hati ya Makubaliano ya Ujenzi wa Bandari ya mafuta na gesi Mangapwani na Bandari ya Mpigaduri Unguja ilisainiwa kati ya Wizara ya Fedha na Mipango Zanzibar na Kampuni ya PT. WIKA pamoja na Benki ya EXIM ya nchini Indonesia. Makubaliano hayo yataiwezesha Zanzibar kupata mkopo wa Dola za Marekani milioni 190 kwa ajili ya ujenzi wa bandari hizo.

132. *Mheshimiwa Spika*, Wizara pia iliratibu ziara ya Mheshimiwa Luhut Binsar Pandjait, Waziri wa Masuala ya Bahari na Uwekezaji wa Indonesia, mwezi Desemba 2019. Lengo la ziara hiyo lilikuwa kukuza na kuimarishe juhudzi za uwekezaji kati ya Tanzania na Indonesia. Kiongozi huyo alifanya mazungumzo na Mheshimiwa Angella Kairuki (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Uwekezaji na Mheshimiwa Stanslaus Nyongo (Mb), Naibu Waziri wa Madini.

133. *Mheshimiwa Spika*, wakati wa ziara hiyo, hati mbili za makubaliano kati ya Taasisi za Tanzania na Indonesia zilisainiwa. Makubaliano hayo ni kati ya SUMA JKT na Kampuni ya PT. WIKA ya Indonesia kuhusu kuanzisha kampuni ya ubia itakayoiwezesha SUMA JKT kutekeleza miradi mikubwa ya miundombinu kuititia uwezo wa kifedha, utaalamu na uzoefu wa kampuni hiyo. Aidha, Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) na kampuni ya TIMAH ya Indonesia zilisaini Hati ya makubaliano yenye lengo la kuanzisha kampuni ya ubia ambayo itatafiti, kuchimba na kuchakata madini.

Jamhuri ya Korea

134. Mheshimiwa Spika, mwezi Agosti 2019, Wizara iliratibu kusainiwa kwa Hati ya Makubaliano kwenye sekta ya kilimo kati ya Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi Zanzibar na Kampuni ya Kolon ya Jamhuri ya Korea ambayo inatekeleza mradi wa miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji. Mradi huo unafadhiliwa kupitia mkopo wenyewe thamani ya Dola za Marekani milioni 50 kutoka Jamhuri ya Korea.

135. Mheshimiwa Spika, mwezi Desemba 2019, Wizara iliratibu na kushiriki kwenye mkutano wa wadau wa kujadili ujenzi wa kijiji cha Tanzania ndani ya bustani ya Suncheon katika Jamhuri ya Korea uliofanyika jijini Dodoma. Mkutano huo uliandaa mpango kazi utakaofanikisha uanzishwaji wa kijiji cha Tanzania katika bustani hiyo ambayo itaiwezesha nchi yetu kutangaza vivutio vya utalii pamoja na utamaduni wetu kwa wageni takribani milioni 10 watakaotembelea bustani hiyo kila mwaka. Kupewa eneo ndani ya Bustani ya Taifa la Jamhuri ya Korea ni heshima kubwa kwa Taifa letu.

Ushirikiano wa Tanzania na Nchi za Mashariki ya Kati

Kuwait

136. Mheshimiwa Spika, mwezi Julai 2019 Wizara iliratibu ziara ya Mheshimiwa Balozi Hamad Al-Mashaam, Msaidizi wa Mheshimiwa Sheikh Sabah Al-Khaled Al-Sabah, ambaye pia ni Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Mambo ya Nje wa Kuwait iliofanyika nchini. Kiongozi huyo alifanya mazungumzo na Mheshimiwa Profesa Palamagamba J. A. M. Kabudi (Mb.), Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kuhusu masuala mbalimbali ya ushirikiano kati ya Tanzania na Kuwait. Miongoni mwa masuala yaliyojadiliwa ni pamoja na umuhimu wa kuharakisha uwekaji saini mikataba ya kutokutoza kodi mara mbili katika uwekezaji na ushirikiano katika sekta ya mafuta na gesi. Viongozi hao walikubaliana pia kuanzisha Tume ya Pamoja ya Kudumu ya Ushirikiano kati ya nchi hizi mbili kwa lengo la kuimarisha uhusiano wa kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni.

Umoja wa Falme za Kiarabu

137. Mheshimiwa Spika, mwezi Septemba 2019 Wizara iliratibu ziara ya Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na MwenyeKITI wa Baraza la Mapinduzi iliyoFanyika katika Umoja wa Falme za Kiarabu. Katika ziara hiyo, Rais Shein alifanya mazungumzo na Sheikh Saud Bin AlQasimi, Mtawala wa Ras Al-Khaimah kwa niaba ya Serikali ya Umoja wa Falme za Kiarabu na alikubali kutoa msaada wa fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Fumba – Uwanja wa Ndege; ujenzi wa Hospitali Kuu ya Rufaa na ya kufundishia ya Binguni; ukarabati wa majengo ya Mji Mkongwe pamoja na ujenzi wa majengo ya Kitivo cha Historia na Mambo ya Kale katika Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar. Aidha, katika ziara hiyo viongozi hao walisaini Hati za Makubaliano kuhusu:

- (i) Msaada wa fedha wa kiasi cha Dola za Marekani milioni 10 kutoka Mfuko wa Maendeleo ya Biashara wa Khalifa kwa ajili ya kusaidia wajasiriMali wadogo na wa katи Zanzibar; na
- (ii) Msaada wa fedha kiasi cha Dola za Marekani milioni 10 kutoka Serikali ya Umoja wa Falme za Kiarabu kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa Hospitali ya Wete iliypopo Mkoa wa Kaskazini Pemba.

138. Mheshimiwa Spika, mwezi Machi 2020, Wizara iliratibu na kushiriki katika makabidhiano ya Kituo cha Afya Paje Zanzibar kilichoJengwa kwa msaada wa Serikali ya Umoja wa Falme ya Kiarabu (UAE). Aidha, pamoja na kituo hicho, nchi hiyo ilioa msaada wa gari moja la kubebbea wagonjwa na vifaa vya shule, vyote vikiwa na thamani ya Shilingi bilioni 1.38.

Qatar

139. Mheshimiwa Spika, mwezi Septemba 2019, Wizara iliratibu na kushiriki ziara ya Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Madini kutoka Taifa la Qatar. Madhumuni ya ziara hiyo yalikuwa ni kuangalia fursa za kununua madini ya dhahabu pamoja na

kuwekeza katika sekta ya madini, hususan uongezaji thamani dhahabu inayozalishwa nchini. Kampuni hiyo ilipatiwa taarifa muhimu zinazolezea taratibu za upatikanaji wa leseni na kuanzisha kampuni, taarifa za masoko ya dhahabu, sheria zinazosimamia biashara ya madini, sheria za kodi na sheria ya uwekezaji. Wizara inaendelea kuwasiliana na kampuni hiyo ili kufanikisha uwekezaji unaokusudiwa.

Israel

140. Mheshimiwa Spika, mwezi Novemba 2019, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania kwenye Kongamano la Nane la Maji na Mazingira liliofanyika jijini Tel Aviv nchini Israel. Kongamano hilo lilifanyika sambamba na Maonesho ya Teknolojia mbalimbali za maji safi na maji taka. Ujumbe wa Tanzania ulipata fursa ya kufanya mazungumzo na viongozi wa Wizara na Mamlaka za Maji nchini Israel. Katika mazungumzo hayo, Serikali ya Israel iliahidi kutoa nafasi za mafunzo kwa ajili ya wataalam wa Tanzania kwenda Israel pamoja na kuleta wakufunzi hapa nchini.

141. Mheshimiwa Spika, kutokana na mahusiano mazuri yaliyopo kati ya nchi yetu na Israel, Wizara iliratibu upatikanaji wa nafasi 100 kwa ajili ya vijana wa Kitanzania kupata mafunzo ya kilimo cha kisasa nchini Israel kwa ufadhili wa nchi hiyo. Mafunzo hayo yalianza rasmi mwezi Septemba 2019 na yanatarajiwa kumalizika mwezi Agosti 2020. Ni matarajio yetu kuwa wanafunzi hao watatumia ujuzi, utaalam na uzoefu watakaoupara nchini humo kuanzisha shughuli mbalimbali za kilimo watakaporejea nchini. Vilevile, mwezi Oktoba na Desemba 2019, Wizara iliratibu ujio wa watalii 2,000 kutoka nchini Israel. Watalii hao walitembelea vivutio mbalimbali vyatatalii Tanzania Bara na Zanzibar.

Oman

142. Mheshimiwa Spika, mwezi Januari 2020, niliwasilisha ujumbe maalum wa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Muadham Sultan Haitham Bin Tariq Bin Taimur Al Said, Mfalme

mpya wa Taifa la Oman, kufuatia kifo cha Kiongozi wa Taifa hilo Muadham Sultan Qaboos Bin Said kilichotokea tarehe 10 Januari 2020. Nilipokuwa nchini Oman, nilipata fursa ya kufanya mazungumzo na Mheshimiwa Yusuf Bin Alawi Bin Abdullah, Waziri wa Mambo ya Nje wa Oman ambaye alimshukuru Mheshimiwa Rais na Watanzania kwa ujumla kwa kumtumia Sultan Haitham salamu za pole kwa kifo cha kiongozi wao na salamu za pongezi kwa kuteuliwa kwake. Mheshimiwa Alawi aliahidi kuwa Serikali ya Oman chini ya utawala mpya itaendeleza uhusiano mzuri wa kihistoria na kidugu uliopo kati ya Oman na Tanzania ikiwemo utekelezaji wa ahadi za Hayati Sultan Qaboos Bin Said. Ziara hiyo ilikuwa muhimu kwa kuzingatia mahusiano ya kidugu na damu kati ya watu wa Oman na Tanzania ambapo wapo wa Oman walitoka Tanzania Bara na Zanzibar.

Ushirikiano wa Tanzania na Nchi za Ulaya na Amerika

Marekani

143. Mheshimiwa Spika, mwezi Machi 2020, niliwasilisha ujumbe maalum wa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Mheshimiwa Donald Trump, Rais wa Marekani. Pamoja na masuala mengine, ziara hiyo iliniwezesha kufanya mazungumzo na Mhe. Balozi Tibor Nagy, Naibu Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani anayeshughulikia Masuala ya Afrika; Bi. Jennifer D. Nordquist, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Dunia anayewakilisha Marekani; Balozi Mark Green, Mtendaji Mkuu wa Shirika la Msaada la Marekani (USAID) na Balozi Kelley E. Currie, Balozi - Kazi Maalum (Ambassador-at-Large) anayeshughulikia Masuala ya Wanawake Duniani.

144. Mheshimiwa Spika, kwa ujumla ziara hiyo imekuwa na mafanikio kwani imeipa Serikali yetu nafasi ya kutoa ufanuzi wa masuala ambayo ama yalikuwa hayaeleweki vizuri kwa wabia wetu wa maendeleo au yalikuwa yanapotoshwa kwa makusudi na baadhi ya watu au kundi la watu wasoitakia mema nchi yetu. Vilevile, kupitia ziara hiyo, nchi yetu

imeongeza idadi ya watakaoisemea vizuri ama kuitetea pindi itakapokuwa ikitembea vibaya.

145. Mheshimiwa Spika, kidiplomasia, kukutana na kufanya mazungumzo na viongozi hao kumeimarisha uhusiano na ushirikiano uliopo na pia kupeleka ujumbe na kuidhihirishia Jumuiya ya Kimataifa kuwa Tanzania na Marekani bado ni wabia wakubwa wanaoshirikiana vizuri katika nyanja mbalimbali za maendeleo.

Poland

146. Mheshimiwa Spika, mwezi Septemba 2019, Wizara iliratibu ziara ya Mheshimiwa Marcin Przydacz, Naibu Waziri wa Mambo ya Nje wa Poland. Lengo la ziara hiyo lilikuwa ni kuimarisha ushirikiano kwenye sekta ya maji ikiwemo uwezekano wa kutumia maji taka kuzalisha nishati katika jiji la Dodoma na Dar es Salaam. Kufuatia ziara hiyo, mwezi Desemba 2019, Tanzania na Poland zilisaini makubaliano ya kuanzisha ushirikiano katika sekta ya maji.

Cuba

147. Mheshimiwa Spika, mwezi Septemba 2019, Wizara iliratibu ziara ya Mheshimiwa Marcelino Gonzalenz, Naibu Waziri wa Mambo ya Nje wa Cuba. Lengo la ziara hiyo lilikuwa ni kuimarisha ushirikiano kati ya Tanzania na Cuba kwenye sekta za elimu, afya, utalii na kilimo. Kufuatia ziara hiyo, majadiliano ya ushirikiano katika sekta ya kilimo yameanza. Aidha, mwezi Januari 2020 Tanzania na Cuba zilisaini makubaliano ya kuleta madaktari bingwa wa mfumo wa fahamu, figo na moyo ili watoe huduma hizo katika Hospitali ya Benjamin William Mkapa iliopo jijini Dodoma.

148. Mheshimiwa Spika, vilevile, katika ziara hiyo Mheshimiwa Gonzalenz alifanya mazungumzo na Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na kukubaliana kuimarisha ushirikiano katika sekta za afya, kilimo, na uvuvi. Majadiliano kuhusu maeneo

ya ushirikiano katika sekta hizo kwa ngazi ya wataalam yanaendelea.

Ukraine

149. Mheshimiwa Spika, mwezi Februari 2020, Wizara iliratibu ziara ya ujumbe wa wawekezaji wa kiwanda cha kusindika nyama cha *Saltivsky Meat Processing Plant INC* cha nchini Ukraine. Ujumbe huo ulitembelea machinjio ya Vingunguti na kukutana na Baraza la Usimamizi wa Mazingira kwa lengo la kupata taarifa na taratibu za kuanzisha kiwanda cha kusindika nyama. Ujumbe huo umeahidi kurejea nchini hivi karibuni kutembelea mikoa ya Shinyanga, Kagera na Dodoma ambayo imependekezwa kujengwa kiwanda hicho.

Uturuki

150. Mheshimiwa Spika, mwezi Februari 2020, Wizara iliratibu ziara ya wawekezaji, wafanyabiashara 38 na wakuu wa vyuo viwili kutoka mji wa Sakarya, Uturuki. Ujumbe huo uliongozwa na Bw. Ekrem Yuce, Meya wa Mji wa Sakarya. Kutokana na ziara hiyo, Chuo Kikuu cha Sakarya (Sakarya University) na Chuo Kikuu cha Sayansi cha Sakarya (University of Applied Sciences) vya Uturuki vilisaini makubaliano ya ushirikiano na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam katika masuala ya utafiti katika sayansi; kubadilishana wanafunzi na wataalam pamoja na ufadhili wa masomo kwenye vyuo hivyo.

151. Mheshimiwa Spika, ujumbe huo pia ulitembelea Zanzibar na kufanya mazungumzo na Mstahiki Suleiman Kinana, Meya wa Jiji la Zanzibar kuhusu ushirikiano wa Jiji la Zanzibar na Jiji la Sakarya ambapo viongozi hao walisaini makubaliano ya awali ya ushirikiano (Letter of Intent) kati ya Majiji hayo. Aidha, ujumbe huo ulifanya mazungumzo na viongozi wa mamlaka za Serikali pamoja na wadau mbalimbali kwenye sekta binafsi ili kuangalia namna ya kushirikiana katika maeneo mengine ya kimkakati.

152. Mheshimiwa Spika, mwezi Novemba 2019, Wizara ilifanikisha ziara ya mwekezaji kutoka kampuni ya *Unit Textile* ya nchini Uturuki. Mwekezaji huyo ana nia ya kujenga kiwanda cha nguo na vyombo vya nyumbani mkoani Simiyu. Uwekezaji huo unatarajiwu kugharimu Dola za Marekani milioni 50 na kutoa ajira zipatazo 2000. Mamlaka za mkoa zimempatia eneo lenye ukubwa wa ekari 100 kufanikisha ujenzi wa viwanda hivyo. Mwekezaji huyo tayari amesajili kampuni hapa nchini itakayosimamia uwekezaji huo ijulikanayo kwa jina la *Tem Unique Simiyu Limited*.

Ubelgiji

153. Mheshimiwa Spika, mwezi Machi 2020, Wizara ilifanikisha upatikanaji wa soko kubwa la maharage machanga ya kijani (green beans) nchini Ubelgiji. Soko hilo limepatikana baada ya kufanya mazungumzo na kampuni ya Charlier - Brabo Group - CBG inayonunua maharage hayo kutoka sehemu mbalimbali duniani. Kampuni hiyo iko tayari kununua kontena takribani 180 ya maharage yenye urefu wa futi 40 kila mwaka.

154. Mheshimiwa Spika, kupatikana kwa soko hili nchini Ubelgiji ni habari njema kwa wakulima na wafanyabiashara wa mazao ya kilimo hususan kwa aina hii ya maharage ambayo tayari yana soko nchini Uholanzi. Tunatoa wito kwa Watanzania kuchangamkia upatikanaji wa soko hili jipya.

Uholanzi

155. Mheshimiwa Spika, mwezi Julai 2019, Wizara iliratibu kusainiwa kwa Makubaliano ya Ushirikiano kati ya Tanzania na Uholanzi kwenye ufugaji wa kuku na samaki. Kufuatia makubaliano hayo mradi wa shamba darasa la ufugaji wa samaki na kuku uliopo Kigamboni, Dar es Salaam ulizinduliwa mwezi Februari 2020. Lengo la mradi huo ni kutoa mafunzo kwa Watanzania wenye nia ya kuwekeza kwenye biashara ya ufugaji wa samaki kwa kutumia teknolojia ya kisasa. Mradi huu, unaendeshwa kwa ubia baina ya Serikali ya Tanzania, Kampuni ya Riga Safina ya Tanzania pamoja na Kampuni tano za Uholanzi.

Ushirikiano wa Kikanda

Jumuiya ya Afrika Mashariki

Mkutano wa 29 wa Baraza la Kisekta la Mawaziri wa Jumuiya ya Afrika Mashariki

156. Mheshimiwa Spika, mwezi Oktoba 2019, Wizara iliratibu na kushiriki kwenye Mkutano wa 29 wa Baraza la Kisekta la Mawaziri wanaohusika na masuala ya Afrika Mashariki na Mipango uliofanyika jijini Arusha. Pamoja na masuala mengine, Nchi Wanachama zilitakiwa kukamilisha zoezi la kuhuisha sheria hususan sheria na vibali vya kazi ili ziendane na matakwa ya Itifaki ya Soko la Pamoja la Jumuiya ifikapo mwezi Septemba 2020.

Bunge la Afrika Mashariki

157. Mheshimiwa Spika, Wizara iliratibu na kushiriki katika mikutano mitatu ya Bunge la Afrika Mashariki. Katika mikutano hiyo, Bunge lilijadili na kupitisha Muswada wa Sheria wa mwaka 2020 wa Kuidhinisha Matumizi ya Ziada ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kiasi cha Dola za Marekani 4,977,475 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya Vyombo na Taasisi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Aidha, Bunge lilijadili taarifa za kamati na kupitisha mapendekazo ya hatua mbalimbali za kuchukuliwa na Baraza la Mawaziri ili kuimarisha maeneo ya ushirikiano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Itifaki ya Umoja wa Forodha

158. Mheshimiwa Spika, mwezi Septemba 2019, Wizara iliratibu na kushiriki kwenye Mkutano wa 36 wa Dharura wa Baraza la Kisekta la Mawaziri wa Biashara, Viwanda, Fedha na Uwekezaji wa Afrika Mashariki uliofanyika Jijini Arusha. Mkutano huo ulipitisha Mkakati wa Miaka Kumi wa Kuendeleza Sekta ya Pamba na Nguo wa mwaka 2019 – 2029. Mkakati huo unalenga kuongeza uzalishaji wa mbegu za

pamba kutoka tani 290,000 hadi tani 1,000,000 kwa mwaka na kuongeza uwezo wa kuchakata pamba na kuwa kitambaa kutoka urefu wa mita milioni 6.9 hadi kufikia urefu wa mita milioni 37.3.

159. Mheshimiwa Spika, vilevile, katika mkutano huo, Nchi Wanachama zilikubaliana kuwa ngozi iliyosindikwa kwa kiwango cha kati (wet blue) inayouzwa nje ya Jumuiya ya Afrika Mashariki itozwe ushuru wa asilimia 10 kuanzia mwaka 2019/2020. Aidha, kiwango hicho kitaendelea kuongezeka kwa asilimia 10 kila mwaka kwa kipindi cha miaka 10 ili kuhamasisha uwekezaji kwenye viwanda vyta kuzalisha ngozi na bidhaa za ngozi ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Itifaki ya Soko la Pamoja

160. Mheshimiwa Spika, katika kuadhimisha miaka 20 ya uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Wizara iliratibu na kushiriki katika Maonesho ya Kitaifa ya Wajasiriamali wa Tanzania yaliyofanyika mwezi Oktoba 2019, mji mpya wa Fumba, Zanzibar. Kupitia maonesho hayo, wajasiriamali wapatao 250 kutoka Tanzania na Kenya walipata fursa ya kuuza na kutangaza bidhaa mbalimbali wanazozalisha.

161. Mheshimiwa Spika, mwezi Desemba 2019, Wizara iliratibi na kushiriki kwenye maonesho ya 20 ya wajasiriamali Afrika Mashariki yaliyofanyika Kigali, Rwanda. Wajasiriamali wapatao 1,500 kutoka Nchi Wanachama wakiwemo 160 kutoka Jamhuri ya Muungano wa Tanzania walishiriki katika Maonesho hayo. Wajasiriamali hao pia walipata fursa ya kubadilishana taarifa za kibashara, ujuzi pamoja na huduma.

162. Mheshimiwa Spika, mwezi Machi 2020, Wizara iliratibu Kongamano la Biashara na Uwekezaji kati ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Chama cha Wafanyakishara wa Uswidi na Afrika Mashariki (SWEACC) liliyofanyika Jijini Dar es Salaam. Kongamano hilo lilihudhuriwa na washiriki zaidi ya 200 kutoka nchi za Afrika Mashariki, Uswidi na Nordic kwa ujumla. Lengo la Kongamano hilo ni kuhamasisha uwekezaji na biashara baina ya Uswidi na Nchi za Afrika Mashariki. Aidha,

kongamano hilo lilitoa fursa kwa kampuni za Uswidi na Norway kutangaza matumizi na uwekezaji wa teknolojia ya udhibiti wa uchafuzi wa mazingira na bidhaa zitakazopelekea ukuaji endelevu wa maisha bora ya wananchi wa Tanzania na Afrika Mashariki. Maeneo matatu ya kipaumbele kwenye Kongamano hilo yalikuwa ni maji na usafi wa mazingira, usafiri rafiki kwa mazingira na urejezaji taka kuwa nishati.

163. *Mheshimiwa Spika*, matokeo ya Kongamano hilo ni pamoja na kusainiwa Hati ya Makubaliano (MoU) kati ya Chama cha Wafanyabiashara wenyewe Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA) na Chama cha Wafanyabiashara wa Uswidi na Afrika Mashariki kuhusu ushirikiano katika kukuza uwekezaji na biashara. Vilevile, wakati wa Kongamano hilo Mheshimiwa Angella Kairuki (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji) alikutana na kufanya mazungumzo na kampuni za SCANIA ambao wana lengo la kurejea nchini kuanzisha kiwanda cha kuanganisha magari.

164. *Mheshimiwa Spika*, mwezi Septemba 2019, Wizara iliratibu na kushiriki kwenye Mkutano wa 13 wa Baraza la Mawaziri la Kisikta la Kilimo na Usalama wa Chakula la Afrika Mashariki uliofanyika Arusha. Nchi Wanachama zilikubaliana kuanzisha Sera na Mikakati ya kuwahusisha vijana kikamilifu katika sekta ya kilimo kwa kuzingatia jinsia. Aidha, Mkutano huo ulizagiza Nchi Wanachama ambazo hazijaridhia Itifaki ya Afya ya Wanyama na Mimea kuridhia kabla ya mwezi Machi 2020.

165. *Mheshimiwa Spika*, mwezi Februari 2020, Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa Saba wa Baraza la Kisikta la Mazingira na Usimamizi wa Maliasili la Jumuiya ya Afrika Mashariki uliofanyika jijini Dodoma. Mkutano huo ulijadili na kupitisha rasimu ya Itifaki ya Mazingira na Usimamizi wa Maliasili, rasimu ya Sera ya Misitu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Mkakati wa utekelezaji wake pamoja na rasimu ya Mpango Kazi Kabambe kwa ajili ya kutekeleza mapendekezo yanayohusu kupunguza na kusimamia maafa.

Itifaki ya Umoja wa Fedha wa Afrika Mashariki

166. Mheshimiwa Spika, mwezi Novemba 2019, Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa Baraza la Kisekta la Mawaziri wa Fedha na Masuala ya Uchumi uliofanyika Jijini Arusha. Mkutano huo, ulijadili utekelezaji wa Maamuzi ya Mkutano wa 34 wa Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Afrika Mashariki ya kufanya mapitio ya Mkataba wa kuanzisha Benki ya Maendeleo ya Afrika Mashariki (EADB). Iliamuliwa kuwa Baraza la Uongozi wa Benki lizingatie mipango ya maendeleo ya Jumuiya wakati wa kuandaa vipaumbele vya Benki hiyo. Vilevile, ilihamuliwa kuweka ukomo wa muda wa nafasi ya Mtendaji Mkuu wa Benki kama ilivyo kwenye benki nyingine za kikanda. Aidha, Mkutano huo ulipitisha rasimu ya Sera ya Benki ya Afrika Mashariki na Mkakati wa Utekelezaji wake.

Masuala ya Siasa, Ulinzi na Usalama

167. Mheshimiwa Spika, mwezi Oktoba 2019, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania katika zoezi la pamoja la vituo vya uamrishaji vya majeshi ya Nchi Wanachama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (CPX USHIRIKIANO IMARA) liilofanyika Jinja, Uganda. Lengo la zoezi hilo ni kuyajengea uwezo majeshi yetu katika kukabiliana na ugaidi, uharamia, maafa na urejeshaji wa amani wakati wa machafuko. Zoezi hilo lilihusisha jumla ya washiriki 360 kutoka majeshi ya ulinzi, polisi na Asasi za kiraia kutoka Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

168. Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea na uratibu wa maandalizi ya rasimu ya Katiba ya Fungamano la Kisiasa la Jumuiya ya Afrika Mashariki ambayo ni hatua ya mpito kuelekea Shirikisho la Kisiasa la Afrika Mashariki. Timu ya wataalam iliyoundwa kwa ajili ya kuandaa rasimu ya Katiba ya Fungamano kama ilivyoagizwa kwenye Mkutano wa 19 wa Wakuu wa Nchi Wanachama, imeanza kukusanya maoni ya wadau katika Nchi Wanachama yatakayowezesha kupendekeza modeli ya Fungamano na maeneo ya ushirikiano.

169. Mheshimiwa Spika, zoezi la kukusanya maoni ya wadau lilianza mwezi Januari 2020 nchini Burundi na litaendelea katika nchi nyingine za Jumuiya. Kwa upande wa Tanzania, zoezi hilo linatarajiwa kufanyika mwezi Agosti 2020. Naomba kutoa rai kwa Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla kujitokeza kwa wingi wakati wa zoezi hilo.

170. Mheshimiwa Spika, mwezi Agosti 2019, Wizara iliratibu ushiriki wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania kwenye Tamasha la Michezo na Utamaduni kwa Majeshi ya Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki lilifanyika Jijini Nairobi, Kenya. Tamasha hilo lilifanyika kama sehemu ya jitihada za kuimarisha ushirikiano na kujenga kuaminiana mionganii mwa askari wa majeshi ya Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

171. Mheshimiwa Spika, mwezi Agosti 2019, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania kwenye Mkutano wa Baraza la Mawaziri la Kiseka la Ushirikiano katika sekta ya Ulinzi uliofanyika jijini Arusha. Mkutano huo pamoja na mambo mengine ulijadili na kupitisha mapendekezo ya kuanzisha Kituo cha Kikanda cha Kuratibu Mapambano dhidi ya Ugaidi cha Jumuiya ya Afrika Mashariki ikiwa ni kuendeleza juhudhi za mapambano dhidi ya ugaidi kwenye Jumuiya hiyo.

172. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha utawala bora na uwajibikaji kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki, Wizara iliratibu ukusanyaji wa maoni kutoka kwa wadau mbalimbali kuhusiana na Rasimu ya Itifaki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa. Maoni ya Tanzania kuhusiana na rasimu ya Itifaki hiyo yamewasilishwa Sekretarieti ya Jumuiya.

Programu za Miundombinu ya Kiuchumi na Huduma za Kijamii

173. Mheshimiwa Spika, mwezi Oktoba 2019 Wizara iliratibu ufunguzi wa Kituo cha Huduma kwa Pamoja Mpakani Tunduma/Nakonde kilichopo katika mpaka wa Tanzania na Zambia. Kituo hicho kilizinduliwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania pamoja na Mheshimiwa Edgar Chagwa Lungu, Rais wa Jamhuri ya Zambia. Uwepo wa kituo hicho katika mpaka huo umerahisisha shughuli za kibashara katika Tanzania na Zambia.

174. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuratibu zoezi la kutoa mafunzo kwa watumishi wa Serikali waliopo katika vituo vinane vyta Huduma za Pamoja Mipakani ambavyo ni Holili / Taveta (Tanzania / Kenya); Mutukula / Mutukula (Tanzania / Uganda); Rusumo / Rusumo (Tanzania / Rwanda); Kabanga / Kobero (Tanzania / Burundi); Namanga / Namanga (Tanzania / Kenya); Sirari / Isebania (Tanzania / Kenya); Horohoro / Lungalunga (Tanzania / Kenya); na Tunduma / Nakonde (Tanzania / Zambia) ili kuwezesha kutoa huduma zinazostahili kwa watumiaji wa vituo hivyo. Aidha, Wizara inaendelea kutoa elimu kwa umma ili kuwawezesha kufahamu huduma zinazotolewa na vituo hivyo na kutumia fursa zilizopo kikamilifu.

175. Mheshimiwa Spika, mwezi Oktoba 2019, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania katika Mkutano wa Pili wa Mawaziri wa Sekta za Miundombinu wa COMESA, EAC na SADC uliofanyika Lusaka, Zambia. Katika Mkutano huo, pamoja na masuala mengine, nchi hizo zilikubaliana kutokuwa na ongezeko la uzito wa jumla wa magari ya kusafirisha mizigo unaoruhusiwa kwa lengo la kulinda miundombinu ya barabara; kuboresha mifumo ya kitaasisi ya utekelezaji wa Programu ya Kuwezesha Sekta ya Uchukuzi na Biashara kwa Nchi Wanachama; kuwianisha mifumo ya kudhibiti uzito wa magari na usajili wa leseni kwa vyombo vyta usafiri kwa njia ya barabara; na kuwianisha mifumo ya usajili wa watoa huduma za usafirishaji na mfumo wa pamoja wa kielektroniki wa kusajili watoa huduma za usafirishaji kwa nchi zote wanachama.

176. Mheshimiwa Spika, mwezi Oktoba 2019, Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa 18 wa Baraza la Mawaziri la Kisekta la Afya la Jumuia ya Afrika Mashariki uliofanyika jijini Nairobi, Kenya. Pamoja na masuala mengine, mkutano huo ulijadili utekelezaji wa Programu ya kuhuisha taratibu za udhibiti wa dawa na vifaa tiba katika Nchi Wanachama.

Mkutano huo ulikubaliana taratibu za usajili wa dawa na ukaguzi wa pamoja zifuate miongozo iliyokubalika ili kudhibiti dawa zisizokuwa na ubora zinazoalishwa na Nchi Wanachama pamoja na zile zinazoingizwa ndani ya Jumuiya.

177. Mheshimiwa Spika, Mkutano huo pia, ulijadili utekelezaji wa Mradi wa Maabara Maalumu Zinazotembea kwa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa ajili ya kudhibiti magonjwa ya mlipuko na kuambukiza. Mradi huo, unahusisha kuingizwa kwa vifaa tiba vya maabara kutoka kwa wazabuni mbalimbali duniani kupitia bandari au viwanja vya ndege vya Nchi Wanachama. Tanzania ilikubali vifaa vya mradi huo vипитие katika bandari ya Dar es Salaam na katika viwanja vyake vya ndege. Baadhi ya vifaa hivyo vimeshapokelewa na Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na tayari zimesambazwa katika Nchi Wanachama.

178. Mheshimiwa Spika, mwezi Septemba 2019, Wizara iliratibu Tamasha la Nne la Jumuiya ya Afrika Mashariki la Utamaduni lijulikanalo kama Jumuiya ya Afrika Mashariki Utamaduni Festival (JAMAFEST) liliofanyika jijini Dar es Salaam ikiwa ni mara ya kwanza kwa Tanzania kuwa mwenyeji wa Tamasha hilo tangu kuanzishwa kwake mwaka 2013. Tamasha hilo limekuwa likifanyika kwa mzunguko kila baada ya miaka miwili katika Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Tamasha hilo lilifunguliwa rasmi na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kufungwa rasmi na Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar. Lengo la Tamasha hilo ni kukuza utamaduni wa jamii za watu wa Afrika Mashariki ambapo maonesho mbalimbali ya kiutamaduni ikiwemo mavazi ya asili, sanaa ya uchongaji, michezo ya kuigiza, mapishi ya vyakula vya asili na michezo ya jadi huoneshwa. Kupitia Tamasha hilo, Tanzania ilipata fursa ya kuonesha tamaduni zake pamoja na kutangaza vivutio vya utalii na utamaduni vilivyopo nchini.

179. Mheshimiwa Spika, mwezi Agosti 2019, Wizara iliratibu ziara ya tatu ya waendesha baisedeli iliyojumuisha vijana 22 kutoka katika Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika

Mashariki. Ziara ya namna hii imekuwa ikifanyika kila mwaka kuanzia mwaka 2016 kwa lengo la kuhamasisha michezo; kutangaza utamaduni na vivutio vya utalii vya Nchi Wanachama; pamoja na kuelimisha jamii kuhusu masuala ya Mtangamano wa Afrika Mashariki. Ziara hiyo ilianzia nchini Uganda tarehe 1 Agosti 2019 na kupita katika nchi za Kenya, Tanzania, Burundi, Rwanda na kuhitimishwa nchini Uganda tarehe 20 Septemba 2019. Aidha, waendesha balskeli hao walipokuwa nchini, walipata fursa ya kutembelea Ofisi za balozi za Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na kutembelea Hifadhi ya Taifa ya Arusha.

180. Mheshimiwa Spika, Wizara iliratibu mafunzo ya wawezeshaji wanawake kiuchumi kupitia mradi wa *50 Million African Women Speak Networking Platform*. Mafunzo hayo yaliyoshirikisha wanawake 40 kutoka Taasisi za Serikali na vikundi vya Asasi Zisizo za Kiserikali vinavyoratibu masuala ya maendeleo ya wanawake yalifanyika jijini Dodoma mwezi Novemba 2019. Lengo la mradi huu ni kujenga mfumo wa kidigitali wa mawasiliano baina ya wanawake ili kupata taarifa za kifedha na kupata masoko ya bidhaa zinazozalishwa na wanawake. Mradi huu unatekelezwa chini ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na kwa upande wa Zanzibar unatekelezwa chini ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wazee, Wanawake na Watoto.

181. Mheshimiwa Spika, mwezi Februari 2020, Wizara iliratibu na kushiriki kwenye Kongamano la Kwanza la Programu ya wanafunzi wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki wanaofadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Ujeruman (German Development Bank - KfW) lillifanyika Entebbe, Uganda. Programu hii inafadhili wanafunzi wapatao 60 wa Nchi Wanachama wenye mahitaji maalum (poor and disadvantaged) wanaosoma masomo ya Hisabati; Uhandisi; Sayansi na Teknolojia; na masomo ya Sayansi ya Biashara kwa ngazi ya shahada ya uzamili na stashahada ya uzamili kwenye vyuo vilivyopo ndani ya Jumuiya. Kila nchi mwanachama inatoa idadi sawa ya wanafunzi 10 watakaogharamiwa mafunzo hayo. Kwa upande wa Tanzania, vyuo vinavyopokea ufadhili huo ni Chuo Kikuu cha

Dodoma, Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine na Chuo cha Ushirika Moshi. Idadi ya Watanzania wanaofadhiliwa kwa sasa ni 10 ambapo wanaume ni sita na wanawake wanne.

182. Mheshimiwa Spika, mwezi Machi 2020 Wizara iliratibu Mkutano wa Dharura wa Pamoja wa Baraza la Mawaziri la Kisekta la Masuala ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Baraza la Mawaziri la Kisekta la Afya uliofanyika kwa njia ya mtandao (*Video Conference*). Mkutano huo ulitoa Azimio la mikakati ya pamoja ya kukabiliana na mlipuko wa homa kali ya mapafu inayosababishwa na virusi vya Corona (COVID-19) na mipango ya kutatua changamoto zinazojitokeza kutokana na hatua zinazochukuliwa na Nchi Wanachama katika kukabiliana na ugonjwa huo.

183. Mheshimiwa Spika, baadhi ya maazimio ya Mkutano huo ni:-

- i. Kutekeleza agizo la kukaa karantini kwa lazima kwa siku 14 kwa wasafiri wote wanaoingia katika Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki;
- ii. Kuendesha mikutano kwa njia ya mtandao hadi hapo hali ya maambukizi itakapodhibitiwa;
- iii. Kuhakikisha malori yanayobeba bidhaa yanakuwa na wafanyakazi wawilli hadi watatu tu; na
- iv. Kuwapima wafanyakazi (*Crew*) wa malori na endapo mmoja wao atapatikana na dalili za ugonjwa wa COVID-19 watatengwa (quarantined) kwa muda wa siku 14 kulingana na miongozo ya kitaifa na nchi husika na lori hilo litapuliziwa dawa kabla ya kuendelea na safari na wafanyakazi wengine.

184. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Azimio la Mkutano wa Pamoja wa Dharura wa Baraza la Mawaziri la Kisekta la Masuala ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Baraza la Mawaziri la Kisekta la Afya, Tanzania ni kiungo muhimu cha usafirishaji wa bidhaa kwa baadhi ya Nchi Wanachama za Jumuiya ya Afrika Mashariki na SADC. Katika kipindi hiki cha mapambano

dhidi ya ugonjwa wa Corona, imeendelea kuacha mipaka yake wazi kwa kuruhusu bidhaa muhimu kuelekea katika nchi zisizo na bandari kupita. Corona ni hatari, lakini kukosekana kwa mahitaji muhimu kwa nchi zisizo na bandari kama chakula, dawa na mafuta ya petroli ambavyo vinapitia katika bandari yetu kuelekea katika nchi zisizo na bandari kunaweza kuwa ni hatari zaidi.

185. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza hilo, tumezielekeza mamlaka zetu za vituo vya pamoja mipakani (OSBPs) kuhakikisha wanaepusha vikwazo visivyo vya lazima kwa kukaa pamoja na wenzao wa nchi jirani waliopo katika vituo hivyo kutatua changamoto za mipakani katika kipindi hiki cha ugonjwa wa Corona bila kuathiri upatikanaji wa bidhaa hizo muhimu katika nchi zisizo na bandari.

186. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Jumuiya ya Afrika Mashariki iliratibu ujenzi wa barabara za: Arusha - Namanga-Arthi River (km240) ambapo Tanzania ina kipande cha kilomita 104.4 uliogharimu Dola za Marekani milioni 63.2; Arusha – Holili/Taveta-Voi (km 260). Ujenzi wa awamu ya kwanza kwa upande wa Tanzania unaohusisha upanuzi wa barabara ya Sakina – Tengeru (km 42) kuwa njia nne na ujenzi wa barabara ya mzunguko (Arusha Bypass) ulikamilika kwa gharama ya Shilingi 183,710,845,663.

187. Mheshimiwa Spika, aidha, Wizara inaendelea kuratibu ukamilishwaji na upatikanaji wa fedha za miradi ya barabara za: Lusahunga – Rusumo/Kayonza kwa kipande cha Tanzania. Upembusi yakinifu wa kipande hicho umekamilika na gharama za mradi zitajulikana baada ya usanifu wa kina; Nyakanazi - Kasulu -Kidahwe - Mpanda unatarajiwa kugharimu Dola za Marekani milioni 373; Malindi – Mombasa – Lungalunga/Horohoro – Tanga – Pangani – Bagamoyo (km 178) kwa upande wa Tanzania ujenzi wa kipande cha Tanga - Pangani - Bagamoyo utagharimu kiasi cha Dola za Marekani milioni 195.5; na Kumunazi – Kasulu/Bukene na ukarabati wa Kyaka – Mutukula (km 252.5) upembusi yakinifu umekamilika na usanifu wa kina umeanza ili kupata gharama za mradi.

Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika

188. Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza kwenye sehemu ya mafanikio ya Wizara kwa kipindi cha kwanza cha Serikali ya Awamu ya Tano kuwa Tanzania ni mwenyekiti na mwenyeji wa mikutano ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) kwa kipindi cha mwaka mmoja kuanzia mwezi Agosti 2019 hadi Agosti 2020. Katika kipindi cha uenyekiti wetu tumejiwekea vipaumbele mbalimbali ikiwemo: uendelezaji wa viwanda; matumizi bora ya rasilimali fedha za Jumuiya; kuondolewa kwa vikwazo vya kiuchumi kwa nchi ya Zimbabwe; na matumizi ya lugha ya Kiswahili katika Jumuiya.

189. Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki Wizara imeratibu kwa mafanikio makubwa na kufanikisha kufanyika kwa Mkutano wa Baraza la Mawaziri wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika ulifanyika tarehe 18 Machi 2020. Mkutano huo ulifanyika kwa mara ya kwanza kwa njia ya mtandao ikiwa ni tahadhari dhidi ya maambukizi ya ugonjwa wa homa kali ya mapafu unaosababishwa na virusi cya Corona (COVID19).

190. Mheshimiwa Spika, pamoja na masuala mengine Mkutano uliazimia yafuatayo: -

- i) Kuendesha mikutano kwa njia ya mtandao hadi hapo hali ya maambukizi itakapodhibitiwa;
- ii) Kupitisha pendekozo la kuzindua shughuli za maadhishimo ya miaka 40 ya SADC;
- iii) Kuunga mkono pendekozo la Umoja wa Afrika la kuwa na mgombea mmoja kutoka Afrika katika nafasi ya Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Kazi Duniani; na
- iv) Kuridhia Dira ya SADC ya mwaka 2050 na Mpango Mkakati Elekezi wa Maendeleo ya Kikanda na kuelekeza iwasilishwe kwenye Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali kwa maamuzi.

191. Mheshimiwa Spika, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaendelea kutekeleza majukumu yake ya uenyekiti wa SADC ambapo katika kipindi hiki tumeendelea kutekeleza ajenda ya mtangamano wetu na kuhakikisha kuwa malengo ya Jumuiya yanafikiwa kama yalivyoainishwa katika Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika, ambapo tumekuwa tukiongozwa na nyaraka mbili za kimkakati ambazo ni Mpango Mkakati Elekezi wa Kanda (RISDP) wa mwaka 2015 – 2020 na Awamu ya Pili ya Mpango Mkakati wa Asasi za Siasa, Ulinzi na Usalama (SIPOLI). Mipango mikakati hii inafikia ukomo wake mwaka 2020. Hivyo, kama ilivyoelekezwa na Wakuu wa Nchi na Serikali na Jumuiya hiyo, Sekretarieti imeanza uratibu wa maandalizi ya mipango mikakati mingine itakayopelekea kutekeleza ajenda ya mtangamano wa Jumuiya baada ya mwaka 2020.

192. Mheshimiwa Spika, ni furaha kubwa kwamba mikakati hii inaandaliwa wakati wa uenyekiti wetu ambapo kukamilika kwake itakuwa ni kukamilika kwa moja ya jukumu katika uenyekiti wetu. Aidha, tumeendelea kusimamia masuala muhimu ya maendeleo ya Jumuiya kwa kuzingatia Kaulimbiu yetu ya "Mazingira Wezeshi kwa ajili ya Maendeleo Endelevu na Jumuishi ya viwanda; kukuza biashara na ajira ndani ya SADC". Hata hivyo, pamoja na jitihada zote za kuhakikisha kuwa tunafikia malengo tuliojiwekea, kipindi hiki kimekuwa kigumu kutokana na athari kubwa inayosababishwa na ugonjwa huu wa homa ya mapafu unaosababishwa na virusi vya Corona (COVID-19).

193. Mheshimiwa Spika, kutokana na mwenendo wa mlipuko wa ugonjwa wa COVID-19 duniani, ni dhahiri kwamba ili kukabiliana nao kunahitajika ufanisi na ushirikiano wa hali ya juu katika ngazi za kitaifa, kikanda na kimataifa. Kufuatia hali hiyo, kwa mara nyingine tena naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa SADC pamoja na Dkt. Stergomena Lawrence Tax, Katibu Mtendaji wa SADC kwa maelekezo na ushauri wanaoendelea kuutoa kwa Nchi Wanachama ili kuhakikisha

kwamba ukanda wetu hauathiriki sana na janga hili la COVID-19.

194. Mheshimiwa Spika, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa mara tu baada ya Shirika la Afya Duniani (WHO) kutangaza kuwa ugonjwa huu ni janga la dunia hatukuzembea na mara moja chini ya uenyekiti wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hatua mbalimbali zilanza kuchukuliwa ili kuhakikisha kuwa tishio kubwa linaloletwa na ugonjwa wa COVID-19 halizoroteshi shughuli za kiuchumi katika ukanda wa Jumuiya yetu endapo kasi ya maambukizi ya virusi hivyo itaongezeka. Tunafahamu fika kuwa ni jukumu letu kuhakikisha kuwa mwenendo wa uchumi, biashara, uwekezaji, na masoko ya fedha hauyumbi kutokana na athari za ugonjwa huu. Kwa hali hiyo, Nchi Wanachama zinaendelea kutathmini madhara ya kiuchumi yanayosababishwa na ugonjwa huu na kutunga sera zitakazosaidia sekta zinazohitaji zaidi msaada wa kiutawala au kifedha.

195. Mheshimiwa Spika, katika mapambano dhidi ya ugonjwa huu zifuatazo ni hatua mbalimbali ambazo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imefanikisha. Hatua hizo ni kufanyika kwa Mkutano wa Dharura wa Mawaziri wa Afya wa SADC kuhusu COVID -19 tarehe 9 Machi 2020 chini ya uenyekiti wa Mheshimiwa Ummy Mwalimu, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Mkutano huu ulifanyika kwa njia ya mtandao ikiwa ni hatua mojawapo ya kudhibiti maambukizi ya ugonjwa huo. Mkutano huo pamoja na mambo mengine, ulipendekeza kuundwa kwa Kamati ya Wataalam kwa ajili ya kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Itifaki ya Afya ya SADC kufuatia mlipuko wa ugonjwa wa homa kali ya mapafu unaosababishwa na virusi vya Corona (COVID-19). Mapendekezo hayo ya Mawaziri wa Afya, yaliridhiwa na Baraza la Mawaziri wa SADC katika mkutano uliofanyika tarehe 18 Machi, 2020. Aidha, tarehe 31 Machi 2020, Kamati ya Wataalam ilifanya kikao kwa njia ya mtandao na kwa kushirkiana na Sekretarieti ya SADC ilipendekeza kuandaliwa kwa mkutano huu wa Dharura wa

Baraza la Mawaziri. Aidha, Kamati hiyo pia iliridhia mapendekezo 11 katika maeneo yafuatayo:

- i. Ufutiliaji na utekelezaji wa Itifaki ya Afya kuhusu magonjwa ya mlipuko,
- ii. Kujiandaa na kukabiliana na virusi vya COVID-19;
- iii. Kubaini wagonjwa, kufutilia waliokutana na mgonjwa na huduma za tiba;
- iv. Uzuiaji na udhibiti wa maambukizi;
- v. Uchunguzi na upimaji wa kimaabara;
- vi. Uelimishaji wa madhara na ushirikishwaji wa jamii;
- vii. Hatua stahiki za Afya ya Jamii;
- viii. Uratibu wa Kikanda wa kukabiliana na virusi vya COVID-19;
- ix. Uwezeshaji na usafirishaji wa bidhaa muhimu mionganoni mwa nchi za SADC wakati wa mlipuko wa ugonjwa wa virusi vya COVID-19;
- x. COVID-19 na masuala ya udhibiti wa biashara katika ukanda;
- xi. Usimamizi wa majanga hatarishi katika ukanda wa SADC.

196. *Mheshimiwa Spika*, tarehe 6 Aprili, 2020 niliongoza Mkutano wa Dharura wa Baraza la Mawaziri uliofanyika kwa njia ya mtandao (video conference). Mkutano huu ulijumuisha jumla ya Nchi Wanachama zifuatazo; Angola, Botswana, Eswatini, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Malawi, Msumbiji, Mauritius, Namibia, Seychelles, Zambia na Tanzania. Mkutano huo ulipokea taarifa ya Kamati ya Wataalam ya kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Itifaki ya Afya ya SADC kufuatia mlipuko wa ugonjwa wa COVID-19

pamoja na mwongozo wa Urazinishaji (harmonisation) na uwezeshaji wa usafirishaji wa bidhaa muhimu na huduma katika nchi za SADC katika kipindi hiki cha janga la COVID - 19.

197. Mheshimiwa Spika, Mwongozo huu unawezesha usafirishaji wa bidhaa muhimu na huduma katika nchi za SADC hatua ambayo inasaidia kuzuia kuenea kwa COVID - 19 kuititia usafirishaji mipakani, kuwezesha utekelezaji na mikakati ya kitaifa ya kudhibiti kuenea kwa COVID-19, kuwezesha upatikanaji wa bidhaa muhimu kama vile mafuta, chakula na dawa, kuzuia usafirishaji usio wa lazima wa abiria kuititia mipakani na vile vile kurazinisha na kuratibu sera, kanuni na hatua za haraka za kitaifa za kukabiliana na COVID-19.

198. Mheshimiwa Spika, hatua hii imetokana na kasi ya maambukizi na vifo vinavyoendelea kutokea na tayari vimeanza kuleta athari hasi katika kanda yetu. Kwa mujibu wa taarifa ya Shirika la Afya Duniani ya tarehe 6 Mei 2020, idadi ya visa ni 9,841 na idadi ya vifo ni 224 katika Ukanda wa SADC kwa nchi 15 isipokuwa Falme ya Lesotho ambayo hadi sasa haina kisa hata kimoja cha maambukizi.

199. Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa SADC ameendelea kuzisisitizia na kuwaomba Washirika wa Maendeleo pamoja na Taasisi za Fedha za Kimataifa kuzifutia madeni na kutoa fedha za dharura kwa Nchi Wanachama wa SADC ili kuzisaidia katika kukabiliana na athari hasi za kiuchumi zinazosababishwa na ugonjwa wa COVID-19. Wito huu wa Mheshimiwa Rais kwa niaba ya Nchi Wanachama wa SADC unaongezea uzito wito alipoutoa tarehe 22 Aprili 2020, wakati alipozungumza na Wakuu wa Vyombo vyta Ulinzi na Usalama kuhusu juhudhi za Serikali katika mapambano dhidi ya COVID – 19 na kuzitaka Jumuiya, Taasisi na Washirika wa Maendeleo watoe msamaha wa madeni kwa nchi zetu ili ziweze kutumia fedha ambazo zingelipia madeni hayo kukabiliana na janga hili la COVID- 19.

200. Mheshimiwa Spika, mwezi Februari 2020, Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa Kamati ya Mawaziri wa nchi za SADC wanaohusika na Menejimenti ya Athari za Maafa uliofanyika Zanzibar. Mkutano huo ulifunguliwa na Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Katika Mkutano huo, Mawaziri waliidhinisha mapendekezo ya Mapitio ya Mkakati wa Kikanda wa Kujandaa na Kukabiliana na Maafa wa Mwaka 2016 – 2030, ili uwiane na Ajenda ya mwaka 2030 ya Malengo ya Maendeleo Endelevu, Makubaliano ya Paris kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi, Ajenda ya Afrika ya mwaka 2063 na Programu ya Utekelezaji wa Mkakati wa Sendai katika Afrika.

201. Mheshimiwa Spika, mwezi Julai 2019, niliongoza ujumbe wa Tanzania katika Mkutano wa 21 wa Mawaziri wenye dhamana ya Mambo ya Nje, Mambo ya Ndani na Ulinzi pamoja na Wakuu wa vyombo vya ulinzi na usalama kutoka Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika uliofanyika jijini Lusaka Zambia. Katika Mkutano huo, Nchi Wanachama ziliazimia kuendelea kuimarisha ushirikiano kwenye nyanja za siasa, demokrasia, ulinzi na usalama; na kuifahamisha Serikali ya Burundi kuhusu tathmini iliyofanyika ya maombi ya nchi hiyo kujunga na SADC.

202. Mheshimiwa Spika, vilevile, mkutano huo uliiteua Jamhuri ya Zimbabwe kuwa Mwenyekiti wa Asasi ya SADC ya Ushirikiano katika Siasa, Ulinzi na Usalama; kuziteua nchi za Tanzania, Angola, Botswana, DRC, Malawi na Afrika Kusini kwa kushirikiana na Sekretariati ya SADC na Ofisi ya Kikanda ya *Interpol*iliyopo Harare, Zimbabwe kuandaa rasimu ya Mkakati na Mpango Kazi wa SADC unaohusika na silaha ndogo ndogo na silaha nyepesi.

203. Mheshimiwa Spika, mwezi Novemba 2019, Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa pamoja wa Mawaziri wa Afya na Mawaziri wenye dhamana ya VVU na UKIMWI wa SADC uliofanyika jijini Dar es Salaam. Mkutano huo ulijadili hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa Itifaki ya Afya ya SADC ya

mwaka 1999 na Mpango Mkakati wake na kuridhia maazimio mbalimbali kuhusu masuala ya afya.

204. Mheshimiwa Spika, wajumbe wa mukutano huo walipata fursa ya kutembelea maeneo ya kimkakati ikiwemo kiwanda cha viuadudu vya malaria cha *Labiofarm* kilichopo Kibaha mkoani Pwani. Lengo la ziara hiyo lilikuwa ni kutangaza bidhaa zinazozalishwa na kiwanda hicho. Kadhalika, Mawaziri hao walitembelea Bohari ya Dawa (*msd*) ikiwa ni mkakati wa kutangaza shughuli zake kwa Nchi Wanachama kufuatia ushindi wa zabuni ya ununuzi, utunzaji na usambazaji wa dawa na vifaa tiba kuititia Mpango wa SADC wa ununuzi wa pamoja.

205. Mheshimiwa Spika, mwezi Novemba 2019, Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa Dharura wa Mawaziri wanaouna TROIKA Mbili za SADC pamoja na nchi zinazochangia vikosi vya kulinda amani katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo uliofanyika jijini Dar es Salaam. Katika Mkutano huo, DRC ilishiriki kama mjumbe mwandalizi. Mkutano huo uliazimia kuwa iwapo Misheni ya Umoja wa Mataifa ya Ulinzi wa Amani nchini DRC (MONUSCO) haitaongezewa muda ifikapo mwaka 2022, kikosi cha dharura cha SADC kiwe tayari kuchukua na kuendeleza jukumu la MONUSCO.

206. Mheshimiwa Spika, mwezi Oktoba 2019, Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa Pamoja wa Mawaziri wanaosimamia Sekta za Mazingira, Maliasili na Utalii wa SADC uliofanyika jijini Arusha. Pamoja na masuala mengine, Mkutano huo uliazimia kuwa Nchi Wanachama zisaini na kuridhia Itifaki ya Usimamizi wa Mazingira na Maendeleo Endelevu mapema iwezekanavyo na kuchukua hatua stahiki kukabiliana na changamoto zinazoikabili sekta ya misitu. Aidha, Mkutano huo, uliazimia Nchi Wanachama kushirikiana katika mapambano dhidi ya ujangili kwa kutekeleza Mkakati wa Kupambana na Ujangili wa Nchi za SADC.

207. Mheshimiwa Spika, mwezi Septemba 2019, Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa Pamoja wa Mawaziri wa

TEHAMA, Habari, Uchukuzi na Hali ya Hewa wa SADC uliofanyika jijini Dar es Salaam. Pamoja na masuala mengine, Mkutano huo uliazimia kuimarisha upatikanaji wa huduma za mtandao wenye kasi; kuanzisha mradi wa satelaiti ya pamoja; matumizi ya teknolojia ya malipo kwa njia ya kielektroniki; kupunguza gharama za huduma ya kuunganisha mawasiliano ya simu za mkononi mionganoni mwa Nchi Wanachama; kuanzisha Kituo cha Kukabiliana na Uhalifu wa Kimtandao; na kuwianisha sheria, kanuni na viwango vinavyohusu masuala ya usimamizi na udhibiti wa uzito wa magari katika ukanda wa SADC.

Nchi za Ukanda wa Maziwa Makuu

208. *Mheshimiwa Spika*, katika kutekeleza Itifaki ya Kupambana na Unyanyasaji wa Kijinsia Dhidi ya Wanawake na Watoto ya Nchi za Ukanda wa Maziwa Makuu (International Conference on the Great Lakes Region - ICGLR), mwezi Septemba 2019, Wizara iliratibu mafunzo ya kuzijengea uwezo Taasisi za Afya, Sheria na Jeshi la Polisi za Tanzania yaliyofanyika jijini Dar es Salaam. Mafunzo hayo, yalilenga kuziongezea Taasisi hizo ujuzi wa kukabiliana na ukatili na unyanyasaji wa kijinsia kwa kuandaa wakufunzi watakaokuwa chachu ya kutoa elimu kwenye Taasisi zao na jamii kwa ujumla.

209. *Mheshimiwa Spika*, mwezi Oktoba 2019, Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa Kamati ya Mawaziri wa Mambo ya Nje wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Nchi za Ukanda wa Maziwa Makuu uliofanyika Brazzaville, Jamhuri ya Kongo. Katika Mkutano huo, pamoja na masuala mengine, Mkutano uliridhia pendekazo la Tanzania la kutaka Kiswahili kuanza kutumika katika mikutano na shughuli nyingine za Jumuiya hiyo na kuagiza suala hilo liwasilishwe katika kikao kijacho cha Wakuu wa Nchi na Serikali wa ICGLR kwa maamuzi.

210. *Mheshimiwa Spika*, mwezi Februari 2020, Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa uwekezaji katika sekta ya madini wa nchi za Ukanda wa Maziwa Makuu uliofanyika jijini Dar es Salaam. Katika mkutano huo, Tanzania ilizindua rasmi

Hati ya Uhalisia wa Madini kwa lengo la kudhibiti uvunaji na usafirishaji holela wa madini nje ya nchi kulingana na miongozo na taratibu za ICGLR. Aidha, Tanzania ilitumia mkutano huo kutangaza fursa zilizopo katika sekta ya madini.

Jumuiya ya Nchi za Ukanda wa Bahari ya Hindi (IORA)

211. Mheshimiwa Spika, mwezi Novemba 2019, Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa 19 wa Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Nchi za Ukanda wa Bahari ya Hindi (IORA) uliofanyika Abu Dhabi, Umoja wa Falme za Kiarabu. Mkutano huo, uliridhia maombi ya Tanzania ya kujiunga katika makundi manne kati ya tisa yaliyopo kwenye mpango kazi wa IORA ambayo ni ulinzi na usalama wa bahari; biashara na uwekezaji; usimamizi wa uvuvi; pamoja na utalii na kubadilishana utamaduni. Aidha, Mkutano ulikubali Taasisi ya *Western Indian Ocean Marine Science Association (WIOMSA)* ya Tanzania kupewa hadhi ya uanganizzi katika IORA.

Umoja wa Afrika (AU)

212. Mheshimiwa Spika, Wizara iliandaa na kushiriki katika mikutano na shughuli mbalimbali za Umoja wa Afrika kwa lengo la kuunga mkono dhana ya umajumui na harakati za ukombozi wa kisiasa, kiuchumi na kijamii wa Bara la Afrika kama ifuatavyo:

213. Mheshimiwa Spika, mwezi Julai 2019, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania kwenye Mkutano wa 12 wa Dharura wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika kuhusu Eneo Huru la Biashara Afrika (AfCFTA) uliofanyika jijini Niamey, Niger. Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alimwakilisha Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika mkutano huo. Pamoja na masuala mengine, Mkutano huo ulizindua mifumo itakayosaidia utekelezaji wa Mkataba huo.

214. Mheshimiwa Spika, mifumo hiyo ni: mfumo wa kutoa taarifa, ufuatiliaji na uondoshaji wa vikwazo vyta kibiashara

visivyo vya kiushuru; mfumo wa kuhifadhi takwimu za biashara wa Afrika; mfumo wa kimtandao wa kubadilishana taarifa, kujadili mapendekezo juu ya ufunguzi wa biashara ya bidhaa; na mfumo wa kimtandao katika tovuti na programu kwa ajili ya taarifa za kibiashara katika Eneo Huru la Biashara la Afrika.

215. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Mkataba wa Eneo Huru la Biashara la Bara la Afrika, mwezi Oktoba 2019, Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa Kwanza wa Mawaziri kutoka Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika wanaosimamia biashara uliofanyika jijini Addis Ababa, Ethiopia. Mkutano huo ulipitisha kanuni zitakazoongoza Baraza la Mawaziri la AfCFTA na kuielekeza Kamisheni ya Umoja wa Afrika kushirikiana na Serikali ya Ghana katika kuanzisha Sekretarieti ya kudumu ya AfCFTA.

216. Mheshimiwa Spika, mwezi Februari 2020, Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa 33 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika uliofanyika jijini Addis Ababa, Ethiopia. Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alimwakilisha Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika mkutano huo. Mkutano ulipokea taarifa ya mwaka ya Hali ya Amani na Usalama na Utekelezaji wa Mkakati wa Kusitisha Matumizi ya Silaha Barani Afrika pamoja na hatua zilizochukuliwa kukabiliana na migogoro katika nchi za Sudan, Sudan Kusini, Libya, Eneo la Sahel na Pembe ya Afrika.

217. Mheshimiwa Spika, katika Mkutano huo, suala la ugaidi lilitajwa kuwa tishio Barani Afrika hususan eneo la ukanda wa Sahel; Pembe ya Afrika; na Bonde la Mto Chad. Aidha, ilielezwa kuwa mabadiliko ya tabianchi ni tishio lingine la usalama kutowana na mvua kubwa, ukame na vimbunga vinavyosababisha vifo, uharibifu wa miundombinu, mali na njaa. Aidha, Mkutano ulisisitiza umuhimu wa kuwa na jeshi la Afrika litakalopambana na ugaidi pamoja na umuhimu wa nchi za Afrika kushirikiana katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi. Vilevile, mkutano ulilaani mataifa ya kigeni yanayoingilia mambo ya ndani ya Afrika na

ukiukwaji wa zolio la kuingiza silaha na kutahadharisha kuwa adhabu itatolewa kwa wale wote wanaokiuka zolio hilo.

218. Mheshimiwa Spika, Mkutano huo pia ulipokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa Ajenda ya Afrika ya mwaka 2063 kwa Nchi Wanachama. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa katika taarifa hiyo, Tanzania ilitajwa kuwa miongoni mwa Nchi Wanachama zilizofanya vizuri, hususan katika maeneo ya utoaji wa huduma za nishati ya umeme, maji safi na salama, utekelezaji wa sera ya viwanda katika kuinua uchumi wa Taifa na ushiriki katika ulinzi wa amani duniani.

219. Mheshimiwa Spika, katika Mkutano huo Mheshimiwa Cyril Matamela Ramaphosa, Rais wa Jamhuri ya Afrika Kusini alichaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika kwa kipindi cha kuanzia Februari 2020 hadi Februari 2021. Vilevile, Bw. Wamkele Mene kutoka Afrika Kusini alipitishwa kuwa Katibu Mkuu wa kwanza wa Sekretarieti ya Eneo Huru la Biashara la Afrika.

220. Mheshimiwa Spika, Mkutano huo ulipitisha Azimio la kuzitaka Marekani na baadhi ya Nchi Wanachama za Jumuiya ya Ulaya kuiondolea nchi ya Zimbabwe vikwazo vya kiuchumi vya muda mrefu.

Ushirikiano wa Ubia Kati ya Tanzania na Nchi Nyingine

221. Mheshimiwa Spika, mwezi Agosti 2019, Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa Saba wa Kimataifa wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Tokyo kuhusu Maendeleo ya Afrika (TICAD VII) uliofanyika jijini Yokohama, Japan. Katika Mkutano huo, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alimwakilisha Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Wakati wa Mkutano huo, Serikali ya Japan ilitangaza kutenga Dola za Marekani bilioni 20 kwa ajili ya utekelezaji wa maeneo ya ushirikiano na nchi za Afrika kwa kipindi cha miaka mitatu (2019-2021). Tanzania iliwasilisha miradi 11 kwa Serikali ya Japan kwa ajili ya

kuiombea fedha za utekelezaji. Miradi hiyo imejikita katika sekta za nishati, kilimo, ujenzi wa maeneo maalum ya viwanda na mafunzo ya kuwajengea uwezo wataalam wetu katika sekta hizo.

222. *Mheshimiwa Spika*, Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa Kwanza wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Afrika na Urusi uliofanyika mwezi Oktoba 2019 jijini Sochi, Urusi. Katika Mkutano huo, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alimwakilisha Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mkutano huo, uliotanguliwa na kongamano la uchumi na biashara uliazimia kufufua na kuimarisha ushirikiano katika sekta za elimu, afya, ulinzi na usalama, nishati na matumizi salama ya nyuklia, mlundombinu ya kisasa na kujenga uwezo kupitia uhawillshaji wa teknolojia ya kisasa.

223. *Mheshimiwa Spika*, katika hotuba yake, Mheshimiwa Waziri Mkuu alieleza fursa za biashara na uwekezaji zilizopo hapa nchini, vivutio vyta utalii pamoja na jitihada za Serikali katika kuweka mazingira rafiki ya kufanya biashara na uwekezaji. Hotuba hiyo ilionekana kumvutia sana Mheshimiwa Vladimir Putin, Rais wa Shirikisho la Urusi. Aidha, wakati wa ziara hiyo, Mheshimiwa Waziri Mkuu alikutana na kufanya mazungumzo na Kampuni nane za nchini humo zinazojishughulisha na utengenezaji wa vifaa vyta treni, kilimo na mitambo ya kufua umeme; utafutaji na uchakataji wa gesi na mafuta; na ujenzi wa barabara.

224. *Mheshimiwa Spika*, katika mazungumzo yake, Mheshimiwa Waziri Mkuu alizihakikishia Kampuni hizo uwepo wa mazingira mazuri ya uwekezaji, masoko na utayari wa Serikali kutoa ushirikiano kuja kuwekeza hapa nchini. Kampuni hizo zimeonesha nia ya kuja kuwekeza na kuanzisha ubia na Kampuni za hapa nchini na Kampuni tatu kati ya hizo tayari zimeanza majadiliano na Wizara za kisekta ili kukamilisha taratibu za uwekezaji huo.

225. Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza kwenye sehemu ya mafanikio ya Wizara, mwezi Novemba 2019, kwa mara ya kwanza nchi yetu ilikuwa mwenyeji wa Mkutano wa Mawaziri wa Mambo ya Nje wa Nchi za Afrika na Nordic uliofanyika jijini Dar es Salaam. Mkutano huo uliofanyika kwa mafanikio makubwa ulifunguliwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

226. Mheshimiwa Spika, Mkutano huo, ulijadili masuala ya ushirikiano na kuainisha vipaumbele na mikakati ya ushirikiano kwenye sekta ya biashara na uwekezaji. Aidha, Tanzania ilipata fursa ya kueleza jitihada za Serikali ya Awamu ya Tano katika kupambana na rushwa; udhibiti wa uchafuzi wa mazingira; pamoja na uboreshaji wa mazingira ya biashara na uwekezaji. Vilevile, Tanzania ilitumia uenyeji wa Mkutano huo kutangaza fursa za biashara, uwekezaji na utalii zilizopo nchini.

227. Mheshimiwa Spika, mwezi Desemba 2019, nilimwakilisha Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mkutano wa Tisa wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Nchi Wanachama wa Kundi la Afrika, Karibeani na Pasifikasi (ACP) ambayo sasa inafahamika kama OACPS uliofanyika jijini Nairobi, Kenya. Katika Mkutano huo, Tanzania ilifanikiwa kuzishawishi Nchi Wanachama kukubaliana na masuala yafuatayo:

- i) Kujumuisha zao la korosho kwenye orodha ya mazao ya kimkakati ndani ya ACP ambayo yatanufaika na Programu ya Mnyororo wa Thamani wa ACP. Programu hii, iliyotengewa kiasi cha Euro milioni 140 itatoa fursa kwa wakulima kupata mikopo kwa ajili ya kuongeza uzalishaji, kuongeza thamani ya bidhaa za kilimo na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi;
- ii) Kufanya maboresho muhimu katika Mkataba wa Georgetown ulioanzisha Kundi hilo kwa kuondoa vifungu visivyokuwa na maslahi kwa Tanzania na ACP kwa ujumla;

- iii) Kujumuisha suala la kuondolewa vikwazo vya kiuchumi kwa nchi ya Zimbabwe kwenye Azimio la Nairobi na hivyo kuongeza msukumo na mshikamano wa kimataifa katika kusukuma mbele wito wa SADC;
- iv) Kuandaa vigezo mahsus, mwongozo na kanuni za kuongoza majadiliano ya kisiasa kati ya nchi za ACP na Umoja wa Ulaya; na
- v) ACP kufanya maridhiano na Umoja wa Ulaya kwa kuzingatia hoja za msingi za nchi za ACP katika maeneo tata ambayo ni kikwazo kwa baadhi ya nchi ikiwemo Tanzania.

228. Mheshimiwa Spika, mwezi Januari 2020, Wizara iliratibu Maadhimisho ya Miaka 40 ya Umoja wa Posta Afrika (PAPU) yaliyofanyika Makao Makuu ya Umoja huo jijini Arusha. Maadhimisho hayo, yalihusisha uwekaji wa jiwe la msingi la ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya PAPU litakalomilikiwa kwa pamoja na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania. Uwepo wa Makao Makuu ya PAPU hapa nchini unatoa fursa za ajira kwa Watanzania; na kuwa mwenyeji wa mikutano ya umoja huo nchini pamoja na mafunzo kwa wataalam wa Tanzania ili kuimarisha utoaji wa huduma za posta.

Ushirikiano wa Kimataifa

229. Mheshimiwa Spika, mwezi Septemba 2019, Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa 63 wa Shirika la Nguvu za Atomiki Duniani (IAEA) uliofanyika jijini Vienna, Austria. Pamoja na masuala mengine, Mkutano huo ulijadili usalama wa matumizi ya mionzi ya nyuklia na ushirikiano wa kiteknolojia katika sekta mbalimbali ikiwemo afya na kilimo. Ili kuhakikisha Tanzania inanufaika na teknolojia ya nyuklia katika sekta hizo, ujumbe wa Tanzania ulifanya vikao na uongozi pamoja na wataalam wa shirika hilo pembezoni mwa Mkutano huo. Miongoni mwa masuala yaliyojadiliwa katika vikao hivyo ni pamoja na hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa miradi mbalimbali nchini inayotumia sayansi na teknolojia ya nyuklia katika sekta za afya, kilimo, maji na mifugo.

230. Mheshimiwa Spika, ujumbe wa Tanzania uliufahamisha Uongozi wa IAEA mpango wa Serikali wa kuongeza vifaa vya uchunguzi na tiba katika Hospitali ya Mnazi Mmoja – Zanzibar, Hospitali ya KCMC- Kilimanjaro na Hospitali ya Rufaa Mbeya, ili kuongeza wigo wa utoaji huduma ya uchunguzi na tiba ya maradhi ya saratani nchini. Aidha, ujumbe ulielezea azma ya Serikali ya kujenga jengo la maabara ya utafiti wa nyuklia na *Multipurpose Radiator* katika Chuo Kikuu cha Nelson Mandela kwa lengo la kupatiwa msaada wa vifaa na kujengewa uwezo wataalam wetu. Utekelezaji wa miradi hiyo unalenga kuzalisha *radioisotopes, radiopharmaceuticals* na kuhifadhi nafaka na vyakula vinavyozalishwa nchini kwa njia ya *irradiation*. Uongozi wa IAEA uliahidi kuendelea kushirikiana na Tanzania kwa kutoa vifaa na kuwajengea uwezo wataalam wetu.

231. Mheshimiwa Spika, Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano Mkuu wa 40 wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni uliofanyika Paris, Ufaransa mwezi Novemba 2019. Katika Mkutano huo, Tanzania iliungana na nchi nyingine kusisitiza matumizi sahihi ya teknolojia na kuimarisha ushirikiano baina ya Nchi Wanachama kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu. Sanjari na Mkutano huo, kulifanyika Jukwaa la Mawaziri wa Utamaduni ambapo Tanzania ilieleza jitihada za Serikali katika kutunza urithi unaoshikika na usioshikika; kuimarisha biashara kwenye bidhaa za kiutamaduni; kukuza viwanda vinavyotokana na ubunifu wa kiutamaduni; na kuheshimu uwepo wa tamaduni mbalimbali katika jamii.

232. Mheshimiwa Spika, juhudu zinazofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano katika kukuza matumizi ya lugha ya Kiswahili hazikuishia tu kwenye Ukanda wa Kusini mwa Afrika (SADC Region). Wizara yangu kupitia Ubalozi na Uwakilishi wetu wa Kudumu katika Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) mijini Paris, Ufaransa, umeanza mazungumzo na Shirika hilo ili lugha ya Kiswahili iweze kutambuliwa rasmi na kuwa mionganoni mwa lugha za kimataifa zinazotumiwa na Shirika hilo. Juhudi hizo zimeanza kuzaa matunda na tarehe 21 Februari 2020, wakati wa

kusheherekea Siku ya Kimataifa ya Lugha Mama (International Mother Language Day), UNESCO kwa kushirikiana na Ubalozi na Uwakilishi wetu wa kudumu Paris, Ufaransa kwa mara ya kwanza katika historia ya kuanzishwa kwa shirika hilo, iliweza kuandaa warsha kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili na kuwaalika wataalam wa lugha kutoka Vyuo Vikuu mbalimbali kikiwemo Chuo Kikuu cha Dar es salaam. Hii ni mmoja ya hatua za mwanzo na nzuri katika kukipeleka Kiswahili katika Shirika hilo, na Wizara yangu inaahidi kuendelea na juhudi hizo.

233. Mheshimiwa Spika, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania kwenye Mkutano wa Tatu wa Dharura wa Umoja wa Posta Duniani uliofanyika Geneva, Uswisi mwezi Septemba 2019. Lengo la Mkutano huo lilikuwa kujadili mapendekezo ya mfumo wa malipo ya ada kwa huduma za posta kufuatia malalamiko ya Marekani kuwa mfumo unaotumika unaisababishia hasara. Katika mukutano huo, Nchi Wanachama zilikubaliana kurekebisha viwango vya ada ya kusafirisha barua, vifurushi na vipeto vinavyozingatia maslahi ya nchi zote.

234. Mheshimiwa Spika, Wizara iliratibu ziara ya kikazi ya ujumbe wa Timu Maalumu ya Umoja wa Mataifa iliyofanyika nchini mwezi Julai 2019. Lengo la ziara hiyo, lilikuwa ni kukusanya maoni kwa ajili ya kufanya tathmini ya hali ya usalama nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na kubaini mahitaji halisi ya Misheni ya Umoja wa Mataifa ya Ulinzi wa Amani (MONUSCO).

235. Mheshimiwa Spika, ziara hiyo ni sehemu ya utekelezaji wa Azimio Na. 2463 (2019) la Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa linalomtaka Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa kufanya mapitio ya muundo na majukumu ya MONUSCO kwa lengo la kuongeza ufanisi wa utendaji wake. Taarifa ya ziara hiyo ilitumiwa na Umoja wa Mataifa kuongeza muda kwa MONUSCO kuendelea kuimarisha usalama katika eneo la Maziwa Makuu. Tanzania ilishiriki kikamilifu kwenye ziara hiyo kwa kuwa ni mdau muhimu katika misheni ya kulinda amani nchini DRC.

Kufuatilia na Kusimamia Utekelezaji wa Mikataba iliyosainiwa

236. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka 2019/2020, Wizara iliratibu na kushiriki katika majadiliano na kusimamia uwekwaji wa saini wa Mikataba na Hati za Makubaliano zifuatazo:

- a) Hati ya Makubaliano ya Ushirikiano kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Zimbabwe katika Ukuzaji wa Biashara Ndogo na za Kat i liyosainiwa mwezi Julai 2019 jijini Harare, Zimbabwe;
- b) Hati ya Makubaliano kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Zimbabwe katika masuala ya Uchumi, Biashara na Uwekezaji iliyosainiwa mwezi Julai 2019 jijini Harare, Zimbabwe;
- c) Hati ya Makubaliano ya Ushirikiano kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Zimbabwe katika masuala ya Wanawake, Jinsia na Maendeleo ya Jamii iliyosainiwa mwezi Julai 2019 jijini Harare, Zimbabwe;
- d) Hati ya Makubaliano ya Ushirikiano kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Zimbabwe katika masuala ya Mashauriano ya Kidiplomasia iliyosainiwa mwezi Julai 2019 jijini Harare, Zimbabwe;
- e) Hati ya Makubaliano ya Ushirikiano kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Zimbabwe katika sekta ya Utalii iliyosainiwa mwezi Julai 2019 jijini Harare, Zimbabwe;
- f) Hati ya Makubaliano ya Ushirikiano kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Uganda katika sekta ya Kilimo iliyosainiwa mwezi Septemba 2019 jijini Dar es Salaam;
- g) Hati ya Makubaliano ya Ushirikiano kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Uganda katika

masuala ya Magereza iliyosainiwa mwezi Septemba 2019 jijini
Dar es Salaam;

h) Hati ya Makubaliano ya Ushirikiano kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Uganda katika masuala ya Uhamiaji iliyosainiwa mwezi Septemba 2019 jijini
Dar es Salaam;

i) Hati ya Makubaliano kati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mfuko wa Maendeleo wa Abu Dhabi kuhusu msaada wa matengenezo na upanuaji wa Hospitali ya Wete, Pemba iliyosainiwa mwezi Septemba 2019 Abu Dhabi; na

j) Mkataba wa Ushirikiano kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Rwanda katika Sekta ya Usafiri wa Anga uliosainiwa mwezi Desemba 2019 Aqaba, Jordan;

k) Mkataba wa Ushirikiano kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Mauritius katika Sekta ya Usafiri wa Anga uliosainiwa mwezi Desemba 2019 Aqaba, Jordan;

l) Hati ya Makubaliano ya Ushirikiano kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Namibia katika sekta ya Utalii iliyosainiwa mwezi Desemba 2019 jijini Dar es Salaam;

m) Hati ya Makubaliano ya Ushirikiano kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Namibia katika masuala ya Utamaduni iliyosainiwa mwezi Desemba 2019 jijini Dar es Salaam;

n) Hati ya Makubaliano ya Ushirikiano kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Namibia katika maendeleo ya Vijana iliyosainiwa mwezi Desemba 2019 jijini Dar es Salaam; na

o) Mkataba wa Ushirikiano wa kitaalam kati ya Hospitali ya Benjamin Mkapa na Wizara ya Afya ya Serikali ya Watu wa Cuba kuhusu kuwaleta madaktari bingwa nchini uliosainiwa mwezi Januari 2020 Jijini Dodoma.

237. *Mheshimiwa Spika*, Mikataba na Hati hizo za Makubaliano zilizosainiwa zinalenga kuimarisha ushirikiano uliopo kati ya Tanzania na nchi marafiki pamoja na Jumuiya za Kikanda na Kimataifa. Tanzania itanufaika na fursa zilizopo katika maeneo yaliyolengwa katika mikataba pamoja na makubaliano hayo.

Kuratibu Mikutano ya Tume za Pamoja za Kudumu za Ushirikiano na Kufuatilia Utekelezaji wa Makubaliano

238. *Mheshimiwa Spika*, mikutano ya Tume za Pamoja za Kudumu za Ushirikiano ni kiungo muhimu katika kuimarisha uhusiano na ushirikiano kati ya nchi yetu na nchi marafiki. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu juu ya mikutano ya Tume za Pamoja za Kudumu za Ushirikiano iliyofanyika kama ifuatavyo:

Zimbabwe

239. *Mheshimiwa Spika*, mwezi Julai 2019, Wizara iliratibu na kushiriki Mkutano wa Nane wa Tume ya Pamoja ya Kudumu ya Ushirikiano kati ya Tanzania na Zimbabwe uliofanyika Harare, Zimbabwe. Katika Mkutano huo, Tanzania na Zimbabwe zilikubaliana kuimarisha ushirikiano katika masuala ya viwanda, biashara, uwekezaji, fedha, madini, uchukuzi, kilimo, mazingira na utalii. Aidha, Hati tano za Makubaliano ya Ushirikiano zilisainiwa kuhusu mashauriano ya kidiplomasia; utalii; ukuzaji wa biashara ndogo na za kati; viwanda na biashara; wanawake, jinsia na maendeleo ya jamii.

Uganda

240. *Mheshimiwa Spika*, Wizara iliratibu na kushiriki Mkutano wa Tatu wa Tume ya Pamoja ya Kudumu ya Ushirikiano kati ya Tanzania na Uganda uliofanyika mwezi Septemba 2019 jjini Dar es Salaam. Katika Mkutano huo, Tanzania na Uganda zilikubaliana kuimarisha ushirikiano katika masuala ya biashara, uchukuzi, kilimo, nishati, ulinzi na usalama. Aidha, wakati wa Mkutano huo Tanzania na Uganda zilisaini hati tatu za makubaliano ya ushirikiano katika masuala ya kilimo, magereza na uhamiaji.

Namibia

241. Mheshimiwa Spika, Wizara iliratibu na kushiriki Mkutano wa Pili wa Tume ya Pamoja ya Kudumu ya Ushirikiano kati ya Tanzania na Namibia uliofanyika mwezi Desemba 2019 jijini Dar es Salaam. Katika Mkutano huo, Tanzania na Namibia zilikubaliana kuimarisha ushirikiano katika masuala ya mifugo, uvuvi, elimu, kilimo, biashara, utalii, utamaduni na vijana. Hati za makubaliano ya ushirikiano zilizosainiwa kwenye Mkutano huo ni katika masuala ya utalii, utamaduni na maendeleo ya vijana.

Masuala ya Diplomasia, Itifaki, Uwakilishi na Huduma za Kikonseli

Kuratibu Ziara za Viongozi Wakuu wa Kitaifa Nje ya Nchi

242. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuandaa na kuratibu ziara mbalimbali za Viongozi Wakuu wa Kitaifa nje ya nchi kama ifuatavyo:

- a) Ziara ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Zambia wakati wa uzinduzi wa Kituo cha Kutoa Huduma kwa Pamoja Mpakani Tunduma/Nakonde mwezi Oktoba 2019;
- b) Ziara ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Niger akimwakilisha Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania katika Mkutano wa Wakuu wa Nchi wa Umoja wa Afrika, mwezi Agosti 2019;
- c) Ziara ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Botswana akimwakilisha Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania katika Sherehe za kuapishwa Rais wa Botswana, Mheshimiwa Dkt. Mokgweetsi E. K. Masisi, zilizofanyika mwezi Novemba 2019;

- d) Ziara ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Ethiopia akimwakilisha Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania katika Mkutano wa 33 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika, mwezi Februari 2020;
- e) Ziara ya Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) mwezi Septemba 2019;
- f) Ziara ya Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Rwanda akimwakilisha Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania katika Maadhimisho ya Ukombozi wa Rwanda mwezi Julai 2019;
- g) Ziara ya Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Misri mwezi Julai 2019;
- h) Ziara ya Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Japan akimwakilisha Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania katika Mkutano wa *Tokyo International Conference on African Development* (TICAD VII) mwezi Septemba 2019;
- i) Ziara ya Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Urusi akimwakilisha Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania katika Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Afrika na Urusi mwezi Oktoba 2019;
- j) Ziara ya Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Azerbaijan akimwakilisha Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania katika Mkutano wa Nchi Zisizofungamana na Upande Wowote mwezi Oktoba 2019; na

k) Ziara za Waheshimiwa Marais Wastaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenye mikutano mbalimbali nje ya nchi.

Kuratibu Ziara za Viongozi wa Kitaifa na Mashirika ya Kikanda na Kimataifa kutoka Nje ya Nchi

243. Mheshimiwa Spika, Wizara iliratibu ziara za Viongozi wa Mataifa mbalimbali na Mashirika ya Kimataifa waliokuja Tanzania kushiriki katika mikutano, makongamano na kutekeleza majukumu mbalimbali ya kitaifa kama ifuatavyo:

- a) Ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Uhuru Kenyatta, Rais wa Jamhuri ya Kenya mwezi Julai 2019;
- b) Ziara za kikazi za Mheshimiwa Yoweri Kaguta Museveni, Rais wa Jamhuri ya Uganda mwezi Julai 2019 na Septemba 2019;
- c) Ziara ya Kitaifa ya Mheshimiwa Cyril Ramaphosa, Rais wa Jamhuri ya Afrika Kusini mwezi Agosti 2019;
- d) Ziara za kikazi za Wakuu wa Nchi na Serikali na Wawakilishi pamoja na Wakuu wa Mashirika mbalimbali ya Kikanda na Kimataifa katika Mkutano wa 39 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa SADC mwezi Agosti 2019;
- e) Ziara ya Mheshimiwa Edgar Chagwa Lungu, Rais wa Jamhuri ya Zambia wakati wa Uzinduzi wa Kituo cha Kutoa Huduma kwa Pamoja Mpakani Tunduma/Nakonde mwezi Oktoba 2019; na
- f) Ziara za wajumbe maalum kutoka nchi mbalimbali kuja kuwasilisha ujumbe maalum kwa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kuanzisha na Kusimamia Huduma za Kikonseli

244. Mheshimiwa Spika, ili kunufaika ipasavyo na diplomasia ya uchumi, nchi yetu imeendelea kufungua balozi katika nchi mbalimbali. Katika mwaka wa fedha 2019/2020 Serikali imefungua Ubalozi mpya Windhoek nchini Namibia. Hatua hii imeiwezesha nchi yetu kufungua balozi mpya nane katika kipindi cha kwanza cha Serikali ya Awamu ya Tano chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Balozi nyingine zilizofunguliwa katika kipindi hicho zipo katika nchi za Algeria, Uturuki, Sudan, Korea Kusini, Israel, Qatar na Cuba. Kwa misingi hiyo, Tanzania ina jumla ya Balozi 43 na Konseli Kuu tatu zilizopo katika nchi mbalimbali duniani.

245. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kutoa huduma za kikonseli kama ifuatavyo:

- a) Kurahisisha upatikanaji wa viza kwa Maafisa na Watendaji wa Serikali, Viongozi wa Vyama vya Siasa, Waheshimiwa Wabunge na Taasisi nyingine zinazostahili huduma hiyo. Aidha, Balozi zetu zimeendelea kutoa viza kwa raia wa nje wanaoitembelea Tanzania;
- b) Kuratibu uwasilishaji wa Hati za Utambulisho kwa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutoka kwa Mabalozi wa nchi za Saharawi, India, Zimbabwe, Angola, Denmark, Finland, Rwanda, Umoja wa Ulaya, Ujerumani, Algeria, Singapore, Qatar, Ureno, Austria, Ufilipino, Jamaica, Venezuela, Israel, Ghana na Djibouti;
- c) Kupokea hati za utambulisho kutoka kwa Wakuu wa Mashirika na Taasisi za Umoja wa Mataifa ambao ni Mwakilishi Mkazi wa Umoja wa Mataifa (UNRC); Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Watoto (UNICEF); na Mwakilishi wa Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Wakimbizi (UNHCR);

- d) Kushirikiana na mamlaka nyingine kutafuta ufumbuzi wa changamoto mbalimbali zinazowakabili Watanzania waishio nje ya nchi; na
- e) Kutatua changamoto na kulinda maslahi ya Watanzania wanaofanya kazi kwenye Balozi mbalimbali na Mashirika ya Kimataifa hapa nchini.

Ushirikishwaji wa Watanzania wanaoishi ughaibuni

246. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuwashirikisha Watanzania wanaoishi ughaibuni (Diaspora) katika kuchangia maendeleo ya nchi yao. Mwezi Septemba 2019 Wizara iliratibu na kushiriki katika ziara ya kampuni ya AVZ Minerals kutoka Australia iliyofanyika jijini Dar es Salaam. Ziara hiyo ilitokana na jitihada za *Diaspora* wanaoishi nchini Australia za kuhamasisha wawekezaji kutoka nchini humo kuja kuwekeza nchini. Kampuni hiyo inayomiliki migodi ya madini ya *Lithium* iliyopo katika eneo la Manono nchini DRC inatarajia kutumia bandari ya Dar es Salaam kupitia reli ya TAZARA na Reli ya Kati (TRC) kusafirisha madini hayo nje ya nchi.

247. Mheshimiwa Spika, Wizara iliratibu na kushiriki katika ziara ya kampuni ya *Eco Systems International* ya Ireland iliyofanyika mwezi Oktoba 2019. Kampuni hiyo inayojishughulisha na utengenezaji wa vifaa vya kupunguza gesi ya ucaa hususan ile inayotokana na matumizi ya vyombo vya moto, imeonesha nia ya kuwekeza nchini. Ujio wa kampuni hiyo ni matokeo ya kongamano la *Diaspora* lilitoratibiwa na Wizara liliyofanyika mwezi Aprili 2019 nchini Sweden. Wizara kwa kushirikiana na sekta husika inaendelea kuchambua maombi ya kampuni hiyo kwa ajili ya kufanikisha uwekezaji huo.

248. Mheshimiwa Spika, Wizara iliratibu na kufanikisha ziara ya timu ya matabibu na wataalam wengine wa afya kutoka Jumuiya ya Watanzania wanaoishi nchini Uingereza ijlikanayo kama *The Tanzania - UK Healthcare Diaspora Association (TUHEDA)* iliyofanyika nchini mwezi Novembra

2019. Ujumbe huo ulitembelea hospitali ya Tumbi iliyopo Wilaya ya Kibaha, mkoani Pwani na kutoa msaada wa vitendea kazi ikiwa ni pamoja na sanamu ya vitendo vyenye thamani ya **Shilingi 100,000,000** na vitabu vyatayari sayansi ya afya vyenye thamani ya **Shilingi 30,000,000**.

249. Mheshimiwa Spika, Wizara iliratibu na kushiriki katika Kongamano la Sita la Watanzania wanaoishi nje ya nchi liliofanyika Zanzibar mwezi Desemba 2019. Kongamano hilo liliifunguliwa na Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na kushirikisha wajumbe wapatao 300 wakiwemo *Diaspora* kutoka nchi mbalimbali, viongozi wa Serikali na sekta binafsi. Kauli mbiu ya Kongamano hilo ilikuwa "Kuendeleza Ushirikiano Uliojengwa na *Diaspora* na Wawekezaji Kama Wadau wa Maendeleo Nchini".

250. Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea na hatua za kukusanya taarifa na kufanya uchambuzi kwa ajili ya kuandaa mwongozo wa kisera wa kuimarisha ushiriki wa Watanzania waishio ughaibuni katika mipango na utekelezaji wa miradi ya maendeleo hapa nchini. Hatua iliyofikiwa sasa ni uchambuzi wa masuala ya kisheria na kitaasisi, ushiriki wa sekta binafsi, pamoja na uwezo na utayari wa Watanzania hao kushiriki katika kuleta maendeleo ya nchi yao.

251. Mheshimiwa Spika, uchambuzi huo umebaini kuwa ukosefu wa takwimu za Watanzania waishio ughaibuni unailazimu Wizara kuendelea kuboresha kanzidata ya takwimu zitakazoonesha sifa na uwezo wao kwanza kabla ya kutunga Sera ili matamko ya Sera hiyo yawe yamezingatia uhalisia uliopo. Wakati Wizara inaendelea kuboresha kanzidata hiyo, masuala ya *Diaspora* yatajumuishwa kwenye rasimu ya Sera ya Mambo ya Nje.

Elimu kwa Umma

252. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu utekelezaji wa majukumu yake kwa kutumia njia mbalimbali ikiwemo kuandaa makala, majarida,

vipeperushi na mikutano na vyombo vya habari. Njia hizo zimewasaidia wadau kunufaika na fursa za masomo, ajira, masoko, uwekezaji, na utalii. Aidha, Wizara imeendelea kutoa elimu kwa umma juu ya fursa zitokanazo na Jumuiya ya Afrika Mashariki; Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika pamoja na jumuiya nyingine za Kikanda na Kimataifa.

253. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi hiki Wizara ilitoa mafunzo kwa waandishi wa habari 60 kuhusu namna ya kuripoti mikutano ya Kikanda na Kimataifa inayofanyika nchini na kutangaza vivutio vya utalii vilivyopo Tanzania kupitia diplomasia ya mikutano. Aidha, Wizara iliratibu ushiriki wa mabalozi wa Tanzania nje katika vipindi mbalimbali vya redio na televisheni kwa lengo la kuelezea namna wanavyotekeleza diplomasia ya uchumi.

Mpango Mkakati wa Wizara kwa Kipindi cha Mwaka 2020/2021- 2024/2025

254. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi hiki, Wizara imekamilisha Mpango Mkakati wa utekelezaji wa majukumu kwa kipindi cha Miaka Mitano (2020/2021- 2024/2025). Mpango huo umezingatia mabadiliko ya muundo wa Wizara pamoja na mabadiliko ya kiuchumi, kisiasa na kijamii yanayoendelea ndani na nje ya nchi.

Utawala na Maendeleo ya Watumishi

255. *Mheshimiwa Spika*, Wizara imeendelea kusimamia masuala ya utawala na maendeleo ya watumishi kwa lengo la kuimarisha utendaji wa kazi. Wizara ina jumla ya watumishi 439 wa kada mbalimbali. Kati ya watumishi hao, watumishi 338 wapo Makao Makuu ya Wizara na watumishi 101 wapo kwenye Balozi zetu nje. Katika kuimarisha utendaji kazi wa Wizara, masuala mbalimbali yanayohusu utawala na maendeleo ya watumishi yameendelea kusimamiwa kama ifuatavyo: -

Uteuzi wa Viongozi

256. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka 2019/2020 Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alimteua Balozi Kanali Wilbert Augustin Ibuge kuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Vilevile, Mheshimiwa Rais aliwateua Mabalozi 17 ambapo 14 kati yao wanaiwakilisha Tanzania katika nchi mbalimbali duniani na watatu ni Mabalozi wanaofanya shughuli zao hapa nchini. Naomba kutumia fursa hii kuwapongeza kwa uteuzi huo na kuwataka waendelee kuchapa kazi kwa bidii, uzalendo na weledi mkubwa.

Mafunzo

257. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2019/2020, Wizara imeendelea kuwajengea uwezo watumishi wake ambapo jumla ya watumishi 93 walihudhuria mafunzo ya muda mrefu na mfupi katika fani mbalimbali ndani na nje ya nchi. Watumishi waliohudhuria mafunzo ya muda mrefu ni 51 na mafunzo ya muda mfupi ni 42. Aidha, katika kipindi hiki, Wizara iliratibu upatikanaji wa nafasi 578 za mafunzo kutoka nchi marafiki 20, kati ya nafasi hizo mafunzo ya muda mfupi ni 225 na ya muda mrefu ni 134. Nafasi hizo zilitangazwa kwa umma wa Watanzania kupitia vyombo vyaya habari ili kunufaika na fursa hizo za mafunzo.

Upandishaji Vyeo Watumishi

258. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2019/2020, watumishi 19 walipandishwa vyeo kwa mserereko. Kati ya watumishi hao, watano walipandishwa kuwa Maafisa Mambo ya Nje Wakuu Daraja I na watumishi 14 walipandishwa kuwa Maafisa Mambo ya Nje Wakuu Daraja II.

Uhamisho

259. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2019/2020, watumishi 15 walihamishwa kwenda Wizara na Taasisi nyingine za Serikali na watumishi 26 walihamia Wizarani kutoka Wizara na Taasisi nyingine za Serikali kwa lengo la kuboresha utendaji kazi katika Utumishi wa Umma. Aidha, watumishi 35 walirejeshwa kutoka balozi mbalimbali za Tanzania nje ya nchi baada ya kumaliza muda wao wa utumishi ubalozini. Hadi sasa watumishi 20 wamepelekwa Balozini kwa lengo la

kuimarisha utendaji. Wizara inaendelea na taratibu za kuwapeleka watumishi zaidi katika Balozi zetu.

Umiliki wa majengo

260. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kujenga na kukarabati majengo yake ikiwa ni utekelezaji wa Mpango wa Miaka 15 (2017/2018- 2031/2032) wa Ujenzi, Ununuzi na Ukarabati wa Majengo ya Ofisi na Makazi ya Watumishi Balozini. Serikali ya Awamu ya Tano inaendelea kutekeleza mpango huo kwa kukarabati majengo ya Balozi za Tanzania nje ikiwemo ukarabati wa Jengo lenye Ghorofa tisa kwenye Ubalozi wetu jijini Maputo kwa ajili ya Ofisi na Makazi ya Watumishi wa Ubalozi. Kwa sasa Tanzania inamiliki majengo 106 pamoja na viwanja 12.

Kuratibu na Kusimamia Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Wizara na Taasisi zilizo Chini ya Wizara

Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Wizara

261. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/2020, Wizara ilipangiwa bajeti ya maendeleo ya Shilingi **4,000,000,000** kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo iliyopo ndani na nje ya nchi.

262. Mheshimiwa Spika, hadi kufikia tarehe 30 Aprili 2020, Wizara imepokea kiasi cha **Shilingi 487,905,996.40** kutoka Wizara ya Fedha na Mipango sawa na asilimia 12.2 ya fedha zilizoidhinishwa. Tayari ukarabati wa makazi ya Balozi wa Tanzania Ottawa nchini Canada umeanza ambao utagharimu **Shilingi 150,000,000.00**. Vilevile, **Shilingi 337,905,996.40** zinatumika katika ujenzi wa vyumba vya madarasa unaoendelea kwenye Chuo cha Diplomasia.

Utekelezaji wa Majukumu ya Taasisi zilizo chini ya Wizara

263. Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki, Wizara imeendelea kuzisimamia taasisi za Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha (AICC); Chuo cha Diplomasia (CFR); na Mpango wa

Kujitathmini Kiutawala Bora Barani Afrika (APRM) katika kutekeleza majukumu yao kama ifuatavyo:

Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha (AICC)

264. Mheshimiwa Spika, Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha kinaendesha biashara ya kumbi za mikutano; na upangishaji wa ofisi na nyumba za makazi. Aidha, kituo kinatoa huduma ya afya kupitia hospitali yake iliyopo jijini Arusha. Kituo hicho kinajiendesha kwa faida na kinatoa gawio kwa Serikali kwa mujibu wa maelekezo ya Msajili wa Hazina.

265. Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia sheria ilioanzisha Kituo, AICC inatekeleza majukumu yake kwa kuongozwa na Mpango Mkakati wa Miaka Mitano (2017/18-2021/2022). Mpango huo unaainisha dira na dhima ya Kituo hususan katika kuitangaza nchi yetu katika nyanja ya utalii wa mikutano na matukio (business tourism) ambayo inajullikana kama ''MICE'' (Meetings, Incentive travel, Conferences, Exhibition/Events).

266. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020, Kituo kimepanga kukusanya mapato ya **Shilingi 16,313,716,937.00**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 15,603,468,044.00** ni kutoka vyanzo mbalimbali vya ndani na **Shilingi 710,248,893.00** zitatokana na mkopo.

267. Mheshimiwa Spika, hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2020 Kituo kimekusanya mapato ya **Shilingi 11,815,516,916** sawa na asilimia **72** ya lengo la mwaka. Mapato hayo yalitokana na:

a) Huduma za kumbi za mikutano (AICC na JNICC) **Shilingi 4,986,883,072** sawa na **asilimia 123** ya lengo la **Shilingi 4,047,496,666**;

b) Upangishaji wa ofisi na nyumba za kuishi **Shilingi 3,514,566,238** sawa na **asilimia 108** ya lengo la **Shilingi 3,264,037,760**; na

c) Huduma za hospitali **Shilingi 3,314,067,603** sawa na **asilimia 107** ya lengo la **Shilingi 3,090,777,602**.

268. Mheshimiwa Spika, vilevile katika kipindi cha 2019/2020, Kituo kilitoa **Shilingi 200,000,000** kama gawio la awali kwa Serikali. Pia, katika kipindi husika hadi tarehe 30 Aprili 2020, Kituo kilifanikiwa kutekeleza yafuatayo: -

- i) Kuhudumia mikutano 144 ya Kitaifa na 24 ya Kimataifa ambayo ililetwa washiriki 52,359 wa Kitaifa na 11,174 wa Kimataifa na kutoa huduma mbalimbali za afya kwa wagonja wapatao 80,190;
- ii) Kuweka matangazo ya vivutio mbalimbali nya utalii kwenye Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha na Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere kwa kushirikiana na Shirika la Hifadhi la Taifa, Bodi ya Utalii Tanzania, Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro;
- iii) Kufanya matengenezo makubwa ya Kituo cha JNICC na AICC (Ukumbi wa Simba);
- iv) Kuhuishwa mifumo ya kielektroniki na kimenejimenti ya usimamizi wa taarifa katika nyanja za uhasibu, miliki na uendeshaji wa hospitali;
- v) Kukamilisha rasimu ya usanifu wa michoro ya mradi mkubwa wa *Mount Kilimanjaro International Convention Centre* (MK-ICC);
- vi) Kukarabati majengo mawili yaliyopo viwanja Na. 46 na 47 *Old Moshi Road*; na
- vii) Kukarabati mtaro mkubwa wa maji katika miliki ya Kaloleni. Ukarabati huu utazuia mafuriko yaliyokuwa yakiingia kwenye baadhi ya nyumba za makazi.

Chuo cha Diplomasia

269. Mheshimiwa Spika, majukumu ya Chuo ni kutoa mafunzo na kufanya tafiti katika masuala ya diplomasia; uhusiano wa kimataifa; stratejia na usuluhishi wa migogoro; na ujenzi wa

amani. Lengo ni kukifanya Chuo kuwa Taasisi iliyobobea katika elimu ya juu na ushauri katika nyanja hizo.

270. Mheshimiwa Spika, Chuo kimeanza kutoa mafunzo ya lugha ya Bahasa (Indonesia) baada ya kusaini makubaliano na Ubalozi wa Indonesia mwezi Agosti 2019. Kuanza kwa mafunzo hayo kumeongeza idadi ya lugha za kigeni zinazofundishwa kufikia nane. Lugha nyingine zinazofundishwa ni Kiarabu, Kifaransa, Kihispania, Kiingereza, Kichina, Kikorea na Kireno. Aidha, Chuo kipo katika hatua za mwisho za kukamilisha mtaala wa mafunzo ya lugha ya Kiswahili kwa wageni.

271. Mheshimiwa Spika, vilevile, Chuo kimefanikiwa kuongeza udahili wa wanafunzi katika ngazi mbalimbali kwa mwaka wa masomo 2019/2020 kutoka wanafunzi 1,029 mwaka 2018/2019 hadi wanafunzi 1,280 mwaka 2019/2020 sawa na ongezeko la **asilimia 24**.

272. Mheshimiwa Spika, vilevile Chuo kimekuwa na utaratibu wa kuwajengea uwezo watumishi wake kwa kuwagharamia kwenye mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu katika fani mbalimbali kulingana na uhitaji na umuhimu. Hadi kufikia mwezi Desemba 2019 mtumishi mmoja wa ngazi ya shahada ya uzamivu alihitim masomo yake na kuongeza idadi ya wahitim katika ngazi hiyo kufikia saba; na watumishi wanne wa shahada ya uzamili walihitim masomo yao na kufanya idadi ya wahitim wa ngazi hiyo kufikia 44.

273. Mheshimiwa Spika, Mkataba wa mradi wa ujenzi wa vyumba vyaya madarasa ulisainiwa kati ya Chuo na mkandarasi *Ms. Casco Construction Limited* na utekelezaji ulianza rasmi tarehe 16 Desemba, 2019. Mradi huu utagharimu kiasi cha **Shilingi 3,937,247,328.00** ambapo hadi kufikia tarehe 30 Aprili 2020 Chuo kilipokea kiasi cha **Shilingi 337,905,996.40** na kumlipa mkandarasi malipo ya awali kwa ajili ya kuanza utekelezaji.

274. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/2020, Chuo kiliidhinishiwa **Shilingi 4,507,986,000**. Kati ya fedha hizo,

Shilingi 2,507,986,000 kwa ajili ya Mishahara, **Shilingi 1,000,000,000** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na **Shilingi 1,000,000,000** kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Aidha, Chuo kilikadiria kukusanya kiasi cha **Shilingi 1,545,001,530** kutoka kwenye vyanzo vyake nya ndani.

275. Mheshimiwa Spika, hadi kufikia tarehe 30 Aprili 2020, Chuo kilipokea Shilingi 2,641,642,486 kutoka Wizara ya Fedha na Mipango. Kati ya fedha hizo, Shilingi 1,637,072,490 ni kwa ajili ya mishahara, Shilingi 666,664,000 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na Shilingi 337,905,996 kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa vyumba nya madarasa. Aidha, Chuo kilikusanya jumla ya Shilingi 1,510,514,650 sawa na asilimia 97 ya lengo la mwaka la Shilingi 1,545,001,530.

Mpango wa Afrika wa Kujitathmini Kiutawala Bora

276. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2019/2020, APRM Tanzania iliendelea kutekeleza majukumu yake kulingana na malengo yaliyoainishwa kwenye Mpango Mkakati wake wa Miaka Mitano (2017/2018 - 2021/2022) unaohuishwa kwa kuzingatia mpango kazi na bajeti ya kila mwaka. Malengo yaliyotekelawa kwa kipindi hiki ni kama ifuatavyo:

- a) Kuimarisha uratibu wa utekelezaji wa Mpango Kazi wa APRM Tanzania;
- b) Kuimarisha uhamasishaji wa mawasiliano kwa umma; na
- c) Kuhakikisha kuwa shughuli za APRM Tanzania zinakuwa endelevu.

277. Mheshimiwa Spika, APRM Tanzania imekamilisha rasimu ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango Kazi wa APRM inayohusu maeneo ya Siasa na Demokrasia, Usimamizi wa Uchumi, Uendeshaji wa Kampuni za Biashara na utoaji wa huduma za jamii. Mara baada ya taarifa hii kuridhiwa na wadau itawasilishwa katika Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika.

278. Mheshimiwa Spika, bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya shughuli za APRM - Tanzania kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ni **Shilingi 948,012,866**. Fedha zilizopokelewa ni **Shilingi 638,240,000** sawa na asilimia 67.

9.0 CHANGAMOTO ZILIZOPO NA HATUA ZILIZOCHUKULIWA

279. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza bajeti ya mwaka wa fedha 2019/2020, pamoja na kuwepo mafanikio ya kiutendaji, Wizara inakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo:

- i) Kuongeza idadi ya watumishi ili kukidhi mahitaji yanayotokana na wingi wa majukumu ya Wizara;
- ii) Kuendelea kuongeza idadi ya magari ili kukidhi mahitaji ya Wizara;
- iii) Kasi ndogo ya sekta binafsi kutumia fursa za biashara na uwekezaji zitokanazo na mtangamano wa Afrika Mashariki na masoko ya kimataifa; na
- iv) Uelewa mdogo wa Watanzania kuhusu masuala na fursa zitokanazo na Mtangamano wa Kikanda.

280. Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na changamoto hizo, Wizara imechukua hatua zifuatazo:

- i) Kuendelea kuwasiliana na mamlaka husika kwa ajili ya kupatiwa vibali vya ajira mpya na kujaza nafasi zilizo wazi;
- ii) Kuendelea kutoa kipaumbele cha upatikanaji wa magari katika bajeti ya Wizara;
- iii) Kuendelea kushirikiana na Taasisi za sekta binafsi, asasi za kiraia na vyombo vya habari katika kutoa elimu kwa umma juu ya fursa mbalimbali zitokanazo na ushiriki wetu katika Jumuiya za Kikanda na Kimataifa; na
- iv) Kuendelea kuhamasisha umma kuchangamkia fursa mbalimbali zinazojitokeza katika nchi mbalimbali, Jumuiya za Kikanda na Kimataifa.

10.0 SHUKRANI

281. Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hii ni Hotuba yangu ya mwisho ya Bajeti katika Bunge la 11, kwa mara nyingine tena, naomba kuchukua nafasi hii kumshukuru kwa dhati kabisa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa imani yake kwangu iliyomfanya kunituea kuwa Mbunge tarehe 22 Oktoba, 2018 na kunituea kuwa Waziri wa Katiba na Sheria nafasi ambayo nilihudumu hadi tarehe 3 Machi, 2019 aliponiteua kuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Kutokana na imani yake kwangu nimeweza kushirikiana na viongozi na watumishi wa Wizara zote mbili nilizohudumu kutekeleza yale yote ambayo Viongozi wangu wakuu wameniagiza. Nichukue fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kunipa fursa ambayo sikustahili kuitumikia nchi yangu katika nafasi hii kubwa kabisa. Nashukuru kuwa nimeweza kutoa mchango wangu katika maendeleo ya nchi yetu na katika kutekeleza llani ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2015 – 2020.

282. Mheshimiwa Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila iwapo sitatoa shukrani zangu za kipekee kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar; na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa miongozo yao ambayo ilikuwa ni nguzo muhimu kwenye utekelezaji wa majukumu yangu katika nafasi zote zilizowahi kushika. Nalishukuru pia Bunge lako Tukufu kwa ushirikiano mkubwa niliopatiwa katika kulitumikia Taifa na kuchangia katika kufanikisha maendeleo makubwa yaliyopatikana katika Serikali ya Awamu ya Tano.

283. Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kwa namna ya pekee kuwashukuru Mabalozi na Wawakilishi wa Taasisi za Umoja wa Mataifa pamoja na Mashirika mengine ya Kimataifa hapa nchini kwa ushirikiano mkubwa wanaoutoa kupitia nchi na mashirika yao kufanikisha mipango mbalimbali

ya maendeleo inayotekelzwa na Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

284. *Mheshimiwa Spika*, Serikali ya Awamu ya Tano imeendelea kupata mafanikio makubwa kutokana na mchango wa wadau na Washirika wa Maendeleo kutoka nchi na asasi mbalimbali za kimataifa, kikanda na kitaifa na sekta binafsi. Naomba nitumia fursa hii kuzishukuru nchi za Algeria, Australia, Austria, Brazil, Brunei, Canada, China, Cuba, Denmark, Ethiopia, Finland, Hungary, Italia, Iran, Ireland, Indonesia, India, Israel, Jamhuri ya Korea, Japan, Kuwait, Malaysia, Malta, Marekani, Mexico, Misri, Morocco, New Zealand, Norway, Oman, Pakistan, Poland, Qatar, Romania, Saudi Arabia, Singapore, Sri Lanka, Sweden, Sudan, Thailand, Ubelgiji, Ufaransa, Uhispania, Uingereza, Uholanzi, Ujeruman, Urusi, Uswisi, Uturuki, Ureno, Umoja wa Falme za Kiarabu, Venezuela na Viet Nam kwa kuchangia kwenye jitihada za maendeleo ya nchi yetu.

285. *Mheshimiwa Spika*, naomba kutoa shukrani pia kwa Benki ya Maendeleo ya Afrika; Umoja wa Ulaya; *African Capacity Building Foundation*; Benki ya Dunia; Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF); Shirika la Nguvu za Atomiki Duniani (IAEA); Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF); *Investment Climate Facility for Africa*; Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa; Shirika la Mpango wa Chakula Duniani; Ofisi ya Mwakilishi Mkazi wa Umoja wa Mataifa (UN RCO); Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA); Shirika la Umoja wa Mataifa la Kupambana na Ukimwi (UNAIDS); Shirika la Umoja wa Mataifa la Kilimo na Chakula (FAO); Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu Sayansi na Utamaduni (UNESCO); Shirika la Afya Duniani (WHO); Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Wakimbizi (UNHCR); Shirika la Kazi Duniani (ILO); Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Uhamaji (IOM); Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF); Programu ya Maendeleo ya Umoja wa Mataifa (UNDP); Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo (IFAD); Mfuko wa Kukuza Mtaji wa Umoja wa Mataifa (UNCDF); Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughukia Maendeleo ya Viwanda (UNIDO);

Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Masuala ya Wanawake (UN WOMEN); Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa (UNEP); Shirika la Umoja wa Mataifa la Biashara na Maendeleo (UNCTAD); Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Madawa ya Kulevyaa na Uhalifu (UNODC).

286. *Mheshimiwa Spika*, vilevile napenda kuwashukuru *TradeMark East Africa*; Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Kiuchumi ya Afrika (BADEA); Benki ya Uwekezaji ya Ulaya; *The Association of European Parliamentarians with Africa*; Mfuko wa Dunia wa Wanyama Pori; *The Belinda and Bill Gates Foundation*; *Global Fund*; *International Committee of the Red Cross*; *International Federation of the Red Cross and Red Crescent Societies*; *Medecins Sans Frontieres* pamoja na Mifuko na Mashirika mbalimbali ya misaada.

287. *Mheshimiwa Spika*, ninayashukuru pia Mashirika na Taasisi zisizo za Kiserikali, Asasi za Kiraia, Sekta Binafsi, Taasisi za Elimu, Vyombo vyta Habari, Taasisi za Dini na wadau wote ambao wamekuwa wakishirikiana na mimi pamoja na Wizara nzima kwenye utendaji wetu wa kazi. Ni dhahiri kuwa ushirikiano wao umeisaidia Serikali katika kutimiza baadhi ya malengo yake.

288. *Mheshimiwa Spika*, kwa moyo mkunjufu, napenda kuwashukuru watendaji na watumishi wa Wizara na Taasisi zake kwa kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu ipasavyo. Kwa namna ya pekee, napenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Damas Daniel Ndumbaro (Mb), Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki; Balozi Kanali Wilbert Augustin Ibuge, Katibu Mkuu; Balozi Ramadhan Muombwa Mwinyi, Naibu Katibu Mkuu; Mabalozi wa Tanzania Nje ya Nchi; Wakuu wa Idara na Vitengo; Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara; na watumishi wengine wote kwa weledi, umahiri na ufanisi wao katika kunisaidia kutekeleza majukumu yangu ya kulinda na kutetea maslahi ya Taifa letu.

289. *Mheshimiwa Spika*, kwa nafasi ya kipekee kabisa, napenda kumshukuru mke wangu mpendwa Dkt. Amina M. M. Kabudi na familia yangu kwa ujumla kwa uvumilivu wao na kuwa karibu na mimi wakati wote wa kutekeleza

majukumu yangu niliyopewa na Mheshimiwa Rais ambayo wakati mwingine yananilazimu kuwa mbali nao kwa muda mrefu.

11.0 MALENGO YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

290. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2020/2021, pamoja na masuala mengine, Wizara imeweka kipaumbele katika kutekeleza majukumu yafuatayo:

- i) Kutekeleza Diplomasia ya Uchumi kwa kuvutia wawekezaji na wafanyabiashara kutoka nje, kuvutia watalii, kutafuta misaada na mikopo yenye masharti nafuu, kutafuta fursa za mafunzo, kushiriki katika Jumuiya za Kikanda kwa lengo la kuongeza ajira na masoko ya bidhaa za Tanzania nje;
- ii) Kukamilisha Sera ya Mambo ya Nje 2020, Sera hiyo itazingatia mabadiliko ya kisasa, kiuchumi na kijamii;
- iii) Kuboresha Kanzidata ya Diaspora itakayotoa taarifa itakayosaidia kuandaa mwongozo wa namna ya kuwashirikisha Diaspora wa Tanzania kuchangia katika maendeleo ya nchi yao;
- iv) Kuendelea kutumia Balozi zetu kutafuta mitaji ya uwekezaji, masoko na kuhamasisha Diaspora kuchangia kwenye maendeleo ya nchi kwa kutangaza vyema miradi ya vipaumbele na vivutio vinavyotolewa na Serikali katika maeneo yao ya uwakilishi;
- v) Kuendelea na utafutaji wa masoko mapya ya bidhaa za Tanzania nje kwa kuendelea kuhamasisha Taasisi za Serikali zinazohusika na biashara kushirikiana na sekta binafsi kushiriki katika maonesho mbalimbali ya Kimataifa ambayo yanatoa fursa kwa nchi mbalimbali kutangaza bidhaa zake pamoja na kujifunza teknolojia na mbinu za kisasa zitakazoboresha bidhaa zetu;
- vi) Kuendelea kutekeleza Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Itifaki zake;

- vii) Kuendelea kuratibu utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Maendeleo wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini kwa Afrika wa mwaka 2015 - 2020 na Mkakati wa Kuendeleza Viwanda wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika wa mwaka 2015 – 2030;
- viii) Kushiriki katika juhudi za kuleta amani, usalama na kukuza demokrasia kwenye Jumuiya za Kikanda ambazo nchi yetu ni mwanachama;
- ix) Kuendelea kutoa elimu kwa umma juu ya fursa zitokanazo na Mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya nyingine za Kikanda;
- x) Kuendelea kusimamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayotekelizwa na Wizara, Balozi na Taasisi zilizopo chini ya Wizara; na
- xi) Kuendelea kusimamia rasilimali watu; rasilimali fedha na rasilimali vitu vya Wizara na Balozi.

12.0 MALENGO YA TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

Mpango wa Kujitathmini Kiutawala Bora Afrika (APRM)

291. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021, APRM inatarajia kutekeleza vipaumbele vifuatavyo:

- i) Kuimarisha Tathmini za Utawala Bora za Mpango wa APRM ikiwa ni pamoja na kuhuisha mbinu za utafiti kwa kupitia upya hojaji ya APRM;
- ii) Kuboresha viashiria vya utafiti, kuzingatia matumizi ya teknolojia katika utekelezaji wa Mpango na kupanua wigo wa zana zinazotumika katika utafiti;
- iii) Kuratibu ufuutiliaji wa utekelezaji wa Mpango Kazi wa APRM kwa kushirikiana na Wizara, Idara na Wakala za Serikali

katika kuandaa taarifa ya mwaka pamoja na kuhakikisha kuwepo kwa mfumo madhubuti wa ufuatiliaji; na

iv) Kuimarisha mawasiliano na utoaji taarifa kuhusu Mpango wa APRM kwa kuendelea kutekeleza Mpango wa Mawasiliano wa Miaka Mitano 2016/17 – 2020/21.

Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Arusha (AICC)

292. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2020/2021, AICC inatarajia kukusanya mapato ya **Shilingi 16,701,559,000**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 16,001,559,000** ni kutoka vyanzo mbalimbali vya ndani ambapo kituo cha Arusha kinatarajia kukusanya **Shilingi 12,785,009,000** na Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere kinatarajia kukusanya **Shilingi 3,216,550,000**. Aidha, mapato ya **Shilingi 700,000,000** yatatokana na mkopo kwa ajili ya mradi wa upanuzi wa Hospitali ya AICC.

293. *Mheshimiwa Spika*, Kituo kinaendelea kufanya taratibu za kuwezesha ujenzi wa kituo mahsusini cha mikutano jijini Arusha kitakachoitwa *Mt. Kilimanjaro International Convention Centre* (MK-ICC). Kituo hicho kitakuwa kichocheo cha utekelezaji wa diplomasia ya mikutano ya kimataifa na maonesho hapa nchini.

Chuo cha Diplomasia

294. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2020/2021 Chuo kinatarajia kutekeleza masuala yafuatayo:

- i) Kutoa mafunzo ya mahusiano ya kimataifa na mbinu za kidiplomasia;
- ii) Kufanya utafiti kubaini mahitaji na changamoto katika fani za mahusiano ya kimataifa na mbinu za kidiplomasia;
- iii) Kutathmini matokeo ya mafunzo yaliyotolewa na mipango ya mafunzo kwa ujumla; na
- iv) Kutoa ushauri na huduma za kitaalamu kwa Serikali na Taasisi zake.

13.0 MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

295. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/2021, Wizara inatarajia kukusanya kiasi cha **Shilingi 2,550,879,000** ikiwa ni maduhuli ya Serikali yatakayopatikana kutohakana na vyanzo vilivyopo Makao Makuu ya Wizara na katika Balozi za Tanzania nje. Vyanzo hivyo vya mapato vinajumuisha pango la nyumba za Serikali zilizopo nje ya nchi; kuthibitisha nyaraka; na mauzo ya nyaraka za zabuni.

296. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2020/2021, Wizara imepangiwa bajeti ya **Shilingi 199,750,684,000**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 179,750,684,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida zinazojumuisha **Shilingi 167,717,723,000** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na **Shilingi 12,032,961,000** kwa ajili ya Mishahara; na **Shilingi 20,000,000,000** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

297. Mheshimiwa Spika, kati ya fedha za bajeti ya Matumizi Mengineyo ya Wizara, **Shilingi 800,000,000** ni kwa ajili ya Mpango wa Afrika wa Kujitathmini Kiutawala Bora (APRM), **Shilingi 1,000,000,000** ni kwa ajili ya Chuo cha Diplomasia, **Shilingi 1,272,000,000** ni kwa ajili ya Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu na **Shilingi 168,200,000** ni kwa ajili ya Bodi ya Ushauri wa Masuala ya Rushwa ya Umoja wa Afrika. Aidha, kati ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya Mishahara, **Shilingi 2,427,064,000** ni kwa ajili ya Chuo cha Diplomasia.

298. Mheshimiwa Spika, katika fedha za bajeti ya Maendeleo, kiasi cha **Shilingi 20,000,000,000** kilichopangwa kwa mwaka wa fedha 2020/21, **Shilingi 1,800,000,000** ni kwa ajili ya ujenzi wa makazi ya Balozi na ofisi katika Ubalozi wa Tanzania Moroni, Komoro; **Shilingi 3,694,439,655** ni kwa ajili ya ujenzi wa ofisi na makazi ya Balozi wa Tanzania Muscat, Oman; **Shilingi 1,500,000,000** ni kwa ajili ya ujenzi wa uzio wa viwanja vya Serikali vilivyopo Kigali, Maputo, Bujumbura, Riyadh na Lilongwe; **Shilingi 3,948,120,345** ni kwa ajili ya ujenzi wa jengo la ofisi ya Ubalozi na Kitega Uchumi katika Ubalozi wa Tanzania Nairobi, Kenya; **Shilingi 2,280,000,000** ni kwa ajili ya

ujenzi wa jengo la ofisi na kitega uchumi katika Ubalozi wa Tanzania Kinshasa, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo; **Shilingi 3,864,440,000** ni kwa ajili ya ukarabati wa majengo ya ofisi yaliyopo Ubalozi wa Tanzania Washington D.C, Marekani; **Shilingi 275,000,000** ni kwa ajili ya ukarabati wa majengo ya makazi ya Balozi na watumishi wa Ubalozi wa Tanzania Harare, Zimbabwe; **Shilingi 260,000,000.00** ni kwa ajili ya ukarabati wa makazi ya Balozi wa Tanzania Kigali, Rwanda; na **Shilingi 2,378,000,000.00** ni kwa ajili ya ujenzi wa madarasa ya Chuo cha Diplomasia.

14.0 HITIMISHO

299. Mheshimiwa Spika, ili kuweza kutekeleza kikamilifu majukumu ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2020/2021, naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi 199,750,684,000**. Katika fedha hizo **Shilingi 179,750,684,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 20,000,000,000** ni kwa ajili ya bajeti ya maendeleo.

300. Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi hii adhimu kukushukuru tena wewe binafsi na Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza.

301. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

NAIBU SPIKA: Hoja imeungwa mkono, ahsante sana Mheshimiwa Waziri tutaendelea na utaratibu wetu, sasa nimuuite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Mambo ya Nje Ulinzi na Usalama. Mheshimiwa Sebastian Kapufi.

MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI – K.n.y MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, kwa kuwa hii ndio Taarifa ya Mwisho ya Kamati yetu kusomwa Bungeni katika kipindi cha miaka mitano cha Bunge la Kumi na Moja. Kipekee naomba kutambua Uongozi mahiri wa Spika wetu Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, katika kuliongoza Bunge akisaidiwa na wewe Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson Mbunge, na Wenyeviti wa Bunge. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati hii kwa ushirikiano mkubwa wakati wote nikiwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati. Shukrani za pekee zimwendee Mheshimiwa Azzan Zungu, Mbunge aliyekuwa Mwenyekiti wa Kamati hii kabla ya kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, kwa Uongozi wake mahiri ambao uliwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee natoa pole kwako, kwa Wabunge wote, na kwa wananchi kwa ujumla, kufuatia vifo vyta Wabunge wenzetu watatu Mheshimiwa Getrude Lwakatare, Mheshimiwa Richard Ndassa na Mheshimiwa Balozi Dkt. Augustine Mahiga, Mwenyezi Mungu azilaze Roho za Marehemu mahali pema peponi, Amina. (*Makofi*)

Mheshimiwa Nailbu Spika, baada ya maneno hayo ya awali kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba sasa kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapatona Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, na kuliomba Bunge lako Tukufu liipokee taarifa hii na kuikubali, kisha kuidhinisha Bajeti ya Wizara hiyo kama ilivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ninayowasilisha inatoa maelezo kuhusu maeneo muhimu nane yakiwemo yatuatayo:-

- (i) Mapitio ya Taarifa ya Wizara kuhusu uzingatiaji wa Maoni yaliyotolewa na Kamati Bungeni wakati wa kujadili Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020;
- (ii) Mapitio ya Taarifa ya Wizara kuhusu upatikanaji wa Fedha zilizoidhinisha na Bunge pamoja na utekelezaji wa majukumu na malengo ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020;

- (iii) Mapitio ya Malengo ya Bajeti na Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021; na
- (iv) Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021; na
- (v) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 ilihu maeneo Makuu matatu. Maeneo hayo ni: -

- (i) Uzingatiaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati;
- (ii) Mapitio ya Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge; na
- (iii) Utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, Kamati ilipitia na kuchambua kwa kina maeneo yote matatu na kama inavyoonekana katika ukurasa wa tano hadi kumi na tisa wa taarifa hii. Hata hivyo naomba nitoe maelezo mafupi katika baadhi ya vipengere kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Uzingatiaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati; Bunge lilipokuwa likijadili hoja ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, Kamati ilitoa ushauri katika masuala kumi na tatu.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla ushauri wa Kamati umefanyiwa kazi na utekelezaji upo katika hatua mbalimbali. Hata hivyo Kamati inaendelea kusisitiza kuwa ushauri wa kamati kuhusu masula ya Kisera kama uandaaji wa Sera ya Mambo ya Nje na Sera ya Diaspora uanapaswa kupewa uzito stahiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uchambuzi wa Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020. Kamati ilipitia Taarifa ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara katika Kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020 kwa kuchambua hali ya Ukusanyaji wa Mapato pamoja na upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina kwa kipindi hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilijulishwa kuwa hadi kufikia Mwezi Machi, 2020, Wizara kupitia Balozi zake ilikuwa imekusanya shilingi Bilioni 5.010 sawa na asilimia 196.4 ya lengo la ukusanyaji lilokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilijiridhisha kuwa ongezeko kubwa kwenye lengo la makusanyo lilokusudiwa halitokani na kushindwa kuweka makadirio yenyue uhalisia bali limetokana na baadhi ya Balozi kuendelea kukusanya maduhuli ya VISA ambayo yanapaswa kukusanya na Idara ya Uhamiaji. Hata hivyo, Kamati ilielezwa kuwa hali hii imeshatatuliwa tangu mwezi Novemba, 2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilibaini kuwa, mbali na fedha za VISA, Wizara ilikusanya Shilingi Milioni 355.6 sawa na asilimia 15 tu ya makadirio yaliyowekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilihoji kuhusu sababu zilizochangia lengo lilowekwa kufikiwa kwa asilimia ndogo. Maeleo yaliyotolewa yalibainisha kuwa baadhi ya Balozi zinaendelea na makusanyo hususan Ubalozi wa Tanzania, New York ambayo makusanyo yake hupatikana mwezi Mei kila mwaka kulingana na ratiba ya malipo ya kodi ya pango kwa majengo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilipochambua taarifa ya upatikanaji wa fedha kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ilibaini kuwa hadi kufikia mwezi Machi, 2020 Wizara ilikuwa imepokea jumla ya shilingi bilioni 113.7 sawa na asilimia 68 ya fedha zote za bajeti zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu. Hali hiyo ni tofauti na mwaka wa fedha 2018/2019 ambapo katika kipindi kama hiki Wizara ilipokea shilingi bilioni

93.1 sawa na asilimia 52.6 ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa mwaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilibaini kuwa ongezeko hilo lilichangiwa pia na kutolewa kwa fedha za maendeleo jumla ya shilingi milioni 487.9 ambapo katika mwaka wa fedha 2018/2019 hakukuwa na fedha zozote za maendeleo zilizotolewa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya fedha za maendeleo zilizotolewa, shilingi milioni 150 zilikuwa kwa ajili ya kukarabati nyumba ya makazi ya Balozi Otawa, Canada na shilingi milioni 337.9 zilitolewa kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa katika Chuo cha Diplomasia Kurasini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Serikali kuendelea kukipanua Chuo cha Diplomasia, Kamati ilipata maelezo kuwa umiliki wa chuo hicho bado ni wa nchi mbili za Tanzania na Msumbuji licha ya kuwa Serikali ya Msumbiji imekuwa haichangii gharama za uendeshaji wake tangu mwaka 1983 na kutoshiriki katika Menejimenti ya Chuo tangu mwaka 1986. Ni rai ya Kamati kuwa suala la umiliki wa Chuo cha Diplomasia ni vyema likashughulikiwa kwa uzito unaostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Taarifa iliyotolewa na Wizara ilibainisha kuwa katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020 Wizara iliendelea kutekeleza Sera ya Mambo ya Nje kwa kushirikiana na Taasisi nyingine za Serikali, Sekta Binafsi na Washirika wa Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kusimamia utawala na maendeleo ya watumishi Wizarani katika mwaka wa fedha 2019/2020, Kamati inampongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuteua Mabalozi 16 kuiwakilisha Tanzania katika nchi mbalimbali, kati ya Mabalozi walioteuliwa, Mabalozi watatu ni wanawake. Kamati inampongeza

Mheshimiwa Rais kwa kuona umuhimu wa kuteua wanawake pia katika nyazifa hizo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uratibu wa shughuli za Watanzania waishio nje ya nchi (*Diaspora*) Kamati ilihoji kuhusu sababu za kutokukamilika kwa mchakato wa kutoa Sera ya *Diaspora*. Majibu yaliyotolewa na Serikali yalibainisha kuwa kuna ukosefu wa takwimu za Watanzania waishio ughaibuni na hivyo kuilazimu Serikali kuandaa kanzidata ya takwimu zitakazoonyesha sifa na uwezo wao kabla ya kutunga sera hiyo ili matamko yake yawe yamezingatia uhalisia uliopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, Kamati ina maoni kuwa ni vyema Balozi zetu zikachukua hatua madhubuti katika kuhamasisha Watanzania wanaoishi nje ya nchi kujianzikisha. Hii ni pamoja na kuimarissha mahusiano mazuri na kuwa mstari wa mbele katika kutatua changamoto zinakabili *Diaspora*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa malengo ya bajeti. Kabla ya kueleza uchambuzi wa makadirio ya matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2020/2021, napenda kutoa taarifa kuwa Kamati ililezea kuwa kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Wizara imepanga kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia vipaumbele 11.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Kamati kuhusu vipaumbele umebaini kuwa ukamilishaji wa Sera ya Mambo ya Nje imekuwa ni kipaumbele kinacho jirudia mara kwa mara licha ya kwamba Kamati imekuwa ikishauri kuhusu umuhimu wa kukamilisha sera hiyo. Kamati ina maoni kuwa ni vyema sasa kipaumbele cha kuandaa sera hiyo kikapewa uzito unaostahili kwani jambo hili limekuwa likizungumziwa na Kamati tangu ilipoundwa mwaka 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilipitia makadirio ya ukusanyaji wa mapato yaliyopendekezwa kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Katika uchambuzi huo Kamati ilibaini kuwa makadirio hayo yanapishana kwa kiasi kidogo sana na

makadirio ya mwaka wa fedha unaoishia katika mwaka wa fedha 2019/2020. Wizara ilikuwa na lengo la kukusanya shilingi 2,550,879,072/= wakati kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Wizara inalenga kukusanya kiasi cha shilingi 2,550,879,000/= ikiwa ni pungufu kwa shilingi 72/= tu. Baada ya kufanya uchambuzi wake Kamati imejiridhisha kuwa lengo lililowekwa limeendana na hali halisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2020/2021 Wizara ilieleza Kamati kuwa inaomba kuidhinishiwa kiasi cha shilingi bilioni 199.7. Kamati ilichambua maombi hayo na kuona kuwa asilimia 84 ya fedha zinaoombwa ni kwa ajili ya matumizi mengineyo, asilimia sita ni kwa ajili ya mishahara na asilimia 10 kugharamia miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuonesha nia njema kwa kutekeleza mpango wake wa miaka 15 wa ujenzi, ununuzi na ukarabati wa majengo ya ofisi na makazi katika Balozi kwa kuongeza bajeti ya maendeleo kwa asilimia 400 kwa mwaka 2020/2021 ikilinganishwa na bajeti iliyotengwa kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati illijiridhisha kuwa miradi muhimu ambayo Kamati imekuwa ikisimamia mara kwa mara tangu mwaka wa fedha 2018/2019 ikijumuisha miradi ya kupanua na kuboresha miundombinu ya Chuo cha Diplomasia, ujenzi wa Ubalozi wa Tanzania Oman pamoja na ujenzi wa uzio katika viwanja vya Serikali umezingatiwa na kutengewa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa niwasilishe maoni na ushauri wa Kamati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, uko umuhimu kwa Serikali kutoa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ifikapo Juni 30, 2020. Katika mwaka wa fedha ni asilimia 12.2 tu ya shilingi bilioni nne zilizoidhinishwa ndiyo iliyotolewa. Kutolewa kwa fedha hizi kutafanikisha utekelezaji wa shughuli

zilizopangwa kutekelezwa katika Balozi za Tanzania nje ya nchi na Chuo cha Diplomasia Kurasini kwa manufaa mapana ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hili Kamati inaisisitiza Serikali katika mwaka fedha 2020/2021 kutoa kipaumbele katika kupeleka fedha za maendeleo kwa miradi ambayo ina umuhimu wa kipekee kiuchumi. Kwa mfano, ujenzi wa Ubalozi wa Tanzania Muscat, Oman. Ni imani ya Kamati kuwa Serikali itapata fursa nyingi za kiuchumi endapo itafanikiwa kujenga Ubalozi nchini Oman ikizingatiwa kuwa Oman ni miongoni mwa nchi zenyet uchumi mzuri duniani. Kamati imekuwa ikilisemea suala hili kwa muda wa miaka miwili sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kutenga jumla ya shilingi bilioni 20 kwa ajili ya miradi ya maendeleo ikiwa ni utekelezaji wa Mpango wa Miaka 15 wa Ujenzi, Ununuzi na Ukarabati wa Majengo ya Ofisi na Makazi katika Balozi Zetu. Hata hivyo, Kamati inaendelea kushauri Serikali kuhakikisha kuwa fedha hizo zinatolewa kwa wakati ili kufanikisha utekelezaji wa mpango huo muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaamini kuwa Serikali itaokoa fedha nyingi zinazotumika kulipia pango. Aidha, Serikali itaongeza mapato yatokanayo na nyumba zake kukodishwa kama ilivyo sasa katika majengo ya Ubalozi ya Tanzania; Maputo, Msumbiji; Lusaka, Zambia; Newyork, Marekani; Paris, Ufaransa; na Harare, Zimbabwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na ushauri uliotolewa hapo juu, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuendelea kuimarisha ushirikiano na wadau wa Kimataifa wa mabadiliko ya tabianchi ili kukabiliana na changamoto na athari za tabianchi bila ya kuathiri masaa, maslahi ya nchi yetu. Kamati inaipongeza Serikali kwa kufungua Ubalozi mpya Windhoek, Namibia ikiwa ni kuendelezo wa kuongeza fursa mbalimbali za kiuchumi nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na ufunguaji wa Balozi mpya, Kamati inatambua kuwa kuna uchache wa watumishi ikilinganishwa na majukumu yaliyopo katika Balozi zetu. Hivyo Kamati inaishauri Serikali kupeleka watumishi wa kutosha kwenye Balozi zetu ikiwemo wataalam wa masuala ya kidiplomasia ya uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kutangaza vivutio vya utalii kupitia Balozi zake nje ya nchi hususan kwa vivutio vilivyoko katika ukanda mpya wa Kusini. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuendelea na juhudhi hizo ili kukuza pato la Taifa. Serikali iendelee kutafuta mbinu za kutumia kikamilifu soko kwa nchi ambazo tuna mahusiano nayo mazuri ya kihistoria kama vile China, India na nchi za Kiarabu katika kuuza bidhaa zetu hususan za kilimo na mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhitimisha, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Taarifa hii. Napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ambapo maoni, ushauri na ushirikiano wao umewevesha kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao kama yalivyoorodheshwa yaingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati, napenda kutumia fursa hii kumshukuru Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Mheshimiwa Prof. Palamagamba Kabudi, Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro, Katibu Mkuu - Balozi Kanali Wilbert Ibuge, Naibu Katibu Mkuu - Ndugu Ramadhan Muombwa pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano na mchango wao wakati wa uchambuzi wa Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge - Ndugu Stephen Kagaigai pamoja na Watendaji wote wa Bunge kwa kuiwezesha Kamati kukamilisha kazi yake kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu liipokee Taarifa hii na likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 kama yalivyowasilishwa na Mto Hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. (*Makofii*)

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA
NJE, ULINZI NA USALAMA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA
WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA
MASHARIKI (FUNGU 34) KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020
PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA
MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA
FEDHA 2020/2021 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

SEHEMU YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, kwa kuwa hii ndio Taarifa ya Mwisho ya Kamati yetu kusomwa Bungeni katika kipindi cha miaka mitano cha Bunge la Kumi na Moja, Kipekee naomba kutambua uongozi wako mahiri katika kuliongoza Bunge, ukisaidiwa na Naibu Spika, Mhe. Dkt. Tulia Ackson, Mb na Wenyeviti wa Bunge. Aidha, nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati hii kwa ushirikiano mkubwa wakati wote nikiwa Makamu Mwenyezekiti wa Kamati. Shukrani za pekee zimwendee Mhe. Mussa Azzan Zungu, Mb aliyekuwa Mwenyezekiti wa Kamati hii kabla ya kuteuliwa na Mhe. Rais kuwa Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, kwa uongozi wake mahiri ambao ultiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vizuri.

Mheshimiwa Spika, kipekee natoa pole kwako, kwa Wabunge wote, na kwa wananchi kufuatia vifo vya Wabunge wenzetu watatu Mheshimiwa Getrude Lwakatare, Mhe. Richard Ndassa na Mhe. Balozi Dkt. Augustine Mahiga, Mwenyezi Mungu azilaze Roho za Marehemu mahali pema peponi, Amina.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, [Kanuni za Bunge], naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020; pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, na kuliomba Bunge lako Tukufu liipokee taarifa hii na kuikubali, kisha kuidhinisha Bajeti ya Wizara hiyo kama iliyowasilishwa na Mtoa Hoja.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kifungu cha 6 (3) (c) cha Nyongeza ya Nane, ya Kanuni za Bunge, Wizara hii ni mionganini mwa Wizara zinazosimamiwa na Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Aidha, Kifungu cha 7 (1) (a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge kimezipa jukumu Kamati za Kisekta ikiwemo Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, kushughulikia Bajeti za Wizara inazozisimamia.

Naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa katika kutekeleza jukumu hilo, Kamati ilikutana na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki tarehe 20 na 23 Machi, 2020.

Mheshimiwa Spika, katika vikao hivyo, Kamati ilipokea Taarifa ya Wizara kuhusu utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 kama inavyoelekeza Kanuni ya 98 (2) ya Kanuni za Bunge kwa lengo la kulinganisha na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, ili kulisaidia Bunge lako Tukufu kufuatilia ipasavyo utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, pamoja na kuishauri vema Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, Taarifa ninayoiwasilisha inatoa maelezo kuhusu: -

- i) Mapitio ya Taarifa ya Wizara kuhusu uzingatiaji wa Maoni yaliyotolewa na Kamati Bungeni wakati wa kujadili Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020;

- ii) Uchambuzi wa ukusanyaji wa maduhuli ikilinganishwa na lengo lililowekwa kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020;
- iii) Mapitio ya Taarifa ya Wizara kuhusu upatikanaji wa Fedha zilizoidhinishwa na Bunge pamoja na utekelezaji wa majukumu na malengo ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020;
- iv) Mapitio ya Taarifa ya Wizara kuhusu Changamoto za Utekelezaji wa Bajeti katika Mwaka wa Fedha 2019/2020;
- v) Uchambuzi wa majukumu na malengo yanayowekwa kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021;
- vi) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021;
- vii) Mapitio ya Malengo ya Bajeti na Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021; na
- viii) Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, lengo la maelezo hayo ni kuliwezesha Bunge kupata taswira ya hali ya utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 na kulinganisha na Makadirio ya Fedha za Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 ili Bunge liweze kuamua kuhusu Maombi ya Wizara hii.

SEHEMU YA PILI

2.0 MAPITIO YA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 ilihusu maeneo Makuu matatu. Maeneo hayo ni: -

- i) Uzingatiaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati;
- ii) Mapitio ya Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge; na
- iii) Utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, Kamati ilipitia na kuchambua kwa kina maeneo yote matatu kama ifuatavyo: -

2.1 Uzingatiaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati

Mheshimiwa Spika, Bunge lilipokuwa likijadili hoja ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, Kamati ilitoa ushauri katika masuala kumi na tatu (13). Katika kufuatilia namna ambavyo Wizara imezingatia Ushauri huo, tarehe 20 Machi, 2020, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki alijulisha Kamati kuhusu utekelezaji wa masuala hayo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuliari Bunge lako Tukufu kwamba, upo ushauri uliozingatiwa, upo unaoendelea kuzingatiwa na upo ushauri unaohitaji kuzingatiwa zaidi katika utekelezaji wake hususan ushauri uliohusu masuala ya Kibajeti.

Mheshimiwa Spika, mionganoni mwa ushauri uliozingatiwa ni kuhusu Serikali kuona umuhimu wa kuendelea kutenga na kutoa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi muhimu ya kimkakati ikijumuisha mradi wa Ujenzi wa Ubalozzi wa Tanzania Muscat-Oman.

Mheshimiwa Spika, maelezo yaliyotolewa yalionesha kuwa Serikali ilizingatia ushauri huo ambapo Mwezi Julai 2019, Wizara kwa kushirikiana na Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) ilifanya usanifu, kuandaa michoro ya awali na makisio ya ujenzi wa Jengo la Ofisi na Makazi ya Balozi jijini Muscat-Oman. Aidha, Waziri aliileza Kamati kuwa Wakala wa Majengo ya Serikali wamekamilisha kazi ya makisio ya gharama za utekelezaji wa mradi huo, na kwamba fedha hizo zimetengwa katika bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 jambo ambalo Kamati ililishauri.

Mheshimiwa Spika, moja ya ushauri unaoendelea kufanyiwa kazi unahusu ukamilishaji wa Sera Mpya ya Mambo ya Nje itakayojumuisha masuala muhimu ya Mtangamano wa Afrika Mashariki.

Maelezo yaliyotolewa yalibainisha kuwa, Wizara imekwishakamilisha Rasimu ya Sera hiyo na inatarajiwa kuwasilishwa kwa Wadau mbalimbalkwa lengola kukusanya maoni kwa ajili ya kuiboresha zaidi. Hata hivyo, Kamati haikuridhishwa na kasi ya mchakato wa rasimu hii kwani katika kipindi cha Machi, 2019 Kamati ilipewa maelezo hayo hayo kuwa Rasimu ilikuwa imeshakamilika na hatua iliyokuwa ikisubiriwa ni kukusanya maoni ya wadau ili kuiboresha.

Mheshimiwa Spika, Kamati ina maoni kuwa ni muhimu Serikali ikakamilisha haraka upatikanaji wa Sera hiyo muhimu ikizingatiwa kuwa Sera Mpya inayoandalishiwa inategemewa kujumuisha masuala ya Mtangamano wa Afrika Mashariki. Kwa kumbukumbu zilizopo, suala hili limekuwa likishauriwa na Kamati hii tangu ilipoundwa Mwaka 2016 na maelezo yanayotolewa na Wizara ni kuwa mchakato huo unaendelea.

Mheshimiwa Spika, sambamba na ukamilishaji wa Sera ya Mambo ya Nje, Kamati ilishauri kuhusu Serikali kuharakisha Mchakato wa Kupata Sera ya Taifa ya Diaspora. Hata hivyo, Kamati ilielezwa kuwa Serikali inaendelea kuandaa Kanzidata ya takwimu zitakazoonesha sifa na uwezo wa Diaspora kabla ya kutunga Sera ili matamko ya Sera hiyo yawe yamezingatia uhalisia ulipo. Aidha, Kamati ilielezwa kuwa masuala ya Diaspora yatajumuishwa katika Rasimu ya Sera ya Mambo ya Nje.

Mheshimiwa Spika, ushauri mwengine unaoendelea kufanyiwa kazi ni kuhusu Mpango wa Kujitathmini kwa Utawala Bora (APRM-Tanzania) kuwezesha kuwa Taasisi yenye Fungu lake la Kibajeti. Maelezo yaliyotolewa yalibainisha kuwa Wizara, kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora inaendelea kufanya tathmini ya suala hilo ili kuwezesha Taasisi hiyo kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Ni rai ya Kamati kuwa suala hili lipewe uzito unaostahili kwani limekuwa likishauriwa na Kamati kwa takribani miaka mitano sasa bila kukamilika.

Mheshimiwa Spika, kati ya ushauri ambao uzingatiaji wake ulikuwa na changamoto za Kibajeti ulihusu Serikali kutoa fedha za maendeleo zilizotengwa katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 kiasi cha shilingi 10,400,000,000/- na kipaumbele kiwekwe kwenye mradi wa ujenzi wa Ubalozi wa Tanzania, Muscat- Oman uliotengewa Shilingi 6,180,676,000/-. Hata hivyo, Taarifa iliyowasilishwa mbele ya Kamati ilibainisha kuwa hadi kufikia mwezi Juni, 2019 Wizara haikupokea fedha hizo kutokana na changamoto mbalimbali za Kibajeti.

Mheshimiwa Spika, Sambamba na ushauri huo, Kamati iliishauri Serikali kuweka juhudzi za dhati katika kutekeleza Mpango wa Wizara wa miaka kumi na tano (2018/2019-2031/2032) wa ujenzi, ununuzi na ukarabati wa majengo ya Ofisi na makazi katika Balozi zetu nje ya nchi. Hii itaisaidia Serikali kuokoa fedha nyingi zinazotumika kulipia Kodi ya Pango kwa majengo yaliyokodiwa kwa ajili ya makazi na Ofisi za Watumishi wa Balozi zetu nje ya nchi.

Hata hivyo, katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 Wizara ilipokea Shilingi 150,000,000.00 tu kwa ajili ya ukarabati wa makazi ya Balozi wa Tanzania Ottawa, Canada kati ya Shilingi 2,250,000,000.00 zilizokuwa zimetengwa kwa ajili ya ukarabati wa majengo katika Balozi za Tanzania Kinshasa- Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Khartoum- Sudan, Lusaka- Zambia, Ottawa- Canada na Ujenzi wa Uzio katika kiwanja cha Serikali kilichopo Ubalozi wa Tanzania Nairobi- Kenya.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla ushauri wa Kamati umefanyiwa kazi na utekelezaji upo katika hatua mbalimbali. Hata hivyo, Kamati inaendelea kusisitiza kuwa, ushauri wa Kamati kuhusu masuala ya Kisera kama vile Uandaaji wa Sera ya Mambo ya Nje na Sera ya Diaspora unapaswa kupewa uzito stahiki.

2.2 Uchambuzi wa Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipitia Taarifa ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara katika Kipindi cha Julai 2019 hadi

Machi, 2020 kwa kuchambua hali ya Ukusanyaji wa Mapato pamoja na upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina kwa kipindi hicho.

2.2.1 Ukusanyaji wa Maduhuli

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 Wizara hii ilikuwa na lengo la kukusanya Maduhuli ya kiasi cha Shilingi **2,550,879,072.00** Kati ya fedha hizo Shilingi **67,980,000.00** ni makusanyo ya Makao Makuu ya Wizara na Shilingi **2,482,899,072.00** ni makusanyo kutoka Balozi za Tanzania Nje.

Kamati ilijulishwa kuwa hadi kufikia Mwezi Machi, 2020, Wizara kuititia Balozi zake ilikuwa imekusanya Shilingi Bilioni **5,010,149,591.26** sawa na asilimia 196.4 ya lengo la ukusanyaji lililokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilijiridhisha kuwa ongezeko kubwa kwenye lengo la makusanyo lililokusudiwa halitokani na kushindwa kuweka makadirio yenyе uhalisia bali limetokana na baadhi ya Balozi kuendelea kukusanya maduhuli ya VISA ambayo yanapaswa kukusanya na Idara ya Uhamiaji. Kamati ilielezwa kuwa hali hii imeshatatuliwa tangu Mwezi Novemba, 2019 mara baada ya Balozi zote kufungiwa mtandao huo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa, mbali na fedha za VISA, Wizara ilikusanya Shilingi 385,627,026.30 sawa na asilimia 15 tu ya makadirio yaliyowekwa. Kamati ilihoji kuhusu sababu zilizochangia lengo liliowekwa kufikiwa kwa asilimia ndogo. Maeleo yaliyotolewa yilibainisha kuwa baadhi ya Balozi zinaendelea na makusanyo hususan ubalozi wa Tanzania Newyork ambapo makusanyo yake hupatikana mwezi Mei kila mwaka kulingana na ratiba ya malipo ya kodi ya pango kwa majengo yetu.

Mheshimiwa Spika, Kamati ina maoni kuwa mwenendo huu wa ukusanyaji wa Maduhuli ni wa kuridhisha na lengo liliowekwa linaendana na hali halisi na linatarajiwa kufikiwa ifikipo Mwezi Juni, 2020.

2.2.2 Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipochambua Taarifa ya upatikanaji wa Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 ilibaini kuwa hadi kufikia Mwezi Machi, 2020, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya shilingi **113,743,812,858.06** sawa na asilimia 68 ya fedha zote za Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu.

Hali hiyo ni tofauti na Mwaka wa Fedha 2018/2019 ambapo katika kipindi kama hiki Wizara ilipokea **Shilingi 93,162,476,521.00** sawa na **asilimia 52.6** ya Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa Mwaka huo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa ongezeko hilo limetokana na ongezeko la asilimia 22 kwa fedha zilizotolewa kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha, ongezeko hilo illichangiwa pia na kutolewa kwa fedha za maendeleo jumla ya shilingi **487,905,996.40** ambapo katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 fedha hizo hazikutolewa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini pia, kati ya Fedha zilizopokelewa katika Mwaka wa Fedha 2019/2020, Shilingi **106,415,481,597.66** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Fedha hizo ni sawa na **asilimia 69.6** ya Shilingi **152,717,723,000.00** zilizotengwa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Aidha, Shilingi **6,840,425,264.00** zilipokelewa kwa ajili ya Mishahara ikiwa ni sawa na **asilimia 67** ya Shilingi **10,209,097,000.00** zilizotengwa kwa ajili ya hiyo.

Mheshimiwa Spika, Aidha, kiasi cha shilingi **487,905,996.40** ni sawa na asilimia 12.2 ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, Shilingi **150,000,000.00** zilitolewa kwa ajili ya kukarabati nyumba ya makazi ya Balozi, Ottawa Canada na Shilingi **337,905,996.40** zilitolewa kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa katika Chuo cha Diplomasia, Kurasini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza Serikali kwa kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa katika Chuo cha Diplomasia, ambapo kwa mwaka wa fedha 2018/

2019 fedha za maendeleo zilitengwa kwa ajili ya Chuo hicho lakini hazikutolewa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Serikali kuendelea kukipanua Chuo hicho, Kamati ilipata maelezo kuwa umiliki wa Chuo bado ni wa nchi mbili za Tanzania na Msumbiji licha ya kuwa Serikali ya Msumbiji imekuwa haichangii gharama za uendeshaji wake tangu mwaka 1983 na kutoshiriki katika Menejimenti ya Chuo tangu mwaka 1986. Ni rai ya Kamati kuwa suala la umiliki wa Chuo cha Diplomasia likashughulikiwa kwa uzito unaostahili.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea maelezo kuwa, jumla ya shilingi **2,250,000,000.00** ambazo hazijatolewa zililenga kutekeleza miradi katika balozi za Tanzania katika nchi za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Sudan, Zambia, kujenga uzlo katika kiwanja cha Serikali katika Ubalozi wa Tanzania uliopo Kenya, na kufanya Hatua za awali za Wizara za ujenzi wa Ofisi ya Makao Makuu ya Wizara iliyopo Mtumba eneo la Mtumba jijini Dodoma.

Mheshimiwa Spika, Naomba kutoa taarifa kuwa Kamati yangu ilitembelea na Kugagua mradi huu na kubaini kuwa Wizara ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji ikiwa ni pamoja na kufanya utafiti wa udongo (*Geotechnical Investigation*) ili kuwezesha usanifu wa msingi wa jengo litakalojengwa. Ni usahuri wa Kamati kuwa Serikali inapojenja jengo hilo la Wizara izingatie mahitaji ya Kidiplomasia katika ngazi za Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ina maoni kuwa kutokutolewa fedha za maendeleo kama zilivyoishnishwa na Bunge lako Tukufu, kunaathiri utekelezaji wa miradi hiyo ambayo ina tija kwa Taifa. Upo muhimu wa Serikali kuhakikisha inatoa fedha hizo kwa ukamilifu wake.

2.3 Utekelezaji wa majukumu ya Wizara

Mheshimiwa Spika, Taarifa iliyotolewa na Wizara ilibainisha kuwa katika kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020, Wizara

iliendelea kutekeleza Sera ya Mambo ya Nje kwa kushirikiana na Taasisi nyingine za Serikali, Sekta Binafsi na Washirika wa Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majukumu yaliyotekelawa, Kamati inapongeza Wizara kwa kuendelea kuratibu ushirikiano wa Tanzania na Nchi za Asia na Australasia, Nchi za Mashariki ya Kati, Nchi za Ulaya na Marekani, ambapo fursa mbalimbali za kiuchumi zilipatikana ikiwemo kupata masoko kwa ajili ya bidhaa za mazao na madini yanayopatikana nchini, kuvutia fursa za uwekezaji na utalii hapa nchini, na vilevile kuimarisha ushirikiano katika sekta za afya, elimu, utalii na kilimo.

Katika Ushirikiano wa Kikanda, Kamati inapongeza Wizara kwa kuendelea kuratibu na kushiriki katika shughuli mbalimbali za ushirikiano na Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika, Jumuiya ya Nchi za Ukanda wa Maziwa Makuu na umaja wa Afrika. Pamoja na mafanikio mbalimbali, Kamati inapongeza makubaliano ya kukifanya Kiswahili kuwa lugha rasmi ya nne ya SADC, pamoja na kuendeleza juhudini zinazofanywa na Jumuiya ya Nchi za Ukanda wa Maziwa Makuu katika kupambana na tatizo la unyanyasaji wa kijinsia kwa kuendelea kuratibu mafunzo ya aina hiyo kwa wataalam kutoka Taasisi za Afya, Sheria na Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la ushirikiano wa Afrika, Kamati ilibaini juhudini za Serikali katika kuhakikisha kwa Mpango wa Maendeleo wa Bara la Afrika wa Mwaka 2063 (Agenda 2063) unaingizwa kwenye mipango ya Taifa ya Maendeleo. Tanzania imeendelea kujengewa uwezo na kushiriki katika warsha mbalimbali katika kuandaa taarifa za utekelezaji wa ajenda 2063.

Kamati inapongeza Serikali kwa kutajwa kufanya vizuri katika maeneo ya utoaji wa huduma za nishati na umeme, maji safi na salama na ushiriki katika ulinzi wa Amani duniani. Pamoja na pongezi hizo, ni rai ya Kamati kuwa masuala muhimu hususan yale yanayohusu matumizi ya silaha yapewe

uzito unaostahili na Taasisi zinazohusika ili kuinua uchumi wa Bara la Afrika kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la ushirikiano wa Kimataifa, Kamati vilevile inaipongeza Wizara kwa kuratibu na kushiriki Mkutano wa Jukwaa la Ngazi za Juu linaloshughulikia tathmini ya utekelezaji wa malengo ya maendeleao endelevu, mwezi Julai 2019. Katika mkutano huo Tanzania iliwasilisha utekelezaji wa Malengo Namba 4, 8, 10, 13, 16 na 17. Hata hivyo, ni rai ya Kamati kuwa Serikali iboreshe ukusanyaji wa takwimu pamoja na kuwekeza katika tafiti na matumizi ya teknolojia. Aidha, katika eneo la ushirikiano wa Kimataifa, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuwa na msimamo kuwa nchi zillizoendelea zitimize ahadi zao kwa kutoa fedha za kutosha utekelezaji wa miradi ya kukabilia na changamoto za mabadiliko ya Tabia nchi badala ya kuhamishia majukumu hayo kwa sekta binafsi zinazoendelea.

Mheshimiwa Spika, Katika kusimamia utawala na maendeleo ya watumishi Wizarani katika Mwaka wa Fedha 2019/2020, Kamati inapongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuteua Mabalozi 16 kuiwakilisha Tanzania katika nchi mbalimbali. Kati ya Mabalozi walioeteuliwa, Mabalozi watatu ni wanawake. Kamati inapongeza Mheshimiwa Rais kwa kuona umuhimu wa kuteuwa Wanawake pia kushika nyadhifa hizo.

Aidha, Kamati inapongeza kufunguliwa kwa Ubalozi mpya wa Tanzania Windhoek- Namibia katika Mwaka wa Fedha 2019/2020. Hii ni hatua nzuri kwa Tanzania kuendelea kunufaika ipasavyo na fursa mbalimbali za kiuchumi nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilihoji na kupewa maelezo kuhusu namna Serikali ilivyoratibu shughuli za Watanzania waishio nje ya Nchi (Diaspora) na kutaka maelezo kwa nini mchakato wa kutunga Sera ya Diaspora haujakamilika.

Majibu yaliyotolewa na Serikali yalibainisha kuwa kuna ukosefu wa takwimu za Watanzania waishio ughaibuni na

hivyo kuilazimu Serikali kuandaa kanzidata ya takwimu zitakazoonesha sifa na uwezo wao kabla ya kutunga Sera hiyo ili matamko yake yawe yamezingatia uhalsia uliopo. Hata hivyo, Kamati ina maoni kuwa ni vyema Balozi zetu zikachukua hatua madhubuti katika kuhamasisha Watanzania wanaoishi nje ya nchi kujandikisha. Hii ni pamoja na kuimarisha mahusiano mazuri na kuwa mstari wa mbele katika kutatua changamoto zinazowakabili diaspora.

2.3.1 Changamoto zilizojitokeza wakati wa kutekeleza Bajeti ya Mwaka 2019/2020

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipopokea Taarifa ya Wizara kuhusu utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka 2019/2020, ilibaini kuwa changamoto mbalimbali zimeendelea kuathiri utekelezaji wa majukumu ya Wizara katika kipindi cha Julai 2019 hadi Februari, 2020. Changamoto hizo ni zile zinazohusu masuala ya kibajeti ambazo Kamati imekuwa ikizisemea mara kwa mara ikiwa ni pamoja na kiwango cha ukomo wa bajeti kutoendana na mahitaji halisi ya utekelezaji wa majukumu, uchakavu na uhaba wa magari balozini na kutopatikana kwa fedha za maendeleo kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto hizo za kibajeti, Kamati imebaini kuwa uchache wa watumishi ikillinganishwa na wingi wa majukumu yaliyopo nayo imekuwa ni changamoto katika kutekeleza majukumu ya Wizara. Kamati ilijadili kwa kina changamoto hii na kubaini kuwa Serikali inafanya juhudini katika kuongeza watumishi zaidi kwa Wizara hii hususan katika Balozi zetu nje ya nchi. Ni maoni ya Kamati kuwa Serikali ipeleke watumishi zaidi kwenye Balozi zetu hususan wenye utaalamu katika masuala ya Diplomasia ya Uchumi ili kuinufaisha nchi yetu kupitia fursa mbalimbali za kiuchumi.

SURA YA TATU

3.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA BAJETI YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

3.1 Uchambuzi wa Malengo ya Bajeti

Mheshimiwa Spika, kabla ya kueleza uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, napenda kutoa Taarifa kuwa, Kamati ilielezwa kuwa, kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 Wizara imepanga kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia vipaumbele Kumi na moja.

Mfano wa vipaumbele hivyo ni pamoja na: -

- i) Kutekeleza Diplomasia ya Uchumi kwa kuvutia Wawekezaji na Wafanyabiashara kutoka nje;
- ii) Kuvutia Watalii na kushiriki katika Jumuiya za Kikanda kwa lengo la kuongeza ajira na Masoko ya bidhaa za Tanzania nje;
- iii) Kukamilisha Sera ya Mambo ya Nje;
- iv) Kuandaa Kanzidata ya Diaspora itakayotoa taarifa itakayotoa mwongozo wa namna ya kuwashirikisha Diaspora wa Tanzania katika kuchangia maendeleo ya nchi yao; na
- v) Kuendelelea kutoa elimu kwa umma juu ya fursa zitokanazo na Mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya zingine za Kikanda.

Vile vile, Wizara kwa kupitia Balozi zetu itaendelea kutafuta mitaji ya uwekezaji, masoko na kuhamasisha Diaspora kuchangia kwenye maendeleo ya nchi kwa kutangaza vyema miradi ya vipaumbele a vivutio vinavyotolewa na Serikali katika maeneo yao ya uwakilishi.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati kuhusu vipaumbele umebaini kuwa ukamilishaji wa Sera ya Mambo ya Nje imekuwa ni kipaumbele kinachojirudia mara kwa mara licha ya kwamba Kamati imekuwa ikishauri kuhusu umuhimu wa kukamilisha Sera hiyo. Kamati ina maoni kuwa ni vema sasa kipaumbele cha kuandaa Sera hiyo kikapewa uzito unaostahili kwani jambo hili limekuwa likizungumziwa na Kamati tangu ilipoundwa mwaka 2016.

Aidha, tofauti na Mwaka wa Fedha 2018/2019, kipaumbele cha kuandaa Sera ya Diaspora hakijawekwa tena. Maeleo yaliyotolewa yalibainisha kuwa masuala ya Diaspora yatajumuishwa katika Sera ya Mambo ya Nje. Kwa msingi huu, ni rai ya Kamati kuwa suala la kukamilisha Sera ya Mambo ya Nje linapaswa kupewa uzito unaostahili hasa kwa kuzingatia kuwa Sera inayoandaliwa itajumuisha masuala hayo ya Diaspora na ya mtangamano wa Afrika Mashariki.

3.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipitia Makadirio ya ukusanyaji wa Mapato yanayopendekezwa kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021. Katika uchambuzi huo, Kamati ilibaini kuwa Makadirio hayo yanapishana kwa kiasi kidogo sana na makadirio ya Mwaka wa fedha unaoishia. Katika Mwaka wa Fedha 2019/2020, Wizara ilikuwa na lengo la kukusanya Shilingi **2,550,879,072/-** wakati kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, Wizara inalenga kukusanya kiasi cha Shilingi **2,550,879,000/-** ikiwa ni pungufu kwa shilingi **72/-** tu.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa makadirio haya yanaendana kwa kuwa Mapato yatokanayo na malipo ya Visa kwa sasa yanakusanywa na Idara ya Uhamiaji kupitia mtandao wa kielektroniki (e-visa) ambapo Fedha hizo zinalipwa moja kwa moja kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali badala ya kukusanywa na Ofisi za Balozi kama ilivyo kuwa hapo awali.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwu kuwa Shilingi **2,550,879,000/-** zinalengwa kukusanywa kutoka katika vyanzo vilivyopo katika Makao Makuu ya Wizara na katika Balozi za Tanzania Nje ya Nchi. Vyanzo hivyo ni pamoja na pango la nyumba za Serikali zilizopo nje ya nchi, kuthibitisha nyaraka na mauzo ya zabuni. Aidha, Kamati ilibaini kuwa ni Balozi tano tu za Tanzania nje ya Nchi katika Majiji ya Lusaka, New York, Paris, Maputo na Harare ambazo zinakusanya mapato ya Serikali kupitia pango la Nyumba za Serikali.

Mheshimiwa Spika, baada ya kufanya uchambuzi wake, Kamati imejiridhisha kuwa lengo lilitolovekwa limeendana na hali halisi.


3.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, Wizara ilileza Kamati kuwa inaomba kuidhinishiwa kiasi cha Shilingi **199,750,684,000/=**. Kati ya fedha hizo, Shilingi **167,717,723,000/=** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC), Shilingi **12,032,961,000/=** ni kwa ajili ya Mishahara na Shilingi **20,000,000,000/=** ni kwa ajili ya kugharamia Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilichambua maombi hayo na kuona kuwa asilimia **84** ya fedha zinazoombwa ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC), asilimia **6** ni kwa ajili ya Mishahara na asilimia **10** ni kwa ajili ya kugharamia Miradi ya Maendeleo kama inavyoonekana katika Chati Na. 1 ya Taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi Kamati imebaini kuwa, kwa uwiano katika Mwaka wa fedha 2019/2020, matumizi mengineyo ilikuwa asilimia 91.5 , mishahara asilimia 6.1 na maendeleo asilimia 2.4. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuongeza fedha za maendeleo katika mwaka huu wa fedha ambapo kiuwiano ni asilimia 10 ya fedha zote zinazoombwa kuidhinishwa kwa ajili ya matumizi ya Wizara hii.

Chati Na. 1: Uwiano wa Fedha zinazoombwa kwa Matumizi ya Wizara



Chanzo: Randama ya Wizara 2020/2021

Mheshimiwa Spika, vile vile, katika uchambuzi wake, Kamati imebaini kuwa Bajeti inayoombwa imeongezeka kwa asilimia 19.7 ikilinganishwa na Bajeti iliyoidhishwa katika Mwaka wa Fedha 2019/2020. Ongezeko hili lipo katika maeneo yote matatu ya matumizi ambayo ni Matumizi Mengineyo (OC), Mishahara na Fedha za Maendeleo. Bajeti ya Mishahara imeongezeka kwa asilimia **17.8**, Matumizi Mengineyo imeongezeka kwa asilimia **19.7** na Maendeleo imeongezeka kwa asilimia **400**.

Mheshimiwa Spika, sura ya uwiano wa Bajeti iliyotengwa kwa vipengele hivyo vitatu kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 na Mwaka wa Fedha 2020/2021 inaonekana katika Jedwali Na. 1.

Jedwali Na. 01: Uwiano wa aina za Bajeti ya Matumizi na ulinganisho wake kwa Mwaka 2019/2020 na 2020/2021

MWAKA	2019/2020		2020/2021		% ONGEZEO
	AINA YA MATUMIZI	KIASI	ASILIMIA	KIASI	ASILIMIA
MISHAHARA (PE)	10,209,097,000.00	6.1	12,032,961,000.00	6	17.8
MATUMIZI MENGINEYO (OC)	152,717,723,195.00	91.5	167,717,723,000.00	84	19.7
MIRADI YA MAENDELEO	4,000,000,000.00	2.4	20,000,000,000.00	10	400
JUMLA	166,926,820,000.00	100	199,750,684,000.00	100	

Chanzo: Randama ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano 2020/2021

Mheshimiwa Spika, kutoekana na uchambuzi wa uwiano wa Bajeti kama inavyoonekana hapo juu, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuonesha nia njema katika kutekeleza Mpango wake wa Miaka 15 wa Ujenzi, Ununuzi na Ukarabati wa Majengo ya Ofisi na Makazi katika Balozi kwa kuongeza bajeti ya Maendeleo kwa asilimia 400 kwa Mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilijiridhisha kuwa miradi muhimu ambayo Kamati imekuwa ikiisemea mara kwa mara tangu Mwaka wa Fedha 2018/2019 ikijumuisha miradi ya kupanua na kuboresha miundombinu ya Chuo cha Diplomasia, ujenzi wa Ubalozi wa Tanzania- Oman, pamoja na ujenzi wa uzio katika viwanja vya Serikali, imezingatiwa na kutengewa fedha.

SURA YA NNE

4.0 MAONI NA USHAURI

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwasilisha uchambuzi wa Kamati kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, naomba sasa niwasilishie Maoni na Ushauri wa Kamati: -

i) Upo umuhimu kwa Serikali kutoa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, ifikapo Juni 30, 2020. Katika Mwaka huu wa Fedha, ni asilimia 12.2 tu ya Shilingi 4,000,000,000 zilizoidhinishwa ndiyo iliyotolewa. Kutolewa kwa fedha hizi kutafanikisha utekelezaji wa shughuli zilizopangwa kutekelezwa katika balozi za Tanzania nje ya nchi na katika chuo cha Diplomasia Kurasini, kwa manufaa mapana ya nchi yetu.

Sambamba na hilo, Kamati inaisisitiza Serikali katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, kutoa kipaumbele katika kuipelekea fedha za maendeleo miradi ambayo ina umuhimu wa kipekee kiuchumi, kwa mfano, ujenzi wa Ubalozi wa Tanzania, Muscat- Oman. Ni imani ya Kamati kuwa Serikali itapata fursa nyingi za kiuchumi endapo itafanikiwa kujenga Ubalozi nichini Oman ikizangatiwa kuwa Oman ni miongoni mwa nchi zenye uchumi mzuri Duniani. Kamati imekuwa ikilisemea suala hili kwa muda wa miaka miwili sasa.

ii) Kamati inaipongeza Serikali kwa kutenga Jumla ya Shilingi Bilioni ishirini (20) kwa ajili ya miradi ya maendeleo ikiwa ni utekelezaji wa Mpango wa Miaka Kumi na Tano (2018/2019-

2031/2032) wa Ujenzi, Ununuzi na Ukarabati wa Majengo ya Ofisi na Makazi katika balozi zetu. Hata hivyo, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuhakikisha kuwa fedha hizo zinatolewa kwa wakati ili kufanikisha utekelezaji wa Mpango huo muhimu. Kamati inaamini kuwa Serikali itaokoa fedha nyingi zinazotumika kulipia pango. Aidha, Serikali itaongeza mapato yatokanayo na nyumba zake kukodishwa kama ilivyo sasa katika majengo ya Ubalozi wa Tanzania Maputo-Msumbiji, Lusaka-Zambia, New York- Marekani, Paris- Ufaransa na Harare Zimbabwe.

- iii) Kwa takribani miaka mitano sasa Wizara imekuwa ikieleza Kamati kuwa inaendelea na mchakato wa kuandaa Sera ya Mambo ya Nje lakini hadi sasa Sera hii hajakamilika. Sera hii, pamoja na mambo mengine, itajumuisha masuala muhimu yanayohusu mtangamano wa Afrika Mashariki na kutoa muongozo wa masuala mbalimbali ambayo kwa sasa hayana muongozo rasmi. Ni rai ya Kamati kuwa Serikali ikamilishe mchakato wa Sera hii ndani ya Mwaka 2020/2021.
- iv) Pamoja na maelezo mazuri ya Serikali kuhusu uandaaji wa Kanzidata ya takwimu za Diaspora kabla ya kutunga Sera yao Mahsus, bado Kamati inasisitiza kuwa upo umuhimu wa kuwa na Sera ya Taifa ya Diaspora. Sera hiyo itawezesha Watanzania wanaoishi nje ya nchi kuchangia zaidi katika Maendeleo ya Tanzania.
- v) Kwa kipindi cha takriban miaka mitano sasa Kamati imekuwa ikishauri Serikali kuona umuhimu wa Mpango wa Kujitathmini kwa Utawala Bora- Tanzania (APRM – Tanzania) kuwa na Fungu lake la Bajeti. Kamati inaishauri Serikali kulipa suala hili uzito unaostahilli na hatimaye APRM-Tanzania ipate Fungu lake la Bajeti kwani suala hili limekuwa likishauriwa kwa muda mrefu sasa. Hii itawezesha APRM-Tanzania kutekeleza shughuli zake kwa ufanisi zaidi.
- vi) Kwa takribani miaka mitatu sasa Kamati imekuwa ikielezwa kuwa suala la umiliki wa Chuo cha Diplomasia linaendelea kushughulikiwa na Tume ya Pamoja ya Kudumu ya Ushirikiano (Joint Permanent Commission) licha ya kuwa Serikali ya

Jamhuri ya Msumbiji imesitisha kuchangia gharama za uendeshaji na uendelezaji wa Chuo hicho.

Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuhakikisha kuwa ajenda hii inafikishwa na kushughulikiwa ipasavyo katika Mkutano wa 15 wa Tume ya Pamoja ya Kudumu ya Ushirikiano kati ya Tanzania na Msumbiji.

vii) Kwa kuwa kumekuwa na kasi ndogo ya sekta binafsi kutumia fursa za biashara na uwekezaji zitokanazo na mtangamano wa Arika Mashariki na masoko ya Kimataifa, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuendelea kutoa elimu kwa Umma kuhusu fursa zitokanazo na Mtangamano wa Afrika Mashariki, Masoko ya Kimataifa na katika Jumuiya mbalimbali za Kikanda ambazo Tanzania ni Mwanachama ikiwemo Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

viii) Kamati inaipongeza Wizara kwa kuendelea kuratibu masuala ya mabadiliko ya tabia nchi katika ngazi ya Kimataifa. Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuwa na msimamo kuhusu nchi zilizoendelea kutimiza ahadi zao kwa kutoa fedha za kutekeleza miradi ya kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya tabia nchi (full support in terms of grants) badala ya kuhamishia majukumu hayo kwa nchi zinazoendela.

ix) Sambamba na ushauri uliotolewa hapo juu, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuendelea kuimarisha ushirikiano na wadau wa Kimataifa wa Mabadiliko ya Tabia Nchi ili kukabiliana na changamoto na athari za tabia nchi bila ya kuathiri maslahi ya nchi yetu.

x) Kamati inaipongeza Serikali kwa kufungua Ubalozi mpya Windhoek- Namibia ikiwa ni mwendelezo wa kuongeza fursa mbalimbali za kiuchumi nje ya nchi. Sambamba na ufunguaji wa Balozi Mpya, Kamati inatambua kuwa kuna uchache wa watumishi ikilinganishwa na majukumu yaliyopo katika Balozi zetu, hivyo Kamati inaishauri Serikali kupeleka watumishi wa kutosha kwenye Balozi zetu ikiwemo wataalam wa masuala ya Diplomasia ya uchumi.

- xi) Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kutangaza vivutio vya utalii kupitia Balozi zake nje ya nchi hususan kwa vivutio vilivyo katika ukanda mpya wa Kusini. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuendelea na juhudhi hizo ili kukuza pato la Taifa.
- xii) Serikali iendelee kutafuta mbinu za kutumia kikamilifu soko la nchi ambazo tuna mahusiano nayo mazuri ya kihistoria kama vile China, India na Nchi za Kiarabu katika kuuza bidhaa zetu hususan za kilimo na mifugo.

SURA YA TANO

5.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Taarifa hii. Napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama amba maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao kama yalivyoorodheshwa yaingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard): -

1. Mhe. Salum Mwinyi Rehani, Mb, **M/Mwenyekiti**
2. Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, Mb
3. Mhe. Mussa Hassan Mussa, Mb
4. Mhe. Prosper J. Mbena, Mb
5. Mhe. Victor Kilasile Mwambalasa, Mb
6. Mhe. Fakharia Shomari Khamis, Mb
7. Mhe. Cosato David Chumi, Mb
8. Mhe. Bonnah L. Kamoli, Mb
9. Mhe. Masoud Abdallah Salim, Mb
10. Mhe. Sophia Hebron Mwakagenda, Mb
11. Mhe. Gerson Hosea Lwenge, Mb
12. Mhe. Shally Josepha Raymond, Mb
13. Mhe. Dkt. Suleiman Ally Yussuf, Mb
14. Mhe. Joram Ismael Hongoli, Mb
15. Mhe. Zacharia Paulo Issaay, Mb
16. Mhe. Joseph Michael Mkundi, Mb

17. Mhe. Mboni Mohamed Mhita, Mb
18. Mhe. Fatma Hassan Toufiq, Mb
19. Mhe. Sebastian Simon Kapufi, Mb
20. Mhe. Silafu Jumbe Maufi, Mb
21. Mhe. Ruth Hiyob Mollel, Mb
22. Mhe. Janeth Maurice Masaburi, Mb
23. Mhe. Augustino Manyanda Masele, Mb
24. Mhe. Almasi Athuman Maige, Mb
25. Mhe. Dkt. Charles John Tizeba, Mb

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kutumia fursa hii kumshukuru Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Mhe. Prof. Palamagamba Kabudi, (Mb), Naibu Waziri, Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro (Mb) Katibu Mkuu Balozi Kanali Wilbert Ibuge, Naibu Katibu Mkuu Ndg. Ramadhan Muombwa pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano na mchango wao wakati wa uchambuzi wa Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini si kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Stephen Kagaigai kwa kuiwezesha Kamati kukamilisha kazi yake kwa wakati. Aidha, nawashukuru Ndg. Michael Chikokoto Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndg. Gerald Magili Mkurugenzi Msaidizi, Makatibu wa Kamati hii Ndg. Ramadhan Abdallah na Bi. Grace Bidya wakisaidiwa na Bi. Rehema Kimbe, kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu liipokee Taarifa hii na likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Salum Mwinyi Rehani, Mb

MAKAMU MWENYEKITI

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI
NA USALAMA**

Mei, 2020

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, sitamwita Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzania Bungeni kwa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, kwa sababu taarifa yake haikuwekwa mbele ya Bunge.

Kwa hiyo, tumemaliza mawasilisho, sasa ninayo majina hapa kutoka vyama mbalimbali vyenye uwakilishi Bungeni. Nitaanza kuwaita kadri ya taratibu zetu lakini niwataje Waheshimiwa Wabunge watakachangia kutoa Msekwa ili waelekee huko sasa kama wapo hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Taska Restuta Mbogo, atachangia kutoka Msekwa; Mheshimiwa Cosato David Chumi, atachangia kutokea Msekwa; Mheshimiwa Ally Saleh atachangia kutoka Msekwa; na kama watatokeza wengine pia nitawataja.

Tunaanza na Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Suzan Alfonsi Kolimba na Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo ajiandae.

MHE. SHAMSI VUAI NAHODHA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kutoa mchango wangu katika Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

(Hapa microphone ilipiga kelele)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Nahodha subiri kidogo. Wataalam wa mitambo sijui kama kuna *mic* imewashwa mahali ama kuna tatizo gani? Kwa sababu tusingetaka uhame kutoka hapo, ngoja niite Mheshimiwa Mbunge mwingine, wakisharekebisha utaweza kutumia tena.

MBUNGE FULANI: Nimeshazima huku.

NAIBU SPIKA: Kuna Mbunge amezungumza! Sijui amezungumza nini?

MBUNGE FULANI: Ilikuwa huku, imeshazimwa.

NAIBU SPIKA: Aah, mmeshazima! Haya ahsante sana. Mheshimiwa Nahodha.

MHE. SHAMSI VUAI NAHODHA: Mheshimiwa Naibu Spika...

(Hapa microphone ilikuwa haisikiki vizuri)

NAIBU SPIKA: Haya, Mheshimiwa Nahodha, nitakupa fursa tena baadaye wakisharekebisha *microphone* yako kwa nini inapiga kelele hapo.

Mheshimiwa Dkt. Susan Alfonsi Kolimba, atafuatiwa na Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo na Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim ajiandae.

MHE. DKT. SUSAN A. KOLIMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi siku ya leo nami niweze kuchangia hoja iliyoko mbele yetu, hoja ya hotuba ya bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Awali ya yote, naomba niwapongeze sana Wizara hii na hasa Waziri wa Mambo ya Nje, Naibu Waziri wa Mambo ya Nje, Mtendaji Mkuu wa Wizara hii pamoja na wataalam pamoja na Mabalizi wote ambao wamekaa, wameweka fikra zao, weledi, wamejitoa muhanga katika kuitetea Tanzania kulinda maslahi yake na kujenga mahusiano yaliyo

bora na kuhakikisha kwamba Tanzania yetu inapata fursa zote na kuweza kuifanya isimame na kuendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa na mambo machache sana ya kuchangia hoja hii na hasa mambo ya ushauri na pia ya kuwapongeza. Suala la kwanza, naomba niipongeze Wizara ya Mambo ya Nje kwa kufanya kazi kubwa sana ya kutumia Sera ya Diplomasia ya Uchumi katika kuhakikisha kwamba wanazidaka na kuzipigania fursa zote zilizoko nje ya nchi kwa kutumia Mabalozi wetu ambao wanafanya kazi usiku na mchana kwa kutumia Maafisa waliloko nje ya nchi ili kuhakikisha kwamba zile fursa zote na miradi yote ambayo inaletwa Tanzania na inayofanywa katika Sekta mbalimbali za Nishati, Elimu, Viwanda na Biashara na Afya zinakamilika na zinatekelezwa ili kuhakikisha kwamba inachangia pato la Taifa. Kwa namna ya kipekee naomba tuwapongeze sana na kuwapigia makofi kwa kazi hiyo kubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kutaka kumpongeza Mwanadiplomasia namba moja wa nchi yetu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli ambaye amefanya kazi kubwa ya weledi, amejitoa muhangaa kwa ajili ya nchi hii, amefanya kazi ya kushawishi kazi ya kujenga diplomasia akiwa ndani ya nchi na nje na vilevile kazi ya kujenga taswira ya nchi kwa kufanya kwa matendo na watu kumuiga kwa yale ambayo anatekeleza ndani ya nchi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, unaweza ukapatwa na wasiwasi pale ambapo unaona baadhi ya Watanzania na baadhi yetu humu ndani ya Bunge hili la Jamhuri wanapobeza kazi kubwa inapofanywa na Mwanadiplomasia namba moja, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, anapopigania nchi katika masuala mbalimbali. Nikienda kwenye suala la kutumia fursa ya lugha ya Kiswahili, Mwanadiplomasia huyu ametumia weledi wake kama Mkuu wa nchi kuteta, kuzungumza na kushawishi Marais mbalimbali katika nchi za Kiafrika ikiwemo Afrika Kusini, Namibia, Ethiopia, Zimbabwe na nchi nyingine nyingi tu, ukiziorodhesha hapa muda utakuwa hautoshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuishauri Serikali na Wizara kwenye suala hili la kuitumia lugha ya Kiswahili kama fursa ya kuweza kutatua changamoto ya ajira kwa vijana wetu na wataalaam wetu waliosomea Kiswahili ambaao wanafanya kazi ya kufundisha na kufasiri Kiswahili. Kwa sababu wataalam hawa tunao, Mheshimiwa Rais ameitendea haki nafasi yake. Wizara hii ya Mambo ya Nje imeitendea haki nafasi yake na Balozi zetu zimetendea haki nafasi zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilikuwa nashauri kwamba Wizara hii ishirikiane na Wizara mtambuka ambazo ni wadau wakubwa wanaohusika na suala la lugha ya Kiswahili wakiwemo Wizara ya Elimu ya Juu, Wizara ya TAMISEMI, mahali ambapo tunao walimu wengi ambaao pengine wamefundishwa na wamefuzu kufundisha Kiswahili na wengine wafasiri waweze basi kutumika katika kuhakikisha kwamba wanatengeneza mkakati wa pamoja wa kuweza kutumia fursa ambazo tayari zimeshawekwa katika nchi hii ili kuweza kuitumia fursa ya kutumia kufundisha na kufasiri Kiswahili katika nchi ambazo nimezitaja na nyngine katika nyanya za Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nimpongeze Mheshimiwa Rais kwenye suala hili ambapo alipokuwa ameshawishi katika Wizara hii kwenye Mkutano wake wa *SADC* ambapo walipitisha kwamba Kiswahili kiwe lugha ambayo inatumika katika Mikutano ile ya *SADC*. Naomba fursa hii isipotee, tuitumie, tuweke mkakati wa haraka wa kuhakikisha kwamba isije ikachukuliwa na watu wengine wakati sisi wataalam tunao.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine, naomba niisemee Wizara hii ; wengine wanaweza kufikiri kwamba Wizara hii inashughulikia tu Mambo ya Nje na kwa uelewa mfupi wanafikiri kwamba labda Wizara hii haishughulikii mambo ya ndani. Ukipikia kwamba inashughulikia masuala ya sera ya nje, lakini pia inashughulikia sera za ndani kwa sababu haya yote ni fungamanishi. Wanaratibu na

kutengeneza mkakati wa kutafuta miradi mbalimbali na fursa mbalimbali nje ya nchi na kuhakikisha wanazileta ndani ya nchi na zinaenda kwenye sekta mbalimbali na sisi tunaona zinatokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Wizara hii sasa naona ina changamoto kubwa sana hasa katika ukomo wanaopewa wa kibajeti kuanzia mwaka wa 2015/2016 mpaka sasa hivi. Naishauri Serikali kwa pamoja wahakikishe kwamba ukomo unaowekwa kwa Wizara hii kwa sababu inafanya kazi kubwa, uwe unatolewa kama ulivyokuwa umepangwa. Nasema hivyo kwa sababu Wizara hii katika kipindi hicho cha mwaka 2016 mpaka sasa hivi walikuwa na mkakati mkubwa wa kukarabati majengo yao nje ya nchi lakini vilevile majengo ya ofisi na makazi waliyonayo ambayo yamechakaa, kiasi kwamba baadhi ya Maafisa au baadhi ya Ofisi za Kibalozi zimekwenda kupanga katika majengo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tukiwekeza kama Serikali na kama nchi tukiamua kuwapa na kuhakikisha kwamba ule mkakati wao wanauwasilisha Bungeni na kuombea pesa wakapewa na pesa hizo zikatumika katika kila mwaka katika mpango wa Bajeti ya Wizara hii, wangeweza kuwa mbali tungepunguza gharama kubwa sana ya uendeshaji kwa Balozi zetu nje ya nchi lakini vilevile tungeweza kuwezesha Wizara hii kuongeza kipato zaidi na hasa ukusanyaji wa Dola kwenye sehemu zile ambazo Ofisi au makazi yanaweza yakapangishwa au yakawekezwa katika sehemu ya biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine ni kwamba katika Wizara hii kwenye mkakati wake wa ukarabati na ujenzi wa majengo tunavyo viwanja takriban katika nchi 12. Viwanja hivi ni vyetu, vina hati zetu. Ninaomba katika miaka mitano ijayo kwenye Bunge lijalo basi tuipe kipaumbele; kwamba hizi ardhi na majengo tuliyonayo nje ya nchi yawekezwe na kuhakikisha kwamba yanatoa kipato na kuongeza kodi kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, niipongeze Wizara hii, kwanza kwa kufanyakazi nzuri ya kuendelea kila mwaka kuhakikisha kwamba wanaratibu, kuhudhuria na kushiriki katika makongamano ya *Diaspora*. Tunazungumza mara nyingi sana kwenye nchi nyingine kwamba *Diaspora* wanatumika vizuri; na wao kama Wizara wameanza vizuri; na tunaona mwaka jana wamefanyakazi kubwa ya kuhakikisha kwamba wameratibu makongamano ya *Diaspora*, makongamano ambayo yanatupa sisi fursa ya kuitanganza Tanzania na kudaka fursa za uchumi zilizopo nje ya nchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu ni kwamba; yanapofanyika makongamano kama haya waendelee kuzitumia pia sekta nyingine kuwaunganisha wale ambaao ni wadau wakubwa, wale ambaao tunaweza tukasema kwamba tunaweza kwenda kuzitangaza fursa humo ndani; ikiwemo Wizara ya Ardhi ambaao kwa kiasi kikubwa wao wamewezesha na kuhakikisha *Diaspora* wanaweza kuwa na nyumba za kutosha na kuweza kununua nyumba, lakini pia kuweza kuwa na ardhi ya kuwezesha uwekezaji.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Kengele ya pili imeshagonga.

MHE. DKT. SUSAN A. KOLIMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja na nawapongeza sana Wizara hii, Waziri, Naibu Waziri na watu wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, ahsante sana, shukurani. Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo atachangia kutoka Msekwa atachangia na Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mheshimiwa Vuai sijaona mtu amekuja hapo lakini nadhani utawenza kuchangia kutoka kwenye Kiti cha Mheshimiwa Spika pale nyuma kabisa kitie cha mwisho pale nyuma hakuna

Mtu anaongea kutokea pale. Sasa nimuite Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo kutokea Msekwa.

MHE. TASKA R. MBOGO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunjpa nafasi kuchangia hoja hii ya Wizara ya Mambo ya Nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda kumpongeza Mheshimiwa Palamagamba Kabudi, Waziri pamoja na naibu wake Mheshimiwa Damas Ndumbaro kwa kazi nzuri wanazofanya kuhakikisha kwamba Tanzania inafahamika ulimwenguni; na dunia inatambua kwamba Tanzania ipo. Kazi imefanyika na ni nzuri. Nawapongeza sana kwa juhudhi zao hizo walizofanya kuhakikisha kwamba masuala ya Tanzania yanakuwa kwenye ramani ya kufahamika duniani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza pia watendaji wote wa Wizara ya Mambo ya Nje kwa kazi nzuri, nawapongeza Mabalozi wote waliopo huko nje wakituwakilisha sisi kama Watanzania, nawapongeza sana.

Ninawaomba tu kwamba waendelee kuitangaza Tanzania kwenye Balozi zao, wachukue bidhaa ambazo zinatoka Tanzania kama majani ya chai, kahawa waziuze kwenye maduka yao ya ubalozi; kwasababu nafahamu kila *embassy* huwa inakuwa na duka pale ubalozini; kuna *embassynyingine* ukienda unakuta kuna duka pale ubalozini; basi niwaombe tu watumie yale maduka yaliyopo ubalozini kwenye *embassy* zetu kwa kutangaza bidhaa zetu za Tanzania. Watangaze bidhaa zote ambazo zinatuletea uchumi nchini Tanzania na pia niwaombe Mabalozi wote na watendaji walioko nje ya nchi pia waitangaze nchi yetu kwamba ni nchi nzuri sana ili watalii wengi waweze kuja nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia niwaombe hao Mabalozi waitangaze Tanzania kwa kututafutia wawekezaji waje kwa wingi nchini kwetu. Maana jinsi wao watakavyokuwa wanailezea nchi yetu kule nje ndivyo jinsi

ambavyo tutapata wawekezaji wazuri kuja kuwekeza nchini kwetu Tanzania. Kwahiyu niwaombe Mabalozi watumie hizo nafasi ambazo wamepewa kuitangaza nchi yetu na kutuletea waekezaji ili tupate wawekezaji wengi nchini kwetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ningependa kuchangia suala lingine, kuhusu Watanzania ambao wanakaa nje ya nchi. Ninafikiri niliwahi kuuliza swali Bungeni kuhusu Watanzania ambao wanakaa nje ya nchi yetu na Mheshimiwa Naibu Waziri Ndumbaro alinijibu kwamba wako Watanzania nafikiri takribani zaidi ya milioni moja nje ya nchi ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naiomba Serikali ijaribu kuangalia utaratibu ni vipi Watanzania hawa ambao wako nje ya nchi wanawezaje wakawa ni Watanzania na pia wakawa raia wa huko waliko. Nalisema hili kwasababu wale watu kule wameeo, wana familia, ina maana wana watoto, watakuwa pia na wajukuu, lakini asili yao ni Watanzania; sasa kama asili yao ni Watanzania Serikali ingejaribu kuangalia utaratibu wa kuleta nchini *duo citizen* ili tusiweze kupoteza kizazi hiki cha Tanzania kilichoko huko Duniani. Kwa sababu tukija na *point* ya kusema kwamba hatutaki kuleta *duo citizen* kwasabbau ya kuogopa mambo ya *security* hiyo *point* nafikiri sasa hivi inaweza ikawa si nzito sana; ukiangalia kwamba sasa hivi tuna vitambulisho vya uraia, ukibonyeza tu *Computer* hapo "*tap*" utakuja jina linatoka Taska Restituta Philip Mbogo, mzaliwa wa wapi? Mpanda-Tanzania sasa na yule aki-*click* itaonesha hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia ili na wao wawewe kuja kuendeleza hii nchi, kwasababu mtu anapokuwa kule nje anachuma, anapata kipato, anapata pesa. Sasa, akijua kwamba mimi bado ni raia wa Tanzania atawekeza zaidi, kuliko ukimnyima unasema kwasababu wewe umeshachukua uraia wa nchi nyingine kwahiyu usirudi tena hata ye ye anaingia ule ubaridi wa kuja kuwekeza huku. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini zaidi ya hapo wanapokuja huku, wanakuwa pia wanasumbuliwa hapo *TIC*, hawapewi ile *greenlight* kama Watanzania. Tuangalie ni jinsi gani tunaweza kubadilisha hizi Sheria zetu kama *Citizenship Act* ili iweze ku-*accommodate* Watanzania walioko nje kuliko kuwapoteza kile kizazi kibaki kukaa; nje kwasababu kile ni kizazi chetu, ni kizazi cha Watanzania inabidi tukifuatilie; na hakuna mtu anasahau kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mzuri naweza nikajitolea mimi mwenyekiti, nimekaa Arusha kwa zaidi ya miaka 30 lakini sijasahau kwenda Mpanda. Hata nilipotaka Ubunge nilienda kugombea Mpanda kwasababu ndiko kwetu, hakuna mtu ambaye anasahau kwao, na Watanzania walioko nje hawawezi kusahau Tanzania. Tuwa-*accommodate* tuone tunakaa nao vipi kuliko kusema kwamba kwasababu wamechukua passport za nje wanakaa nje basi tuwaache.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kusema *security* kwa sasa hivi kwa mambo ya uraia na jinsi dunia ilivyo kwenye simu mtu akibonyeza tu hapa tulipo simu zetu hizi zinaonesha mpaka *location*; sasa suala hilo hatuweze tukasema hatutaki kuwa-*accommodate* kwasababu ya *security*. Tuangalie kama hatutaki kuja kugombea nafasi za siasa wanaweza wakapewa uraia pacha lakini wakawekewa *condition* kwamba wasiingie kwenye nafasi za kuchanguliwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini zaidi ya hapo, juzi juzi hapa Serikali ilitoa uraia kwa wageni wakimbizi ambao hawajazaliwa Tanzania laki moja na nusu, ni namba kubwa sana...

MHE. RASHID A. SHANGAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa

MHE. TASKA R. MBOGO: ...sasa unaweza kuniambia wale watasahau kwao walikotoka? Lazima watakuwa na mawasiliano.

MHE. RASHID A. SHANGAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa

TAARIFA

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Taska Mbogo kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Rashid Sangazi.

MHE. RASHID A. SHANGAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Napenda tu kumpa taarifa mzungumzaji anayeendelea kusema kwamba tunaposema raia wa nje haimaanishi nje ni Ulaya, labda na mataifa ya mbali hata hizi nchi nane ambazo tunapakana nazo hapa pia ni nje ambapo pia kuna Watanzania walioko huko wanafanya shughuli ndogo ndogo hata za kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda tu kumpa hiyo taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo unaipokea taarifa hiyo?

MHE. TASKA R. MBOGO: Naipokea kwa mikono miwili taarifa hiyo, ni sahihi. sisi tumezungukwa na Malawi, Zambia, Uganda, Rwanda na Burundi; kuna Watanzania huko wanafanya biashara na wao pia wanakuja huku nchini kwetu wanafanya biashara; na tunao wengi mpaka maeneo ya Kariakoo, wakati mwininge mpaka hapa hapa Dodoma wapo wanakuja kufanya biashara. Kwahiyo tuangalie jinsi gani tutaweza kuwa-*accommodate* Watanzania hawa, tusipoteze kizazi chetu kikabaki huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, na sheria zilitungwa, lakini kwa wakati ule labda mambo ya *security* yalikuwa ndiyo namba moja na wakati huo hakukuwa na hizi *computer*, hazikuwepo na hata simu za mkononi hazikuwepo. Sasa hivi kila kitu kinakuwa *controlled* kwenye simu, dunia ipo mkononi, iko kwenye simu; kwahiyo suala la kusema kwamba mtu

akiwa na uraia pacha ata-*damage security* hilo nafikiri tujaribu tuliangalie tunalifanyaje kazi na tujaribu kuangalia jinsi gani tuta-*accommodate* kizazi chetu kisipotee nje ya nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuchukue mfano; kuna wale wacheza mpira wawili wale mtu na mdogo wake, mapacha wale wa timu ya Senegal wanachezea Ujerumanu na Senegal. Kwahiyu tunaweza tuka-*accommodate* vitu kama hivi na sisi tukaweza kuishi navyo humu nchini kwetu Tanzania; na ukiangalia na nchi nyngine za jirani zimeweza ku-*accommodate* hilo suala la uraia pacha.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo ningependa kulizungumza ni suala la *East African Community*. Ningependa suala la *East African Community* elimu itolewe. Ukianiambia vijijini, ukienda kule Mpanda ukimuuiliza mtu mambo ya Jumuiya ya *East Africa* haelewi na wala haelewi tumeungana nini na kitu gani hatujaungana. Kwahiyu, naomba elimu itolewe watu waelewe maana hii *East African Community* tumeungana nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim atafuatiwa na Mheshimiwa Shams Vuai Nahodha, Mheshimiwa Joseph Raman Selasini ajiandae.

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

Namshukuru Mwenyezi Mungu sub-hanahu wataala ametujaalia afya njema katika Mwezi huu Mtukufu wa Ramadhanu tuliendelea na kumi hili la maghfira kuomba kusamehewa madhambi na Allah subhanahu-wataala kwa matendo ya kibinadamu tunayoyafanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala zima la ugonjwa huu wa *covid19* au *corona* limekuwa ni tatizo kubwa na tumeshuhudia kwenye vyombo veya habari au kwenye picha mbalimbali. Hata leo taarifa ya Mheshimiwa Waziri akieleza juu ya safari yake ya Madagascar kurudi hapa na kupokea zile dawa. Mheshimiwa Waziri ni vyema ukatuhakikishia kwa ukatuambia hasa, je, dawa hiyo mafanikio yake hadi sasa yakoje na manufaa yake yakoje na utafiti wake kama ilivyosemwa kwenye vyombo veya habari ukoje? Utupe maelezo juu ya dawa hii kutoka Madagascar.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tumeona Mabalozi wale wa Uingereza, Ufaransa na Umoja wa Ulaya wakitangaza kwamba wameisaidia Tanzania dawa ya kupambana na *covid19* au dawa hizi za *corona*. Sasa utuambie sasa Mheshimiwa Waziri kama nchi hizi hawajatangaza au wametangaza au kama kuna nia yoyote juu ya nchi hizi kuweza kutusaidia. Kama wametangaza, kama nilivyosema awali, lakini tumekuwa tukiona kwenye vyombo veya habari wakijaribu kutupa moyo wka muda mrefu, sasa mtuambie je, kuna nini zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nilitaka kufahamu; kuna mukutano ulifanyika Nairobi Disemba, 2019; na Mkuutano huu ni loile kundi la *African, Caribbean and Pacific (ACP)* na sisi Tanzania tuliongozwa na Mheshimiwa Waziri wetu, Mheshimiwa Profesa Paramagamba Johh Aidan Mwaluko Kabudi, majina matano hayo kama nikikosea naomba radhi sana. Kubwa katika safari yake hii katika maandishi inaonekana kwamba walikuwa wakitafuta mazao ya kimkakati; korosho hasa ikapewa nafasi yake na mahindi yakapewa nafasi yake, na nchi zile zikatoa *Euro* milioni 1,400 huu ni mwezi wa tano. Mheshimiwa Waziri hebu tuambie kwakuwa wewe ndiyo uliongoza safari hii, na kwa kuwa wewe ndiwe uliyewakilisha Tanzania; tuambie mafanikio hasa yakoje?

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni baadhi ya mambo; kuna miradi ambayo imekuwa ikitajwa kila kila wakati. Kuna miradi ambayo kila mara ilikuwa ikitajwa

kutekelezwa katika mwamvuli wa Afrika Mashariki katika Bajeti hii; lakini mara nydingi inaletwa hapa Bungeni na mara nydingine inaachwa. Kuna mradi ule wa Bandari ya Wete-Pemba kuna miaka unaletwa baadaye inaachwa. Mpigaduru-Unguja nayo ilikuwa inaletwa baadaye inaachwa. Uwanja wa Ndege-Pemba hebu tuambie miradi hii kwanini kwenye bajeti nydingine inatajwa, bajeti nydingine inaachwa na hii ni miradi muhimu kweli kweli? Kwahivyo tunataka kusikia kwamba wka upande wa kule Zanzibar na sisi Mpigaduru, Uwanja wa Ndege-Pemba, Bandari ya Wete kuona kwamba tunakwendaje. Hili ni jambo muhimu sana tuone kwamba je, kwanini inaletwa na kuachwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ningependa kujua suala zima la ufungaji wa mipaka. Suala la *corona* hili limetikisa. Tarakea kule mmefunga, Rombo mmefunga, Namanga kumefungwa, Tunduma ndiyo usipime. Yaani sasa hivi ukiangalia vyombo vya habari Tunduma, Tunduma na sisi ni hapo na hapo tu majirani tu hapo; lakini sisi tukifuatilia ile historia, kwamba hawa ni wenzetu, majirani wazuri wa TAZARA, tumekwenda na lile bomba lile mafuta la TAZAMA na reli ya TAZARA. Kwahiyoo utaona kwamba hapo kuna nini zaidi. Mheshimiwa Waziri, Profesa Paramagamba John Aidan Mwaluko Kabudi tuambie hasa hatua ambazo umezichukua katika suala zima la hasa hapa Tunduma limefikia hatua gani? Mtuambie sasa. Kuna malori zaidi ya 100 yamekaa pale, malalamiko yamekuwa ni mengi. Mtuambie kuna nini zaidi na hatua ambazo mmezichukua kwa manufaa ya Watanzania?

Mheshimiwa naibu Spika, Kuhuau suala la Sera ya Mambo ya Nje. Sera ya Mambo ya Nje imekuwa ikijadiliwa sana lakini tunaona kwamba bado haijakaa vizuri katika uhalisia wake; na kumekuwa na hatua kadhaa ambayo Serikali imekuwa ikituambia hapa Bungeni kwamba mmekuwa mkichukua hatua ya kwanza, hatua ya pili, hatua ya tatu; sasa iko katika hatua gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na Sera ya Mambo ya Nje pia kuna Sera ya Watanzania wanaoishi nje

ya nchi (*Diasporas*) mtuambie na sera yao mpaka sasa ikoje. Hawa ni watu muhimu sana, wanaingiza fedha nyigi ndani ya nchi yetu; mtuambie mpaka sasa mikakati na sera ya *diaspora* imefikia katika hatua gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili ni kubwa na Watanzania hawa wamekuwa na malalamiko yao, kwamba wanataka wapate chombo au taratibu ambazo zinawasimamia. Mheshimiwa Waziri utakapokuja hapa utupe taarifa rasmi.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho; mwaka huu ni mwaka wa uchaguzi, 2020 inshallah Mwenyezi Mungu atujaalie gonjwa hili la *covid-19* au *corona* basi Mwenyezi Mungu atuondoshee ili twende kwenye uchaguzi wa salama na amani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kawaida uchaguzi unapofanyika huwa kunakuwa na mialiko ya mataifa mengine. Tumekuwa tukiona kwamba katika nchi nyingine jirani uchaguzi unafanyika lakini je, mkakati wa kuwaalika hawa watu mapema; maana wakija hapa kuna muda wa kukaa *quarantine*, kuna muda wa kukaa hapa siku 14; sasa zimebakia siku 150 kufika Uchaguzi Mkuu tunatarajia Mwezi Oktoba. Mheshimiwa Waziri, Profesa tuambie na Serikali ituambie mkakati wake za ziada sasa kuwaalika mapema hawa waangalizi kuja kuangalia uchaguzi wa haki na huru utakaofanyika Mwezi Oktoba, 2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkichelewa kuwaalika tutafanya uchaguzi wa sisi wenyewe kwa wenyewe, ndani kwa ndani tu, jambo ambalo siyo zuri. Ni vizuri kupata waangalizi kutoka mataifa ya nje ili pale ambapo tukisema kwamba uchaguzi wetu ulikuwa wa haki na huru basi kuwe hakuna shida yoyote na mataifa yale ambayo tunakwenda nayo sambamba. Hilo lilikuwa ni jambo moja kubwa, jambo moja zuri na mimi nina imani; namfahamu Mheshimiwa Waziri Kabudi atawaalika mapema kabisa ili isionekane kwamba make quarantine siku 14 ongezeni siku 20, a' a'.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri utakapotengeneza Kamati ya Mapokezi ya hao wageni, Mheshimiwa Masoud awemo wa kupokea hao wageni, itasaidia sana kujua kwamba wamefika na pia kujua kama waende karantini ama vipi. (*Kicheko*)

Ahsante sana Mheshimiwa Mosoud. Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha, atafuatiwa na Mheshimiwa Abdallah Majura Bulembo na Mheshimiwa David Ernest Silinde ajiandae.

MHE. SHAMSI VUAI NAHODHA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze mchango wangu kwa kunukuu kauli za magwiji wa siasa wa Bara la Afrika Mwalimu Nyerere na Kwame Nkrumah, Marehemu Kwame Nkrumah aliwahi kuulizwa na waandishi wa habari anafuata siasa na itikadi gani, katika ya ujamaa na ubepari? Alisema maneno yafuatayo, *we neither look east nor west, we look forward*; kwa tafsiri isiyo rasmi hatufuati siasa ya ujamaa wala ubepari tunaelekeea mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, Marehemu baba wa Taifa mwaka 1987 alipokuwa akihutubia Mkutano wa Halmashauri Kuu ya Chama cha Mapinduzi alisema maneno yafuatayo: Waafrika wasipofanya hima ya kutumia akili zao na kufikiri na wakawachia Wazungu wafikiri kwa niaba yao, Bara la Afrika litaangamia. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona niyaseme maneno haya, kwa sababu zipo dalili baadhi ya viongozi wa kisiasa Afrika wanadharau kila linalofanywa na Waafrika wenzao lakini wanasifu kila linalofanywa na Wazungu hata kama ni la kijinga na kipuuzi. Nimenukuu maneno ya waasisi wetu ili kuwakumbusha vijana wenzangu waasisi wa Bara la Afrika walitamani kujenga Bara la aina gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania kwa miaka mingi imekuwa ikiheshimika sana duniani tangu wakati wa Baba wa Taifa na harakati zake za ukombozi Kusini mwa Afrika na kutetea wanyonge katika sehemu mbalimbali za dunia.

Katika zama za sasa Waafrika wana matumaini makubwa sana kwamba Tanzania itatoa uongozi katika kuleta mapinduzi ya fikra na kuleta ukombozi wa uchumi katika Bara la Afrika, tunategemewa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili tuweze kutekeleza wajibu huo kwa Watanzania na kwa Waafrika wenzetu naishauri Wizara yetu ya Mambo ya Nje izingatie mambo mawili yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, Tanzania itumie ushawishi wake wa kidiplomasia kuuomba Umoja wa Afrika kwanza ukamilishe mchakato wa kuridhia mkataba wa eneo huru la biashara na hatimaye kuutekeleza mkataba huo haraka iwezekanavyo. Nasema hivi, kwa sababu pengine huu ungekuwa wakati mzuri sana kwa Bara la Afrika kuhakikisha kwamba tunafanya biashara miongoni mwetu katika kipindi hiki ambacho hakuna biashara kubwa na ya maana itakayoendelea kati ya Bara la Afrika na sehemu nyingine ya dunia kutokana na maradhi ya *corona*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wa pili, Tanzania iuombe Umoja wa Afrika uunde Mfuko Maalum wa masuala ya Ulinzi na Usalama utakaoweza kugharamia mafunzo ya kijeshi kwa Jeshi la Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo ili Taifa hili liweze kusimamia majukumu ya Ulinzi wa Taifa lake. Nalisema hilo kwa sababu zipo dalili ambazo ni dhahiri sana kwamba Jumuiya ya Kimataifa sasa inaanza kuchoka kuendelea na *operation* za muda mrefu katika nchi ya Kongo. Naamini amani Kongo ikipatikana bila shaka amani hii itatoa mchango mkubwa sana wa uchumi katika Bara la Afrika na naomba nitoe takwimu, wataalam wa uchumi na maendeleo wanasesma nchi ya Kongo ina rasilimali zenye thamani ya trillioni 24 dola za Kimarekani. Bila shaka hizi ni fedha nyingi sana iwapo Kongo itapata amani na nchi za Kiafrika zikafanya biashara na nchi ya Kongo bila shaka uchumi wa Afrika utaimarika sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, Nchi ya Kongo inasemekana ina maporomoko ya Mto Kongo ambayo yenye

uwezo wa kuzalisha umeme unaokadiriwa kufika kati ya *megawatt* arobaini elfu na laki moja, bila shaka umeme huu unatosheleza mahitaji yote ya viwanda katika Bara la Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Abdallah Majura Bulembo, atafuatiwa na Mheshimiwa David Ernest Silinde na Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, ajiandae.

MHE. ABDALLAH M. BULEMBO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kupata nafasi hii ya kuchangia katika Wizara hii nyeti. Awali ya yote nichukue nafasi hii nimpongeze Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana katika Wizara hii, Mheshimiwa Naibu Waziri, Simba mwenzangu, Katibu Mkuu Kanali Ibuge na Watendaji wote katika Wizara hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaingia kwenye ajenda yangu niseme machache kidogo. Mheshimiwa Waziri hoja yangu ya leo hapa ndani ni kwa sababu nimemtafuta mara mbili, tatu tukutane hatujakutana, lakini asisahau yeye ni pacha mwenzangu, alivyoteuliwa kuwa Mbunge, tulikuwa wote siku moja, yule mzee alituona pamoja. Sasa asinisahau sana na kule nyuma wakati wa Serikali mbili, Serikali tatu tulikuwa na kijiwe chetu Mlimani City yeye, ndugu Polepole na mimi. Sasa ndugu Polepole na yeye simsikii, tuisahafuliane sisi wote wamoja, ni wanasiasa na tunategemeana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu ya leo kwa sababu haikuweza kupata nafasi tukaijadili na wewe pembedni, naomba niiweke hapa ili usikilize hayo niliyonayo na niweze kupata angalau majibu mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja hii ilijitokeza ukiwa kwenye kiti kama leo mwaka 2018/2019, ulikuwa umekaa wewe kama ulivyokaa leo, ilijitokeza ajenda moja, Serikali ya

Awamu ya Tano ikalaumiwa sana na Mheshimiwa Mbunge mmoja humu ndani, ooh ninyi Mwalimu Nyerere hayupo, siku hizi Tanzania hii hamjali wanyonge wenzenu, watu wanaonewa, watu wanafanya nini! Ajenda hii ilikuwa inahusiana na neno linaitwa *Polisario* na Morocco, kikao hiki hiki hapa ndani. Ukiangalia kwenye *Hansard* utakumbuka alikuwa anayo Mbunge fulani sijui wa *ACT* sijui wa wapi! Alitusema sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikasema na mimi leo nije nayo hapa ndani, niwapongeze Ofisi ya Mheshimiwa Waziri mwaka huu au mwaka jana nimeona, hoja za yule bwana aliyekuwa anasema tunafanya mabaya, tunafanya nini nimeona wamefungua tena ubalozi wa watu wanaitwa *Polisario*.

Mheshimiwa Naibu Spika, taabu yangu ni moja, kwenye Serikali ya Awamu ya Nne *Polisario* hawa walikuwapo kwa miaka sita wakati huo Mheshimiwa Membe akiwa Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje. Wizara hii ilipopata mwana diplomasia mmoja anaitwa Mheshimiwa Mahiga Mungu amrehemu huko alipo, akatuambia na akakushaurini kwamba haiwezekani tukawa na ubalozi na nchi ambayo haipo, wapigania uhuru, tutakuwa tunakiuka taratibu za *UN* (Umoja wa Mataifa) na Umoja wa Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa lawama zangu nazielekeza kwenye Ofisi ya Mambo ya Nchi za Nje, watendaji wale kwa sababu ni sababu ipi iliondoa wale watu kwa miaka sita wakaondoka kwenye ubalozi huo na ni sababu zipi amekuja Mheshimiwa Kabudi wakarudishwa? Kwa sababu watendaji ndio wenye ofisi, ndio wanajua zile sababu, kwa nini wanatugonganisha vichwa katika nyie Waheshimiwa Mawaziri. Amekuja Waziri huyu akaondoa akatupa sababu, amekuja Mheshimiwa Waziri Kabudi, wanasema tuanze, simsemi vibaya Mheshimiwa Waziri, lakini nasema watendaji walioko chini pale hawako salama sana na wao. Kwa sababu walitakiwa wawaambie ni madhara yapi yamesababisha *Polisario* iondoke, lakini wameenda pale mwaka mmoja wamemaliza wameshawishi tayari mambo yamefanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimesema kwamba neno hili lilitokea nimeangalia kwenye *hansard* wakati ule na wewe ukiwepo, mwenye hoja ile alisema maneno mengi sana ya kuidhalilisha Serikali ya Awamu ya Tano, sana. Sasa neno lile nilivyoona linakuja, khaa! Tumetii, tumekiri au tumefanya nini!

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nchi hii katika Mabara 54 ya Afrika inao ubalozi kwenye nchi saba. Nchi saba zenyewe kwa kuangalia angalia iko Algeria, Angola, Ghana, Zimbabwe, Nigeria, Tanzania na Afrika Kusini. Wale watu wengine wote hajakubali kwa sababu mtu huyu hajakubalika kwenye Umoja wa Mataifa, hajakubalika kwenye Umoja wa Afrika, sasa kama huyu *Polisario* tunamtaka sana kwa nini Wizara ya Mambo ya Nje inaikataa *OIC* ambacho ni chombo kikubwa kinatengeneza miradi, kina faida na nchi lakini hatukipi nafasi, lakini tunamleta huyu atugonganishe vichwa kila siku ambaye sisi faida yake sijui labda kwenye majibu wataniambia.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili lina historia ndefu tangu enzi ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Mwaka 1983 Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Mzee Mugabe walisema hawa Morocco hawaondoki kwa sababu *Polisario* haipewi haki yake, wakafutwa kwenye *OAU*. Wamekaa huko Morocco zaidi ya miaka 30 wakaomba Umoja wa Mataifa ukawakubali, Umoja wa Afrika wakakubali wamekuja hata sisi kwetu siku hiyo tunawapokea waliokuwa wanapinga ni *ACT*. Magazeti yanaandika kila siku tumetengeneza nao mikataba, wanatusaidia Kinondoni tumepata msikitii, haya mbolea zinakuja kutoka kule, yako na mambo mengine makubwa ambayo siwezi kuyasema wanayajua wanatufanya. Kwa nini tunawagombanisha hawa Morocco na *Polisario*? Kwa nini inakuwa ajenda yetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini tuisache *Polisario* akapata uhuru, akaja kuwa balozi kama balozi, kwa sababu tukimpa mtu bendera ina maana sisi tutakwenda kwake kwa bendera. Sasa leo Mheshimiwa Waziri akiteua balozi pale anakwenda wapi, kwenye janga la vita? Anaenda

kusimamia wapi kuiwakilisha nchi yetu? Kwa hiyo Mheshimiwa Naibu Waziri anasema ngoma hii tumeicheza, mimi nasema zaidi kilichoniudhi ni kwamba tumecheza ngoma inaitwa wapinzani, na mpinzani mwenyewe alikuwa mtu mmoja anaitwa Zitto Kabwe alisema maneno mengi sana ukiingia kwenye *hansard*. Alisema sana hii Serikali, sasa tunaanzaje kucheza ngoma ya mtu ambaye sisi anatuona kama hatufai, anatetea maslahi yake, leo tumeenda kubeba jukumu lile liwe halali kwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nina imani kwa sababu amekuja balozi pale, amekuja Katibu Mkuu Kanali ni mwanadiplomasia, ameshakaa nje, ameshabobe. Mimi kwenye kitabu cha Mwalimu Nyerere mwaka 1972 anasema kusahihishwa siyo kosa uwe unasahihishwa ili uende mbele ukirudi jipange ili uweze kufanya mambo mazuri zaidi. Yako mema wanafanya, ni mengi sana kidiplomasia, tuklenda nje tunayaskia, lakini kwenye hitimisho naomba na mimi nijibiwe hoja yangu hiyo lakini siwezi kupinga bajeti. Mimi ni mteule, bajeti naikubali ipite bila kupingwa, lakini naomba majibu hayo kwa ajili ya faida ya kizazi chetu watendaji waache kugombanisha Waheshimiwa Mawaziri wetu katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa David Ernest Silinde, atafuatiwa na Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq na Mheshimiwa Khatib Said Haji ajandae.

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia fursa hii kuchangia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021. Wizara ya Mambo ya Nje ndiyo taswira ama jicho la nchi yetu. Ukiangalia kwa juu juu unaweza kuona ni kama Wizara haina kazi yoyote, lakini ukiangalia kwa sababu dunia ya sasa ni kijiji utagundua kwamba jukumu la Wizara ya Mambo ya Nje ni kubwa sana kuliko kitu kingine. Ndiyo maana kwenye Mataifa mengine, ukiangalia Marekani

yule ambaye anatumika kama *Secretary* wa Masuala ya *Foreign Affairs* utaona nguvu yake. Ndiyo kiongozi wa tatu kwenye mamlaka ya kimaamuzi kwa sababu ndiyo masuala yanayohusu diplomasia yetu ambayo ina-*involve* masuala ya kiuchumi na masuala ya kijamii na kisiasa, hii ndiyo Wizara yenye.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ikiwa *dormant* isipokuwa inajibu baadhi ya changamoto zinazojitokeza, maana yake taswira ya Taifa letu inakuwa haionekani vizuri nje ya nchi na ndiyo maana kuna mambo ambayo ni lazima tuyaseme yanayohusu mazogo yanayotokea mipakani kwetu, lakini kwa nini? Ni kwa sababu sisi sote kama Taifa tunajua dhamira ya Mheshimiwa Rais kwenye kuhakikisha nchi yetu inakwenda mbele kiuchumi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa sababu tunajua hakuna uchumi wa nchi yoyote duniani inapotaka kukua, lazima kutakuwa na vikwazo. Sasa vile vikwazo vyta kiuchumi ambavyo vinaweza kusababishwa na maeneo mengine, Taifa lisipopatiwa majibu lazima kutakuwa na mgogoro. Mheshimiwa Rais Edgar Lungu wa Zambia tumesikia katika vyombo vyta habari, wamefunga mpaka wa Nakonde-Tunduma kwa kisingizio cha *Covid 19* kwamba madereva wa Tanzania wengi wana *corona* na wakatoa takwimu kwamba Zambia ina wagonjwa 76 ambayo haikuwa *classified fully*, sasa matokeo yake sisi tunaokaa mpakani Tunduma ambao tunafanya shughuli zetu ndogo ndogo za ujasiriamali pale, tunaona changamoto ambayo inatokana na magari yale kuzuiliwa na ule mpaka kukosa biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa maswali kama haya Mheshimiwa Waziri asipoyajibu, maana yake taswira kwa wananchi inaonesha kwamba utendaji wetu umekuwa mdogo. Sasa hata nchi wanachama wanaotuzunguka ukiangalia mpaka wa Horohoro na Lungalunga kule kuelekea Mombasa, Kenya na Tanga Tanzania, kwa maana ya Tanzania na upande wa Kenya. Sasa pale na kwenyewe unaona wamechukua hatua watu wa Kenya. Ukiangalia mpaka wa Tarakea ni hivyo hivyo, ukiangalia mpaka wa

Rusumo ni hivyo hivyo; ukiangalia mpaka wa Mtukula, mpaka wa Holili, Namanga na Ngara nchi jirani zimechukua hatua kwa sababu ya Covid 19. Sasa haya ndio Wizara yetu ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki inapaswa kulieleza Bunge na Taifa, ni hatua zifi Serikali imezichukua kurejesha maeneo hayo katika ule utaratibu wa awali, biashara zifanyike na mambo mengine yaendelee.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hata nchi wanachama wanaotuzunguka ukiangalia mpaka wa Horororo Lungalunga kule kuelekea Mombasa, Kenya, Tanga na Tanzania na upande wa Kenya. Sasa pale na kwenyewe unaona wamechukua hatua watu wa Kenya ukiangalia mpaka wa Tarakea ni hivyo hivyo, ukiangalia mpaka wa Rusumo, ukiangalia mpaka Mtukula, mpaka wa Holili, Namanga na Ngara nchi jirani zimechukua hatua kwasababu ya Covid 19. Sasa haya ndio Wizara yetu ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki inapaswa kulieleza Bunge na Taifa ni hatua zifi Serikali imezichukua kurejesha maeneo hayo katika ule utaratibu wa awali biashara zifanyike na mambo mengine yaendelee.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili wenzetu wamechukua hatua kwa mfano watu wa Rwanda miongoni mwa hatua walizochukua ni kwamba wale madereva wa Tanzania wanapotoka mfano Rusumo kwenda Kigali pana kilometra kama 160 lakini utajikuta dereva wa Tanzania ama mmiliki wa lile gari anapaswa kulipa dola 500 kwenye kilometra 160 kwa Serikali ya Rwanda. Wakati huo huo Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania unafikiria mtu akitoka Kigali akafika Rusumo kwenda Dar es Saalam zaidi ya kilometra 1000 watu hawa sisi hakuna *measures* ndio maana ukiangalia wenzetu kama Marekani na China, China akifunga upande mmoja na Marekani naye ana-react hiyo ndio diplomasia ya uchumi lazima naye a-feel the pinch sasa sisi naona tumekuwa watakatifu na malaika wa muda mrefu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni vizuri sasa na Serikali ikaangalia haja ya kutumia *loop hole* hiyo kwa mizigo

iliyoko bandarini na sisi tukaongeza tozo ili na wao wa-*feel the pinch* na bahari nzuri sisi ni nchi ambayo kijiografia tuko vizuri yaani *geographically position* yetu yaani hawawezi kufanya chochote bila kupata msaada kutoka kwetu lakini vyombo vya habari bado vimekuwa vikieleza mambo mengi ambayo ndio sintofahamu ambazo tunazipata. Unaona kwenye *social media* Rais Ramaphosa ameitisha mkutano wa *SADC* tunaambiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye ndiye Mwenyekiti wa *SADC* hajashiriki sasa haya ndio maswali ambayo watanzania wanapaswa kujibu kwamba ule ulikuwa ni mkutano wa *SACU* yaani kwa maana zile nchi kuna Umoja wa *SACU* na kuna *SADC* sasa tujue taratibu hapa ni zipi ambazo zilifanyika. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Iakini tumeona kwenye media mkutano wa nchi nne za Afrika Mashariki Rwanda, Kenya, Uganda na South Sudan wamekaa pale sisi hatukuwepo kwa nini hayo maswali Serikali ikishatujibu maana yake na sisi tunaondoa ile hofu ambayo imekuwepo kwetu sisi.

Kwa hiyo, ni vitu ambavyo ukiviacha kila mmoja anaweza akatoa tafsiri yake na akapotoshwa vile anavyotaka lakini vikipatiwa majibu maana yake ile hofu ambayo ipo ama yale majibu ambayo kila mwananchi anajipa maana yake tunaiondoa ile na tutawaelimisha wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye masuala haya ya *COVID-19* kumekuwa na mapendelezo mbalimbali kwamba mashirika ya ndege ya kimataifa mengi yamesitisha safari na tumeona athari kubwa zinazotokana na mashirika haya kushindwa kufanya biashara katika nchi zetu. Sasa sisi tunaomba kama kuna uwezekano ni kwa nini sasa Serikali isiruhusu *private jets* watu wakaja kwa ndege binafsi ama wakaruhusu ndege za mizigo zikaja ndani ya nchi lakini watu wakaendelea kuchekiwa kwa sababu *private jet* haiwezi kuchukua watu wengi kama ambavyo inakuja ndege kubwa kutoka nje ya nchi. Kwa hiyo, haya ni mambo ambayo tulikuwa tunaomba yapatiwe ufanuzi ikiwemo na Serikali

imejipangaje kuhakikisha inawarudisha wananchi wake kutoka India, Uingereza, Oman na China ambao imetokana na athari za Covid 19. Ahsante sana kwa kunipatia fursa hii. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana katika mchango wa Mheshimiwa Silinde pamoja na mambo mengine aliyozungumza amezungumza kuhusu mambo aliyoyasema au kuyafanya Mheshimiwa Rais wa Zambia Mheshimiwa Edga Lungu sasa kwasababu hayo sijayaona na sina taarifa juu ya Serikali kuwa na mawasiliano ya namna hiyo na kwasababu hapa ni Bungeni hayo yataondoka yanayomhusu Rais lakini kuhusu kilichotokea mpakani kitabaki mchango wa Mheshimiwa Silinde. Kwa hiyo, yale yaliyozungumzwa kuhusu alichokisema Mheshimiwa Rais wa Zambia kitaondoka kwenye Taarifa Rasmi za Bunge. Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq Khatib Said Haji, atafuatiwa na Mheshimiwa Almas Athman Maige, Mheshimiwa Hadija Nasri Ali ajiandae.

MHE. FATMA H. TOUFIQ: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa fursa na mimikuchangia hoja hii iliyopo mbele yetu lakini sambamba na hilo naomba niendelee kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na kuweza kuchangia katika Bunge lako tukufu. Naomba niendelee kuungana na wenzangu kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara ya Mambo ya Nje Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa kuandaa hotuba hii ya Bajeti ya mwaka wa fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, *ni-declare interest* ni mjumbe wa kamati kwa hiyo moja kwa moja naunga mkono hoja sambamba na hilo naunga mkono maoni ya kamati yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Nailbu Spika, katika ukurasa wa 16 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri amezungumzia kuhusu watanzania 1550 ambao wameweza kupata vibali vya

kufanya kazi katika nchi nyinginezo wanachama katika Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapongeza sana hatua hii, lakini nilikuwa na ushauri kwamba idadi hii ya hawa watanzania ambao wameajiriwa au kupewa vibali katika kufanya kazi katika hizi nchi kwa kweli ni ndogo sana. Kwasababu watanzania wasomi wanaopatikana sasa hivi ni wengi sana na vijana wengi sana wanamaliza shule, soko la ajira limekuwa ni dogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilikuwa naomba nitoe ushauri kwamba hebu wizara ione itaweza kufanya utaratibu gani wa kuhakikisha kwamba idadi kubwa zaidi ya vijana wanaweza kupata vibali ili kusudi waweze kuajiriwa maeneo mbalimbali ughaibuni. Nikiamini kabisa watanzania hawa iwapo watapata hiyo nafasi ya kwenda kuajiriwa huko ughaibuni basi pale itakapotokea sasa na Wizara ikaamua kutengeneza ile sera ya mambo ya nje pamoja na *diaspora* basi ukawekwa utaratibu ili kusudi sasa ile faida itakayokuwa ikipatikana iweze kuleta tija nchini hali kadhalika wale watanzania watakaokuwa wamekwenda kufanya kazi kule nje warudi na utaalamu katika nchi yetu kwa hiyo hiyo inaweza ikaleta tija katika nchi yetu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa wa 155 wa hotuba ya waziri imezungumzia kuhusu masuala ya utawala, maendeleo ya utumishi pia niendelee kuipongeza wizara katika kusimamia masuala ya maendeleo ya watumishi. Lengo kuu ilikuwa ni kuimarisha utendaji. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo naomba nimpongeze sana Rais kwa kuwateua mabalozi yote hiyo ni katika kuimarisha utendaji. Lakini naomba nitoe ushauri kama vile kamati ilivyobainisha ni kwamba bado kuna baadhi ya balozi watumishi hawatoshelezi.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba wizara ifanye hima kuona kwamba watumishi wanaweza kupatikana kwa uharaka kwa kuomba kibali nakadhalika ili kusudi sasa wale ambao ni wa

kada zile ambazo wanatakiwa katika zile balozi waweze kuwepo na hatimaye waweze kufanya kazi kwa weledi ili nchi yetu iweze kupata tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri amezungumzia pia kuhusu umiliki wa majengo naipongeza sana Wizara kwa kuweza kumiliki haya majengo 106. Pia waziri ametuambia kwamba kuna viwanja 12 basi tuone kwamba wizara inafanyaje kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kuharakisha ujenzi wa hivi viwanja 12 ili kusudi mwisho wa siku sasa viwanja hivi au majengo haya yakijengwa wizara nayo au balozi zile zinaweza zikapangisha na hatimaye tunaweza tukapata kipato na kupunguza makali fulani katika balozi hizo lakini pia nchi kuweza kupata tija. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipenda pia nizungumzie suala la visa rejea. Ni kweli ni kwamba nchi yetu imekuwa ikisisitiza sana kupokea wageni tumekuwa tukipokea watalii tumekuwa tukipokea wafanyabiashara mbalimbali kwa ajili ya uwekezaji kwa ajili ya biashara mikutano na semina na pia watu wamekuwa wakitembeleana na ndugu zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa kuna malalamiko kuhusiana na hili suala la visa rejea kwamba kuna baadhi ya nchi ambazo ziko kwenye visa rejea zimekuwa zikicheleweshea sana kwamba watu wake wakitaka kuja hapa nchini inakuwa ni tatizo kupata hizi visa rejea. Najua umuhimu wa visa rejea lakini nilikuwa natamani wizara ione kujaribu kupunguza yaani ule urasimu ili ikiwezekana basi wale watu wanaotaka kuja wanaotaka kuja kutoka ughaibuni kwa ajili ya kufanya shughuli mbalimbali basi upatikanaji wa visa rejea uwe ni rahisi ili mwisho wa siku nchi iweze kupata tija. Kwa hiyo, nilikuwa naomba wizara iangalie upya umuhimu wa kutoa hizi visa rejea ili kusudi hawa wananchi wanaotaka kuja kutoka nchi hizo waweze kupata fursa hizo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nizungumze kuhusu sera ya mambo ya nje kwenye kamati tumelizungumza sana lakini pia naomba nitoe msisitizo sasa wizara ifikie mwisho sasa kwasababu tangu tumeanza

imekuwa karibu zaidi ya miaka mitano imekuwa ikizungumziwa sana kuhusu sera ya mambo ya nchi za nje. Naomba nimshauri waziri sasa iwe imefikia ukomo ili kusudi sasa hii sera ya mambo ya nje ikipatikana pamoja na sera ya *Diaspora* ikipatikana ina maana kwamba basi vitu vyote vitakuwa vikienda kwa kanuni, taratibu na sharia. Kwa hiyo, kwa mtindo ule idadi ya watanzania wanaoishi ughaibuni tutawajua wanaofanya kazi ughaibuni tunawajua kwa hiyo na zile zote *returns* ambazo zinatakiwa zirudi nchini na faida tukaipata vitu vyote hivi vinaweza vikawezekana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilikuwa naomba nitoe msisitizo kwa Mheshimiwa Waziri kwamba kuhusu hii sera ya mambo ya nje basi ifikie mwisho ili mwisho tuendelee na mambo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba nishukuru sana kwa kunipa fursa naunga mkono hoja ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Khatib Said Haji, atachangia kwa dakika tano, atafatia na Mheshimiwa Almasi Athuman Maige, Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele ajandae.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kunijalia kusimama hapa siku ya leo na kutoa mawazo yangu. Kipekee kabisa leo naomba kabla sijaanza kuchangia kwa vile ninadhani huenda ikawa ni siku yangu ya mwisho kusimama hapa kuzungumza katika Bunge hili kama Mbunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuchukua nafasi hii kwanza kabisa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa muda wa kipindi chote cha miaka mitano hii ambayo nimekaa hapa na nimekaa na wenzangu katika hali ya usalama nitoe shukrani za dhati kwa Spika wa Bunge hili, kwa jinsi ambavyo alituongoza binafsi niseme ahsante sana nikushukuru wewe Naibu Spika na uongozi mzima wa Bunge hili kwa kipindi hichi ambacho tunakimalizia.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile niwashukuru Wabunge wenzangu wote kwamba katika kipindi hiki chote tumekaa yamesemwa mengi tunesema iwapo yalipotokea yale mengine ambayo tulikwazana binafsi nawasamehe Wabunge wenzangu na ninyi naomba mnisamehe kwa sababu kuna maisha baada ya Ubunge huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kusema ingawa wenzangu wamesema na dakika zenyewe ni chache kuhusu suala hili la mahusiano ya nchi yetu nan chi nyininge. Katika kipindi hichi cha hii janga la Corona yamekuwa yakisemwa mengi kuhusu nchi yetu juu ya hatua ambazo inazichukua kukabiliana na maradhi haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, binafsi tunaanza watanzania kukwazika sana pale inapoonekana kama sisi nchi yetu ni mazalia ya ugonjwa huu hali ambayo si kweli. Leo ashirio la kufungwa kwa mipaka hiyo ambayo wenzangu wameendelea kuitaja si jambo jema na ni jambo ambalo ni hatari sana kwa uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje kama kuna mambo binafsi sibezi hatua ambazo nchi yangu imechukua katika kukabiliana na maradhi haya sibezi kabisa. Lakini nadhani kwasababu mwanadamu yeote ana mapungufu pale tunapodhani kuna haja ya kuchukua hatua za zaidi katika kukabiliana na kwenda sambamba na dunia lazima tukubaliane nalo kwasababu Tanzania si kisiwa, Tanzania tunahitaji mashirikiano ya kikanda, majirani zetu na dunia kwa ujumla. Leo mfano inaposemwa katika media mbalimbali za ndani nan je ya nchi kwamba Tanzania imezuia kutoa idadi yamaambukizi ya wagonjwa wa *COVID-19*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naridhika na kauli iliyotolewa na Mheshimiwa waziri kwamba kuna mchakato wa kuangalia mapungufu yallyojitokeza katika maabara kuu ambayo imapelekea kutokutangazwa kwa maambukizi mapya. Lakini bado naona ipo haja ya kulifanyia haraka hilo zoezi na ikaendelea kutolewa idadi ya waathirika na

maendeleo katika gonywa hili kuna umuhimu sana kwanza kibinadamu. Binadamu ni waja tulioumbiwa hofu binadamu anayepanga kufanya maovu leo akifiwa na ndugu yake akienda msibani yale maovu kwa siku hiyo na pengine wiki na mwezi anaweza akasema hapana jinsi alivyokishuhudia kifo.

Mheshimiwa Naibu Spika, inatuhofisha na inatupa uangalifu zaidi pale tunapoona maambukizi yanakwendaje tunajenga matumaini yanapopungua na tunazidi kuchukua tahathari pale tunapoona yanaongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu lazima tukubali wanakuwa lakini kwa sasa hatujui wanakuwa kwa Corona au vifo vya kawaida, ni vizuri wale wanaokufa kwa gonywa hili ambalo ni tatizo la dunia ni muhimu sana tutangaziwe bado iko haja ya kupewa taarifa ya maendeleo ya ugonjwa huu ndani ya nchi yetu na dunia ifahamu na majirani zetu wafahamu ili waache kueneza *propaganda* ovu ya kuonekana kwamba sasa Tanzania ni nchi ambayo imeridhia na haya yanayoendelea sio sawa hata kidogo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili nataka kulizungumzia ni suala ambalo Mheshimiwa Masoud ameligusia. Zanzibar tumekwama, ziko ajenda zilizowekwa za Afrika Mashariki kusaidia miradi ya Zanzibar, miradi ya kimkakati kabisa, mradi wa bandari uliotajwa, bandari ya Wete, bandari ya Mpiga Duri na *Airport* ya Pemba. Hii miradi imekwama na tumekuwa tukipewa matumaini baadaye yanafilia hili jambo kwa maendeleo ya Zanzibar niwape tu taarifa kwamba Zanzibar bandari illyonayo ina uwezo wa kupokea meli moja ambayo tuliridhishwa na wakoloni toka miaka hiyo, meli moja peke yake. Katika kipindi kilichopita tayari mashirika ya meli ya kimataifa yalianza kukataa kuja Zanzibar kutokana na ucheleweshwaji mkubwa wa meli zinapokaa nje kungojea kufunga katika badari ya Zanzibar kupakua mizigo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, suala lile ambalo tayari tuliaminishwa wazanzibar kama ni mradi ambao

ungeweza kutusaidia wazanzibar wanaulilia sana na nikuambie katika maslahi ya Zanzibar ni mzalendo namba moja wa Zanzibar, kuangalia chama baadaye lakini kuangalia Zanzibar kwanza. Kwa hivyo, tunasema kwamba wazanzibar wanahitaji maelezo ya kina mmefikia wapi juu ya miradi ile ambayo ilainishwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki?

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho kama muda utaruhusu...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Kengele imeshagonga Mheshimiwa ahsante sana.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana asante sana.

NAIBU SPIKA: Asante sana Mheshimiwa Almas Athuman Maige atafatiwa na Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele Mheshimiwa Wifred Muganyizi Lwakatare ajiandae.

MHE. ALMAS A. MAIGE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana pia leo kuniruhusu nichangie hoja hii ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki bajeti yake ya mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwasababu uchangiaji humu ndani ya ukumbi wako umekuwa tabu nafasi hazitoshi muda hautoshi naomba nichukue fursa hii pia kuwashukuru wananchi wangu wa Uyuwi Tabora Kaskazini kunichagua nije niyawakilishe humu ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia namshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuniletea miradi ambayo nimeweka alama jimboni kwangu. Sasa kuhusu bajeti hii ya Wizara ya Mambo ya Nje na ushirikiano

wa Afrika Mashariki kwanza nimshukuru sana na nimpongeze Waziri Prof. Kabudi na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Dkt. Ndumbaru wamefanya kazi kubwa sana kuielezea nchi yetu huko nje pia watendaji wote wa wizara hii kwa ushirikiano wao wamefanya kazi kubwa ya kuitangaza nchi yetu pia kusimamia maslahi ya nchi kila ambapo palitakiwa kufanywa hivyo na hivyo kuleta mafanikio makubwa ya uwakilishi wetu katika SADC na Afrika Mashariki na taasisi nyingine za kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikirejea kwenye Kamati yangu na ushauri wake, sisi tumeshauri sana Wizara hii kuhusu mambo ambayo tunafikiri ni muhimu na moja ilikuwa ni kuhusu nyumba na Ofisi za Mabalozi. Tumependekeza mara nyingi kwamba ni muhimu sana Serikali ikawa na mpango mzuri wa kuwa na nyumba zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nasimama hapa kwa furaha kubwa sana kwamba Kamati yangu tumesikilizwa. Hivyo Wizara hii imeanza kwenda mbele katika kujadili na utekelezaji wake wa kujenga nyumba za Ofisi za Balozi na makazi ya Mabalozi hasa kule Muscat. Pia kipo kiwanja kile cha Nairobi, nacho pia kingepewa umuhimu wake kwa sababu siku ambayo sisi tulipewa kiwanja hapo Nairobi, nasi tuliwapa kiwanja wenzetu hapa Dar es Salaam. Sasa wenzetu wameshajenga kiwanja kile na jengo limekamilika wanatumia ofisi, lakini sisi kile cha Nairobi bado hakijapata msukumo ambao unatakiwa kufanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasifu sana wenzetu wa Wizara ya Mambo ya Nje. Juzi nilimwona Mheshimiwa Prof. Kabudi anabeba madawa kwa niaba ya Watanzania kutoka Madagascar kuja hapa. Pia usemajji wao Wizara hii huko nje umeleta mafanikio makubwa ya kujibadili kwanza kutoka kwenye Diplomasia ya Kisiasa na kuwa na Diplomasia ya Kiuchumi. Kwa hiyo, wamejitatihidi sana kutangaza fursa za Tanzania huko nje na kuleta wawekezaji hapa nchini. Jambo hili ni la kuwapongeza sana. Ingawa mabadiliko yamefanyika ndani ya miaka mine, lakini matokeo yake ni makubwa na tumeyaona.

Mheshimiwa Naibu Spika, nijikite kwenye vipaumbele ambavyo Wizara hii imejipangia. Mfano wa vipaumbele hivyo ni pamoja na utekelezaji wa Diplomasia ya Uchumi kwa kuvutia wawekezaji na wafanyabiashara kutoka nje, pia kuvutia watalii na kushirikiana katika Jumuia za Kikanda kwa lengo la kuongeza ajira, masoko na bidhaa za Tanzania huko nje na kukamilisha Sera ya Mambo ya Nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera ya Mambo ya Nje ni muhimu sana. Ni sera ambayo itatuwekea nafasi nzuri katika kuendesha siasa zetu na uchumi wetu kwa vile inagusa pia *diaspora* na utendaji wa Wizara hii ya Mambo ya Nje huko nje. Kwa hiyo, ni muhimu sana sera hii ikakamilika. Sera hii tangu mwaka 2016 mpaka leo haijapiga hatua kubwa sana. Napenda Mheshimiwa Waziri atakapokuja atuelezee kidogo sera hii imefika wapi na imekwama wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, pia wana kipaumbele cha kuandaa kanzidata ya *diaspora* itakayotoa taarifa na mwongozo wa namna ya kuwashirikisha *diaspora* hawa Tanzania katika kuchangia maendeleo ya nchi. *Diaspora* katika nchi nyingine wanaingiza hela nyingi sana lakini wanafanya hivyo kwa sababu wanakuwa na mategemeo fulani. Kwa mfano, wana uraia wa nchi mbili; kwa hiyo, wanawenza kuja huku na kutoka huko wakafanya kazi kule, wakachuma kule wakafaidika na kule waliko lakini pia wakaja huku nchini na kujiona kama raia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, naunga mkono hali ilivyo sasa kwamba *diaspora* hawa waje kwa mpango ambao sasa upo na wana haki zote. Watu wengi wanafikiri watu wa *diaspora* wamebanwa sana, lakini wana haki zote za kuishi kama Watanzania isipokuwa kupiga kura tu. Hii iko ndani ya Katiba na ilitajwa katika Katiba inayopendekezwa na imerudiwa mara nyingi, lakini kikatiba sasa hivi raia wa Tanzania hawezu kuwa na uraia wa nchi mbili mpaka atakapoukana uraia wa nchi nyingine akapata wa kwetu na akikana wa kwetu anapata wa nchi nyingine. Suala hili libakia hivyo kwa sababu ya maslahi ya nchi yetu; siyo

usalama tu, ni pamoja na kwa maslahi makubwa ya ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanasema kipaumbele kingine ni kuendelea kutoa elimu kwa Umma juu ya fursa zitokanazo na mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya nyingine za Kikanda. Nimesikitika sana, hata mimi nilipoona tangazo la wale viongozi wa nchi nne za Afrika Mashariki wanakutana bila Tanzania kuwemo ndani. Pia kama alivyosema msemaji mmoja, wanakutana hawa wa Afrika Kusini bila kutukaribisha sisi. Sasa sijajua, lakini siyo vibaya atakapokuja Mheshimiwa Waziri akatueleza, akatufafanulia mambo haya ambayo mimi nayaita madogo kwa sababu hayazui; meli kwenda Zanzibar inakwenda ingawa kuna mawimbi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimependa kuchangia hayo, naunga mkono hoja. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele, atafuatiwa na Mheshimiwa Wilfred Muganyizi Lwakatare na Mheshimiwa David Cosato Chumi, ajiandae.

MHE. AUGUSTINO M. MASELE: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kutoa mchango wangu katika Wizara hii nyeti ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kama Kamati yangu ilivyo. Tuko tunajadili Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Mambo ya Nje ni Wizara ambayo kimsingi huwa inaitwa *first line of defense* kwamba Wizara ya Mambo ya Nje na Wizara ya Ulinzi ni Wizara pacha, kwa maana hiyo, ili vita ipiganwe, Wizara ya Mambo ya Nje inahusika pakubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia Vita vya Pili vya Dunia kati ya *Soviet Union* na Ujeruman, Molotov aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje alihusika pakubwa. Hata

Ujerumanî ilipoivamia Urusi, Stalin alipochanganyikiwa, ilibidi Molotov ye ye mwenyewe ndio asimame mpaka baada ya hali kuwa imetulia vizuri ndiyo akaenda kumfuata Stalin kumwambia kwamba bwana njoo kwenye kitî chako uzungumze na usimamie masuala ya Taifa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo, historia inaonesha wazi kwamba Wizara ya Mambo ya Nje inahusika pakubwa. Yanapozungumzwa habari ya mambo ya amani, Wizara ya Mambo ya Nje inakwenda kuzungumza kwa niaba yetu. Baada ya hapo sasa vita ikitokea shughuli inaanza kuhusisha Wizara ya Ulinzi na vyombo vya ulinzi na usalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo, mchango wangu ambao nataka niuzungumze hapa sasa, kwa sababu Wizara ya Mambo ya Nje ndiyo Wizara ambayo inatuwakilisha huko nje, inalo jukumu kubwa la kuhakikisha kwamba tunapata teknolojia za kisasa za mambo ya ulinzi na usalama. Kwa maana hiyo, naomba kabisa Wizara ya Mambo ya Nje pamoja na Diplomasia ya Uchumi, ni vizuri Wizara hii ikahusika pia kuhakikisha kwamba tunapata teknolojia za kisasa za mambo ya ulinzi katika vyombo vyetu vya ulinzi na usalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, nazungumza haya kwa sababu katika Kamati yetu tumekuwa tukikutana na Jeshi la Ulinzi na kuna Mashirika yetu mawili ya Nyumbu na Mzinga. Mashirika haya yanaonekana kwa kweli bado hatujayatendea haki. Kwa mfano Nyumbu, kazi ambayo wanafanya ya kutengeneza haya magari ya zimamoto siyo tarajio la Kitaifa kuwa na Shirika la Nyumbu la Serikali litengeneze magari ya zimamoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitarajia Wizara yetu ya Mambo ya Nje ikakaribishe wawekezaji, kwa sababu yapo matukio kwenye ulimwengu huu wanakofanya maonesho ya teknolojia mbalimbali za ndege, za kutengeneza vifaru na vitu mbalimbali. Katika Wizara hii tuna watu wetu wa kutosha huko duniani; kwa nini tusishughulike kwenye maeneo hayo, kwenda kukaribisha wawekezaji wakaja kushirikiana nasi tukatengeneza hivyo vifaa hapa hapa ndani, ili hali ikitokea

kama ilivyotokea mwaka 1978 na 1979 zana hizo ziwe ziko hapa hapa na zimetengenezwa hapa hapa?

Mheshimiwa Naibu Spika, wale wanaofuatilia vizuri Vita vya Pili vya Dunia kati ya Urusi na Ujeruman; Ujeruman iliwa iko mbele ya Urusi, lakini kwa sababu Urusi iliwa na teknolojia ya kutengeneza vifaru na ndege. Pamoja na kwamba ilipoteza watu wengi, lakini iliweza kulihami Taifa lake wakaweza kushinda Vita vya Pili vya Dunia kwa sababu walikuwa na uwezo wa kutengeneza zana za kijeshi nyumbani kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa sasa hivi mchango wangu mkubwa katika hili, naomba sana Wizara yetu ya Mambo ya Nje ihusike kikamilifu kuhakikisha kwamba teknolojia mbalimbali ambazo zipo duniani zinazoendelezwa na wenzetu nasi tuzipate na watu wakaribishwe. Tumeona vizuri tu makampuni kutoka Uturuki yamekuja kutujengea Reli ya *SGR*. Wenzetu pamoja na kwamba tumekuwa na ushirikiano nao kwa muda mrefu, Wachina, walishindwa. *Offer* yao ilionekana iko juu zaidi kuliko watu wa Uturuki. Waturuki hawa wametengeneza vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo, hata katika nchi hii kuna mashirika ya *defense industry* wako tayari na wako sokoni. Kwa sababu tumekuwa na uzoefu wa kuweza kuwa-*engage* watu kama hawa, nina imani kubwa kwamba mashirika ya utengenezaji wa vifaa vya kivita wanaweza wakaja kushirikiana na Serikali yetu. Tuwe tayari kulpia gharama kama kutakuwepo na gharama yoyote ile ili kuhakikisha kwamba nchi yetu inapokua kiuchumi, basi ikue pia kiviwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, maneno yangu machache kwa leo katika Wizara hii, yalikuwa ni hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makof*)

NAIBI SPIKA: Ahsante sana. Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Wilfred Muganyizi Lwakatare, atafuatiwa na Mheshimiwa David Cosato Chumi na Mheshimiwa Ally Saleh ajiandae.

MHE. WILFRED M. LWAKATARE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja ambayo imeletwa Mezani. Vile vile namshukuru Mheshimiwa Spika kwa kutambua hali halisi inayozunguka mazingira ya kisiasi yanayotuwezesha kuwepo humu, kwamba bila kutarajia tunatambua humu ndani kuna aina mbalimbali ya Wabunge wanaoingia kwa njia tofauti. Wapo wanaotokana na vyama vyao kwa kugombea, wengine Viti Maalum na wengine nafasi za Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa tumeanza kushuhudia kwamba mazingira yanatibuka mpaka inasababisha kuwepo mhimili mwingine wa kuingiza Wabunge, kwamba kuna Wabunge wanaotokana na Jimbo la Mheshimiwa Spika na hasa sisi ambao hatuna chama imara. Hata hivyo, tutakwenda hivyo hivyo tutafika mwisho, nafikiri tutamaliza kazi hii salama. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyozungumza mwenzangu, Mheshimiwa Silinde, Wizara hii ni kioo cha nchi. Mabalozi au watumishi wetu walioko nje, lolote lile, tabia zozote zile wanazoweza kuzifanya na matamko yoyote wanayoweza kuyatoa au shughuli zozote zinaoweza kufanyika huko wao ndio wanakuwa *reflection* ya nchi yetu. Kwa hiyo, napenda Serikali ichukue hatua na iwe makini, hasa kwa matamko yanayotolewa. Wanaobeba mzigo wa kufafanua na kuwekwa kitimoto ni Mabalozi waliopo nje na hasa pale kunapotokea mambo yenyе utata ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mauaji ambayo hayana maelezo yanayoelewka; utekwaji wa watu ambao wanatekwa lakini maelezo hayatolewi; au chaguzi zinavyofanyika zikatawaliwa na vitendo ambavyo kimsingi siyo uchaguzi ulio huru na wa haki; na watu kupigwa risasi, ni

vitu ambavyo wenzetu walioko nje wanabanwa na wanakosa maelezo ya kutoa. Kwa hiyo, naomba hili liangaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata sheria tunazopitisha humu ndani, tunapokinzana na mikataba ambayo tumesaini huko nje Mabalozi wetu wanapata shida kweli kweli. Kwa hiyo, tunapofanya mambo yetu kama mzungumzaji aliyezungumza kwamba sasa hivi dunia ni kijiji, yanayotendeka humu usifikiri ni ya kwako tu kwa sababu uko Tanzania, ujue yatawahusu na wengine ambaao sio Watanzania, ni wa nchi nyininge.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mfano mwingine ambaao ningetaka kuzungumza. Suala la *Corona* limekuwa likitolewa tafsri nyangi na *approach* nyangi ambazo zinatofautiana. Nyingine zinakuwa za kipekee kuliko hata zile ambazo zinakuwa zimeelekezwa na *WHO* ili kuweka misingi inayofanana kidunia. Sasa zinapotoka tafsiri, maelezo au *approach* ambazo kimsingi zinatofautiana na wengine, nataka kuwahakikishia tunajichanganya na mahali pengine tunaweza tukasusiwa ikifika kipindi fulani kwamba tulijifanya wajanja, sasa inafika mahali pa kuomba misaada na misaada haitoki. Nao wanakuwa na jambo wanalolifirkira kwamba hawa si wajanja, wana mambo yao na *approaches* zao, acha waipate *fresh*. Sasa nafikiri hayo mambo tuyafahamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nirejee wakati wa kipindi cha Rais Mkapa, wakati huo Mheshimiwa Kikwete akiwa Waziri wa Mambo ya Nje. Naomba kama itawezekana niseme kwamba, kipindi hicho mimi nilikuwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani ndani ya Bunge, nilikuwa naongoza vyama vitano bila mgogoro wowote. Nakumbuka Mheshimiwa Mboge alikuwa Waziri Kivuli wangu wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Dkt. Slaa alikuwa Waziri wangu wa Katiba na Sheria, Marehemu Mheshimiwa Ndesamburo alikuwa Waziri wangu wa Maliasili na Utalii na Mheshimiwa Cheyo alikuwa Waziri wangu wa Fedha na Mipango. Kwa hiyo, nilikuwa na mchanganyiko wa viongozi kutoka vyama mbalimbali na

nilitengeneza taratibu na kanuni za kusimamia kambi ambazo iliweza kuzisimamia mpaka tukamaliza tukiwa vyama vyote. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa na utaratibu wa kila mwaka wakati wa bajeti, nilikuwa naalika vyama vyote vyenye usajili wa kudumu ili kuja kuvipa somo namna ya *ku-link* na kututetea huko wanapokuwa nje ili tuwe kitu kimoja. Wabunge nilikuwa nawaongoza walikuwa wanachangia na hawa viongozi wanakuja wanakaa siku nne Dodoma, tunaandaa watoa mada na mambo yanakwenda vizuri. Nafikiri kuna wakati mwininge mambo mengine ni kupeana vijiti ili watu tuweze *ku-share experience*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimezungumza wakati wa Mheshimiwa Kikwete; Mheshimiwa Kikwete alikuwa anaandaa kikao cha Mabalozi kule Arusha, Ngurdoto. Nilikuwa naalkwa kama Kiongozi wa Kambi ya Upinzani kwenda kutoa *lecture* kwamba upande wa Upinzani mnasemaje? Pia Mabalozi walikuwa wanaweza kutoa *experience* kule nchi nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekuwa nalizungumza suala la *three-line whip*, kwamba Mheshimiwa Msekwa alikuwa anaandaa watu wa kutoa *lecture* kwa Wabunge ili kuelewa masomo na kutu-*link* na nchi nyingine zinavyofanya na kwa njia hiyo tunapata *experience*. Nimetoa semina sana kwa Mabalozi na wengine walishawishika kabisa hata kunikaribisha kwenye baadhi ya nchi zao ili kwenda kuonesha taswira ya Upinzani wa Tanzania ukoje.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili jambo liliikuwa zuri...

MHE. JUMA S. NKAMIA: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Lwakatare, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Juma Nkamia.

TAARIFA

MHE. JUMA S. NKAMIA: Mheshimiwa Naibu Spika, anavyoonesha Mheshimiwa Lwakatare, ana uzoefu mkubwa sana. Nataka nimpe taarifa kuwa kwa kipindi chote hiki cha miaka mitano ambapo Wabunge wa Upinzani hasa Chama chake cha CHADEMA wamekuwa wakisumbua sana, kwa nini hakutumia nafasi hii kuwapa hii elimu anayoutuambia hapa leo? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Lwakatare. (*Kicheko*)

MHE. WILFRED M. LWAKATARE: Mheshimiwa Naibu Spika, ni suala la uelewa. Atambue kabisa kwamba kila kitabu kina *pages* tofauti na kila nyakati zina alama tofauti. Kwa hiyo, lazima ukubaliane na *principle* hiyo na ndivyo tunavyoenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo semina zile tulikuwa tunapeana ufahamu. Nimesema nimetoa *lecture* nyingi kwa Waheshimiwa na kipindi kingine alihudhuria Mheshimiwa Mkapa kwenye semina hiyo, nikaeleza mambo ambayo yako upande wa pili na ambayo kwa kweli yanakinzana na demokrasia.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshim iwa Naibu Spika, Taarifa.

MHE. WILFRED M. LWAKATARE: Mungu wangu!

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Lwakatare kuna Taarifa nyiningine kutoka kwa Mheshimiwa Khatib Haji.

TAARIFA

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimpe taarifa muongeaji anayeongea kwamba anachokiongea kinafanana kwa sababu, ni kweli, hata kipindi hiki alichofanya mapinduzi hapa ya kuchukua hii kambi mambo yamekwenda mazuri. (*Kicheko/Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Lwakatare!

MHE. WILFRED M. LWAKATARE: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa aliyoitoa Mheshimiwa Khatib naipokea na ni kweli. Japo nataka kumfahamisha mimi siko hapa kwamba, nimekuwa KUB au nimepindua ili niwe KUB, kiongozi wa kambi ya upinzani, mimi nataribu wenzangu ambao wako humu ndani waiokubali kuingia humu ndani. Na ndiyo maana Kiti cha Mheshimiwa Mbewe kiko hapa nimekalia kiti ambacho huwa tunakuja kumshauri na kuzungumza mambo mengine, na cha *Chief Whip* kiko pale kwa hiyo, sijaingilia mtizamo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kuhusu suala la mapinduzi. Kama nafikiri katika *Genius Book* ya dunia iwekwe rekodi kwamba, kumewahi kufanyika mapinduzi, kama wewe unaamini kwamba ni mapinduzi, basi ni mapinduzi ambayo hakujamwagika damu wala hata ukucha hata unyayo; asante sana. (*Makofi*)

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa. Muda wako umekwisha, kengele ya pili imegonga. (*Kicheko/Makofi*)

MHE. WILFRED M. LWAKATARE: Mheshimiwa Naibu Spika, dakika zangu utazitunza, taarifa zimekuwa nyingi.

NAIBU SPIKA: Kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa, maana yake dakika zako zimekwisha. Ahsante sana.

MHE. WILFRED M. LWAKATARE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Asante.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa David Cosato Chumi, atafiuatiwa na Mheshimiwa Ally Saleh, Mheshimiwa Ali Hassan King ajiandae.

Mheshimiwa Cosato David Chumi kutokea Msekwa!

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi, na ninawapata vizuri kutokea huku Msekwa kama sehemu ya tahadhari tulizochukua dhidi ya corona, lakini hii barakoa kwa muda tu ikae kando.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa kwa niaba ya wananchi wa Mafinga tunapenda kutoa pole sana kwa Mheshimiwa Rais, Bunge lako, Wizara ya Mambo ya Nje na Jumuiya nzima ya Kimataifa, mpaka kule Somalia ambako Mheshimiwa Balozi Augustine Mahiga alipata kuhudumu. Kwa wasio fahamu Mheshimiwa Balozi Mahiga alikuwa *Care Taker President* wa nchi ya Somali ambayo kwa miaka 23 ilikaa bila Serikali. Yeye aliongoza pale kutengeneza mfumo wa kuwa na Serikali kuanzia Bunge, Jeshi, Polisi na vyombo vyote muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, napenda kuchukua nafasi hii kuwapa pole wana Iringa na Taifa kwa ujumla, lakini na Jumuiya ya Kimataifa kwamba, tumepoteza mtu mahiri, lakini pia na mimi kama mtu ambaye kwa nyakati tofauti nilifanyanaye kazi akiwa Ubalozi wa *Newyork*, napenda pia kumshukuru Mungu kwa sababu yake kwa sababu alitenda mema mengi katika taifa hili na dunia hii. Pia pole kwa watu wengi wa *Foreign Affairs* ambao wamepitia mikononi mwake. Nasema raha ya milele umpe ee Bwana na mwanga wa milele umuangazie, apumzike kwa amani, amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo niseme kuhusu diplomasi, lakini pia kuhusu masuala yote ya *foreign policy*. Diplomasi kwa tafsiri nyepesi tunasema kwamba, *is the art of dealing with people in a sensitive and tactful way*, lakini pia tunasema *foreign policy* ni extension ya *domestic policy*. Kwamba mambo yako ya ndani sasa namna gani utashirikiana na wengine ili kuyafanya yaweze kuwa na manufaa kwa watu wako. Kwa hiyo mambo ya nje kama wizara na kama taifa pia tunapofanya mambo hatukurupuki tunaangalia kwanza *domestically*

tumejipangaje, ili sasa kutokana na jinsi tulivyojipanga ndipo tuweze kushirikiana na wengine kwa manufaa na tija ya taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema haya kwa sababu jana kulikuwa kunazunguka *communique* au Taarifa Rasmi kuhusiana na baadhi ya masuala yanayoendelea ndani ya *East Africa* kuendana na jambo hili la corona. Na kuna baadhi ya watu wanahoji, mbona katika taarifa ile inaonekana tu viongozi wa baadhi ya nchi wa kwetu hayupo? Wanasema hajashiriki na wapo wanaosema kwamba Mheshimiwa Rais siku hizi hasafiri, hashiriki mikutano, eeh? Sasa katika mambo haya ya *diplomacy* ushiriki wako unaangalia kwanza, kama nilivyosema, ni *foreign poliscyni extension* ya *domestic policy*; unaangalia kwanza ndani ya taifa lako ushiriki wangu katika manbo haya nitanufaika viperi?

Mheshimiwa Naibu Spika, na si kwamba, sisi kama taifa hatushiriki, hapana. Unapima uzito wa jambo linaloenda kujadiliwa. Na katika mambo ya diplomasi kuna masuala unaweza uka-*attend*, ukahudhuria tu, lakini kuna masuala unaweza uka-*participate* kwamba, ukashiriki; na kuna masuala inapofikia kwamba, yanatakiwa yaamuliwe kwa kupiga kura unaweza kupiga kura ya hapana, ya ndio au uka-*abstain*; kwamba ukaamua mimi kwa jinsi nilivyoona hili jambo nkipiga kura ya hapana au ya ndio itakuwa haina tija kwangu, basi haupigi kura yoyote. Kwa hiyo ushiriki wetu katika masuala haya unaendana na mambo yetu *domestically* yamekaa viperi.

Mheshimiwa Naibu Spika, na kulingana na uzito wa jambo ndipo ambapo taifa linawenza kuamua jambo hili atumwe mtu wa ngazi ya afisa, jambo hili labda aende mtu wa ngazi ya balozi au jambo hili aende Waziri fulani au jambo hili mkuu wa nchi aweze kwenda. Na kuna mambo kwa unyeti wake unaweza kukuta taifa linaamua hata kutuma mjumbe maalum, *special envoy* kwa sababu, tunaona tuna maslahinalo kitaifa katika wakati huo. Kwa hiyo dhana ya kwamba hatushiriki au hatukushiriki huo mkutano mimi kwangu naona kwamba, kwanza nampongeza Mheshimiwa

Rais kwa kutoshiriki kwa sababu, unaenda kushiriki na wenzako ambao wao wameshafanya maamuzi kwamba, sisi tunafanya *lockdown*, sasa unaenda wewe kushiriki nini kitu ambacho wenzako wameshafanya?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili Mheshimiwa Rais tangu mwanzo amesema vyombo vyakifedha vyakimataifa katika wakati huu tunapopambana na janga la corona viweze kuziangalia nchi za Kiafrika na nchi nyingine katika suala zima la masuala ya mikopo. Na maoni ya Mheshimiwa Rais ni mazuri, kwamba wenzetu hawa wenye fedha wakati huu watoe hata, ikibidi kama si kusamehe basi *grace period* kwa muda fulani. Sasa ni kama vile mtu una mgonjwa unauguliwa, jamaa anayekudai uliyekuwa umlipi mwezi huu badala akwambie bwana kwa sababu sasahivi hali ni tet kidogo naomba nikuongezee muda, anakuja anakubendi-bendi, anakupeti-peti anakwambia sasa ngoja nikukopeshe kingine, *that is almost a killing.*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Mheshimiwa Rais anasema jamani hebu twende taratibu tushauriane na wenzetu, wenzetu wengine wameshakwenda wameshakopa. Sasa hatuendi hivyo, je katika hali hiyo unataka tukurupuke tukashiriki tu? Jambo hili je, lina tija kwetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi niseme jambo moja; sisi katika uhehe tuna msemo unasema, "*Kawo kobita, kawo kopiluka,*" yaani kwamba, mkono utoao ndio upokeao. Sasa hawa wenzetu wanataka sisi tuwe tunatoa tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa amesema Mheshimiwa Silinde na Waheshimiwa wengine, wamefunga mipaka hata bila ya kufanya mashauriano fulanifulani. Sasa na mimi nashauri, *I might be not diplomatic enough*, lakini lazima tufanye *reciprocity*, ndio hiyo kawo kobita, kawo kopiluka kwamba, mkono utoao ndio upokeao. Kama wao wamefunga mipaka na sisi tuwe na *mechanism* ambazo tufunge mipaka kwa sababu, haina maana wao leo hii unakuta ma-fuso yao yako mpaka Mtandika, yako llula

yanachuku nyanya, lakini sisi malori yanayoenda kule pale Namanga wameyazuia. Sasa lazima iwe kawo kobita, kawo kopiluka, hii wala sio kitu cha ajabu *reciprocity* katika *diplomacy* kwa sababu gani, narudi kulekule *foreign policy* ni *extension* ya *domestic policy*, unaangalia ndani hapa unanufaika vipi, kuna tija ipi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo wala Serikali isiwe na wasiwasi. Mimi naamini sisi Wabunge kama tunawashauri Serikali kwenye hili tukonayo, ichukue hatua zozote ambazo zitatusaidia kama taifa.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Naibu Spika, na hapa nitoe mfano, muda unakimbia kweli kweli, nchi ya Uturuki kwa miaka na miaka imeomba kujinga *European Union*, walikataa, lakini badaye ikaamua kuchukua njia yake. Saa hizi Uturuki *is becoming a giant* katika dunia hii. Kwa hiyo kuna wakati unakuwa na wenzako kama unaona wana tija na wewe kama hawana tija na wewe *you look for another option*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nasema tuangalie hata kule Ziwa Tanganyika bandari zetu tuimarishe. Sisi watu wa Njombe, Mbeya na Iringa ni rahisi kupeleka bidhaa Kongo kule ya Kusini na Mashariki kuliko kupeleka baadhi ya nchi tunazopakananazo. Kwa hiyo tujiimarishe ki-*domestic* ili tuweze kujiimisha kwa kushurikiana na watu ambao wana tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la mwisho...

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Kengele ya pili ilishagonga Mheshimiwa, ahsante sana.

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Naibu Spika, basi huku Msekwa hatusikii vizuri. Basi, nikuombe kwa kuhitimisha kusema kwamba, naunga mkono hoja na niombe

Kiswahili tuwekeze Wizara kwa kufundisha watu Kiswahili na lugha nyingine kiarabu, ki-Spanish maana huwezi kuwa mkalimani kwa kujua tu Kiswahili, lazima uje na hizo lugha nyingine ili ile dhana ya kufanya Kiswahili kiendelee kusikika katika dunia na kuwa kama zao la biashara iweze kuthibitika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Asante sana kwenye hiyo hoja yako inabidi kufahamu lugha zote kwa ufasaha. Maana sisi wenyewe tukichangia tunachanganya lugha hapa, tunachanganya lugha halafu wakati mwingine hata sio kwa usahihi kwa hiyo, tuna changamoto kidogo, lakini tutie bidii kwenye hilo.

Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Ally Saleh atachangia kutoka Msekwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Ali Hassan King, Mheshimiwa Salum Mwinyi Rehani ajiandae.

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Naibu Spika, asante sana kunipa fursa ya kuchangia na kwanza nataka kusema naunga mkono yale mambo yote ambayo Wizara imeweza kufanikiwa kufanya, kuongeza idadi ya balozi nje, balozi nyingine zaidi kufunguliwa Tanzania na yote yale, lakini sisi kama Wabunge tuna wajibu wa kuonesha yale maeneo ambayo Serikali haikufanya au haikufanya vizuri kwa ajili ya maslahi ya kunyoosha na kuwezesha nchi yetu kufanya vizuri zaisi. Kusifu ni sehemu moja lakini kuonesha vilivyokuwa havijafanywa ndio muhimu zaidi kwa sababu, vile ndio vimeshafanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza nataka kuzungumzia juu ya habari ya corona; nafurahi kwamba Wizara imeliona jambo hili la corona kwamba ni sehemu ya mambo ya nje kwa sababu, corona ni afya, ni uchumi, ni jamii, lakini pia ni *issue* ya mambo ya nje, na katika hili nina mambo mawili tu ya kukazia; la kwanza ni lile la uwazi. Kusema kweli kama hatukuwa wazi, nafikiri watu wamesema hapa, kama hatukuwa wazi ya kueleza nini tunafanya, kama

hatukufuata vigezo vya kimataifa nini tunafanya kwa sababu, vigezo vyote tutakavyovifanya hata hivyo vitu vyenyewe vifanane na *standards* na *models* zile ambazo zinatakiwa na WHO. Si lazima tufanane na Marekani, si lazima tufanane na Uingereza wala Italy, lakini ziwe ni *models* ambazo zinafanana au zinakubalika na WHO, ili baadaye tunawekeza. Tukifika wakati wa kutaka kujifungua tusije tukaambiwa kwamba, hamkutimiza masharti haya au hamkutimiza masharti yale, hilo lwa kwanza katika corona.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ningetaka kusema kwamba, nilifikiria ningedhani kwamba kwa kuwa sasahivi mvua imeanuka kidogo ilikuwa ni wakati wa sisi kama nchi kuanza kuchukua raia wetu ambaao wako nje. Na ninasikitika sana kusema kwamba tumeiacha hii ya raia wetu kutoka nje mpaka mtu binafsi, Dimelo kutoka Zanzibar kwa sababu, tu ya kutaka kurudi kwenye biashara zake Zanzibar akaamua akodi ndege kwa ajili ya kuleta Watanzania wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, na juzi nilisema na kwa bahati wewe ulikuwa katika MKiti kwamba, si vizuri kwamba zoezi hilo limeratibiwa na mtu binafsi. Ningefikiri hili lisimamiwe na Wizara ya Mambo ya Nje kwa raia wetu walioko pengine nchi za kiarabu na wengine wote wanaotaka kuja na sio lifanywe na mtu mmoja, matokeo yake ni kuongeza nauli kuwa kubwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, na la mwisho katika hili la corona nilikuwa naona kwamba, najiuliza, hivi, pamoja na kauli ya Waziri kusema kwamba, alikwenda kumuwalilisha Rais. Pamoja na kauli ya Waziri kwamba, alisema anakwenda Madagascar kupewa zawadi ile kwa ajili ya Rais, nilikuwa najiuliza, hivi kweli kulikuwa kuna haja ya Waziri wetu wa Mambo ya Nje kwenda kule kisha akanywa dawa ambayo haijapitishwa vigezo vyake?

Mheshimiwa Naibu Spika, *it was risking* kusema kweli. Haikuwa na haja ya kumtuma Waziri katika vitu ambavyo vingeweza kutiwa katika *diplomatic beg vikaletwa* Tanzania, hilo kwenye corona.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni kuhusiana na nafasi yetu Tanzania *in a leadership*. Kweli tulikuwa na nafasi kubwa sana katika Afrika, na Mheshimiwa Waziri ameelezea hapa kwamba tuliachiwa misingi mizuri na Rais wa kwanza wa Tanzania. na tumekuwa na sera ambayo hajabadihilia kwa muda mrefu, unajiuliza ile misingi ile inakwendaje na usasa ikiwa sera yetu hatujaibadilisha?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo najiuliza hapa kuna malalamiko ya haki za binadamu, kuna malalamiko ya chaguzi, kuna malalamiko ya watu ku-*disappear* kila siku. Na haya ndio ambayo yanafanya Tanzania tuweze kuzuiliwa baadhi ya misaada au kuhojiwa tukiwa nje na tukiulizwa tunasema aah, sisi ni nchi huru, lakini kama ni nchi huru umo katika mikataba ya kimataifa kwa hivyo, ni lazima uwajibike kimataifa. Na ndiyo maana wengine tunasema kwamba, *impunity* imekuwa kubwa sana nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili Mheshimiwa Waziri anasema alivyokwenda Geneva kwenda kujibu hoja alijibu hoja Tanzania afya nzuri, makazi mazuri, kuna *social rights*, lakini Mheshimiwa Waziri anajua kwamba katika mikataba miwili ya Umoja wa Mataifa kuna unaoitwa *Convention of Civil and Political Rights* na kuna unaoitwa *Social Economic Rights* na zote hili zinakwenda pamoja. Huwezi kusema kwa sababu, unawapa wananchi wako malazi mazuri, umeongeza idadi ya *dispensary*, sijui watu wanaenda *school* kila siku, umwambie haki zake za *civil zisiwepo*, asiwe na haki ya kusema, asiwe na haki ya kujitetea, watu wanapotea Serikali haijibu kitu, aah, hiyo haiwezekani. Kama unafanya *social and economic rights* basi pia, *civil and political rights* zitimizwe kama kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ni kuhusiana, na hii inaleta athari kwa mfano kutoka 2015 mpaka leo kwa sababu, ya hayo niliyoyasema *FDI* zimeshuka kutoka 7 percent mpaka mwaka huu ni 5.6 ya *FDI, Direct Foreign Investimet*. Kwa hivyo, hiyo ni hasara ambayo tunaipata.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ninachotaka kuzungumzia ni kuhusiana na *diaspora*. *Diaspora* ni eneo zuri sana kuchuma, Ethiopia wanachuma vizuri sana, Rwanda wanachuma vizuri sana, seuze India, seuze na nchi nyingine. *Imagine* tunasema tuna watu labda milioni moja nje, *imagine* tunatandika mazingira mazuri, *emagine* kila Mtanzania huyo au huyo aliyeko *diaspora* alete dola 3,000 tu kwa njia yoyote nyingine ina maana tuna *three billion* kutokana na *diaspora* peke yake kwa hiyo, tukijipanga katika hili tunaweza tukafanya vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, na mwisho kabisa nilitaka kuzungumzia juu ya miradi ya Afrika Mashariki ambayo Mheshimiwa Mbunge Khatib amezungumzia. Kusema kweli hili linatusononesha sana Wazanzibari. Miradi hii tunasema sisi ni sehemu ya Afrika Mashariki, Zanzibar haiwezi kwenda kujiwakilisha peke yake ndani ya Afrika Mashariki, Zanzibar haiwezi kwenda kujiwakilisha peke yake nje ya Afrika Mashariki. Yapo hapa, mbele ya macho yetu na Serikali ya Muungano haihimizi Afrika Afrika Mashariki, haitii *pressure* Afrika Mashariki, haisimamii Afrika Mashariki ili ile miradi ije kwa Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna mpaka sasa utaratibu wowote wa *investment* ya moja kwa moja ya Serikali ya muungano, isipokuwa mwaka huu ndio imeanza kutokana na mpango wa miaka mitatu uliopangwa ndio angalao kuna miradi imepangwa kutekelezwa kuhusu Zanzibar. Kwa hivyo, nataka tupate maelezo ya kutosha kutoka kwa Mheshimiwa Waziri kwa nini miradi hii ndani ya Afrika Mashariki na Kati wanakwenda kila siku, wanarudi kila siku hajatekelezwa hata moja?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu, tunatazamia kwamba, tutapata haki yetu kuititia Serikali ya muungano, lakini kama hatuipati mnatunyong'onyesha sana; kwamba hata ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki hamuwezi kutusimamia. Ndiyo maana wakati mwingine tunasema basi, angalao twende kwenye ile katuba pendekezwa kwamba angalao Zanzibar katika mambo mengine iwe inajisimamia

yenyewe kwa sababu, mnaonekana hamna hamu, hamna *interest*, hamna wakati wa kutusimamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Asante sana. Mheshimiwa Ali Hassan King, atafuatiwa na Mheshimiwa Salum Mwinyi Rehani, tutamalizia na Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete.

MHE. ALI HASSAN OMAR KING: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Awali ya yote, nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametupa uhai na kutufanya kuwa wazima tukasimama leo katika Bunge hili tukaongea mambo yetu haya ya utangamano na dunia kwa sababu mtu huwezi kuishi katika dunia ikawa kama uko peke yako, ni lazima ushirikiane na wenzako. Kwa hiyo nashukuru sana kwa kupata nafasi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na kisa kimoja, kuna kisa kimoja cha kobe na ndege mmoja anaitwa chozi. Chozi ni ndege mmoja mdogo pengine labda kama simu hii ya tochi, lakini alitua kwenye mgongo wa kobe. Sasa wakati anataka kuondoka yule chozi akasema nakuaga kobe jitayarische sasa, nataka kuruka kutoka mgongoni kwako. Kobe akamjibu, ulipotua wewe ilipaswa uwe na vishindo vikubwa sana kuliko hivi unavyotaka kuruka. Ruka tu nenda zako, ulivyotua hukuwa na kishindo, je wakati wa kuruka? Kwa hiyo ruka wewe nenda zako huwezi kusumbua kitu chochote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, maana ya mfano huu nimechukulia kwamba hivi kweli hata Rwanda anatufungia mpaka? Rwanda anao ushirikiano na Burundi, Rwanda anao ushirikiano na Uganda, mipaka yake iko wazi kweli? Halafu akaseme kwamba madereva wa Tanzania wakalipe dola 500 kwa kwenda Rwanda wakati yeye ana kilometra 1,000 na zaidi kutoka Rwanda mpaka Dar es Salaam? Hivi huyu si chozi juu ya mgongo wa kobe na sisi bado tunamtazama? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpe hongera sana Mheshimiwa Waziri alipoelezea *balance of trade*, kwamba sisi tuna *positive*, lakini tukaja tukapima baadhi ya mataifa haya mengine ambayo yanasema yatafanya hivyo kwamba yatafunga mipaka. Kwa nini na sisi yetu tusifunge? Kwa sababu wakati mwingine diplomasia ya kubembelezana, inapaswa kwamba tujaribu kuitazama. Pamoja na yote, katika *East African Community, Article 24* ambayo imeeleza tukiwa wastaarabu, imeeleza *East African Community Committee on trade remedies*, hapa kama kuna *disputes, certain mechanism* imeelezwa hapa na hapa inatakiwa kuwepo na Kamati. Kamati hii ikiundwa ina maana kwamba haya yangewahiwa mapema kufanyika kabla ya kufikia hapa tulipo sasa hivi. Kwa mujibu wa sasa hivi tutasikia atakwenda Waziri kuzungumza na huyu, atakwenda nani kuzungumza, wakati mfumo upo!

Mheshimiwa Naibu Spika, hii *article* iko tangu mapema tukiwa nchi tatu kwa sababu hii *committee* imeeleza kwamba itakuwa ina wajumbe watatu kutoka kila nchi na wajumbe wote jumla watakuwa tisa. Kwa maana hiyo ni wazi, wakati huo hakuwemo Rwanda, Burundi na Sudani ya Kusini. Kwa hiyo tunaomba kama tunataka mambo yetu yawe yanakwenda vizuri, tujaribu kuitazama hii ili twende vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo amemalizia kulizungumza Mheshimiwa Ally Saleh, niipongeze sana Serikali kwa kufanikisha, katika mafanikio wametaja hapa katika ukurasa wa 14 katika miradi ile ya kipaumbele ya Afrika Mashariki, kweli Julius Nyerere mkituambia tunaiona tunapiga makofi kwa hilo, barabara tunaziona, lakini vingine vimetajwa kwenye mafanikio hapa kama uwanja wa ndege wa Pembra na Bandari ya Mpigaduri, hii naona kwamba sijawahi kuviona hivi vitu. Ndiyo itakuwa yale kwamba samaki anakula mwingine vumba linanukia kwingine. Sasa *at least* Mheshimiwa Waziri aje atueleze kwamba kwenye hii miradi mingine ambayo kimacho hatuioni, lakini imo katika mafanikio kwamba mafanikio/hatua zake ni zippi, hatua hizo zimepigwa kutoka wapi mpaka wapi? Hata hivyo,

napongeza kwa kuiweka miradi hii ya kipaumbele katika maeneo hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine, niipongeze sana Serikali, wameelezea katika sehemu ya pili ukurasa namba saba aya ya 14 kwamba tumeongeza Balozi mpya. Tumeongeza Balozi mpya nane, tunapongeza sana na sasa hivi tuna Balozi 43, tunapongeza sana, nchi yetu imesonga mbele na tunakwenda vizuri. Hapa nataka nitoe ushauri wangu na huu ushauri naomba uniruhusu nieleze jinsi ya kuzungumza na mtu mkubwa. Mwenyezi Mungu alivyokuwa anataka kutoa mifano ya wafalme waliofanya uadilifu katika vitabu vitakatifu, alikuwa anamtumia Daudi na Suleiman.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwenyezi Mungu anasema kwamba walikwenda watu wawili wamegombana mbele ya mfalme Daudi ambaye pia ni Nabii huyu, mmoja akamshakti mwenzake akasema *Inna hadhii, afiyalahu, tisuu watsiuna naaja*, huyu ndugu yangu ana kondoo 99; *walia naajatun wahida* na mimi nina mmoja; *Faqala Filniha waazani filhitwab* akasema tuchangane halafu akanishinda kwa hoja. Nabii Daudi akajibu, *Faqad dhwalamaka akhuka fiswali najatika illa-nniaj* amekudhukumu huyu ndugu yako. Nabii Daudi akajua pale pale kumbe yeye ndiye alikuwa na wake 99 lakini kuna na mke wa mwenzake mmoja alikuwa pia naye anamtaka. Kwa hiyo Nabii Daudi alipotanabahi kwamba lile ni fumbo amepigwa yeye, Nabii Daudi akarukuu akasujudu akamwomba Mungu *maghfira*, amsamehe.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa nina maana kwamba Balozi hizi 43, ajira zake zikoje katika uwiano? Mungu amemtumia Daudi, Daudi ni mfalme na mimi naomba kwamba tuelezwe hili kwa sababu uwiano unatakiwa, lakini Balozi hizi mpya nane, je, ajira zimetimia? Kuna baadhi ya ofisi baada ya Balozi na Mhasibu, hakuna kitu kingine kinachoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ambacho napenda kukizungumza katika nchi zote za *East Africa*, zina *policy*. Tunawapa Wabunge wa Afrika Mashariki, tunawapa kitu gani

cha kwenda kusimamia kule? Wenzetu wana *policy*, *policy* inazaa mkakati, mkakati wanajivekea malengo yao. Je, wale Wabunge wetu sisi wa *East Africa* kila mmoja akili yake kichwani mwake, anachokiona mbele yake ndicho anachowea kufanya. Kwa hiyo tuwe na hiyo *policy* na tuweze kuwafanya hiyo *evaluation* ya vile vitu ambavyo wanaenda navyo kule ili na wao wakija siku nyingine watuambie wamefanya kitu gani ili tuweze hicho kitu kiweze kwenda katika mustakabali mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jambo lingine, Wakuu wa Nchi zetu hizi, walipokaa walizungumza mambo matatu. Nilitazama kwenye mafanikio ya Wizara nilifikiri ningeviona kwa sababu Wizara ndiyo mratibu wa mambo haya. Suala moja, *Food Security Action Plan*, 2009 je, mafanikio yake tumefikia wapi? je tunafanya *monitoring and evaluation*? Tunaripoti wapi hiki kitu? Pia *climate change policy*? Je, kiko chini ya uratibu wa hii Wizara katika *East Africa*, je kimefikia wapi? Pamoja na *industrialization policy*, tunajua Wizara hizo hapa zipo, lakini *as far as East Africa Community* ambayo Waziri wake yupo katika hii *International Relation* atatuelezea vipi hii *connection* na mafanikio yake yakoje. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, nashukuru sana. (*Makofî*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nilishamtaja Mheshimiwa Salum Mwinyi Rehani, atafuatiwa na Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete. Mheshimiwa Balozi Adadi atachangia kwa dakika tano. Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro ajiandae.

MHE. SALUM MWINYI REHANI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia kwenye Wizara hii. Wizara ambayo ni moja katika wizara ninazozisimamia katika Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Nimshukuru sana Waziri, Mheshimiwa Profesa Kabudi kwa ushirikiano ambao tumekuwa tukishirikiana katika kuhakikisha kwamba mambo yanakwenda katika Wizara hii sambamba na Naibu wake Mheshimiwa Dkt. Ndumbaro, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu

na watendaji wengine wa Wizara hii. Vile vile niishukuru Kamati kwa ujumla tunavyoweza kushirikiana na kutoa mawazo mbalimbali ya kuishauri Wizara hii na kuhakikisha kwamba Wizara inatekeleza mapendekezo na ushauri tunaoutoa wakati wa vikao vyetu nya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Serikali kupitia Wizara ya Fedha hasa kwa ule ushauri tuliooutoa kwa hali ambazo Balozi zetu katika nchi za nje zilivyokuwa. Zilikuwa na hali mbaya sana kwa kweli, majengo yake yalikuwa ni ambayo kwa kweli hayastahiki kukaa Mabalozi, lakini leo fedha ziliweza kutoka hasa kwa ukarabati wa Balozi ya Sudan nchini Sudan pale, *DRC Congo*, hata ile ya Lusaka na hata ukiangalia Canada, Sweden, zimeleta mwelekeo mzuri sasa na kuona kwamba Mabalozi wetu wanafanya kazi katika ofisi zinazostahiki. Kwa hili kwa kweli nikupongeze sana Waziri wa Fedha, nikushukuru sana kwa imani yako na kuwafanya Mabalozi wale kuweza kuwa na mwelekeo mzuri wa kazi zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili sambamba na kwamba tunaimarisha miundombinu ya Balozi zetu, lakini tunahitaji *outcome* itoke kwa Mabalozi hawa. Mwelekeo wetu tuliokuwa nao kama nchi ni diplomasia ya uchumi na kipimo kikubwa cha Balozi kwa nchi anayoiwakilishi, tunahitaji tuone kwamba analeta uwekezaji au anashawishi utalii kwa kiasi kikubwa ambacho ndiyo itakuwa dira na mwelekeo wetu wa hapa nchini na sio Balozi anakwenda miaka mitano lakini anashindwa kuleta hata mradi mmoja ndani ya nchi. Hili vile vile tulimshauri Waziri awaeleze Mabalozi kupitia Kamati, tunahitaji tuone matokeo chanya ya uwakilishi wao katika nchi ambazo tumewapeleka. Tuone matunda haya ndani ya miaka mitano kama nchi inavyoweza kutekeleza miradi mikubwa ya kiuchumi, basi tuone Balozi zetu hizi zinatuletea miradi mikubwa ya uwekezaji ndani ya nchi na kuweza kunufaika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine tunataka diplomasia hii ya uchumi iweze kukabiliana na changamoto ambazo zinajitokeza katika maeneo yetu mbalimbali. Tumeona wenzetu walichoanza kukifanya, tunafungiwa mipaka kwa

sababu ya Bandari ya Dar es Salaam inavyofanya kazi. Ukitfunga mpaka wa Zambia umefunga mipaka ya nchi nyngi tu wasiweze kutumia Bandari ya Dar es Salaam. Sasa ni wajibu wa Mabalozi wetu, si tu Waziri peke yake, wao ndiyo wako kule watekeleze wajibu wao wa kukutana na Mabalozi na viongozi wa nchi husika kuweza kuingilia kati hili suala na kueleza dhima na dhamira yetu, kwa nini tumeacha mipaka wazi, tuna nia gani na malengo yetu ni nini? Si kama nchi haikufikiria kuamua kuacha hii mipaka wazi ili kuwe na dhamira maalum na lengo mahsusili la kufanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande mwingine ukiliangalia wenzetu wanatuangalia kwa sura nyngine. Kitendo cha kuacha mipaka yetu wazi ni kuimarisha bandari yetu, ni sahihi lakini za kwao zikoje na wameshafunga? Kwa hiyo wanachoona ni kwamba Tanzania inaweza ikafaidika na ikaondokana na mtikisiko huu wa *corona* usiwakumbe zaidi kuliko wao. Kwa hiyo ili twende sambamba au tutikisike sote, wanaamua kutuletea hizo figisu. Kwa hiyo, nimwombe Waziri atoe wito maalum kwa Mabalozi wetu kuweza kusimamia hili suala kwa sababu likiachwa hapa, leo umefungwa wa Kenya, Zambia lakini kesho utafungwa wa Msumbiji na keshokutwa utafungwa wa Malawi na mingineyo. Sasa hizi zinakuwa ni hujuma za makusudi. Naomba sana tuliangalie kwa upana zaidi na tuweze kuwashauri Mabalozi wetu, haya ni mambo ambayo wao wanatakiwa wayafanyie kazi na kuleta mrejesho huku utakaoweza kusaidia ustawi wa uchumi na biashara katika maeneo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nataka kulizungumza ni suala zima la *standard*. Nchi yetu ina tatizo la *standard* hasa kwenye maeneo mengi ya bidhaa hizi ambazo zinaingia katika biashara kwenye Afrika Mashariki, *SADC* na masoko mbalimbali ya duniani. Kama nchi kwa mfano, hatuna *standard* za kilimo mpaka sasa, kitu ambacho kinafanya bidhaa zetu ziuzwe kijumla na sio kwa viwango/*grade* ambazo zimepangwa kwa mujibu wa unavyotakiwa katika masoko ya nje. Linatukwaza kwa sababu *East African Standards*sasa hivi wanamalizia kuzitengeneza. Zitapomalizika

zitakuja kutukwaza na bidhaa ambazo sisi tunataka kupeleka ndani ya Soko la *East Africa* kwa sababu sisi zetu hatujaziwekea mkakati na kuzitengeneza na kuzitoa zikaweza kutumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa wenzetu wanatutega kwa sababu wenzetu sasa hivi wako mbele sana kuhakikisha kwamba wanakuwa na *standards* zao. Rwanda zao wameshazitangaza, Uganda wameshatoa, Kenya tayari, sisi zetu kama nchi hatujatoa, *standards* ambazo zingeweza kusaidia sasa kuelekeza mazao yetu na bidhaa zetu kuuzwa katika *common market* ambayo iko ndani ya soko la *SADC* na soko hili la *East Africa*. Sasa sjui Waziri...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa muda umeshaisha, kengele mbili zimeshagonga. Ahsante sana.

MHE. SALUM MWINYI REHANI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Haya shukran. Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete, atafuatiwa na Mheshimiwa Balozi Adadi Rajabu atakayechangia kwa dakika tano na Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro ajiandae.

MHE. SALMA R. KIKWETE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ili niweze kutoa mchango wangu kidogo kwenye Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika ya Mashariki. Kabla sijaanza lolote, naomba nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu na nikushukuru wewe kwa kazi kubwa na nzuri ambayo umeifanya katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama mwanamke na tunasema wanawake ni lazima wapate nafasi. Sisi tunajivunia wewe kama mwanamke kuwa ni kiongozi wetu katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tunakupongeza sana na Mwenyezi Mungu azidi kukubariki na uendelee na hatimaye urejee tena uendelee

kufanya kazi hii na wewe uwe ni kama kigezo kwa wanawake ndani ya Taifa letu, barani na duniani kwa ujumla. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo, naomba nitoe pongezi zangu kwa Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama nilivyo sema kwa kazi kubwa na nzuri anazozifanya. Sambamba na hilo, Waziri Mkuu, Mawaziri na Spika kwa ujumla wake pamoja na Wabunge wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niende kwenye Wizara husika. Hongera sana Mheshimiwa Waziri Profesa Kabudi, kwa kazi ambayo anaifanya pamoja na Naibu wake pamoja na wataalam wote katika Wizara hii husika. Hongereni sana kwa kutupa mwelekeo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka kusema leo, mimi ni Balozi wa Kiswahili Barani Afrika. Nataka kuiongelea lugha na lugha yenyewe ni ya Kiswahili. Lugha ni sauti za nasibu zinazobeba ujumbe na ujumbe ule unakubalika katika jamii ya watu ili waweze kufanya mawasiliano. Lugha kama nilivyo sema ni chombo cha mawasiliano. Sisi kama Watanzania tuna lugha yetu na lugha hii si nyingine bali ni lugha ya Kiswahili, lakini lugha inaweza kukua na inaweza kufa. Inakua kwa sababu gani na inakufa kwa sababu gani? inakua kwa kuwa na watu wengi wanaozungumza lugha hiyo katika maeneo husika na lugha ili iweze kukua ni lazima siku hadi siku iongeze msamati wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaona kwamba lugha ya Kiswahili sasa hivi ina watu zaidi ya 200,000,000 wanaozungumza duniani kote. Kwa hiyo lugha yetu inajipambanua yenyewe katika kuzungumzwa na watu mbalimbali katika mabara mengi tofauti. Lugha inaweza kufa, kufa kwa lugha ni kinyume chake cha yale ambayo nimeyaeleza hapo mwanzo. Sasa tunachotakiwa kufanya ni kuandaa wataalam, kuandaa watu wawepo kwa wingi zaidi ili waweze kuzungumza lugha hiyo. Tukiwa na wataalam

wengi, tukiwa na watu wengi, tunaweza kueneza lugha hii sio ndani ya nchi yetu, sio Afrika ya Mashariki bali sehemu kubwa katika mabara tuliyokuwa nayo hapa duniani.

Kama nilivyosema suala zima la lugha, ninachoshauri au ninachokiomba ni kwamba sisi kama Watanzania kwa sababu nchi zimejipangia utaratibu wake. Nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wetu kwa kuongeza kipaumbele zaidi lugha ya Kiswahili kuwa ni lugha ambayo itazungumzwa kwenye maeneo ya *SADC*. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nikiwa mke wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Awamu ya Nne nilikuwa nahudhuria vikao vyta wake wa Marais Barani Afrika na kule kwenye *AU* hii ni lugha ambayo inazungumzwa na inautaratibu wake wa kisheria na inazungumzwa kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kuzungumzwa Afrika ya Mashariki ni jambo kubwa na jema kama *AU* wanazungumza kwa nini isiwe ni lugha ya dunia. Kikubwa tunapozungumza hatuna maana kwamba tuache Kifaransa, Kiingereza, Kireno na lugha nyingine, ni lazima hizi lugha tuzungumze na Kiswahili iwe ni miongozi mwa lugha zinazozungumzwa katika Bara kwasababu tunapozungumza lugha zile nyingine si lugha zetu, ni lugha ambazo waliotutawala walituletea lakini kama tuna kitu chetu ambacho ni kizuri kwanini tusikiweke na tukakiendeze hatimaye tukajivunia chetu kwasababu lugha ya Kiswahili... hatusemi lugha ya Kiswahili ni ya yule wala yule, lugha ya Kiswahili ni yetu inayotokana na sisi wenye. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nachopenda kushauri zaidi ya hii, wageni wanapoingia kwenye nchi yetu iwe ni ajenda ya kudumu wajifunze lugha ya Kiswahili kama ilivyokuwa maeneo mengine tukienda tunajifunza lugha zao. Vilevile, kwenye Balozi zetu kuwe na waambata wa lugha ya Kiswahili; ni wakati muafaka sasa hivi Kiswahili kukiendeze kwa nguvu zetu zote kuhakikisha kwamba siku hadi siku kinaendelea Tanzania, Afrika Mashariki, Afrika na duniani kwa ujumla. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, mchango wangu ulikuwa ndiyo huo, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja kwa mia moja. Na ninawashukuru watu wote pamoja na maeneo yale niliyokuwa nayafanyia kazi Mkao wa Lindi na Mkao wa Pwani kwa ushirikiano mkubwa walionipatia katika kipindi changu cha Ubunge. Ahsante sana, nakushukuru sana, Mwenyezi Mungu akubariki. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Amina, ahsante sana. Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro, mto hoja ajiandae.

MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kupata nafasi hii ya kuchangia hoja hii ya Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje, Wizara ambayo nimeitumikla kwa kadri ya miaka kumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ningependa kumpongeza sana Prof. Kabudi, Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na wakurugenzi na Mabalozi wote ambao wanatuwakilisha huko nje za nchi. Kazi ambayo wanafanya ni kubwa na inajulikana na kwa kweli inabidi ipongezwe sana. Nampongeza pia Prof. Kabudi kwa kazi nzuri anayofanya kwa ajili ya kuangalia mikataba mibovu ambayo ilisainiwa hapo nyuma na hususan mkataba wa Barrick ambao Watanzania wengi wanaupongeza sana, hongera sana Mheshimiwa Profesa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ni Wizara muhimu sana kwasababu ni Wizara ambayo ni kioo cha ukitaka kujua Tanzania iko vipi basi unakwenda kwenye Balozi zetu ambazo zipo kule nje ya nchi. Sasa nimeona kwenye bajeti suala la makazi na ofisi za Balozi hususan kwenye maendeleo ambayo wamepewa bilioni 20. Hii ni hatua moja ambayo inapongezwa sana lakini ni kuhakikisha kwamba kweli hizo fedha zinatoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, makazi na ofisi za Balozi ambazo zipo nje ya nchi kwa kipindi kirefu sana zimekuwa

na hali mbaya sana. Na zimekuwa na hali mbaya utakuta mpaka Mabalozi wengine imebidi wahame kwenye zile nyumba wapangishe nje na kitendo hicho imeangalia kwenye *CAG report* ya mwaka huu nyingine zimewaletea query. Lakini ni vizuri sasa fedha hizi ambazo zipo basi zihakikishe kwamba zinaangaliwa Balozi zile ambazo zina matatizo makubwa ili ziweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, isitoshe hivyo viwanja 12 vipo huko karibu miaka 20, ni muda mrefu sana na Mabalozi wamepata tabu sana kuvitetea viwanja hivyo visiweze kuchukuliwa. Vingine vimekuwa ni mapori, mwenyewe nilikuwa nakaa kwenye nyumba ambayo ni heka karibu 6 pale Harare lakini nyumba ambayo imejengwa ya Ubalozi nilikuwa nakaa kwenye heka 3 kubwa kabisa na heka 3 nyingine ni pori tu. Kwa hiyo, nimekaa pale kwa muda mrefu lakini utakuta usumbufu ambao unaupata kwa nini unaweka pori Mheshimiwa Balozi wanakuwa ni wanaku heshimu tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni vizuri ikawekwa mikakati maalum ambayo hivi viwanja vitajengwa nyumba kama Ubalozi wa Msumbiji hapa, ghorofa lile la ghorofa 9 ambalo limemalizika kujengwa na nafikiri litakuwa limeshaanza kupangishwa, ni kitu ambacho ni cha kujivunia kwasababu fedha ambazo zitapatikana pale zitaweza kulisha Balozi zote Kusini mwa Afrika na bei ya nyumba Msumbiji ni kubwa. New York kuna jengo zuri sana ambalo limejengwa na Ubalozi na Washington. Kwa hiyo, mambo kama yale ndiyo mambo ambayo yanatakiwa. Lakini ili iweze kufanya vizuri ni vizuri tukatumia hata hifadhi zetu za jamii ili ziweze kusaidia kujenga majengo kama yale.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ambalo ningependa kuongelea ni suala la diplomasia ya uchumi...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa
Mzungumzaji)*

MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, diplomasia ya uchumi, Wizara hii ni mtambuka na kama mtambuka Mheshimiwa Rais ametoa maagizo kwa Waheshimiwa Mabalozi na amewapa changamoto kila *quarterly* lazima walete taarifa kitu gani ambacho wanakifanya, ni suala la msingi sana lakini nilikuwa naomba kwamba wasaidiwe hawa Mabalozi kwasababu Wizara hii kama mtambuka Mabalozi wanashughulika na Wizara nydingi; mambo ya utalii, biashara na viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tulikuwa tunaomba kwamba Wizara ya Maliasili na Utalii itenye bajeti kusaidia Mabalozi hawa kuweza kuwawezesha ku-move kwenda sehemu mbalimbali ambazo wanatakiwa kufanya na Wizara ya Viwanda na Biashara pia aingalie kupeleka *ma-trade attaché* kwenye sehemu ambazo ni muhimu kwenye zile nchi ambazo zinaweza kuwasaidia Mabalozi wale waweze kufanya kazi. Mabalozi wanashindwa kusafiri kwenda kwenye sehemu nyagine kwasababu kwa mfano yupo Washington kitu kipo Santiago ziko California huko sasa anakwendaje kule ni Wizara hii ya Maliasili inatakiwa iweze kusaidia kuweza kunanii, kufanya matangazo pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wakati Wizara ya Utalii ilitoa matangazo mazuri sana kwenye mipira hii ya *Premier League* ya Uingereza ambayo ulikuwa unaona wanavyotangaza Ngorongoro, Serengeti na vivutio vyetu vyote vya utalii. kwa hiyo, ni vizuri Wizara mtambuka na zenyewe ziweze kuchangia kwenye Wizara hii ya Mambo ya Nchi za Nje. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunivumilia na naunga mkono hoja, asante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. ORAN M. NJEZA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano

wa Tanzania; Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Waziri, Naibu MaWaziri na viongozi wote wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa uongozi wao na utendaji uliotukuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na uongozi wote wa Bunge kwa uongozi wenu mahiri na wenye ubunifu wa hali ya juu katika kuongoza mhimili wa Bunge hasa katika kipindi hiki tunapopambana na janga la Covid-19.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha miaka minne iliyopita, Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki imetekeleza miradi mingi na pia kuboresha mazingira ya ufanyaji kazi wa Balozi zetu kujielekeza zaidi kwenye diplomasia ya kichumi. Balozi zetu zilijielekeza zaidi kuchochaea kukua kwa mauzo ya mazao yetu na madini pamoja na bidhaa zingine kwenye masoko ya kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza Serikali iendelee na msukumo wa kutumia Balozi zetu kutafuta masoko ya mazao yetu na bidhaa zingine kwenye masoko ya nje. Pia nashauri msukumo zaidi kuimarisha Jumuiya zetu za Afrika Mashariki, SADC na AU.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi hiki tunapopambana na janga la corona virus (Covid-19), tumejifunza umuhimu wa kuwepo kwa mikakati mbadala kama vile kufanya kazi kwa kutumia TEHAMA. Napendekeza Balozi zetu zifanye mikakati ya kuunganisha Soko letu la Bidhaa (*TMX*) na masoko mengine ya kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. PROSPER J. MBENA: Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa uongozi wake mahiri katika kuliongoza vyema

Taifa letu. Napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Profesa Kabudi, Mbunge na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa hotuba yake nzuri ya bajeti alioisoma hapa Bungeni leo 13 Mei, 2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekuwa Mjumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama hivyo mambo mengi yanayohusiana na bajeti ya Wizara hii tuliyajadili kwenye vikao husika. Hata hivyo napenda kutoa maoni yafuatayo:-

Kwanza, Sera ya Mambo ya Nje inayotumika hivi sasa ni ya mwaka 2001; ni muda mfupi tu uliopita lakini kama kuna mabadiliko kimtaalamo ya nchi yetu ni vyema sera hiyo ikapitiwa tena upya kwa lengo la kuiboresha na kujumuisha mambo mapya muhimu yaliyojitokeza. Kwa mfano mahusiano ya kidiplomasia kati ya Tanzania na Israel kwa sasa ni mazuri na yamerudi katika hadhi ya kila nchi kufungua Balozi kamili.

Pili, kutotolewa fedha za ujenzi wa Ubalozi wa Tanzania huko Muscat, Oman. Pamoja na matatizo ya fedha tuliyonayo, bado nasisitiza umuhimu wa kujenga ubalozi huo kutokana na umuhimu wake kiuchumi na kidiplomasia. Toka mwaka 2014 kiwanja cha ujenzi huo kilishakuwa tayari na fedha za ujenzi ziliombwa kuanzia mwaka 2017/2018 hadi mwaka huu, lakini hakuna fedha iliyotolewa. Tunafahamu kwamba gharama za ujenzi hupanda mwaka hadi mwaka hivyo kuchelewesha ujenzi wa Ubalozi huo utaongeza gharama ya mradi huu muhimu na pia kuchelewesha nchi kupata faida ambazo zingepatikana kwa kuwepo Ubalozi Oman.

Tatu, umiliki wa Chuo cha Diplomasia - Kurasini sasa upatiwe ufumbuzi wake. Sio sahihi kwa chuo hicho kinachomilikiwa kwa pamoja Tanzania na Msambiji lakini Msambiji hawalipii chochote na wala hawajihusishi kwenye uendeshaji lakini badala yake Msambiji imeanzisha chuo chake chenyewe cha diplomasia nchini Msambiji. Kinachotia hofu zaidi Serikali inagharamia upanuzi wa chuo hicho kwa

fedha zake pasipo kwanza kupata ufumbuzi wa suala la umiliki wake. Wizara kwa zaidi ya miaka mitatu imekuwa haina maelezo ya kuridhisha. Kutoptana kwa *Joint Permanent Commission* kati ya nchi mbili hizi ndio imetumika kama sababu ya kutopata ufumbuzi wa jambo hili. Naunga mkono hoja.

MHE. ENG. CHRISTOPHER K. CHIZA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote kwa kazi nzuri Wizara inazofanya kuishirikisha nchi yetu na Mataifa mengine. Naomba kuishauri Wizara katika mambo mawili yafuatayo:-

Kwanza, nimemsikia Mheshimiwa Waziri akiongelea uhuru wa kuwashirikisha *diaspora* katika masuala mengi ya maendeleo ya nchi. Nakubaliana na suala la kuanzisha kanzidata ya *diaspora* ili kujua nani, yuko wapi na anajishughlisha na nini. Uzoefu wangu katika nchi nilizotembelea ni kwamba *diaspora* wengi hawapendi kujitambulisha kwenye Ofisi za Balozi. Aidha, baadhi ya *diaspora* nilioongea nao wanalamikia ushirikiano mdogo wanaopata kutoka kwa wafanyakazi ubalozini. Nashauri katika zoezi la sera inayowagusa *diaspora*, mnganza na changamoto ya mahusiano ya *diaspora* na Ofisi za Ubalozi.

Pili, Wizara iratibu na kufuatilie utekelezaji wa maazimio yote ambayo nchi yetu inafanya ili tusikose ushirikiano na wenzetu kwa kutotekeleza tulyokubaliana. Kwa mfano, mwaka 2004 nchi wanachama wa *SADC* kuitia *Maputo Resolution* zilikubaliana kutenga asilimia 10 ya bajeti zao kwenye sekta ya kilimo. Je, Tanzania inaweza kuonesha tangu mwaka 2004 tumekuwa tunatenga kiasi gani (*on an incremental basis*). Huo ni mfano tu lakini maazimio yako mengi na mengine tunayapitisha mara kwa mara humu Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. KANGI A. LUGOLA: Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea kukupongeza Dkt. Tulia ambaye ametulia kwa

namna ulivyo na weledi na umahiri wa kuliendesha na kuliongoza Bunge lako tukufu pamoja na Spika Mheshimiwa Job Ndugai.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimpongeze Mheshimiwa Rais wetu kipenzi cha Watanzania Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kuliongoza Taifa hili kwa ujasiri na umahiri mkubwa. Vilevile niendelee kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa SADC na weledi na umahiri alionao katika kuiongoza Jumuia hiyo.

Aidha, nimpongeze Mheshimiwa Waziri ndugu yangu na rafiki yangu mkubwa kwa uwezo wake mkubwa wa kuweza kuiongoza vizuri na kuiimarisha Wizara hii katika medani za kidiplomasia ama kweli kipere kimepata mkunaji. Nimpongeze pia Naibu Waziri ambaye tulsoma naye *Box 2*, kwa namna anavyochapa kazi tangu kuteuliwa kwake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mambo machache ya kuzungumza; jambo la kwanza ni kwamba nchi yetu tumeendelea kutekeleza na kufaidi sera yetu ya uchumi wa kidiplomasia. Kutohana na ugonjwa hatari wa mlipuko wa virusi vya Corona ambao umesambaa katika nchi mbalimbali duniani ni dhahiri kwamba kutakuwepo na mtetereko na m dororo katika sekta ya uchumi wa kidiplomasia. Kama tulivyoitahadharisha Serikali kwenye sekta ya utalii ni vyema Wizara hii ikajiandaa kwa mikakati mizuri ya *fallback position*, vinginevyo bila kijiandaa tunaweza tukawa katika hali ngumu sana katika sekta hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili niishauri Serikali kupata ufumbuzi wa kudumu juu ya umiliki na uendeshaji wa Chuo cha Kidiplomasia kilichopo Kurasini, Tanzania kwani toka mwaka 1983 ni muda mrefu sana. Katika hali ya kawaida nchi ya Msumbiji kutoendelea kushiriki kutoa michango yao ya uendeshaji wala kushiriki katika menejimenti ni dalili tosha kwamba nchi hiyo haina nia wala uhitaji tena wa chuo hivyo. Ni vyema ufumbuzi wa jambo hilo ukafanyika ili kuwa na umiliki na uendeshaji unaoeleweka na ni pamoja na

kurekebisha takwimu za idadi ya vyuo vinavyomilikiwa na Serikali ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu ni kuitaka Wizara hii kutupia macho kwenye ajira za Jumuiya ya Afrika Mashariki yaani EAC kwani baadhi ya nchi zimekuwa zikifanya *lobbying* ya hali juu kuajiri zaidi watu wao. Katika Bunge la Jumuiya hiyo yaani EALA nchi yetu hajjawahi kushika nafasi ya Katibu wa Bunge ilhali nchi waanzilishi wa Jumuiya hiyo yaani Tanzania, Kenya na Uganda tayari Kenya na Uganda watu wao walishakuwa Makatibu. Taarifa nilizonazo ni kwamba Katibu ambaye ni Mganda amestaafu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache, naunga mkono hoja.

MHE. HASNA S. K. MWILIMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa namna anavyochapa kazi katika Wizara hii hasa kusimamia masuala muhimu ya nchi yetu hasa kusimamia rasilimali za nchi kama vile madini, kufanya marekebisho ya Sheria za Madini ambazo sheria hizo zimepelekea kulinda maslahi ya nchi na maslahi ya wachimbaji wazawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo nianze sasa kutoa mchango wangu, natambua Serikali ina nia njema ya kuchukua maduhuli yanayokusanywa na Balozi zetu na kurejesha asilimia fulani ya maduhuli hayo, changamoto inayowakuta Mabalozi ni maduhuli hayo kutotolewa kama Serikali ilivyokusudiwa na kuwasababishia Mabalozi kupata shida ya kutatua mahitaji muhimu ya kiofisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi lao ni Serikali kuwaangalia ili kila wanapoleta maduhuli basi Serikali iwe inawarejeshea mapema ili na wao waweze kutatua changamoto zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ningependa kuishauri Serikali kuona umuhimu wa kutoa viza ya USD 50 wanayolipa raia Congo kuja Tanzania kwani sote

tunafahamu ni namna gani wanavyoingizia nchi yetu pesa za kigeni kwani mahitaji yao kwa zaidi ya asilimia 80 wanachukua Tanzania kupitia mikoa ya Mbeya, Katavi, Kigoma na Rukwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichangie kidogo suala la Covid-19 *around East Africa countries*. Hivi karibuni tumeona baadhi ya nchi za umoja huu wakiwanyanya madereva wa malori toka Tanzania kuwa wao ndio wanaingiza Corona nchini mwao hivyo kuwakatalia wasiingie nchini mwao na badala yake walale kwenye malori yao na kuna tukio lilitokea la dereva kujisikia vibaya na kwenda kwenye zahanati na nchi fulani mpakani na kukataliwa kutibiwa kwa kigezo cha ye ye kuwa Mtanzania, hii ni ukiukwaji wa haki za binadamu na hata ukiukwaji wa ushirikiano wa nNchi za *East Africa*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi kwa Wizara ni vyema Umoja wa Mawaziri wa nchi hizi mkakaa na kulijadili kwani kwa taarifa zilizopo Rwanda wanatumwa askari wao kupokea malori kutoka mpakani na kuingiza Rwanda kisha kuwarejeshea madereva wetu wa Tanzania magari yao baada ya kupakuwa mizigo, huu ni zaidi ya unyanyapaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee kidogo suala la Wabunge kuwa na *Diplomatic Passport* na wenza wao kukosa pamoja na watoto suala hili binafsi nimeli-experience wakati nikiwa naumwa na natumia *wheel chair* mimi na kuwa *treated* tofauti na familia jambo ambalo linapelekea usumbufu mkubwa. Kwa nini tusipewe wote kwani hizi *passport* ni miaka mitano tu ya Ubunge wetu kimkataba na za watoto na mwenza pia zinaisha miaka mitano ili kupunguza usumbufu unaojiteza kwa Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili katika hili ni familia za Wabunge waposafiri wako Wabunge ambao wamekuwa wakirejeshwa *VIP* na kufukuzwa kuwa wakapite *terminal* ya kawaida, hii ni kuwadhalilisha Wabunge wakati hadhi yao ni kupita *VIP* na wapo Wabunge wamekuwa wakiwasindikiza watoto, wake zao wazazi wao na kupita VIP na wao pia

kufukuzwa ili hali familia hizi ziko na mbung kwa kugezo cha eti wanasafiri bila mbunge Mhe waziri Kabudi ni vema hili likaangaliwa upya kwani kwa mujibu wa stahili za mbunge ye yote mi ongoni mwa hao wanapo umwa na kutakiwa kupelekwa nje ni bunge na Serikali ndio wanao ghamaria, iweje kwenye kupita *VIP Terminal/na Diplomatic Passport* ndio iwe shida?

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali ili angalie hili kwa mapana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naunga mkono hoja.

MHE. SILAFU J. MAUFI: Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya, nguvu na uwezo wa kuchangia kwa kusisitizia kasi ya maendeleo ya kuweka sura ya nchi kuwa yenyе hadhi stahiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Mambo ya Nje ni Wizara inayohusika ndani na nje katika kushirikisha Wizara zote za nchi katika kuzitangazia, kuzifuatilia kwa mafanikio ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, maombi ya fedha za maendeleo shilingi 4,000,000,000 kwa mwaka 2019/2020 ambayo imetoka kwa asilimia 12.2 kiasi ambacho hakikidhi mahitaji. Napenda kuishauri Serikali yangu kwamba kutokuwa na majengo bora ya ofisi na makazi ya Tanzania huko ughaibuni kuwa hoi ni kujidhalilisha wenyewe. Hivyo tunaomba Hazina kutoa fedha kwa mujibu wa Bajeti inayopitishwa na Bunge kwa mwaka 2020/2021 kama siyo kwa 100% basi angalau 85% kwani nchi yetu sasa inaheshimika kuliko, basi tuijengee heshima huko kuendana na ofisi na makazi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri sasa tusichukue muda mrefu wa utekelezaji wa ujenzi wa majengo yetu katika viwanja hivyo, kwa matumizi yetu na kupunguza ghamara za kupanga na wakati huo huo tutaingiza mapato, mfano

Ubalozi wa Muscat - Oman ni muhimu kwa sasa wapo vizuri kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naunga mkono hoja.

MHE. DKT. STEPHEN L. KIRUSWA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia kwa maandishi hoja iliyoko mezani ya Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuwapongeza Waziri na Naibu wake pamoja na watendaji wote wa Wizara hii kwa jinsi wanavyolitumikia Taifa letu kupitia kazi kubwa na nzuri wanayofanya katika Wizara hii.

Baada ya pongezi hizi, naomba kuchangia hoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia kuzuka kwa ugonjwa wa homa kali ya mapafu inayosababishwa na virusi vya Corona (Covid-19) duniani, biashara na shughuli za kujikimu kimaisha kwa wananchi wanaoishi karibu na mpaka kwenye baadhi ya nchi jirani hasusan nchi jirani ya Kenya kwenye eneo la mpaka la Kamwanga, Wilayani Longido kumetokea dhahama kubwa sana kwa wakulima wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina taarifa kuhusu adha ambayo wakulima wa vijiji vya mpakani na Kenya katika Kata ya Kamwanga wameanza kuipata wiki hii. Ni kufuatia Kenya kufunga mpaka na kuweka maaskari wake wa Jeshi mpakani kuwadhibiti Watanzania wasivuke mpaka kuendelea shughuli zao za kujikimu kimaisha kwani wako wengi wamekodisha mashamba upande wa Kenya ambao sasa hawaruhusiwi kwenda kupalilia wala kuvuna mazao yao juu ya ardhi ambayo walikwisha ilipia. Naomba Serikali itoe msaada wa kidiplomasia kuwasaidia wananchi hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia Kenya kuweka vikwazo kwa Watanzania kutoruhusiwa kuingia kufanya

biashara na kutoka ndani ya nchi yao kwa kizingizio kuwa sisi Watanzania ndio tunawaletea ugonjwa wa Corona, naomba Serikali iweke mitambo ya kupima na kutoa majibu ya haraka mipakani ili wananchi wetu waweze kuthibitishwa afya zao ili kuendelea na biashara zao nchi jirani na kwa kuwa upande wa pili wao wameweka mitambo ya upimaji Corona, na ili kuondoa iwezekano wa wananchi wetu kunyanyapaliwa kwa kusomewa majibu *fake*, hatuna budi na sisi kuweka mitambo yetu ili tuwe na *mechanisms* za kufanya *double check* badala ya kufungiana mipaka na kusababisha mporomoko wa uchumi kwa nchi zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa haya machache naunga mkono hoja.

MHE. LUCIA M. MLOWE: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia katika hoja hii kama ifuatavyo; kwa kuwa kuna Watanzania wengi nje basi naiomba Serikali ione ni namna gani inawatumia Watanzania hao kwa ajili ya kukuza uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa katika nchi yetu kuna wanawake wajasiriamali ambao wamekuwa wabunifu wa kutengeneza bidhaa mbalimbali kama vile ushonaji wa vikapu ambavyo vinapendwa sana na watu kutoka Ulaya. Naiomba Serikali iwahamasishe Mabalozi kutafuta masoko huko nje ili kuuza bidhaa hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa sera ya *diaspora* imechukua muda mrefu basi naiomba Serikali iweke bajeti ya kutosha ili kuweza kukamilisha sera hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. ZAINAB M. AMIRI: Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mungu kwa kunipa afya njema ili niweze kutoa mchango wangu katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni yangu naishauri Serikali fedha zinazoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya miradi

ya maendeleo zitolewe kwa wakati ili kuwekeza kutekeleza miradi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali mbali na kuwa na Chuo cha Diplomasia, Kurasini ipo haja kwa Serikali kujenga vyuo vingine katika mikoa yote au ikiwezekana vyuo vijengwe kwa kanda za nchi yetu ili kuweza kudahili wanafunzi wengi na hii itasaidia kupata wataalamu kwenye fani ya diplomasia.

Naishauri Serikali wakati wa uteuzi wa Mabalozi mbalimbali katika nchi za nje angalau izingatie uwiano wa jinsia. Pia naishauri Serikali kila mwaka itoe takwimu sahihi za Watanzania wanaoishi nje ya nchi kwa kila nchi husika. Naishauri Serikali iboreshwe ofisi za Mabalozi zote ziwe na hadhi maana nyngi ni chakavu. Pia naishauri Serikali kupitia Mabalozi wetu itafute wawekezaji, soko la bidhaa zetu tunazosalisha viwandani na mazao yetu tunayolima ili kuweza kuinua kipato cha Mtanzania na nchi kiumbla, pia hii itaweza kuitangaza nchi katika soko la kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naishauri Serikali iwaelimishe Mabalozi wetu umuhimu wa kuitangaza nchi yetu kwa kupitia lugha yetu ya Taifa ya Kiswahili ili iweze kutumika katika nchi wanazowakilisha.

MHE. ABDALLAH HAJI ALI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru Mwenyeizi Mungu muweza wa mambo yote. Pili, nakupongeza wewe binafsi kwa kutuongoza vizuri hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ya Mambo ya Nje na Ushrikiano wa Afrika Mashariki ni kiungo kati ya nchi yetu na mataifa ya nje. Tanzania tunazo ofisi nyngi za kibalozi takribani nchi nyngi za dunia kama ilivyo kwa nchi nyngi za dunia kuwa na Balozi zake hapa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo makuu ya Balozi zetu zilizoko nje na zile za wenzetu zilizopo hapa ni kuunganisha fikra za kidiplomasia kwa kufanikisha ustawi wa

dunia kuititia nyanja mbalimbali; mambo kama ya kiuchumi, afya biashara, elimu, utalii na mengi mengineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo sera madhubuti juu ya utekelezaji wa diplomasia hivyo naiomba Serikal kutilia mkazo zaidi juu ya utekelezaji wa sera ya mambo ya nchi za nje. Hii itatupeleka katika malengo tuliojipangia kuititia diplomasia.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunao Watanzania wengi wanaoishi mataifa mbalimbali duniani ukilinganisha na janga hili la Corona, ni vyema na naishauri Serikali kwa kutumia ofisi zetu za kibalozi duniani kote kuweza kujua ni raia wetu wangapi wameathirika na Corona, wangapi wamepona na vifo pia ni vingapi, kujua takwimu hizi kwa nchi pia nadhani ni jambo jema.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na malalamiko ya uhaba wa wafanyakazi katika ofisi zetu nyingi nchi mbalimbali duniani, ni jambo jema Serikali ikaongeza bajeti yake ili kukidhi matakwa ya ofisi zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kuna malalamiko juu ya baadhi ya majengo ya ofisi zetu za kibalozi sehemu mbalimbali hayako katika hali ya kuridhisha ni vyema Serikali ikalionia jambo hili pia kwa kuyafanyia matengenezo ili yawe katika hali nzuri. Ahsante.

MHE. ENG. RAMO M. MAKANI: Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi nyingi sana kwa Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. John P. J. Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wasaidizi wake kwa karibu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa kwa kuendelea kuonesha kuwa inawezekana kufanya mambo makubwa na mageuzi katika utekelezaji wa llani ya CCM.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakipongeza sana chama changu cha CCM kwanza kwa kuandaa llani kabambe, kushinda uchaguzi, kuunda Serikali kabambe na hatimaye kuwa na utekelezaji maharishi wa llani.

Hongera sana Mheshimiwa Waziri wa sekta hii, Mheshimiwa Profesa Palamagamba Kabudi na msaidizi wako Mheshimiwa Dkt. Ndumbaro kwa kuiongoza Wizara hii vema.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina jambo moja la kuchangia; hili ni kuhusu matumizi na umuhimu wa lugha katika kuleta maendeleo hususan katika nyanja za jumuiya za nchi mbalimbali. Utafiti unaonesha nguvu kubwa iliyomo ndani ya matumizi bora ya lugha. Nashauri Katiba/Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ufanyiwe marekebisho ili Kiswahili nacho kiwe lugha rasmi badala ya kubakia kuwa lugha tu ya mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, muhimu zaidi, muelekeo uwe katika matumizi ya lugha nydingi zaidi kwa kuwa imethibitika pia kuwa jumuiya zinazotumia lugha zaidi ya mbili, *UN, SADC, ECOWAS* na kaadhalika wanatumia lugha nydingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha.

MHE. JUMA OTHMAN HIJA: Mheshimiwa Naibu Spika, natoa shukurani zangu za dhati kwako kwa kinipatia fursa hii ya kuweza kutoa mchango wangu katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa kuweza kutayarisha hotuba hii na hatimaye kuiwakilisha katika Bunge lako tukufu kwa umakini kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuchangia hotuba hii napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo; kwanza umiliki wa majengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali yetu kwa juhudhi kubwa inazochukua katika kuimarisha ofisi zetu. Kama inavyojulikana kuwa Jamhuri ya Muungano ni muungano wa nchi zetu mbili, bado mpaka sasa upande wa pili wa Muungano haujaweza kumiiliki jengo lake kwa ajili ya ofisi yake. Aidha, jengo ambalo linatumika halina hadhi ya Kiwizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu katika jambo hili kwa Serikali ni kuendeleza juhudini za kuipatia upande wa pili wa Muungano ofisi ya kudumu yenye hadhi ya kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwapongeza kwa kazi nzuri, pamoja na mchango wangu wa kuongea, nashauri kwa maandishi suala la *posting* hasa katikati vituo ambavyo ni *multilateral* hasa New York ambako ni muhimu sana kuwa na maafisa katika Kamati ya kwanza na ya nne ambazo zinahusika na *peace keeping* na *operation* ya kulinda amani kwa sababu nchi yetu ni mshiriki mkubwa wa kulinda amani.

Pili kule Geneva ambako masuala ya haki za binadamu hujadiliwa ni muhimu tuingie tuwe Wajumbe wa Baraza la Haki za Binadamu ili kutetea maslahi ya nchi hasa wakati huu ambao tunapigwa sana vita kwa sababu ya hatua nzuri tunazopiga kiuchumi. Kwa hiyo, ushauri wangu vituo ambavyo ni *multilateral/tuvitazame* kwa macho mawili.

Kuhusu Kiswahili, nashauri Wizara iwe *the leader* kuhakikisha tunapata hata *scholarship* za masomo ya lugha ili tupate watu wengi watakaojua lugha kubwa sambamba na Kiswahili kwa nia ya kupata wakalimani na walimu wa lugha ya Kiswahili. Nafahamu ni suala la Wizara ya Elimu na *PM Office-Kazi na Ajira*, lakin *Foreign mnaweza ku-take lead*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. ZACHARIA PAULO ISSAAY: Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kuungana na viongozi wote wa ngazi mbalimbali katika Taifa letu kuendelea kuiombea nchi yetu ili tuweze kukua Kijamii, kiuchumi, kisiasa na kidiplomasia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kuwakumbusha Watanzania na viongozi wenzangu wote kuendelea kumwombwa sana Mwenyezi Mungu kutuepusha

na janga hili la Corona linalotikisa dunia nzima kwa sasa. Aidha, kama ilivyo desturi ya jamii yetu katika kuwaombea ndugu zetu waliotangulia mbele za haki Mwenyezi Mungu awapokee katika ufalme wake usiona mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mkutano huu wa Bunge la Bajeti ya mwaka wa mwisho wa ukomo wa miaka mitano, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mbulu Mjini na kwa moyo wangu wa dhati nachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Job Yustino Ndugai - Spika wetu na watendaji wote Serikalini kwa jinsi walivyosimamia utekelezaji wa Ilani ya CCM ya mwaka 2015-2020 kote na hususan Jimbo la Mbulu Mjini kwa ajili miradi mbalimbali ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nitoe mchango wangu wa kuishauri Serikali kuitia hotuba na taarifa ya Wizara hii kama ifuatavyo; kwanza Serikali yetu ione umuhimu wa kuharakisha mchakato wa sera yetu ya mambo ya nje ili kuweza kutumika kwa manufaa ya Taifa letu na kuchochea maendeleo.

Pili, kwa kuwa Watanzania waishio ughaibuni ni wengi na bado nchi yetu inahitaji mchango wa hali na mali kutoka kwao, Serikali iangalie utaratibu mzuri wa kuhuisha takwimu ya *diaspora* ili waweze kuchangia maendeleo ya nchi yetu katika nyanja mbalimbali na kuhamasisha uthalii na fursa mbalimbali.

Tatu, kutokana na upungufu na ukosefu wa miundombinu ya majengo, katika Balozi zetu hali inayofanya Serikali kupata gharama kubwa ya kodi za majengo ya ofisi na makazi ya Balozi na watumishi wa Balozi zetu nchi nje. Hivyo basi kwa zile nchi ambazo Serikali yetu tayari ina viwaja vyta kujenga majengo hayo, Serikali itafute mkopo wa masharti nafuu kujenga majengo hayo kulingana na

vipaumbele. Pia Serikali kuptitia bajeti zetu ichambue baadhi ya miradi ambayo tunaweza kujenga kwa awamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naunga hoja asilimia 100 na naomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro, mtoya hoja ajiandae.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchukua fursa hii awali ya yote nimshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kuweza kumsaidia Mheshimiwa Prof. Kabudi katika Wizara hii kwa kipindi chote ambacho nimehudumu. Pia nimshukuru sana Mheshimiwa Prof. Kabudi kwa uongozi wake shupavu ndani ya Wizara ambao umesabisha Wizara hil kupata mafanikio makubwa sana kama ambavyo tumeeleza katika bajeti. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ni mpongeze Prof. Kabudi mwalimu wangu kwa kazi kubwa ambayo anaifanya kwa Taifa hili la Tanzania. Sote tunafahamu ameshughulikia mambo magumu ambayo yalishindikana kwa muda mrefu lakini kwa kipindi kifupi kwa uhodari na ushujaa wake mambo hayo yameweza kukamilika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa kifupi niweze kutoa maelezo au ufanuzi kwa baadhi ya hoja ambazo Waheshimiwa Wabunge wamezieleza. Nawashukuru Wabunge wote 17 ambao wametoa hoja na wale ambao wametoa hoja zao kwa njia ya maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya kwanza ambayo nitaenda kuitolea ufanuzi ni suala la Polisario ambalo liliulizwa na Mheshimiwa Bulembo au kwa wengine wanaita Sahrawi. Sisi Tanzania katika misingi yetu ya Sera ya Mambo ya Nje kama ambavyo tumeeleza kwenye kitabu cha hotuba ni kwamba hatufungamani na upande wowote na siku zote tunafanya kila tunaloliweza kuhakikisha kwamba

tunadumisha mahusiano ya kindugu na kirafiki na nchi hizo zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa na uhusiano na Sahara ya Magharibi kwa muda mrefu na tumekuwa tukiunga mkono juhudzi zao kwa muda mrefu, msimamo huo bado haujabadilika na hautabadilika pamoja na kwamba tumekuwa sasa na mahusiano na Morocco pia. Na hii inatokana kwamba Umoja wa Mataifa pamoja na *AU* wametoa maelekezo au maazimio kwa jinsi gani mgogoro wa Sahrawi pamoja na Morocco uweze kumalizwa. Maelekezo hayo ni kwamba nchi hizi mbili zikae mezani zижадилие chini ya uongozi wa *AU* lakini chini ya wasuluhishi mbalimbali. Sisi Tanzania kama nchi kazi yetu ni kutekeleza na kusimamia hayo pasipo chembe ya ubaguzi kwa mtu ye yeyote. Kwa hiyo, tutaendelea kuwa na mahusiano ya kidiplomasia na Sahrawi na Morocco. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wengi wameongelea kuhusiana na miradi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Miradi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki imejikita kwenye maeneo yafuatayo;

Moja, ujenzi wa barabara;

Pili, ujenzi wa reli;

Tatu, ujenzi wa viwanja vyta ndege; na

Nne, ujenzi wa mabwawa ya kuzalisha nishati ya umeme. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi hii inajadiliwa kwa pamoja na nchi za Afrika Mashariki na lazima ihushe nchi zaidi ya moja, ikishajadiliwa na kuchakatwa, wajibu wa kuigharamia ujenzi au utekelezaji wa miradi hiyo unarudi kuwa kwa nchi husika. Kwa upande wa Zanzibar miradi hii ikishachakatwa na ikishakaa vizuri inakabidhiwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ili iweze kuitekeleza na kama kuna mkwamo wowote basi sisi tutaendelea kushirikiana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme wazi Jumuiya ya Afrika Mashariki imekuwa na faida kubwa sana kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pasipo ubaguzi wa aina yoyote. Taasisi ya Kiswahili (*Kiswahili Commission*) ambayo ni taasisi chini ya Jumuiya ya Afrika Mashariki makao yake makuu yapo Zanzibar. Na hata katika Wabunge ambao wanawakilisha Tanzania katika Jumuiya ya Afrika Mashariki mgawanyo ni tatu kwa sita; sita wanatoka Tanzania Bara na watatu wanatoka Tanzania Zanzibar. Kwa hiyo, katika utekelezaji huo mambo yanakenda vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Iakini niwahakikishie tu Watanzania wote, Wazanzibar na Watanzania Bara kwamba utekelezaji wa miradi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki unakwenda vizuri na una mafanikio makubwa na Tanzania tumenufaika kwa zaidi ya asilimia 53 kutoka kwenye miradi yote ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia limeongelewa suala la Sera ya Mambo ya Nje. Wizara imekuwa ikiandaa Sera ya Mambo ya Nje kwa muda mrefu, Sera hiyo sasa andiko la kwanza lipo tayari na muda wowote sasa tutaita wadau mbalimbali kuliangalia na kutoa maoni yao ili tuweze kupata andiko la mwisho na Sera hii iweze kukamilika. Na katika Sera hiyo, masuala ya *diaspora* nayo itakuwa ni sehemu katika Sera hiyo na yatajadiliwa vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, niweze kukupa taarifa kwamba katika utekelezaji wa Sera ya *Diaspora*, Wizara imejitahidi sana; hapo awali *database* yetu ilikuwa na watu 100,000 tu ambao tumeweza kuwasajili, hivi leo nasimama mbele yako nikisema kwamba idadi hiyo imeongezeka kutoka 100,000 mpaka watu 1,300,000. Kwa hiyo, tumesajili *diaspora* 1,300,000 ndani ya kipindi cha mwaka mmoja. Na juhudhi hizo zitaendelea na tutavyoweza kuwasajili ndipo tutakapoju mahitaji yao, sifa zao za kitaaluma na tuweze kuwashughulikia vipi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho; imeongelewa ujenzi na ukarabati wa Balozi zetu. Katika hotuba ambayo

Mheshimiwa Waziri ameisoma ukurasa wa 182 tumeelezea Balozi 11 ambazo zitafanyiwa ukarabati ndani ya mwaka huu mmoja wa fedha na tayari kuna bajeti ya shilingi bilioni 20 ambayo pia ni ongezeko la asilimia 400 kutoka bajeti ya mwaka jana. Haya yote tumeyafanya ili kuhakikisha kwamba maelekezo ya kamati na Bunge hili Tukufu yanatekelezwa katika kukarabati hizo Balozi, kujenga pale ambapo inahitaji kujenga ili kuhakikisha kwamba viwanja vyetu 12 haviwezi kupotea. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Salma kwa kuweka msisitizo kwenye suala la Kiswahili; sisi kama Wizara tumeweka msisitizo mkubwa sana. Tunajua Kiswahili ni lugha muhimu sana, lugha ya tatu kuzungumzwa Barani Afrika na lugha ya kumi kuzungumzwa duniani na watu zaidi ya milioni 200 wanazungumza Kiswahili. Ndiyo maana tulihakikisha kwamba kinaenda kuongelewa SADC lakini pia kinaweza kuongelewa Maziwa Makuu. Kwa hivi sasa tuna kazi moja tu ya kukiipeleka Kiswahili katika Umoja wa Mataifa na hiyo hatutashindwa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa nitumie fursa hii kwa namna ya kipekee na kwa unyenyekevu wa hali ya juu kuwashukuru wananchi wa Songea Mjini ambao walinipa dhamana ya kuingia katika Bunge hili. Nitaendelea kuwatumikia kwa juhudhi zangu zote, nawaambia nipo nao na mwaka huu 2020 kitaeleweka. Ahsante. (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri Dkt. Damas Ndumbaro, Mbunge wa Songea Mjini. Mheshimiwa Prof. Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, karibu sana uhitimishe hoja yako. (*Makof!*)

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tena nitumie fursa hii kwa unyenyekevu mkubwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Rahim kwa kuniwezesha kuwasilisha hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Mambo

ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa maoni na ushauri wao ambao wameutoa kuhusu mapato na matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge mbalimbali waliota hoja zao kwa Wizara yetu. Nawashukuru Wabunge wote waliochangia kwa kuongea na wale waliochangia kwa maandishi na kuichambua bajeti yetu kwa kina. Jumla ya Wabunge 18 wamechangia kwa kuongea na Wabunge 11 wamechangia kwa maandishi, jumla ni Wabunge 30.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya maswali na maoni yaliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge tutayajibu kwa maandishi. napenda nikuhakikishie wewe binafsi na Waheshimiwa Wabunge kuwa michango yenu ya leo imekuwa ya tija na manufaa makubwa sana kwetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kifupi, kabla sijaanza kujibu baadhi ya hoja, nitumie nafasi hii tena kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa imani yake kwangu kwanza kwa kunateua kuwa Mbunge tarehe 16 Januari, 2017 saa 10:16 jioni nilipokuwa nafundisha wanafunzi wa mwaka wa pili kule Yombo. Namshukuru sana, tarehe 23 Machi, 2017 kunateua kuwa Waziri wa Katiba na Sheria, nafasi ambayo nililhudumu kwa mwaka mmoja na miezi 11 na baadaye tarehe 3 Machi, 2019 kunateua kuwa Waziri wa Mambo Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami niseme kama alivyosema Hanna katika sala yake maalum katika Agano la Kale na katika ile Zaburi ya shukrani: " *Ee Mungu ni wa ajabu, maana huwatoa wale walio mavumbini na kuwaketisha katika viti vya wafalme.*" Namshukuru pia kwa kuniamini na

kunipa majukumu mengine nje ya Wizara hizo ambayo yamenipa nafasi ya kuitumikia nchi yangu adhimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii pia kuwashukuru Mheshimiwa Dkt. Damas Daniel Ndumbaro, Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Kanali Wilbert Augustine Buge - Katibu Mkuu, Balozi Muomba Mwinyi - Naibu Katibu Mkuu; Mabalozi wa Tanzania nje ya nchi, Wakuu wa Idara na Vitengo, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara na watumishi wengine wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, napenda kumshukuru sana mke wangu mpenzi Dkt. Amina na familia yangu kwa ujumla kwa uvumiliwao na kuwa karibu nami wakati wote wa kutekeleza majukumu yangu niliyopewa na Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Nawashukuru watoto wangu, sasa wamekuwa na ngozi ngumu ya kuvumilia mengi yanayosemwa kwa kudhalilishwa wakati mwingine. Pia namshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Harrison George Mwakyembe, Mshenga wangu kwa Dkt. Amina kuwa nami kwa muda wote. (*Makofi/Kicheko/Vigelegele*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nawe wajua Dkt. Amina anatoka huko kwenu na amekuwa mtu muhimu sana kwangu. Mheshimiwa Dkt. Harrison George Mwakyembe, hukunipeleka kubaya, umenipeleka kuzuri sana, ahsante. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nianze na hoja zilitotolewa na nydingine tutazijibu kwa maandishi. Nataka niwaambie, Zambia hajafunga mpaka na Tanzania. Narudia tena, Zambia hajafunga mpaka na Tanzania; na haya siyo maneno yangu, ninayo barua kutoka kwa Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje wa Zambia, rafiki yangu mkubwa sana, Joseph Malanji, ambaye Mungu amemjaalia kujua lugha nydingi na hapa Tanzania anazungumza Kinyakyusa, anazungumza Kinyiha, anazungumza Kinyamwanga na jana na leo tumezungumza kwa Kiswahili. Nimemwomba nisome barua yake, jambo ambalo siyo la kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, ameniandikia barua ambayo imefika leo baada ya mazungumzo ya siku mbili na ananiambia:-

Your Excellence and Dear Brother,

I have the honor to refer to the excellent bilateral relations between our two countries and recall the strong historical and cultural tides that bind our two nations in business. It is with regret that I wish to inform you that the government of Republic of Zambia decided to temporarily impose restrictions on boarder movement of goods and services across the Nakonde - Tunduma boarder for an initial period of five days. I must point out at the out state that this decision was arrived on at enhanced due to the unusually high number of Covid-19 cases that were recorded at the border town. The imposition restriction is inter alia intended to facilitate for mass screening, contact tracing and to ensure that various intervention measures are implemented to avoid further spread of the virus from Nakonde to other parts of Zambia.

Honorable Minister, Zambia remains committed to implement the SADC guidelines on the harmonization and facilitation of cross border transport operation across the region during the Covid-19 pandemic and the specific provisions for the observance of national regulations and bilateral arrangements. It is for this reason that the government of the Republic of Zambia is desirous to engage with the government of the National Republic of Tanzania at all levels in a joint efforts towards mitigation against the further spread of the pandemic. To this effect the multilateral sectorial technical team from Zambia is ready to meet your team at the earliest possible time convenient yourself to harmonize and implement joint efforts. (Applause)

This is the message from my colleague, The Foreign Minister of Zambia and I would want to acknowledge this letter and thank him for assisting me to show this Parliament

and the world that this is the position of Zambia and this is the letter from Zambia of which all of us should know. (Applause)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hii ndiyo barua kutoka Zambia, imeeleza wazi kabisa, Zambia haijafunga mpaka, ilichukua hatua kwa siku tano kusimamisha ile hali ili kukabiliana na hali na wamerudia kutueleza kwamba Kamati ya pamoja ya Tanzania na Zambia zitakutana ili sasa kuweka mambo sawa huduma zirejee. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka hilo niliseme; na ndiyo maana nimesema siyo kawaida kusoma barua hizi, lakini nimemwomba mwenzangu nisome ili wale wasiotutakia mema waelewe. Nami niseme kwa Kiingereza, *during this time will have to learn to suffer many fools.* (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Rwanda; nilikuwa nasoma Kitabu cha Douglas Hurd aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Nje ya Uingereza amesema "*Choosing Your Weapon.*" Nikakumbuka masomo niliyoyasoma Misri Oktoba, mwaka 1984 wakati najifunza mambo ya Diplomasia; kuna wakati wa kusema na kuna wakati wa kutokusema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi na Rwanda tumekuwa na majadiliano yanayoendelea kuhusu *Central Corridor.* Tarehe 7 na 8 Mei, mwaka huu 2020 Kikao cha Wataalamu kilikaa kuona ni jinsi gani bidhaa na huduma ziendelee kati ya sisi na Rwanda. Tarehe 11 Mei Kikao cha Mawaziri kilikaa kwa njia ya mtandao na kuna mambo hayo mliyoyazungumza yote ya dola 500, hayo yalikuwa ni mapendekezo, hayajakubaliwa. Sasa tutakuwa na *round* nyingine ya mazungumzo Ijumaa *Inshaallah* Mungu akipenda, kwa sababu baada ya majadiliano kuna hoja tulizozitoa na wenyewe wakaomba waende nazo Rwanda. Sasa Ijumaa Mungu akipenda tutakaa tena na kuona Waziri Kamwelwe atakuwepo, Waziri Bashungwa atakuwepo, Waziri Ummy atakuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu tunaendelea kuongea na Rwanda, ndiyo maana jana kwa walioona,

Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Mheshimiwa Eng. Kamwelwe alikwenda kuzindua safari ya ndege ya *RwandAir* ambayo inachukua minofu ya samaki kutoka Mwanza na jana ilichukua tani nane kuzipeleka *Brussels* na *Amsterdam*. Sasa kama mahusiano yetu ni mabaya, kwanza Rwanda wangekubali? Ndege yao ingekuja kuchukua mizigo hiyo! Kabla ya *RwandAir* kuchukua mizigo yetu ya samaki kutoka Mwanza kwenda Ulaya, mizigo hiyo iliwa inasafirishwa na magari mpaka Nairobi na Entebbe. Ndugu zangu, watazoza sana. (*Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme Mkutano wa Nchi Nne uliofanyika ni Mkutano wa *Northern Corridor*, ni Mkutano wa *corridor* ya Kaskazini na walituarifu na tulijua kwa nini walituarifu. Ndugu zangu, kumbukeni huko nyuma hawakufanya hivyo, walianza kutubagua. Ndiyo maana mwaka 2013 Mheshimiwa Rais Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete alichukua hatua isiyokuwa ya kawaida kuja kulihutubia Bunge hili kueleza masikitiko ya Tanzania ya wenzetu katika *Northern Corridor* kuanza kufanya mambo peke yao, kukutana peke yao na kufanya shughuli zao peke yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu wakati huo *Northern Corridor* wakikutana wanatuarifu, lakini kwa nini tuhudhurie Mkutano wa *Northern Corridor*? Ni wa kwao, ule haukuwa Mkutano wa *EAC*. Sitaki kurudia aliyojasema Mheshimiwa Kikwete hapa mwaka 2012, hayo yamepita. Tusiruhusu maadui zetu kutaka kuitingisha Jumuuya ya Afrika Mashariki, wana yao, nasi tusiwe sehemu ya hayo. Ndwele siyo sifa, lakini Tanzania haijawahi kuacha kusimamia maslahi yake. Pamoja na udogo wa nchi hii, kiuchumi nchi hii imefanya mambo makubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka niwahakikishie, Mkutano ule wa zile nchi nne ulikuwa ni *consultative meeting* ya *Northern Corridor*, lakini sisi na Rwanda tumekuwa na *Bilateral Consultative Meeting* ya *Central Corridor*, ndiyo maana sisi na Burundi hatukwenda, kwa sababu Burudi ni *Central Corridor*. Ingekuwa umefanyawa Mkutano kuhusu *Central Corridor*, kwanza utafanyikaje bila

sisi kualikwa? Kwa hiyo, nilitaka hilo lieleweke na watu wasipuuze. Tumshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Jakaya Kikwete mwaka 2013 alipolisemea hilo na hali imebadilika. Nami *Foreign Minister* wa Rwanda aliniarifu kwamba patakuwa na Mkutano; ni wa kwao, umeendelea. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mkutano wa Rais Ramafosa. Rais Ramafosa hakuita Mkutano wa *SADC*. Mikutano ya *SADC* inaitishwa na Katibu Mkuu wa *SADC* kwa kushauriana na Mwenyekiti. Hiyo ndiyo Mikutano ya *SADC*. Mkutano ule ulikuwa ni Mkutano wa *SACU* wa majirani wa Afrika ya Kusini, wengi wao wakiwa ndani ya *SACU*, ukiondoa Zimbabwe (ingawa inapakana na Afrika ya Kusini), Msumbiji na Angola. Ndiyo maana nchi nane hazikuhuduria. Tanzania haikushiriki, Zambia haikushiriki, Malawi haikushiriki, Madagascar haikushiriki, Mauritius haikushiriki, Comoro haikushiriki na *DRC* haikushiriki; na *quorum* ya vikao vya *SADC* ni watu 11.

Mheshimiwa Naibu Spika, mliyemsikiliza Ramafosa, alisema kwamba Mkutano wa *SADC* haukuitishwa kwa sababu ya *logistics*. Ndiyo, kwa sababu anayeitisha Vikao vya *SADC* kwa mujibu wa *Treatyni Katibu Mtendaji wa SADC* na ambaye kwa sasa ni Dkt. Stegomena Lawrence Tax. Nchi zote hizo tuna mahusiano mazuri, siyo vizuri kusema. Mheshimiwa Rais amekuwa na mahusiano na nchi zote hizo kwa nyakati mbalimbali na hajashindwa kufanya majukumu yake; na mengine amenipa heshima ya kimya kimya kwenda na kurudi na kufanya mambo. Kwa sababu mambo ya diplomasia siyo yote mnayoyafanya hadharani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nisingependa kusema, lakini napenda niseme Mheshimiwa Rais, Dkt. Magufuli alinituma *Brussels* mara mbili nikiwa Waziri wa Katiba na Sheria kwenda kuweka hali sawa na Umoja wa Ulaya, *twice!* Amenituma, *special envoy Kenya* kwa Kenyatta. Nilipofika sikutegemea Kenyatta angenipa heshima ya kulihutubia Taifa la Kenya. Amenituma kama *special envoy* kwenda Marekani kupeleka barua kwa Trump. Nataka niwaambie leo, baada ya Rais Trump kupokea barua ya Rais, Mheshimiwa Dkt. Magufuli

ameamua kuiongezea Tanzania Mkataba wa AGOA kwa mwaka 2020 bila masharti yoyote; lakini katika diplomasia husemi kila kitu hadharani. Nimelazimika kuyasema haya ili tu watu wajue kazi inafanyika na kazi inasonga mbele. Hiki siyo kipindi cha kunyoosheana vidole. (*Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la *Covid*, nalo pia niseme, sikutaka kusema. Wiki hii nimekuwa na Mkutano wa *Video Conference* na Mabalozi wa nchi za *Nordic*, Balozi wa Sweden, Balozi wa Norway, Balozi wa Denmark na Balozi wa Finland. Katika mazungumzo hayo, Finland imeamua kutuongezea dola milioni 20 kwa Bajeti ya Elimu. Sweden imeamua kutupa dola milioni 10 kwenda *TASAF* kusaidia watu wenye kipato cha chini wakati wa *Covid*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hatuwezi kuwa kila siku tunayasema hayo, lakini nimelazimika kuyasema. Unajua uwazi una mipaka. Mtu ambaye hana mipaka, huyo siyo binadamu. Hata wanyama wanaoishi na binadamu kama paka na mbwa wana mipaka, wana usiri. Nani amewahi kumwona paka anajisaidia? Kila jambo lina mipaka yake, lina staha yake. Hata akizidiwa atajificha, atakwenda chini ya meza. Sasa huyo ni paka: Je, binadamu (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, yapo mambo ambayo siyo vizuri yakasemwa hadharani yote, lakini nimetoa mifano hii michache ili watu tuelewe mambo yanavyokwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu zangu, moja nalo pia niliseme, tunamshukuru sana Rais wa Madagascar, Andry Rajoelina na Waziri wa Mambo ya Nje. Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje wa Madagascar tunafahamiana, alikuwa Prof. Geneva wa *International Law*. Alinipigia simu mapema kabisa kwamba tuna shughuli tunafanya. Taasisi yetu hii tuliyonayo, mionganoni mwa watu waliochangia ni Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. (*Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baadaye akaniandikia barua kwamba Rais wangu amenitura umwambie Rais

wako tuna hii dawa ya mitidawa, tumeitengeneza kwa lengo la kusaidia kutoa *the African solution to a global problem*, njoo ni mchukue muione. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, nilimwarifu; Mheshimiwa Rais nimepewa *donation* hii, wanataka tukaichukue. Akasema, basi sawa. Naye akampigia Rais wa Madagascar, wakawa na maongezi ya simu muda mrefu siku ya Jumatano. Usiku huo akaniambia bwana Ijumaa Madagascar kachukue ule mzigo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi kweli Mheshimiwa Ally Saleh, mwanafunzi wangu mpPENDWA, Waziri mwenzako amekuandikia barua ya salamu za Rais wake, njoo uchukue mzigo, wewe umwambie hilo ni jambo dogo sana, mimi ni Waziri. Sijawahi kuwa ni kiburi hicho na sitakuwa nacho. Ndiyo maana nilikwenda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Rais, aliniambia, usiende peke yako, nenda na wataalam. Nilikwenda na wataalam wafuataao: Mganga Mkuu wa Serikali (*Chief Medical Officer*) - Prof. Abel Makubi; *MD Dar es Salaam, Master of Science Medicine Norway, Ph.D Medicine Sweden, MPH Harvard*. Nikaenda na mwanafunzi wangu mwingine Prof. Yunus Daudi Mgaya - Mkurugenzi Mkuu wa *NIMR*. Tukaenda na Dkt. Fidelis Mafumiko - Mkemia Mkuu wa Serikali, ambaye yeye mwenyewe katika *Masters* yake Chuo Kikuu cha Dar es Salaam aliweza kutoa kidonge cha kutibu Malaria kutoka kwenye mitishamba. Tukaenda na Dkt. Paul Muhamed ambaye mwaka 2003 alifanya kazi katika taasisi hiyo ya Madagascar ambao ndio wametengeneza hii dawa ambayo tumepeewa. Tumepewa dawa ya aina mbili; moja ya kutibu na nyingine ya kukinga, zipo maabara zinafanyiwa utafiti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme, tulijua wabaya wetu wanatusubiri hapo. Tumefuata *WHO Regulations*, dawa zinafanyiwa uchunguzi. Mimi nilipata heshima ya kuonja kwa sababu mwenzangu aliniambia tuonje. Ndiyo maana kama mliona, tulionja kama Wahehe. Yeye aliweka, nami niliweka; nami kidiplomasia, nikagonga! (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana ile *cartoon* ambayo naonekana nimeshuka kwenye ndege nagonga, wenzangu wote na maboksi, nimeitengeneza kubwa ili niitundike ukutani. Kwa hiyo, namshukuru Mungu nimegonga; na nimegonga ya kinga. Nyote kama mnavyofahamu, niliambiwa mimi nimerudi kutoka Ufaransa na nina kikohozzi cha kama mtu aliyevuta ugoro. Kwa hiyo, maradhi haya yamenipata. Maradhi haya hatupendi, walioyapata tuwaombee Mwenyezi Mungu awape afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema sisi watu wa imani, jambo lolote linalotokea wakati wa Ijumaa Kuu na Pasaka na Mfungo wa Ramadhani, mwisho wake huwa Mungu anafanya miujiza. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wasio amini wasiamini wanao amini jambo lolote Ijumaa Kuu, Pasaka halafu inaunganika na Ramadhani subirini miujiza ya Mungu. Hata hivyo, nchi hii Mheshimiwa Rais na sisi wote tumechukua tahadhari zote. Mimi tu nimevua hii barakoa ili kidogo nisikie, lakini barokoa mnaziona. Nawapongeza Watanzania kwa ubunifu mkubwa. Tumekuwa na barokoa za kila aina za kanga, za vitenge, nini zaidi?

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wana nawa na mimi niseme kama mzaha tu nilikwenda Kanisa Kuu hapa na hapa mji wetu wa Dodoma na eneo letu hili sisi tumeishi kwa amani sana sasa mmoja akasema bwana unajua wote sasa wote tumekuwa waislamu nikamwambia vipi wenzetu ndio walikuwa wakienda kwenye ibada wanawana sasa sisi wote lazima tunawe na mimi naona utaratibu huo mzuri kama watanzania wote sasa wakristo na waislamu wanawana kabla ya kuingia kwenye nyumba ibada. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kila jambo linakuwa na jambo lake nami naamini baada ya hii Corona tutakuwa tumejenga utamaduni wa kuzoea kufanya nini kunawa. Sasa suala la Mheshimiwa Rais kuzungumzia kwamba nyumba za ibada zibaki wazi, nataka niwaambie Tanzania *is a secular state*, Tanzania haina dini hivyo kweli mnategeme Rais wa

nchi atoe amri yakufunga nyumba za Ibada? Sisi si *ni secular state*? Lakini wote tunafahamu, kuna Maaskofu wameamua kufunga makanisa, kwani Serikali imekwenda kuwaambia fungueni? Si wamefunga mamkanisa sitaki kusema. Kuna walifunga misikiti nani amewalazimisha wafungue? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ni muhali na Rais Magufuli angesema afunge misikiti na makanisa hao hao wanaosema leo wanasesma si unaona amemaliza huku sasa amehamia na huko. Suala la dini ni la imani.

Mheshimiwa Naibu Spika, na wenzetu mimi si semi bila waga makanisa huna haja ya kufunga yalishajifunga yamekuwa *museum*. Sasa huko tusiende maana niko *foreign minister* nisikosee zaidi. Lakini kila watu wanafanya wanayoyafanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimalize kwa kusema, niseme tunatekeleza Diplomasia na kama alivyosema *Diplomat is an art* na *art* hiyo inategemea mazingira. Kwa hiyo maoni mengine yote tumeyapokea na nina ahidi tutauajibu kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, unajua nimechanganyikiwa na mambo mengi sana mpaka nashindwa kujua.

Mheshimiwa Naibu Spika sasa naomba sasa kwa heshima kubwa Bunge lako Tukufu ndiyo hii au aaa! Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashiriki fungu 34 kwa Mwaka wa fedha 2020/202. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Naomba kutoa hoja. (*Makof*)

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANA NA MICHEZO:
Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana hoja imeungwa mkono, ahsanteni sana; hapo sitii neno nitatia neno baadaye.

HOJA ZA KISERA

NAIBU SPIKA: Lakini Waheshimiwa Wabunge kuna Waheshimiwa Wabunge wawili wameomba ufanuzi hapa kwa Mheshimiwa Waziri kwenye mambo ya jumla na mambo mahsus ya kisera. Tutaanza na Mheshimiwa Ally Saleh kutokea Msekwa anahitaji ufanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri. (*Makof*)

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, Nilichokuwa nataka kuuliza mimi ni kuhusiana na sera ya mambo ya nje ambayo kusema kweli imekuwa ya muda mrefu inahitaji na marekebisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna vitu vingi vimetokea hapa katikati, dunia imebadilika sana na mahitaji ya Tanzania yamekuwa mengine. Vilevile pia katika mjadala wa leo umejitokeza suala la *diaspora* namna ambavyo *diaspora* inavyoweza kuchangia mara kumi zaidi kuliko inavyochangia hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nataka kuuliza nipate ufanuzi kwa sababu imekuwa muda mrefu suala Sera ya Mambo ya Nje namna ambavyo tunahusiana na watu wengine. Lakini kama alivyosema Mheshimiwa Waziri ni *refraction* yetu sisi ndani ndio maana ya Sera ya Mambo ya Nje. Kwa nini Sera hii imechelewa au kwa maana nyingine ni lini sera hii itakuwa imekamilika ili Tanzania iweze ku-*benefic* na mahusiano yake ya nje kuliko ambavyo sasa hivi tunavyo-*benefic* na mahusiano yetu na nje na tunavyohusiana na watu wengine. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano Wa Afrika Mashariki.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano Wa Afrika Mashariki ningepeda kutoa ufanuzi wa swali la Mheshimiwa Ally Saleh Ally (Albeto) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeongelea Sera ya Mambo ya Nchi za Nje. Unapotengeneza Sera ya Mambo ya Nje una jukumu kubwa sana ya kuifanyia tathimini dunia nzima nchi zote duniani, fanya tathimini ya Mashirika yote ya Kimataifa ambayo mna mahusiano nayo, ndipo ufanye ulinganifu sasa kwa hapa ndani. Kwamba mahitaji yetu ni nini kwenye nchi hizo na kwenye jumuiya hizo, sio kitu rahisi. Kwa hiyo uchelewaji wa sera hii unatokana mchakato huo mrefu amba unahitajika kufanyika; lakini kama nilivyosema katika majibu ambayo niliyasema sera hii sasa utekelezaji wake au utungaji wake umefikia hatua nzuri sana, *first draft* ipo tayari. Tunachohitaji sasa sera hii ipelekwe kwenye Balozi zetu zote 43 ili mabalozi wetu wakaae na *diaspora* amba tumesema tumeshawasajili tayari, milioni moja na laki tatu, tupate maoni yao ya rudi hapa na hapa sasa ndio tuanze mchakato wa wadai wa ndani likiwemo Bunge lako Tukufu. Sasa nimwamble Mheshimiwa Ally Saleh tuombe Mungu katika Bunge lijalo aweze kurejea ili tuweze kujadili sasa kwanza *draft* ambayo tunayo na maoni ambayo tumeyapata kutoka kwa *diaspora* ili tutoe sera ambayo itaangalia maslahi yote ambayo yamesemwa bayana.

Mheshimiwa Naibu Spika, na katika mambo ya msingi mapya ambayo lazima tuyasingize, moja ni suala *diaspora* lakini pili lazima tuweke msisitizo si suala jipya, msisitizo katika diplomasia ya uchumi, lakini tatu tuweze kuangalia diplomasia ya sasa inasemaje. Diplomasia ya sasa inakwenda zaidi kwenye *artificial intelligent*, kwa hiyo mambo hayo nayo yaweze kuinga kwenye sera hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Wilfred Lwakatare ufanuzi.

MHE. WILFRED M. LWAKATARE: Mheshimiwa naibu Spika, ahsante, na nimponeze Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa kutoa ufanuzi mzuri kwenye bajeti yao, lakini kufatia hoja nilizozzungumza wakati wa mchango wangu, nilizungumzia kuhusu kauli tatanishi zinazopelekea wenzetu

wasituelewa huko nje, au Mabalozi wetu kukosa majibu. Itakumbukwa kwamba Mheshimiwa Rais aliwaandalia hafla mabalozi kwa ajili ya mwaka mpya, na miongoni kwa kauli aliyoitao mbele ya Mabalozi ni kwamba mwaka huu ni mwaka wa uchaguzi na anawahidi kwamba uchaguli huu utakuwa ni uhuru na haki.

Sasa utata unakuja, kwamba uchaguzi ni maandalizi, hapa tupo mwezi wa tano, mwezi wa kumi ndio uchaguzi. Hata hivyo ukiangalia ahadi ya Mheshimiwa Rais *versus* mambo yanayotekelzeza naona kama mambo yako *silent*. Sasa labda sijui hata suala hili Mheshimiwa Waziri anataka kutuambia nalo wanaliandalia chumbani huko? Kama alivyosema? Kwamba kuna mambo wanafanya kimya kimya? Sasa kama ni hilo mimi nafikiri kuna haja ya ku – *reflect* pia, kwamba suala hili si la kwenda huko kufanya chumbani, lina wadau wanaohusika kama vyama vyaya siasa kushirikishwa. Kuna mambo ya mapema ya kufahamishwa kwamba yakoje, ratiba, *schedule* ikoje sasa Mheshimiwa Waziri ningeomba maelezo kuondoa utata huu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri, Kiti kinakulinda, kama unataka kujibu unaweza kupewa fursa lakini hilo jambo ilishaelezwa chini ya Wizara inayohusika. Wakati tunajadili Bajeti ya Waziri Mkuu ilishaelezwa kwa ufanuzi mkubwa sana. Lakini sasa naona umesimama unalindwa na Kiti kama uko sawa basi nadhani hilo limekaa vizuri.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kusema hilo hilo tu kwamba, ndugu yangu anauliza swali ambalo halianguki kwangu lakini namshauri aandike *memoirsya* haya aliyoyazungumza alipokuwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani. Ni mazuri sana awaandikie watu wajue. Hata mimi sikuwa kujua kwamba uliwahi kuwa Mkuu wa Kambi ya Upinzani na ulifanya vizuri zaidi kuliko. (*Makofi/Kicheko*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Waheshimiwa Wabunge kwa utaratibu wetu Waziri alishatoa hoja hapa na ilishaungwa mkono. Sasa kwa mabadiliko ambayo tumeyafanya

naangalia kura hapa zilizopigwa, Wabunge wengi ambao wengine wapo Msekwa, wengine wapo humu ndani na wengine wapo kwenye vyumba vingine. Ambavyo vinatumika kwa ajili ya Bunge kipindi hiki wamepiga kura. Idadi kubwa kabisa ya Wabunge, na Wabunge wengi katika ya hao waliopiga kura wamesema ndiyo. (*Makofii*)

*(Hoja ilitolwa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2020/2021 – Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki iliridhiwa na Bunge kama ifuatavyo:-

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 34 – Wizara ya Mambo ya Nje na
Ushirikiano wa Afrika Mashariki Sh.....179,750,684,000

MIPANGO YA MAENDELEO

Fungu 34 – Wizara ya Mambo ya Nje na
Ushirikiano wa Afrika Mashariki.....Sh. 20,000,000,000

NAIBU SPIKA: Kwa hiyo sasa Bunge limekubali na limepitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Kwa hiyo nichukue fursa hii kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri na Watendaji wote waliopo hapa, chini ya Katibu Mkuu; tunawapongeza kwa kazi nzuri. Waheshimiwa Wabunge wengi wamepongeza hapa kwamba kazi kubwa imefanyika na maana yake ni kwamba mnamsaidia vizuri sana Mheshimiwa Rais katika hilo eneo. Kwa hivyo tunawapongeza sisi sote kwa pamoja; na Waheshimiwa Wabunge kwa upande wa Kamati yetu tunawashukuru sana pia kwa kazi nzuri miliyofanya. Mmeleta taarifa ambayo imetupa mwelekeo kwamba Serikali yetu

inaelekea wapi, na ninyi kama Bunge mmetoa ushauri na mengine mmesema mlishawashauri Serikali na wameyafanya kazi. Kwa hiyo tunawapongeza sana Kamati kwa Kazi nzuri mliyoifanya

Vilevile pia Waheshimiwa Wabunge mbalimbali ambao mmeshiriki katika kuchangia wengine kwa maandishi na wengine kwa kuzungumza. Mengine ambayo mmeyazungumza kama ushauri wataalamu wako hapa tunaamini wameyachukua na watayafanya kazi na yumkini yatasaidia zaidi kwenye kuboresha huko tunakoelekeea.

Pia tunawashukuru sana Waziri na Naibu Waziri kwa ufanuzi mlioutoa, tunaamini vyombo vyetu vya habari vitawapelekea sasa Wananchi ili waelewe haya mambo yanaendaje, na pia ufanuzi mlioutoa unasaidia kuondoa hofu hizo za kwamba mipaka ya majirani zetu imefungwa; kwa hiyo tunawashukuru sana kwa huo ufanuzi mlioutoa.

Kwa hiyo tunawashukuru sana kwa huo ufanuzi mlioutoa. Naona kuna wakati hapa mezani walikuwa wananiangalia kila wakati wanankumbusha kengele ya pili sasa nikawa nawaza hapa mimi ndio niko hapa mbele; lakini sasa huyu anayezungumza ni mwalimu wangu hii sio sehemu yake ya kuzungumza mambo mengi kuhusu yeye. Lakini labda jambo moja tu la kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Kabudi rekodi yake pale Chuo Kikuu cha Dar es Salaam haijavunjwa mpaka leo. (*Makofi*)

Kuwa mwanafunzi aliyejewa na ufaulu mkubwa sana tangu Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kianze mpaka sasa hiyo historia haijavunjwa. Wakati yeye anasoma "A" ziliikuwa zinaitwa Kabudi, kwa hiyo mtu akiulizwa umepata "A" ngapi alikuwa anaulizwa una Kabudi ngapi (*Makofi*)

Vilevile jambo lingine nililojifunza ni kwamba ukifika Mambo ya Nje, pengine na kuzungumza kunabadilika sijui kama mmeionna swaga ya Mheshimiwa Waziri. (*Makofi/ Kicheko*)

Naona mambo mazito kabisa, namna ya kuzungumza na nadhani ni mambo mazuri kukaa kaa karibu unajifunza namna ya kuzungumza ili kuvutia watu wakusikilize. Kwa hiyo nikupongeze sana Mheshimiwa Waziri naona mambo yamebadilika kuelekea sehemu nzuri zaidi. Kwa hiyo tumejifunza hapo.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo ninawashukuru nyie wote kwa pamoja na sasa naahirisha Shughuli za Bunge mpaka kesho saa nane mchana.

*(Saa 11.56 Jioni Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi,
Tarehe 14 Mei, 2020 Saa Nane Kamili Mchana)*